# HADHRAT MAULAWII NURUDDIN[ra]

# KHALIFATUL MASIHI I

NA

Muhammad Zafrullah Khan[ra]

Mfasiri

Jamil R. Rafiq

Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya

Tanzania

**HADHRAT MAULAWII NURUDDIN**[ra]
**KHALIFATUL MASIHI I**


© Islam International Publications Ltd.

Chapa ya Kwanza ya Kiswahili: 2008
Nakala: 2000

Kimeenezwa na:
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania
Mnazi mmoja, Dar es Salam.
Simu: +255222110473
Fax: +255222121744

Kimechapwa na:
Ahmadiyya Printing Press
Dar es Salam. Tanzania
Simu: +255222111031

**ISBN 9987 - 438 - 08 - 3**



**HADHRAT ALHAAJ MAULAWII NURUDDIN[RA] KHALIFATUL MASIHI I**

# YALIYOMO

YALIYOMO .... ... ... ... ... ... .... ... ... ... ... ... .... ... ... ... ... ... .... V
MAELEZO YA MWENEZI .. ... ... ... ... .... ... ... ... ... ... ... .... VI
KUHUSU MWANDISHI .. ... ... ... ... .... ... ... ... ... ... ... .... VII
NENO LA MBELE ... ... .... ... ... ... ... ... .... ... ... ... ... ... .... IX
MANDHARI YA NYUMA ... ... ... ... ... .... ... ... ... ... ... .... 1
KATIKA UTAFUTAJI WA ELIMU ... .... ... ... ... ... ... .... 8
KUKAA BHOPAL ... ... .... ... ... ... ... ... .... ... ... ... ... ... .... 19
WASAA MZURI WA KWENDA HIJAZI ... ... ... .... 30
TABIBU MJINI BHERA ... ... ... ... ... .... ... ... ... ... ... .... 42
MGANGA WA MAHARAJA .. ... ... ... .... ... ... ... ... ... .... 52
MTAFUTA NA MTAFUTWA ... ... ... .... ... ... ... ... ... .... 67
KUHAMA .... ... ... ... ... ... .... ... ... ... ... ... .... ... ... ... ... ... .... 81
MFUASI BORA HALISI ... ... ... ... ... .... ... ... ... ... ... .... 88
MTAALAMU MTUKUFU ... ... ... ... ... .... ... ... ... ... ... .... 96
MSHAURI MWENYE BUSARA ... .... ... ... ... ... ... .... 114
KHALIFATUL MASIHI .... ... ... ... ... ... .... ... ... ... ... ... .... 133
CHEO CHA KHALIFA.... ... ... ... ... ... .... ... ... ... ... ... .... 149
UKHALIFA .... ... ... ... ... ... .... ... ... ... ... ... .... ... ... ... ... ... .... 171
UGONJWA.... ... ... ... ... ... .... ... ... ... ... ... .... ... ... ... ... ... .... 198
MAWAIDHA YA MWISHO ... ... ... ... .... ... ... ... ... ... .... 216
KUMBUKUMBU LANGU ... ... ... ... ... .... ... ... ... ... ... ....246
MANDHARI YA MWISHO ... ... ... ... .... ... ... ... ... ... ....267

بِسۡمِ اللّٰہِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِیۡمِ

نَحۡمَدُہٗ وَنُصَلِّیۡ عَلٰی رَسُوۡلِہِ الۡکَرِیۡمِ

# MAELEZO YA MWENEZI

Sir Muhammad Zafrullah Khan r.a. aliandika kitabu katika lugha ya Kiingereza kiitwacho *'Hadhrat Maulawii Nuruddin r.a.'* juu ya maisha ya Khalifatul Masihi I, kilichochapishwa zamani. Kitabu kinaeleza kwa urefu na mapana historia ya Al-Haj Hadhrat Hakim Maulana Nuruddin r.a.

Maulana Sheikh Jamil R. Rafiq, Amir na Mbashiri Mkuu wa zamani wa Tanzania na Kenya, amekifasiri kitabu hicho kwa Kiswahili. Tafsiri hii inaonyesha taaluma yake ya hali ya juu na ya ajabu sana ya lugha ya Kiswahili.

Tafsiri hii ya Kiswahili ilisomwa kwa makini na Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani na Sheikh Mubarak Mahmud wabashiri wa zamani wa Tanzania, ambao wakatoa baadhi ya mashauri mema. Vile vile katika kukamilisha kazi hii Bwana Muhammad Shafiq Sehgal, Bwana Farrukh Javed na Bwana Sherifu Tanwir Mujtaba wakasaidia kwa njia mbalimbali. Tafsiri hii ni tunda la *'Dawati la Kiswahili'*.

Mfasiri na wote walioshughulikia kazi hii kubwa wanastahili kuombewa. Mwenyezi Mungu Awajalie malipo bora na Akubali juhudi na huduma yao. Amin.

Ch. Muhammad Ali,
Wakilut Tasnif,
Tahrike Jadid,
Rabwah Pakistan.
20 Aprili, 2008.

## KUHUSU MWANDISHI

Sir Muhammad Zafrullah Khan r.a. (1893-1985), Sahaba wa Masihi Aliyeahidiwa a.s, mtu mwenye ufahamu na uwezo wa ajabu sana wa kukumbuka, msemaji mzuri, mwandishi sana na mtaalamu wa hali ya juu wa mtaala wa kulinganisha dini mbalimbali, alizaliwa nyumbani mwa Ch. Nasrullah Khan mjini Sialkot. Aliungana na Uahmadiyya, pamoja na wazazi wake, kwa mkono wenye baraka sana wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. mnamo mwaka 1904. Alisoma katika shule ya msingi Municipal Board School, kisha American Mission High School. Ingawaje alikuwa hana afya njema, akapata kuwa wa kwanza katika shule katika mtihani wa darasa la kumi alipokuwa mwenye umri wa miaka kumi na minne. Akapata shahada baada ya kufaulu mtihani wa chuo kikuu (katika daraja I) katika Government College Lahore mnamo 1911, na alikuwa mwanafunzi wa kwanza kutoka India aliyepata kuwa wa kwanza katika London University katika mtihani wa mwisho wa L.L.B. mnamo 1914. Alianza kufanya kazi ya uwakili mjini Sialkot katika mwaka 1915. Ijapokuwa mdogo wa umri na uzoefu, akachaguliwa kuwa mwalimu kufundisha katika Chuo cha Sheria Lahore mnamo 1919. Alianzia kazi kama mwanasiasa akateuliwa kuwa mjumbe wa Baraza la kutunga Sheria la Panjab mnamo mwaka 1926. Alifanikiwa kutetea kesi ya Waislamu katika Baraza la ‘Meza ya Duara’ lililofanyika huko London mnamo 1930, 1931 na 1932. Alichaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Indian Muslim League mnamo mwaka 1931. Kwa miaka sita alikuwa mwanachama wa Halmashauri ya Gavana-Jenerali ya British India na alihudumia katika nyanja mbalimbali kama vile afya, uchumi, maarifa ya mambo ya kale, reli na kadhalika. Katika kipindi hicho alihudumia kama mjumbe wa India isiyogawanyika katika mabaraza mbalimbali huko ng’ambo na akapata fursa ya kutoa fikra ya Mataifa-Mawili mbele ya wakuu wa

nchi nyingi. Ndiyo sababu siku zote yeye na wenzake akina Qaide Azam Muhammad Ali Jinnah walikuwa ni miongoni mwa watu waliotegemewa.

Alikuwa Waziri wa Mambo ya Nje mnamo 1947, na kwa miaka mingi aliongoza Pakistan katika Baraza kuu La Umoja wa Mataifa. Alikuwa Mwenyekiti wa kipindi cha kumi na Saba cha Baraza Kuu La Umoja wa Mataifa. Akakamilisha kazi yake yenye sifa akiwa jaji wa korti ya Mataifa mjini Hague, Uholanzi (1954-1961), kwanza akiwa Makamu wa Raisi (1958-1961) kisha Raisi kutoka 1970 hadi 1973.

Miongoni mwa maandiko yake kuna Tafsiri ya Kurani Tukufu kwa Kiingereza, *Riyadhus Salihina* (kitabu cha Hadithi) kwa Kiingereza na *Tadhkirah* (mkusanyiko wa wahyi, ruya na kashfi za Masihi Aliyeahidiwa a.s.) pia kwa Kiingereza. Aidha, aliandika zaidi ya dazeni ya vitabu juu ya mambo mbalimbali kuhusu dini na siasa.

# NENO LA MBELE

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s, Masihi aliyeahidiwa na Imam Mahdi, Mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiya, alifariki baada ya kuugua kwa masaa machache, tarehe 26 Mei 1908, mjini Lahore. Yeye alipokea habari za ukaribu wa kufariki kwake kwa njia ya ufunuo aliofunuliwa na Mungu majuma kadha kabla. Hata hivyo, habari hizi zilipotimia za kifo chake wanajumuiya walipata pigo kubwa mioyoni mwao.

Wapinzani wake wakali wakafarijika, na wale waliokuwa wabaya zaidi walifanya shangwe isiyofaa kwani walidhani kwa vyovyote hatari kubwa kabisa kwa baadhi ya itikadi na imani zao na kwa mienendo yao waliyoyazoea iliondolewa. Wakadhani kwamba Jumuiya aliyoanzisha haraka itazikwa katika historia na itasahaulika kama kiwimbi kisichofungamana juu ya uso wa imani sahihi ya Islam.

Wenye busara miongoni mwa Waislamu, ingawaje hawakukubaliana na madai yake, walihisi kwamba wamefiwa na shujaa mkubwa wa Islam ambaye kifo chake ni hasara kubwa isiyoweza kurekebishwa. Hata wasiokuwa Waislamu walikiri na kuusifu sana utaalamu wake, unyofu wake mkubwa na uhalisi na wema wa maisha yake.

Katika wakati huo muhimu sana katika historia ya Jumuiya, ya dini, na ya binadamu, kabla hajazikwa yeye huko Qadian tarehe 27 Mei, Hadhrat Maulawii Nuruddin alitangazwa kuwa *Khalifa* wake wa kiroho ambaye alikuwa mfuasi wake mkuu na mwaminifu wa hali ya juu, aliyeipenda ajabu Kurani Tukufu, naye alikuwa pia tabibu maarufu sana. Wanajumuiya wote walifanya baiati kwake akiwa Khalifatul Masihi. Akiwa na cheo hicho, yeye aliwajibikiwa

kutekeleza kazi ile aliyowajibikiwa kutekeleza Hadhrat Abu Bakr r.a., *Khalifa* wa kwanza wa Mtume Mtukufu s.a.w. wa Islam wakati wa hatari kubwa zaidi kwa Islam na kwa binadamu, miaka elfu moja na mia tatu hapo kabla. Mungu Mhisani akamjalia Hadhrat Maulawii Nuruddin kutekeleza kazi hiyo vizuri sana hata kwamba wakati wa kifo chake kilichotokea mnamo Machi 1914, Jumuiya iliyokwisha timiza robo karne mpaka wakati huo, ilikuwa imekwisha imarika na kukingwa isiweze kuvunjika na kusambaratika. Majaribio ya jambo hili yakaja haraka kwa sura ya tambio ya hatari kwa kawaida yenyewe ya kuwepo kwa *Ukhalifa* kutokana na wanajumuiya kadha mashuhuri waliodai kwamba wanajumuiya asilimia 95 wanawaunga mkono. Lakini muda si muda wakafumbuliwa macho. Sehemu kubwa zaidi ya Jumuiya ikaipinga tambio vikali na kwa imara, na Jumuiya inaendelea kusonga mbele ikipata ushindi baada ya ushindi chini ya uongozi mwema na wenye hekima na ulezi bora wa Hadhrat Khalifatul Masihi II (1914-1965) na Hadhrat Khalifatul Masihi III. Hadi sasa matawi yake yameenea duniani kote, na idadi ya wanajumuiya inayoongezeka kila siku inazidi milioni kumi. Inatambuliwa sana kuwa ni ufufuo wa Islam uliokuwa umeahidiwa na Mungu (9:33).

Daraja la Hadhrat Maulawii Nuruddin, Khalifatul Masihi I r.a. limeimarika barabara katika historia ya Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya. Lakini wale wanajumuiya na wengine watafutao ukweli wasiojua Kiurdu hawajui sana kuhusu maisha na khulka zake. Hili ni jaribio la kueleza kidogo sana habari hizo. Kwa njia hii mwandishi anataka kulipa sehemu ndogo sana ya deni kubwa la kumtolea shukrani analowiwa na mtu huyu mpendwa mwenye adhama, mtukufu, maarufu na mkarimu ambaye kutoka kwake mwandishi alipata baraka nyingi na ukarimu mwingi.

Mwandishi amechukua maelezo karibu yote, isipokuwa mlango

wa 17, kutoka katika kitabu cha Kiurdu kuhusu maisha ya Hadhrat Khalifatul Masihi I kilichotungwa na Sheikh Abdul Qadir (jina lake la zamani Saodagar Mal). Kila habari iliyoelezwa ndani ya kitabu hicho chenye thamani imeelezwa pamoja na marejeo yake. Lakini kwa kuwa marejeo yote ni kwa Kiurdu, kwa hiyo imeonelewa si lazima kuyataja katika kitabu hiki, kwani kwa msomaji wa kawaida hakutakuwa na manufaa yoyote. Mchunguzi aweza kuyakuta bila shida katika *Hayate Nur*.

Marejeo yote ni ya Kurani Tukufu isipokuwa yaliyotajwa tayari.

# I

# MANDHARI YA NYUMA

Hadhrat Maulawii Nuruddin r.a. alizaliwa mjini Bhera, wilaya ya Shahpur, Panjab, mnamo mwaka 1841. Alikuwa mdogo kabisa baina ya nduguze saba na madada wawili. Yeye alikuwa wa 34 katika mnyororo wa nasaba ya wanaume kumfikia moja kwa moja Hadhrat Umar r.a. aliyekuwa *Khalifa* wa pili wa Mtume wa Islamu s.a.w. Babake Hafidh Ghulam Rasul na mara kabla yake kwa akali wanaume kumi katika jadi yake walikuwa wamehifadhi Kurani Tukufu nzima kwa ghaibu. Mamake, Bi Nur Bakht, alitokana na ukoo wa Awan, mkazi wa kijiji kimoja maili chache kutoka Bhera. Yeye alikuwa anawafunza watoto wadogo wa jirani zake tafsiri ya Kurani Tukufu kwa Kipanjabi na kuwafundisha vitabu vya mwanzo vya fik'hi ya Kiislamu. Kadhalika mtoto wake mdogo pia alifundishwa naye. Katika uzee alikuwa anasema mara nyingi kwamba yeye alipata kusikia Kurani Tukufu ikisomwa na mama yake pindi alipokuwa tumboni mwake na alinyweshwa mapenzi ya Kurani pamoja na kunyonyeshwa na mamaye. Bibi huyo pia alikuwa mwalimu wake wa kwanza. Baba yake vilevile alikuwa anaipenda ajabu Kurani. Alikuwa tajiri na alitumia fedha nyingi kununua nakala za Kurani hata kutoka mahali pa mbali kama Bombay na kuzigawa bure.

Yeye alikuwa mzazi mwenye moyo wa kupenda, mkarimu na mpole. Aliwawekea watoto wake shabaha kubwa sana na kuwatia moyo kwa kila hatua. Mwanawe mdogo ambaye baadaye alikuwa mashuhuri safari moja alisema: 'Baba yangu alipenda sana maendeleo yetu kiasi hiki kwamba kama yeye angekuwa hai wakati huu angenipeleka Amerika kwa ajili ya kujielimisha.'

Kijana Nuruddin alipokua kidogo alipelekwa shuleni. Katika

zama zile za udogo wake madrasa ya shule hayakuwa na watoto wengi; kila mwanafunzi aliangaliwa vizuri na mwalimu. Kwa hiyo uhusiano wa dhati uliimarika baina ya mwalimu na mwanafuuzi. Kadri uhusiano huo ulivyokuwa mkubwa ndivyo alivyonufaika zaidi mwanafunzi. Mpaka wakati huo desturi ya kufundisha baada ya saa za shule kwa kuwatoza wanafunzi fedha ilikuwa bado haijajulikana. Waalimu walitosheka na chochote walichopata kama mshahara, na katika nafasi yao waliwasaidia bure wanafunzi waliostahili na wengine wa kutumainiwa. Waliheshimiwa sana na wanafunzi wao ambao kabisa hawakushindwa kulipa deni kubwa la shukurani waliyowajibikiwa kuwatolea. Bwana Nuruddin, kwa fadhili tupu ya Mungu, alijipatia cheo kikubwa maishani mwake. Sikuzote alimtaja kila mwalimu wake kwa heshima na kumtolea shukurani. Kaka yake mkubwa, Maulawii Sultan Ahmad, alikuwa mtaalamu mkubwa wa dini na alimlea yeye kwa moyo wa mapenzi sana. Mama yao aliwawekea wote hao mfano bora wa utawa na maisha mema na kuwatilia nyoyoni mwao ukweli halisi katika Kipanjabi cha kawaida. Kiurdu hakikutumika kwa kawaida siku hizo katika jimbo la Panjab. Bwana Nuruddin mara ya kwanza alikisikia kikitumiwa na askari mmoja mkazi wa mjini Deoband na akaingiwa moyoni mwake mapenzi ya lugha hiyo. Alipatwa na shauku ya kusoma vitabu vya Kiurdu na akafaidika sana kwa kusoma vitabu vilivyoandikwa na waandishi waliotokana na ukoo wa Shah Waliyyullahi wa Delhi. Alipata kuvipenda vitabu tangu alipokuwa mdogo na akaanza kuvikusanya.

Tangu utotoni alichukia kutumia lugha chafu. Wenzake waliocheza pamoja naye walikuwa wakijihadhari kuhusu jambo hili walipokuwa naye. Alipenda sana kuogelea, alikuwa anakwenda kuogelea katika mto Jhelum hata katika kipupwe.

Kaka yake mkubwa alimiliki mtambo wa uchapishaji mjini

Lahore, naye alilazimika kutembelea Lahore mara kwa mara kwa sababu hiyo. Safari moja Bwana Nuruddin alipokuwa mwenye umri wa miaka kumi na miwili takriban alifuatana na kaka yake kwenda Lahore ambako alipata kuugua na akatibiwa vizuri na Bwana Hakim Ghulam Dastagir wa Said Mitha. Akiathirika na mwenendo wake na adhama yake, Bwana Nuruddin alipata shauku ya kusoma utabibu; lakini kaka yake akamwelekeza asome Kiajemi na akafanya mpango ili afundishwe na mwalimu mmoja mashuhuri wa lugha ya Kiajemi, Bwana Munshi Muhammad Kasim Kashmiri, ambaye alimfundisha kwa jitihada na upole hata kwamba yeye akajua lugha hii vizuri. Alijifunza mwandiko mzuri kwa stadi mmoja wa ufundi huu, Mirza Imam Verdi. Waalimu wake wote wawili walikuwa Mashia, hivyo mwanafunzi wao alipata ujuzi kiasi fulani wa imani, mafundisho na matendo ya Kishia.

Huko Lahore alipata kukaa miaka miwili. Baada ya kurejea Bhera aliendelea kujifunza Kiajemi kwa Haji Mian Sharfuddin. Baada ya muda kidogo nduguye Maulawii Sultan Ahmad pia alirejea Bhera na akaanza kumsomesha mafunzo ya lugha ya Kiarabu. Alitumia njia rahisi sana ya kumfunza iliyompendeza na kumvutia hata kwamba alianza kupata maendeleo mema katika kujifunza lugha inayofikiriwa kuwa ngumu.

Panjab, miaka michache hapo kabla, iliokolewa na Uingereza katika machafuko ya kisiasa, utawala mbovu, udhalimu, mauaji na ukosefu wa usalama ambamo iliangukia baada ya kifo cha Maharaja Ranjit Singh mnamo mwaka 1839. Hali ya elimu, maarifa na ustaarabu ilikuwa chini kabisa. Watu, hata masheikh, hawakujua tafsiri ya Kurani Tukufu; na kuitaali hakukutiliwa nguvu. Upendo wa Bwana Nuruddin kujifunza Kurani Tukufu ulichochewa wakati huo kwa sababu ya tukio moja zuri. Mwuza vitabu wa Kalkata (Calcutta, India) aliwasili

Bhera mnamo mwaka 1857 na akakaa kwa babake Nuruddin kwa siku chache akiwa mgeni wake. Bwana huyo akamsihi sana bwana Nuruddin kujifunza tafsiri ya Kurani Tukufu na akampatia nakala moja ya sura tano kubwa za Kurani Tukufu zilizochapishwa pamoja na tafsiri kwa Kiurdu. Hilo likathibitika kuwa jambo jema lisilokuwa limetazamiwa ambalo Bwana Nuruddin akalipokea kwa furaha.

Mara baadaye mfanya biashara mmoja wa Bombay alimsisitizia kusoma vitabu viwili vya Kiurdu, *Taqwiyatul-Iman* na *Mashariqul Anwari*, ambavyo vilitoa maelezo ya baadhi ya sehemu za Kurani Tukufu. Hivyo akawekewa msingi wa kujitolea kwake kwa kitabu kitukufu ambacho kikawa upendo wake mkuu maishani mwake na kumtawala hadi pumzi yake ya mwisho.

Katika muhula huo yeye akatembelea Lahore mara ya pili na akaanza kujifunza utabibu kwa mganga maarufu Hakim Allah Din wa Gumti Bazar, lakini kukaa kwake Lahore kulikatishwa, hivyo masomo yake nayo yaliahirishwa.

Mnamo 1858, alipokuwa mwenye umri wa miaka kumi na saba, alianza kusoma katika Normal School mjini Rawalpindi ili kupata diploma ya ualimu. Mwalimu mkuu wa shule hiyo, Maulawii Sikandar Ali, alifurahi sana kwa maendeleo yake hata kwamba akamruhusu kutokuhudhuria katika masomo kadha ya kawaida. Alitumia nafasi hiyo kwa njia bora sana kwa kujipatia maendeleo katika masomo mengine zaidi kwa kusaidiwa na waalimu wake binafsi. Kozi ya miaka minne ilipokwisha, yeye alikuwa amepata ustadi katika masomo mengi sana. Alipita vizuri kabisa katika mtihani wa diploma hata kwamba katika umri mdogo wa miaka 21 akapatiwa kazi ya kuwa Mwalimu Mkuu wa shule moja ya Pind Dadan Khan, maili chache kutoka Bhera, ng'ambo ya pili ya mto Jhelum. Aliendelea na kazi hii kwa miaka minne.

Pindi alipokuwa huko Pind Dadan Khan, yeye aliendelea

na mafunzo ya Kiarabu chini ya uongozi wa nduguye Maulawii Sultan Ahmad. Pia akaanza kupata ndoto za kweli zilizochangia kukuza nguvu zake za kiroho na ufahamu wake. Mtaala wake wa Kurani Tukufu ulikuwa umenoa busara yake ya kiroho mapema zaidi. Alipokuwa anasoma katika Normal School ya Rawalpindi, alielekezwa kumtembelea Bwana Alegzander, mhubiri mmoja wa Kikristo, asiyekaa mbali naye. Padre huyo alimpatia vitabu viwili vikubwa, *Mizanul Haq* na *Tariqul Hayat*. Akavisoma kwa makini, lakini akavikuta havimtulizi, bali ni bure tu.

Safari moja alipokuwa akipita kijijini katika kitongoji cha Pind Dadan Khan, msifu mmoja wa babake alimkaribisha na kumkirimu sana. Na alipotaka kuondoka, Bwana huyo akamwomba amwandikie hirizi au amtolee mawaidha au amwambie jambo litakalomfaa au kumsaidia. Yeye alimsomea tu aya hii ya Kurani Tukufu: Sema, 'Mimi siwaambii, Ninazo hazina za Mwenyezi Mungu, au najua mambo ya siri; wala siwaambieni, Mimi ni Malaika.' (6:51)

Kujiuzulu kwake katika madaraka ya kuwa Mwalimu Mkuu kukatokea ghafla kwa njia ya ajabu. Mwenyewe anafafanua kama ifuatavyo:

> 'Safari moja Mkaguzi wa mashule alifika muda nilipokuwa nikila chakula. Nikamkaribisha kwenye chakula. Lakini yeye akasema: 'Naona hujanitambua. Jina langu ni Khuda Bukhsh, nami ndiye Mkaguzi wa Mashule.'
>
> 'Ee, kweli. Vyema. U mtu mheshimiwa. Huwezi kushiriki katika chakula pamoja na mwalimu! Vizuri sana!' Nilipokwisha sema hayo, niliendelea kula. Na yeye akimshika farasi wake mdogo akangoja ili niwatume baadhi ya wanafunzi waje kumshikia farasi wake. Alipoona sikutikisika, akaniomba: 'Tafadhali mwambie mwanafunzi

yeyote amshike farasi wangu.'

Nikamjibu: 'Bwana, u mtaratibu sana hata kwamba huli chakula ukaribishwapo na mwalimu ukidhania ni rushwa. Basi nawezaje kumwambia mwanafunzi yeyote amshike farasi wako. Wanakuja shuleni kujifunza siyo kutumika kama watumishi katika banda la farasi. Isitoshe, waweza pengine kuomba kwamba farasi afungashwe na kulishwa pia; lakini farasi awezaje kulishwa ilhali wewe mwenyewe hupendi kukubali ukarimu wa mwalimu?'

Farasi akaanza kuwa na wahaka, lakini wakati huo wasaidizi wa Mkaguzi wakawasili na kuanza kushughulikia mambo yote hayo.

Halafu akataka kwenda kuwatahini wanafunzi; ndipo nikawapanga wanafunzi na mwenyenwe nikajitoa na kukaa kando. Mkaguzi akawatahini, kisha kaniambia: 'Nilipata kusikia kuwa u stadi sana, nawe unayo diploma ya fahari kutoka katika Normal School. Labda hiyo ndiyo sababu ya kiburi chako.'

Nikajibu: 'Bwana, siiamini karatasi ya inchi chache mraba kuwa Mungu. Kisha niliagiza kuletewa diploma hiyo, nikaichana vipande vipande mbele ya macho yake, nikafafanua kwamba simshirikishi Mwenyezi Mungu na chochote kiwacho. Mkaguzi akasikitikia yote yaliotendeka na akajilaumu kwa diploma yangu kupotezwa hivyo. Lakini ukweli wenyewe ni kwamba kuichana diploma kukawa jambo kuu maishani mwangu na hilo likanifungulia milango ya fadhili ya Mungu.'

Akiisha ondolewa vizuio na mipaka baada ya miaka minne, sasa

kijana Nuruddin mwenye umri wa miaka ishirini na mitano akarudia kwenye shughuli yake aliyoipenda, yaani kutafuta elimu. Baba yake alimfanyia mpango ili kujifunza Kiarabu kwa Maulawii Ahmad Din wa Buggewala. Lakini Sheikh huyo mtaalamu siku hizo alikuwa anakwenda huko na huko kwa shughuli zake za kujenga msikiti mmoja mkubwa, na wanafunzi wake walilazimika kusafiri naye. Bwana Nuruddin alipitisha mwaka mzima katika shughuli ya kwenda huko na huko na akijiona hakunufaika mwishoni mwa muda huo wote akamweleza nduguye Maulawii Sultan Ahmad kutokuridhika kwake. Basi nduguye akamchukua kumpeleka Lahore na kumweka chini ya usimamizi wa Bwana Hakim Muhammad Bakhsh na baadhi ya walimu wengine. Katika siku chache mwanafunzi mmoja mwenzake alimshawishi kwamba wote wawili waende Rampur kujipatia elimu ya juu zaidi. Yeye alipomweleza babake shabaha hiyo, akampa idhini mara moja na kumsihi: ‘Nenda kutafuta elimu mbali sana hata usipate habari zetu; lakini usieleze habari hii kwa mamako isije akaudhika kwa kutazamia kutengana naye kwa muda mrefu, na kukushawishi uachane na shabaha yako hii.’

Wakati wa kujitayarisha kwa safari yake alikumbuka nasaha hii ya mtaalamu mmoja mheshimiwa mwenye hekima: ‘Popote utakapokuwa mkazi, jenga uhusiano wa kirafiki na mkuu wa polisi wa mji, daktari mmoja hodari, mtawa mmoja wa hapo na mzee wa mji.’

# II

# KATIKA UTAFUTAJI WA ELIMU

Katika umri wa miaka ishirini na saba Bwana Nuruddin aliondoka Lahore kuelekea Rampur kwa miguu pamoja na wenzake wengine wawili ili kutafuta elimu. Safari ikawa ngumu na ikachukua siku nyingi kidogo. Walikuwa hawamjui mtu yeyote huko Rampur. Walipofika huko wakauendea msikiti mmoja ambao haukuendewa na watu sana na wakajikalia humo. Msichana mmoja mwenye umri wa miaka saba ama minane aliwaletea chakula asubuhi na jioni kwa siku mbili. Siku ya tatu alipowaletea asubuhi chakula chao akasema: 'Mama yangu anakuombeni mmwombee kwamba mumewe amtendee vema kwa upole.' Bwana Nuruddin akafuatana naye kwenda nyumbani na kumsihi babake kwa maneno yafaayo ya kumwelekeza. Motekeo yakawa ni kuwasuluhisha mume na mke. Na kwa sababu ya rehema hii ya Mungu, yeye akamtolea Mwenyezi Mungu shukurani.

Jioni hiyo, wakati wa kutembea katika mtaa wa Wapanjabi alipata kuonana na Sheikh mmoja, Hafidh Abdul Haq, aliyemkaribisha ahamie msikitini mwake. Bwana Nuruddin akampasha habari kwamba tupo watu watatu. Akaambiwa wote watatu wanakaribishwa. Hapo yeye akamweleza mhisani wake ya kwamba sisi tumekuja Rampur kwa kutafuta elimu, wala haitupasi tuombe-ombe kwa kupata riziki au tuwe waangalizi wa watoto wa mtaa kwa shabaha hii. Pia tutahitaji vitabu na walimu. Akahakikishiwa mambo yote yataangaliwa. Wakaelewana juu ya mambo yote na Bwana Hafidh Abdul Haq akatimiza yote aliyoahidi. Katika hali hii isiyo na matatizo yoyote Bwana Nuruddin akapata maendeleo haraka katika masomo yake.

Safari moja kundi moja kubwa la wanafunzi walikuwa wanajadiliana juu ya swala moja gumu. Akitafakari kidogo Bwana

Nuruddin akatangaza kwamba amekwisha litatua hilo. Wanafunzi wengi wakamwona sura yake haivutii wakajaribu kumdhihaki. Lakini wanafunzi Wapanjabi wakasisitiza kwamba lazima tumsikilize. Pendekezo hilo likakubaliwa. Hapo Bwana Nuruddin alitoa shauri ya kwamba mtaalamu mmoja mashuhuri awekwe kuwa mwuamuzi. Ndipo Maulawii Ghulam Nabii aliyekuwa mtu mwenye heshima akawekwa kuwa mwuamuzi. Huyo bwana akafurahia sana mno maelezo aliyotoa Bwana Nuruddin na akamtaja kuwa Maulawii, jambo ambalo akaliona kuwa ni heshima kubwa aliyotunukiwa.

Maulawii Nuruddin – sasa ni haki kabisa atajwe hivyo –hakuridhika kabisa na njia ya kufundisha iliyofuatwa siku hizo. Mwanafunzi zaidi alikuwa anaachwa afuate njia zake mwenyewe wala hakuelekezwa na kuongozwa ilivyohitajiwa. Wakati mwingine baadaye alisema:

> “Mara nyingi nimehisi ya kwamba kama Waislamu wangeagiza vitabu vya mafundisho kwa mashule na idara za kielimu baada ya kutafakari ipasavyo kwa kuzingatia mahitaji ya dini na maisha ya wanafunzi wangeinufaisha sana jamii ya Waislamu. Mafundisho yasiofululiza wala kupangwa yanaleta matatizo ya aina mbalimbali. Tatizo kubwa zaidi nililokabili ni kwamba walimu hawawaongozi wanafunzi kuhusu darasa ama vitabu vya masomo, wala wanafunzi hawajioni huru kuweza kurekebisha masomo yao kulingana na mahitaji ya kukuza ipasavyo akili zao na vipawa vyao ambavyo Mungu Amewajalia. Wala khulka njema hazikuangaliwa ili zikuzwe na kutendwa sawa nazo. Nasema kwa yakini kwa kushuhudia mwenyewe ya kwamba mwalimu yeyote wa siku hizo hakujali kabisa kuinua hali ya khulka bora za vijana. Nasikitikia utovu huo hata leo. Hakuna mwalimu wangu yeyote awaye

> aliyeangalia vitendo vyangu, maneno, mazoea na khulka zangu. Wala hayakuangaliwa mambo kuhusu itikadi na imani."

Shah Abdur Razzaq alikuwa ni mja wa Mungu huko Rampur aliyetembelewa na Bwana Maulawii Nuruddin mara kwa mara. Safari moja yeye alimwendea baada ya siku nyingi sana. Hapo akamwuliza: "Nuruddin, kitu gani kilichokuzuia usije kwa muda mrefu hivi?"

Akajibu: "Bwana, nilishughulika sana katika masomo, na pengine nilipitiwa kidogo."

"Je, umewahi kupita dukani kwa mchinjaji?"

"Ndiyo, Bwana, mara nyingi sana."

"Basi haikosi uliona kwamba mchinjaji anapoendelea kukata nyama ya mnyama aliyekwisha chinjwa, visu vyake vyasenea kwa mafuta; hapo yeye huvinoa kwa kuvisugua-sugua kimoja kwa kingine."

"Ndiyo, Bwana. Lakini nimeshindwa kuelewa unakusudia nini."

"Haya, ni hivi tu ya kwamba kupoteana kwatufanya wasahaulifu kidogo, na kuonana kwatunoa sote wawili."

Maulawii Nuruddin mara nyingi alikuwa anasema kwamba alinufaika sana na nasaha hiyo ya Bwana Shah Abdur Razzaq. Kukaa na wema humhimiza mtu kuwa macho kiroho.

Alikaa huko Rampur miaka mitatu takriban na akaendelea na masomo kwa jitihada na bidii kubwa hadi akapata kuugua sana. Kuugua kwake kuliamsha shauku yake ya kujisomea utabibu. Akifanya utafiti akagundua ya kwamba tabibu mashuhuri zaidi nchini humo ni Hakim Ali Husain wa Laknau (Lucknow). Basi akaamua

mara moja kuondoka kuelekea Laknau. Njiani akashinda kidogo mjini Muradabad ambako alipata kuonana na mtawa mmoja, Maulawii Abdur Rashid wa Benares ambaye alimsaidia vizuri kabisa mpaka akapona na kupata afya barabara katika muda wa majuma machache. Yeye sikuzote alifurahia kukumbuka hisani zake nyingi na akawa na moyo mkunjufu wa kumtolea shukurani.

Maulawii Abdur Rashid alikuwa mseja na akaishi maisha ya kawaida sana katika chumba kimoja kilichofungamana na msikiti mmoja. Siku moja jioni sana alifikiwa na mgeni, basi ikawa shida kwake namna atakavyoweza kumpatia mgeni chakula. Akamwambia kujinyosha kidogo na kupumzika hadi chakula kitakapokuwa tayari. Mgeni akalala kujinyosha na akapata usingizi. Maulawii Abdur Rashid akatawadha kama kwa ajili ya kusali na akakaa kuelekea kibla na akaanza kumwomba Mungu hivi: ‘Namkabidhi Mwenyezi Mungu jambo langu; hakika Mwenyezi Mungu ndiye Awaonaye watumishi wake.’ (40:45). Akashughulika sana katika maombi. Na baada ya kupita muda uliotosha kupika chakula akamsikia mtu fulani akisema: “Bwana, tafadhali, njoo haraka, mkono wangu unauma.” Maulawii Abdur Rashid akainuka, akamkuta mtu akishika sahani kubwa ya shaba iliyojaa pilau motomoto sana. Akaichukua, kamwamsha mgeni wake na kumpatia ale chakula hicho kitamu sana. Sahani hiyo ya shaba ilibaki chumhani wala hakuna aliyekuja kuichukua ijapokuwa ilitangazwa mara kwa mara na Maulawii Abdur Rashid kwamba mwenye sahani aje kuichukua. Maulawii Nuruddin naye akatimiziwa mahitaji yake mara nyingi sana kwa njia zisizo za kawaida asizozitambua sawa na ahadi ya Mungu iliyomo ndani ya Kurani Tukufu: ‘Na anayemwogopa Mwenyezi Mungu, (Mwenyezi Mungu) Humtengenezea njia ya kuokoka, na Humpa riziki kwa mahali asipopatazamia; na anayemtegemea Mwenyezi Mungu, basi Yeye Humtoshea.’ (65:3-4).

Alipoondoka Muradabad, Maulawii Nuruddin alishinda Kanpur siku moja kwa rafiki mmoja wa nduguye, kisha akaendelea na safari yake kuelekea Laknau. Hizo zilikuwa siku za kiangazi kikali sana na barabara zilijaa vumbi tupu. Na wakati alipowasili kwenye kituo cha Laknau alikuwa amefunikwa na mavumbi na akaonekana si mstaarabu wala si safi. Alipotoka tu kutoka kwenye gari alimosafiri alimwuliza mtu mmoja wapi anapoweza kumwona Hakim Ali Husain. Akaambiwa kwamba huyo bwana anakaa upande anaotazamana nao. Basi akachukua mzigo wake, akaingilia jengo bila kujali kitu katika hali hiyo hiyo aliyokuwa nayo. Kupita mlangoni akakuta chumba kikubwa ambamo katika upande wake wa pili alikuwa amekaa mtu mmoja kama malaika, mwenye ndevu nyeupe, mzuri wa sura, mwenye kuvutia, aliyevalia mavazi meupe pe, mgongoni mwake na mbavuni kuna matakia mazuri. Mbele yake vilikuwa vimewekwa baadhi ya vifaa vyake kwa kupangwa vizuri ambavyo angependa kuvitumia. Karibu na kuta watu wengi waheshimiwa walikuwa wamekaa kwa adabu nzuri. Sakafu yote ilikuwa imefunikwa kwa mashuka meupe sana. Mandhari hiyo yote kwa jumla aliiona msafiri kama ni ndoto. Hakushuhudia mfano wake kabisa hapo kabla. Hata hivyo hakuna kilichomwogofya. Akauweka mzigo wake katika kona ya mlango na akasonga mbele kwa uthabiti ndani ya chumba, akielekea moja kwa moja kwa mkuu wa hapo aliyemdhania sawasawa kabisa kwamba ndiye Bwana Hakim. Miguu yake iliyo na mavumbi ikaacha alama mbaya juu ya mashuka meupe ya sakafuni, jambo ambalo likamtatiza kidogo, lakini kulikuwa hamna la kufanya. Akifika mbele ya yule mheshimiwa akamsalimia kwa sauti ya juu akitamka: “Assalamu alaikum” (Salamu iwe kwako) na akanyosha mikono yake. Bwana Hakim akamjibu salamu zake kwa upole na akashika mikono yake yenye vumbi kwa mikono yake myororo. Mgeni akakaa mbele ya Bwana Hakim. Watu waliopo wakachukizwa sana na yote

yaliyotendeka. Hata maamkizi yake yalisikika masikioni mwao kama kitu cha kigeni. Mheshimiwa mmojawapo hakuweza kujizuia na akamwuliza: "Bwana, watokea mahali gani penye ustaarabu?" Yeye akajibu: "Ukosefu huu wa kawaida rasmi na maamkizi yangu pasipo hofu ni matokeo ya mafunzo ya yule asiyejua kusoma na kuandika, wa bonde lile lisilozaa, ambaye kwa muda alifanya kazi ya kuchunga mbuzi, baraka na amani ziwe kwake, na baba yangu na mama yangu wajitolee kwake." Maneno yake yaliwapiga waliopo hapo kama radi, na Bwana Hakim alielemewa na maono. Akamwuliza mwulizaji: "Umewahi kuwa mfuasi wa Mfalme, je, siku yoyote hapo kabla ulitunduwazwa hivyo?"

Baada ya kunyamaa kidogo, Bwana Hakim akamwuliza mgeni wake kwamba amejia nini. Naye akaambiwa kwamba yeye amefika ili kujifunza utabibu kutoka kwake. Bwana Hakim akamjibu: "Uonavyo, mimi ni mzee sasa, kufundisha hakunifai. Nimekwisha amua kabisa kwamba sitafundisha tena." Mgeni akalikabili akisema kwa mshangao na kuumia: "Maana yake yule Mshirazi, mtaalamu wa falsafa, alikosea alipoyakinisha kwamba ni dhambi kumwumiza mtu moyo." Bwana Hakim akaathirika sana na akifikiria upya akashauri: "Maulawii Nur Karim ni tabibu hodari, ningekushauri ujifunze kwake. Yeye atakufundisha vizuri." Mgeni akakimbilia methali nyingine ya Kiajema: "Ardhi ya Mungu si ndogo, nami si mwenye kilema." Hapo Bwana Hakim akakiri ameshindwa kabisa na akasema: "Naliachilia mbali azimio langu la kutokufundisha tena."

Bwana Hakim akaenda kupumzika na waliokuwapo nao wakaondoka. Maulawii Nuruddin akachukua kifurushi chake akaelekea nyumbani kwa Ali Bakhsh Khan, aliyekuwa rafiki wa nduguye ambaye alimkaribisha na kumburudisha. Akaoga na kubadili nguo na akaenda kwa makazi yake aliyopewa na Bwana Ali Bakhsh

Khan ambako alitakiwa kujitunza mwenyewe. Jaribio lake la kwanza kupika chapati halikufua dafu. Katika hali hiyo ya kushindwa akaomba: "Mola wangu, sielewi kabisa kuoka au kupika. Kumpatia kazi hiyo mtu kama mimi ni kuipoteza bure na kuiharibu riziki yako."

Akiwa safi na kuburudika akarejea kwa Bwana Hakim ambaye akamlaumu kidogo kwa sababu ya kutokuhudhuria: Ulipotea pasipo kupata ruhusa, jambo ambalo halimfai mwanafunzi. Hapa ndipo utakapokaa, lakini ukistahabu kukaa mahali pengine, hata hivyo utakula hapa. Kisha akauliza: "Kiasi gani cha maendeleo unakusudia kupata katika utabibu?" Jibu lake likawa: Nimekusudia kuwa sawasawa na tabibu mkubwa kabisa aliyewahi kuishi! Bwana Hakim akatabasamu na akasema: "Utawahi mahali fulani. Kama ungalikusudia chini kuliko hii ningalivunjika moyo."

Bwana Hakim akaanza kumfundisha mafunzo fulani; lakini yeye hakutosheka na somo moja tu kutwa nzima. Akajitahidi kupanga mafunzo mingine zaidi lakini matokeo yake hayakuwa ya kuridhisha, ijapokuwa alijifunza kwa Maulawii Fadhlullahi wa Farangi Mahal vilevile. Hapo ndipo akaamua kumwomba Bwana Hakim ruhusa ya kurudi tena Rampur. Alipoeleza mpango wake huu kwa Bwana Hakim, akaulizwa: "Niambie, je, ni afadhali kwa mtu kama mimi kuendelea na shughuli yangu hii ama kukubali kazi yenye kufaa nikipatiwa?" Maulawii Nuruddin akamshauri kuchagua hiari ya pili yaani kukubali kufanya kazi ya kufaa, na akatoa sababu zake pia. Hilo likamvutia Bwana Hakim, na ndipo akamwonyesha simu ya maandishi (telegram) aliyoipokea kitambo kidogo kabla kutoka kwa Nawab Kalbe Ali Khan, Mtawala wa Rampur, ambamo alimwahidi kupatiwa kazi imfaayo, na kamsisitizia kuwasili haraka Rampur na kumtibu Bwana Ali Bakhsh, hadimu mwaminifu wa Nawab, aliyekuwa mgonjwa sana. Bwana Hakim alisema: "Sasa kwa kuwa umenishauri, nitakubali maneno ya

Nawab, nasi tutakwenda Rampur sote wawili."

Baada ya kuwasili Rampur, Bwana Hakim alimsisitizia sana Maulawii Nuruddin kumwombea Bwana Ali Bukhsh apate afya. Lakini yeye akasema kwamba hana maelekeo ya kumwombea, bali mgonjwa atakufa tu. Na ndivyo ilivyotokea. Mganga mwingine, Bwana Ibrahimu, pia wa Laknau, akamlaumu Bwana Hakim utabibu wake mbele ya Mtawala – jambo ambalo likamwudhi Bwana Hakim. Maulawii Nuruddin akamfariji akimhakikishia kwamba uhai na mauti vimo mkononi mwa Mungu, na kwamba yawezekana mtu mwingine mwenye shida kama ya Bwana Ali Bakhsh apate kufa akitibiwa na Mganga Ibrahimu. Muda si muda hadimu mwingine mwaminifu wa Nawab alipatwa na ugojwa huo naye akafa akitibiwa na Mganga Ibrahimu. Hilo likamkomesha Mganga Ibrahimu kumchongea Bwana Hakim.

Masomo ya Maulawii Nuruddin chini ya usimamizi wa Bwana Hakim kwa bidii yake na busara yake kali yakasonga mbele kwa haraka sana. Mwongozi wake akamtahini mara kwa mara na sikuzote akamkuta hodari zaidi ya kawaida hata kwamba akaanza kuyaheshimu maoni yake na kuyategemea. Lakini mwanafunzi wa kutumainiwa hakutaali tu uchunguzi wa maradhi na kutibu pekee. Kiu yake ya kupata elimu ilikuwa kali sikuzote. Safari moja akamwendea Mufti Saadullah ili kusoma *Mutanabbi* (Diwani ya Kiarabu ya mshairi Mutanabbi) kwake, lakini mtaalamu huyo Mufti akamkawiza kwa udhuru kwamba hana nafasi. Basi yeye akaondoka akisema: "Haya, bwana, nitangoja hadi utakaponiomba nisome kwako!" Akirejea kwa Bwana Hakim akamwuliza: "Bwana, elimu inamfaa nini mtu?" Akajibu: "Elimu husaidia kustawisha adabu njema; lakini kwa nini wauliza?"

"Bwana, nilimwendea Mufti Saadullahi ili aniruhusu kusoma

*Mutanabbi* kwake; lakini akanikawiza kwa kutoa udhuru kwamba hana nafasi."

Bwana Hakim mara moja akampelekea Mufti barua akimtaka ampitie atakapokuwa anarejea nyumbani toka afisini kwake. Saa ilipowadia, yeye akamwambia Maulawii Nuruddin asubiri katika chumba cha pili. Bwana Mufti alipowasili, baada ya kusalimiana na kuamkiana akamwuliza: "Bwana Mufti, kama nikipenda kujifunza kwako kitu fulani, je, utakubali kunitolea nafasi?"

"Bila shaka, nipo tayari saa zote, na nina shauku ya kukutumikia."

"Na kama mtu fulani ninayemheshimu kama mwanafunzi wangu wa kiroho akikuomba, je?"

"Hapo, ningependa kumwendea mimi mwenyewe popote alipo yeye."

Kitambo kidogo baadaye Bwana Hakim akamwita Maulawii Nuruddin. Akimwona tu, Bwana Mufti akaangua kicheko, akasema: "Njoo, Bwana, sasa mimi nakuomba usome kwangu."

Safari moja kikundi kimoja cha wanafunzi walijadili swala hili kwamba je, wale waliopata daraja la juu la kiroho huelekea kuwafundisha wengine hekima zao? Maulawii Nuruddin akathibitisha kwamba ndiyo, lakini wanafunzi wengine wakasema hapana. Hatimaye ikaamuliwa swala hilo lipelekwe kwa Bwana Amir Shah, mtu aliyejulikana kuwa mwenye daraja kubwa katika mambo ya roho. Bwana huyo akasikiliza pande zote mbili na akatangaza kwamba Bwana Nuruddin ndiye aliyetoa majibu barabara. Bwana Nuruddin alipokuwa aondoke, Bwana Amir Shah akamwambia: "Hebu nikuambie jambo ambalo unapaswa kulizingatia vizuri. Unapofikiwa na mtu anayekuletea tatizo fulani, elekea kwa Mungu na kumwomba:

Mola wangu, sikumwita huyu. Wewe ndiwe Uliyemwelekeza kwangu. Kama Huyapendi anayotafuta, basi nasikitikia ile dhambi ambayo kwa sababu yake Umeniletea wakati huu ili nifedheheke. Halafu, kama mtu huyo aking'ang'ania kupata mashauri yako, Mwombe Mungu mwongozo, kisha umshauri unavyoona vizuri."

Maulawii Nuruddin akafaidika sana na nasaha hii ya Bwana Amir Shah.

Akaendelea kukaa kwa Hakim Ali Husain zaidi ya miaka miwili. Kisha akamwomba ruhusa baada ya kutuzwa naye hati rasmi. Bwana Hakim akamwuliza ananuia kuelekea wapi? Akasema, anapenda kuendelea na masomo ya Kiarabu na Hadithi za Mtume s.a.w. Bwana Hakim akapendekeza aende Mirat na kusoma kwa Hafidh Ahmad Ali; halafu aelekee Delhi na kujifunza kwa Maulawii Nadhir Husain. Akamwahidi pia kumsaidia vya kutosha mahali hapo pote pawili.

Alipowasili Mirat akapata kujua kwamba Hafidh Ahmad Ali amekwisha hamia Kalkatta. Basi akaelekea Delhi ambako alimkuta Maulawii Nadhir Husain ameshtakiwa sheriani kwa kosa la kisiasa, naye hakuweza kupatikana. Akishindwa hivyo, akanuia kwenda Bhopal; akafunga safari. Huko Gwalior akawahi kuonana na mheshimiwa mmoja aliyekuwa mwanafunzi wa walii mmoja mashuhuri Hadhrat Seyyid Ahmad wa Bareilli. Akaamua kukaa naye kwa siku chache. Alipoanza tena safari yake, Mwafghani mmoja, Mahmudu, akawa mwenzake katika safari hiyo. Wakawasili kambi la Gunnah ilhali miguu yao ikiumia sana na wakachoka kabisa wasiweze tena kutembea. Wakapitisha usiku katika msikiti mmoja usioendewa sana na watu. Mtu mmoja akafika msikitini kusali akiwa amechelewa sana. Alipoulizwa sababu ya kuchelewa sana akaeleza ya kwamba kulikuwa na wakati ambapo msikiti huo uliendewa na watu wengi

wenye kusali, lakini kwa bahati mbaya ubishi ulizuka baina yao juu ya jambo dogo sana kuhusu utaratibu wa sala. Na hitilafu ikawa kubwa kabisa hadi ikahofiwa kwamba mauaji mabaya yatatokea. Na ili kuepukana na hatari hiyo ikaamuliwa kila mmoja asali nyumbani mwake. Mtu huyo hakuafikiana na uamuzi huo, basi akaja msikitini kwa kuchelewa sana ili mtu yeyote asipate kumwona. Maulawii Nuruddin alimshauri kuwaita watu msikitini ili bidii ifanywe kumaliza mzozo. Bwana huyo akaondoka lakini punde si punde akarejea na sahani moja ya wali uliotosha kwa wasafiri hao wawili. Kesho yake, huyo Bwana akawaleta watu wengi sana msikitini ambao waliongozwa na Maulawii Nurddin aliyetoa maelezo ya kuridhisha hata kwamba wakakubali kuanza tena kuhudhuria msikitini kama kawaida kwa ajili ya sala.

# III

# KUKAA BHOPAL

Wasafiri hao waliweza kusafiri maili chache tu baada ya kuondoka Kambi la Gunnah, mara wakaonywa na mkulima mmoja kubadilisha njia yao, kwani eneo wanaloelekea limepatwa na ugonjwa wa kuambukiza wa kipindupindu. Maulawii Nuruddin alikuwa na maoni ya kutia maanani onyo hilo, lakini Bwana Mahmudu hakutia uzito habari hiyo akisema kwamba hayo ni madai tu ya mtu mmoja yasiyoweza kuaminiwa. Dakika chache tu baadaye, Bwana Mahmudu akashikwa na kipindupindu. Wakakataliwa kuingia kijiji kilichokuwa karibu, hivyo wakalazimika kushinda usiku chini ya mti mmoja. Hakim Nuruddin alimshughulikia kwa bidii kumtibu na kumtunza mwenziwe msafiri, lakini akapatwa na faradhi baada ya kuugua siku mbili au tatu. Jumbe wa kijiji akabembelezwa kufanya mpango wa kuchimba kaburi kwa malipo ya fedha nyingi. Hakim Nuruddin akamsalia sala ya jeneza na kumzika peke yake bila kusaidiwa na mwingine yeyote awaye. Mashaka hayo yote na uchovu na kubanwa vikamfanya dhaifu na hoi.

Muda si muda, Jumbe akaja mbio akifadhaika. Mwanaye wa pekee aliugua maradhi ya kipindupindu, akamwomba Hakim Nuruddin afike nyumbani mwake na kumtibu kijana, naye akafanya hivyo. Kwa sababu ya utabibu wake na msaada wake kijana akapata nguvu tena na akaanza kupona. Hapo baadaye yeye akawatibu wagonjwa wengine wengi vijijini ambao wakapata ahueni. Jumbe na mkewe wakamkirimu na kumtunza. Jumbe huyo, siyo tu akamrudishia fedha zile alizochukua kwa kuchimbisha kaburi la Bwana Mahmudu, bali pia akamfikisha Bhopal pamwe na mzigo wake.

Alipowasili Bhopal, akaweka furushi lake katika nyumba moja

ya kupokea wageni, nje ya mji; akajinadhifisha, akaelekea mjini akiwa na Rupia moja tu. Njiani akala chakula kwa mwoka mikate kwa nusu Rupia. Akiisha pata ruhusa ya mlinzi penye lango akaingia mjini, na mara akagundua kwamba amepoteza nusu Rupia yake pasipo kujua. Aliporejea hotelini akalikuta furushi lake salama lakini fedha hamna ndani. Kesho yake akachukua furushi akielekea mjini akapita karibu na duka la mwoka mikate alipokula chakula jana. Mwoka mikate akamtolea salamu na kumkaribisha kula. Akaweka furushi lake kwake na akala hadi akashiba.

Mjini humo akafikia msikiti mmoja mkubwa uliopendeza ukiwa kando ya bwawa la maji. Akaukuta ni mahali pazuri na akapitisha wakati wake mwingi humo. Baada ya siku mbili au tatu za kukaa bila chakula akajiona dhaifu sana na akafahamu hatapona kwa muda zaidi. Baada ya sala ya adhuhuri akajilaza mahali palipoinuka upande mmoja wa msikiti akiwa na jasho baridi. Munshi Jamaluddini, Waziri Mkuu wa serikali, aliyehudhuria katika sala akapata kumwona na akamtuma Imam wa msikiti aende kujua habari zake. Maulizo ya Imam yakajibiwa kwa kifupi na mgeni aliyekuwa ameishiwa nguvu. Waziri Mkuu alipopata taarifa ya Imam, mwenyewe akaja pamwe na wafuasi wake na kumwuliza maswali kadha, kisha akamwomba kuchungua mpwito wake naye akafanya na kumwambia ana ugonjwa wa tumbo kutokuweza kumeng'enya chakula. Waziri Mkuu akaomba amwandikie dawa naye akaandikisha dawa iliyo ghali sana. Kisha Waziri Mkuu akawaamuru wafuasi wake waondoke hapo na kumwomba akubali kula chakula naye. Akakataa akisema hana moyo wa kula. Hapo Munshi Jamaluddin akamkumbusha: "Mtume Mtukufu s.a.w. ameagiza kukubali mwito wa chakula." Hapo yeye akaridhika na kakubali. Baada ya kitambo kidogo akaja mjumbe mmoja na kumwambia afuatane naye hadi makazi ya Waziri Mkuu. Akamwarifu hana nguvu ya kutembea. Mjumbe akajitolea kumbeba mgongoni, na

hatimaye akampeleka mpaka makazi ya Waziri Mkuu na kumweka karibu na Waziri Mkuu katika chumba cha kulia. Yaliyotokea baadaye yafaa yaelezwe kwa maneno ya Bwana Maulawii Nuruddin mwenyewe:

> "Chakula kililetwa, nami nikaangalia nile nini. Pilau ndiyo chakula ninachopenda zaidi, basi nikachukua mmego mmoja, lakini kwa kufikiria kwamba baada ya njaa ya siku nyingi huo waweza kunisonga koo nikauweka kando. Halafu nikashika bakuli la mchuzi wa kuku, nikanywa kidogo, ukanikongesha. Nikanywa tena kidogo, kisha nikaanza kula tarabibu. Hapo ndipo mwenyeji akamwita mpishi na kumwuliza: 'Pilau hii ina kasoro gani?' Akajibu: 'Hamna, isipokuwa nyama ya kuku ilipata kupikika mno katika sehemu kidogo kwa sababu ya moto, nami nikakiweka kipande hicho chini kabisa katika pilau.' Hapo Yeye akauliza: 'Chakula kipi ni kizuri zaidi jioni hii?' Mpishi akajibu: 'Mchuzi.' Kwa kifupi, nikatumia huo mchuzi ulionipa nguvu kabisa.
>
> Baada ya chakula Bwana Munshi akaongea nami faraghani na akaniuliza habari zangu na shughuli zangu. Nikamweleza kwamba mimi natoka Panjab nami nimekuja Bhopal kutafuta elimu. Nadhani alinifikiria kuwa mtu mwenye hali nzuri ambaye amepatwa na masaibu na kwamba najisingizia tu kuwa nimekuja kutafuta elimu. Basi akaniambia kwamba nitakuwa mgeni wake, na yeye atafanya mpango wa mafunzo yangu. Akanipatia makazi na kumwagiza msimamizi wa maktaba yake ya kwamba niwe na uhuru wa kupata kitabu chochote. Aidha, akaagiza pia vitabu vyangu na furushi langu na akamfanya Maulawii Abdul Qayyum kuwa mwalimu wangu. Nikaanza kusoma kwake *Sahih Bukhari*

na *Hidayah* (Kitabu cha Fik'hi)."

Munshi Jamaluddin kila siku saa za magharibi alikuwa anatoa darasa la Kurani Tukufu. Siku moja Maulawii Nuruddin pia alihudhuria darasa lake. Aya hii ilikuwa inaelezwa: Na wanapokutana na wale walioamini, husema: "Tumeamini, na wanapokuwa peke yao wao kwa wao..." (2:77). Hapo yeye akaomba ruhusa kuuliza swali. Akaruhusiwa. Akauliza: Katika aya hii na katika aya 2:15 wanafiki wa Madina wametajwa. Hapa wametajwa kuwa 'wao kwa wao'; lakini katika 2:15 wametajwa kama mashetani wao. Haikosi kuna sababu maalumu ya tofauti hii. Bwana Munshi alikiri hajui sababu yake, na akasema, je, Maulawii Nuruddin ataieleza! Hapo yeye akasema: Mjini Madina kulipatikana wanafiki wa aina mbili: waliotokana na Mayahudi na wengine waliotokana na Washirikina (Wapagani). Katika aya tunayozungumzia (2:77) Mayahudi wametajwa. Hao kwa kuwa walikuwa watu wa Kitabu wametajwa tu kama wenzi wa ndugu zao wanafiki. Lakini katika 2:15 wapagani wametajwa nao wametumiwa maneno makali ya 'mashetani wao'. Bwana Munshi alishtushwa sana na maelezo hayo hata kwamba aliinuka kutoka katika mahali pake na kumkaribisha Maulawii Nuruddin akae hapo na kuendelea na darasa. Pia akasema kwamba toka sasa Maulawii Nuruddin atatoa darasa, na yeye atahudhuria kufaidika na ujuzi wake.

Safari moja katika kikao kimoja rasmi chini ya Bwana Munshi kuwa mwenyekiti akiwa Waziri Mkuu, Kadhi akamtaja Hadhrat Shah Isihaka kwa maneno ya kumdharau. Maulawii Nuruddin aliyekuwapo hapo akaudhika sana na papo hapo akaondoka kikaoni. Siku hiyo yeye hakwenda kula chakula cha usiku pamoja na Bwana Munshi ambaye naye hakula kwa sababu hiyo. Kesho jioni akatafiti ni wapi anapoweza Maulawii Nuruddin kusali sala ya Alasiri. Akaambiwa kwamba yaelekea sana atasali katika msikiti uliopo karibu na makazi

yake. Bwana Munshi akauendea huo msikiti na kumkuta Maulawii Nuruddin akisali na akakaa upande wake wa kuume. Alipomaliza sala yake akaelekea kulia, kama ilivyo kawaida, na akatamka: "Assalamu alaikum wa Rahmatullahi." Haraka sana Bwana Munshi akasema: "Ahaa, umefurahi kunisalimia!" Na akishika mkono wake akamnyanyua juu. Akamwongoza nje ya msikiti na kumkalisha katika gari lake la farasi na akamwagiza mwendeshaji kuongoza nje ya mji. Mji ulipomalizika na kubaki nyuma sana akadakuliza:

> "Jana ulinifanya mimi pia nishinde na njaa." Bwana Maulawii akajibu: "Hadhrat Shah Isihaka alivunjiwa heshima mbele yako, nami nampenda sana na kumheshimu."
>
> Bwana Munshi akauliza: "Je, umewahi kuonana na Hadhrat Shah Isihaka?"
>
> "La."
>
> "Nilijifunza Kurani Tukufu kwa Bwana Shah. Nilikuwa Mshia mshupavu. Huko Delhi nyumba yetu ilikuwa karibu na nyumba yake nami naipitia mara nyingi. Hatimaye nikaanza kuhudhuria darasa lake la Kurani Tukufu na matokeo yake ndiyo kama uonavyo."

Kisha Bwana Munshi akaeleza habari zake kikamilifu jinsi alivyogeuka kuwa Msunni imara ilhali hapo kabla alikuwa Mshia mshupavu. Basi, kamalizia, "Mimi namsifu sana Bwana Shah na kumheshimu. Tukio la jana lilitokea katika kikao rasmi cha kiserikali, nami niliona haitafaa kuingilia kati. Watu hao wana mawazo mafupi; usiwajali sana."

Wakarejea mjini kwa gari la farasi, wakala pamoja chakula cha usiku. Mambo yakawa shwari.

Ilivyotajwa mapema, Maulawii Nuruddin alisoma Bukhari na

Hidaya kwa Maulawii Abdul Qayyum. Alifundishwa Hadithi arobaini za Mtume s.a.w. na Mufti wa Bhopal alizopokea kutoka kwa wasimulizi waliofululiza kutoka Mtume s.a.w. hadi huyo Bwana. Bwana Mufti alifundishwa hizo na Bwana Mahmud bin Nasir Hadhrami aliyekuwa mtawa sana na mfano wa ukinaifu. Mufti Jamaluddin alieleza tukio lifuatalo kama mfano:

> “Muhammad bin Nasir Hadhramii alikuwa mtu mashuhuri aliye mcha-Mungu sana. Safari moja alipokuja kunitembelea, nikaweka mbele yake mfuko wenye Rupia elfu moja nikiwa na nia ya kumpa zawadi. Nikaona kwamba amechukizwa; haraka akausogeza mbele yangu. Akatabasamu na kusema: ‘Nilinuia kukusomea Hadithi arobaini za Mtume s.a.w, lakini ulipoweka fedha mbele yangu nikakasirika na nikadhani u mtu wa dunia. Ningeweza kuzikubali fedha, lakini tena nisingekusomea Hadithi. Sasa nakuona u mtu mwenye busara, basi ningependa kukutembelea na kukusimulia Hadithi hizo. Mimi sihitaji fedha. Mashamba yangu ya mitende hutoa tende za kutosha kutimiza mahitaji yangu. Ninamiliki pia ngamia kadha. Naenda Makkah kila mwaka kuhiji. Naweka mzigo wa tende juu ya ngamia mmoja na mtumishi mmoja anapanda huyo ngamia. Mimi napanda juu ya ngamia mwingine ambaye pia anachukua maji. Zaidi ya hayo mtu anahitaji nini? Mungu asifiwe.”

Bwana Munshi alisema ya kwamba Bwana Hadhramii alikuwa anazungumza haraka sana; maneno yalimiminika midomoni mwake pasipo shida; lakini msamiati wake wote ulitokana na Kurani Tukufu na Hadithi.

Iktisadi ya nyumbani ya Bwana Munshi ilikuwa haina matata. Safari moja alieleza ya kwamba miaka yote aliyokaa Bhopal hakutumia

kwa jumla zaidi ya Rupia tatu kwa kununua nyama. Alizoea kula mara moja tu kutwa na akawaalika watu wengi pia kula pamoja naye. Kilo moja tu ya nyama ya mkono wa mbuzi ndiyo iliyohitajika kila siku. Kila asubuhi yeye alinunuliwa mbuzi mmoja kwa Rupia tatu. Akiisha chinjwa tayari, kilo moja ya nyama ikawekwa kando kwa ajili yake, na nyama iliyobakia ikauzwa papo hapo kwa bei nafuu. Watu wakanunua mara moja waliyohitaji, na kwa njia hiyo mapato yasiyozidi Rupia tatu, yakapatikana ambayo Bwana Munshi akarudishiwa. Hakuna shaka ya kwamba yeye alitumia njia kama hiyo kuhusu mahitaji yake mengine ya nyumbani. Hata hivyo yeye alikuwa mkarimu na mkunjufu. Kwa mfano, yeye katika robo nzima ya mji akawapatia makazi vipofu ambao walitunzwa kwa gharama yake. Alipenda sana kuwastawisha. Akafanya mipango kwa hao watu kuoana wao kwa wao. Akawafurahia sana watoto wenye macho maangavu ambao akaanzisha shule kwa ajili yao.

Zama Maulawii Nuruddin alipokuwa Bhopal, yeye alishikwa na homa kali sana na kinywani mwake ute mweusi unukao ukaanza kutokea. Akashauriana na Hakim Farzand Ali, ambaye akamwambia anaumia vibaya sana kwa ugonjwa wenye virusi usioweza kupona. Akamshauri aondoke haraka sana kwenda kwao. Muda si muda mheshimiwa mmoja aliyekuwa msimamizi wa wanafunzi akamjia na kumweleza kwamba kwa sababu ya uzee udenda unamtoka kinywani mfululizo, akamwomba amwandikie dawa. Akamwagiza kutumia mraba wa zeituni, mbegu za iliki na waraka wa dhahabu. Bwana huyo baada ya muda usio mrefu akarudi na chupa ya mraba na mbegu za iliki kiasi fulani na waraka wa dhahabu ambavyo vyote hivyo akampa zawadi akisema: “Unayo shida ile ile niliyo nayo mimi, kwa hiyo nimekununulia pia ulivyoniandikia ambavyo waweza kutumia.” Bwana Maulawii Nuruddin akamshukuru kwa wema wake huo. Akatumia dawa hizo na haraka sana akapona kabisa.

Safari moja, yeye alikuwa na vizibao viwili vya kitambaa kizuri sana. Kabla hajawahi kuvaa hivyo, kimojawapo kikaibiwa. Hakuhuzunika kwa sababu ya hiyo hasara. Na akiwa na imani ya kwamba Mungu Atamjalia badala yake kilicho bora zaidi akasoma kwa moyo wa kweli aya hii: "Sisi ni wa Mungu, na kwake tutarejea." (2:157), na akatoa sadaka kizibao cha pili. Baada ya siku chache mwanawe tajiri mmoja mwanamji akaanza kuugua kwa kisonono. Yeye akamwomba rafiki yake mmoja kumleta daktari asiyejulikana zaidi. Rafiki huyo alijuana na Hakim Nuruddin, basi akamwomba kumtembelea kijana huyo. Akiishasikia habari zake, Bwana Hakim akanena, "Hiki ndicho kizibao changu kilichopotea," na akafuatana na mjumbe huyo akielekea kwa mgonjwa aliyemkuta amekaa bustanini. Mgonjwa akaeleza alama zake na akamwomba kumwandikia dawa ambayo aweze yeye mwenyewe kutengeneza. Palikuwa na migomba hapo bustanini, Bwana Hakim akamwagiza kutumia maji ya ndizi na mchanganyiko wa kalisiamu iliyoweza kupatikana mara moja. Upesi sana mgonjwa akatengeneza dawa na kuimeza. Mganga akaondoka, na alipokuja keshoye kumtembelea, mgonjwa akamwambia ya kwamba kile kiasi cha dawa alichotumia mara moja tu kimemponya, na kwamba sasa hana haja tena ya kuendelea kutibiwa. Bwana mganga akaamini kwamba tukio hilo zima ni onyesho la rehema ya Mwenyezi Mungu. Kesho yake, rafikiye mgonjwa akamletea mavazi mengi ya zari na nguo nzuri na ghali kabisa pamoja na fedha nyingi sana taslimu, ambavyo vyote hivyo mgonjwa akamletea kama shukurani. Mganga kasema tena: "Hiki ndicho kizibao changu.» Yule mjumbe (rafikiye mgonjwa) akapenda kujua siri ya kizibao hicho. Bwana Hakim akamweleza habari yote na akasema ya kwamba kwa kuwa yeye hawezi kutumia mavazi hayo ghali sana, basi yauzwe na thamani yake apatiwe. Hayo yakauzwa kwa fedha nyingi sana. Fedha hizo pamoja na zile fedha taslimu zikawa nyingi mno hata kwamba akanuia kwenda

Hijazi kufanya hija.

Wakati wake wa kuondoka Bhopal ulipowadia, akamwomba Munshi Jamaluddin ruhusa kwa upendo, kisha akifuatana na wacha Mungu na walio mashuhuri akamwendea Maulawii Abdul Qayyum kuagana naye. Akiagana naye akamwomba amwambie chochote kitakachomfaa na kumchangamsha. Akaambiwa:

> "Usipende kuwa Mungu wala Mtume Wake." Akasema kwa adabu: "Mheshimiwa, nimeshindwa kutambua muradi wako; nami nina shaka kama mmojawapo wa hawa wataalamu watukufu ameweza kuelewa."
>
> "Haya, basi, unamwonaje Mungu?"
>
> "Mheshimiwa, sifa mojawapo ya Mungu ni kwamba Yeye Anafanya Apendavyo."
>
> "Sawa. Hiyo ndiyo niliyomaanisha. Pindi mpango wako mmojawapo uvunjikapo, hapo jikumbushe wewe si Mungu. Na Mtume wa Mungu anapokea maamrisho kutoka kwa Mungu na anajua ya kwamba wale watakaomwasi watakwenda Motoni. Kwa hiyo yeye huwa anahuzunika kwa uasi wao. Lakini kama mtu yeyote akikataa fatwa yako, siyo lazima huyo apate kukasirikiwa na Mungu. Hivyo, huna sababu yoyote kumhuzunikia."

Alipokwisha ondoka Bhopal njiani akatua kidogo Burhanpur ambako rafikiye babake, Maulawii Abdullah, akampokea vizuri kwa upendo na kumkirimu. Wakati wa kuagana naye, bwana huyo akampa kikapu kimoja cha tamutamu. Alipokifungua kumbe akakuta humo hawala ya Rupia elfu moja kuchukuliwa kutoka kwa mfanya biashara mmoja wa Makkah pamoja na fedha kiasi fulani taslimu. Akatumia fedha zile taslimu lakini hakupeleka hawala ili kuchukua zile pesa.

Habari za maisha ya Maulawii Abdullah ni za kuvutia. Yeye alitokana na Sahiwal, wilaya ya Shahpur. Kwa vyovyote akapata kufika Makkah ili kuhiji. Alikuwa hana njia ya kujipatia riziki, basi akaanza kuombaomba. Siku moja akajiwa na fikira ya kwamba kama akipatwa na ugonjwa atakuwa hoi moja kwa moja. Basi haraka sana akaenda Kaaba, akashika pembe ya funiko lake, akaahidi: "E Mola, siwezi kukuona, lakini kwa kushika pembe ya funiko la Nyumba Yako nafunga ahadi kwamba tangu sasa sitakiomba kiumbe chako chochote kiwacho." Akiisha fanya ahadi yake akaliacha funiko na akarudi nyuma, akaketi. Muda si muda, akamjia mtu mmoja na akaweka mkononi mwake pesa (sarafu ndogo sana ya zamani katika India) sita. Kwa kuwa alikuwa hakumwomba yeyote, basi akazichukua hizo pesa. Akala mkate kwa pesa mbili, na kwa pesa nne zilizobakia akanunua vibiriti ambavyo akaviuza kwa pesa sita. Akanunua tena vibiriti alivyouza kwa pesa tisa. Akaendelea kurudia hivyo hata kwamba saa za jua kuchwa akapata Anna nne (pesa kumi na sita). Katika siku chache tu bunda la vibiriti vyake likawa zito sana. Hapo akaanza kuuza vifaa vya mapambo ya akinamama. Biashara yake ikaendelea kufana na alipokwisha pata fedha kiasi fulani akarejea Bombay ambako akaanza kununua nakala za Kurani Tukufu na kuziuza katika miji na vijiji vilivyo karibu na Bombay. Biashara yake hiyo ikastawi sana hata kwamba safari moja akanunua nakala za Kurani Tukufu zenye thamani ya Rupia elfu thelathini. Akazipeleka Bhera ambako zote hizo akamwuzia babake Maulawii Nuruddin kwa faida nyingi. Hatimaye Bwana huyo akawa mfanya biashara ya vitambaa, akajenga nyumba mjini Burhanpur ambako akafanya makazi. Akasema mbinu yake ilikuwa kuchukua faida ndogo na kuuza haraka bidhaa.

Mjini Bombay, Maulawii Nuruddin alionana na Maulawii Inayatullahi na kumwambia afanye mpango wa kumtafutia nakala moja ya kijitabu *'Al-fauzul Kabir'* cha Hadhrat Shah Waliyyullahi,

ambacho ana shauku sana kukisoma na kuwa nacho. Keshoye akaambiwa kijitabu kipo hapa, na bei yake ni Rupia hamsini. Haraka sana akamkabidhi noti ya Rupia hamsini na akinyakua kijitabu akainuka kuondoka. Maulawii Inayatullahi akamwuliza sababu ya kuwa na haraka hivyo, akaeleza kwamba baadhi ya wanasheria (wataalamu wa elimu ya fik'hi) wanaona ya kuwa ununuzi hautimii mpaka mwuzaji na mnunuzi waondokane naye akapenda kukamilisha ununuzi usipatwe na hatari yoyote ya kutanguka. Maulawii Inayatullahi akamwambia kurejea haraka. Aliporudi Maulawii Inayatullahi kwa kuona shauku yake kubwa ya vitabu akapendezwa naye sana na kumrudishia Rupia hamsini, ijapokuwa alihakikishiwa kwamba anazo fedha za kutosha kuweza kulipa bei.

# IV

# WASAA MZURI WA KWENDA HIJAZI

Kutoka Bombay, Maulawii Nuruddin akapanda meli kwenda Jeddah. Melini akawakuta watu watano wa sehemu za kwao walionuia kwenda kuhiji ambao walimtunza na kumpa raha kwa kila namna. Safari ya bara toka Jeddah hadi Makkah ilifanywa juu ya ngamia. Alikuwa amewahi kusikia ya kwamba dua inayoombwa wakati tu Nyumba ya Mungu inapoonekana hupokelewa daima, kwa hiyo alipoiona Kaaba kutoka mlimani akisogelea Makkah akaomba: "E Mola, wakati wote nahitaji msaada wako. Nakuomba sana, basi, kwamba wakati wowote nikikuomba, Unipokelee kwa huruma Yako." Hakuwa na hakika ya ushahidi wa imani hii ya watu wote kuhusu kupokelewa dua inayoombwa wakati Kaaba ionekanapo, lakini majaribio yake ya baadaye yalimhakikishia ya kwamba dua yake iliyoombwa wakati huo ilipokelewa.

Huko Makkah yeye alikaa kwa mtu mmoja mwema, mzee kidogo, aliyejulikana kwa jina Makhdumu na akaanza kutaali Hadithi za Mtume s.a.w. kwa wataalamu watatu wakubwa sana. Akasoma kitabu cha Hadithi *Abu Duwud*, kwa Sheikh Muhammad Khazrajii, kitabu cha *Muslim* kwa Seyyid Husain na *Muwatta* kwa Maulawii Rahmatullahi. Kati ya hao, yeye akaendelea kwa muda mrefu zaidi kwa Seyyid Husain ambaye alikuwa anazungumza kidogo na msamiati wake ulitokana na Hadithi pekee. Maulawii Rahmatullah alimwambia ya kwamba yeye anamjua Sheikh Husain tangu miaka ishirini lakini hamjui yeyote ambaye anajuana naye sana, wala hakuweza kukisia anapataje riziki yake. Maulawii Nuruddin aliona ya kwamba watu walipomjia ili kupata mwongozo, yeye akawasihi wazoee kumkumbuka Mungu kwa kumwita: *'Ya Basit'* (E Mwenye

fadhili nyingi) na kwa kumwita: *'Ya Ghanii'* (E Mkwasi) au *'Ya Hamidu'* (E Uhimidiwaye) au *'Ya Majidu'* (E Mtukufu) na kadhalika. Akanuia kumwuliza hekima iliyomo katika nasaha yake hiyo lakini hakuweza kudiriki kwa kuheshimu ukimya wake.

Maulawii Rahmatullahi alikuwa mtukufu, mjuzi sana, aliyejulikana kwa ubingwa wake wa kujadiliana, hususan kuhakikisha ubatili wa imani za siku hizi za Kikristo. Kinyume cha wataalamu wengi wa dini, yeye hakujibizana vikali na wapinzani. Hata akikabiliana na mjinga mkaidi, hakuachana na subira na aliendelea kutabasamu na kuwa makini.

Sheikh Muhammad Khazrajii alikuwa mzoevu sana wa *Sihah Sittah* (vitabu sita mashuhuri vya Hadithi za Mtume s.a.w.). Safari moja katika masomo ya *Abu Dawud* hitilafu kidogo ilizuka baina ya mwalimu na mwanafunzi wake kuhusu swala la kwamba kipindi cha *Itikafu* (kushinda msikitini katika kumi la mwisho la Ramadhani) chaanzia lini. Sheikh akaona swala hilo kuwa gumu. *Itikafu* ikianzia asubuhi ya tarehe 21, yawezekana usiku uliopita kuwa *Lailatul-Qadri*. Na haiwezekani ianzie jioni ya tarehe 20, kwa kuwa Mtume Mtukufu s.a.w. alipendelea kuanza asubuhi. Hapo Maulawii Nuruddin akasema: "Hamna mushikili wowote; *Itikafu* yaweza kuanza asubuhi ya tarehe ishirini." Sheikh akanena: "Hiyo itakuwa kinyume cha *Ijmai* (mapatano ya wataalamu wote)."

Maulawii Nuruddin: "Bwana, Ningependa kukuelekeza kwa heshima kwenye maneno ya Imam Ahmad bin Hambal kuhusu *Ijmai.* Hiyo huonyesha tu maoni ya wanasheria wengi wa madhehebu fulani maalumu."

Hilo likamwumiza sana Sheikh ambaye hakusema lolote katika nafasi yote ya masomo. Jioni Maulawii Nuruddin akaenda kusoma kwa Maulawii Rahmatullahi ambaye akamwuliza: "Ulijadiliana na

Sheikh wako asubuhi kuhusu jambo fulani?"

"Bwana, haiwezekani kufanyike mdahalo baina ya mwanafunzi na mwalimu. Mimi ni mwanafunzi tu, na Sheikh ndiye mtu mkubwa wa dini. Mimi nilijaribu tu kufafanua jambo moja dogo."

"Haikosi hilo ndilo swali la muhimu. Sheikh akaja kwangu, akasema: 'Baadhi ya wanafunzi ni wajasiri mno, nao wanaleta shida.' Kisha akanieleza kisa chote."

"Bwana, hilo lilikuwa jambo dogo kuhusu ibada ya kidini. Kwa kuanza *Itikafu* asubuhi ya tarehe 20 ya Ramadhani badala ya asubuhi ya tarehe 21, hitilafu baina ya Hadithi kuhusu habari hii yaondolewa."

"Lakini hapo ni kupinga *Ijmai* (mapatano wa wataalamu wote)."

"Bwana, ijmai gani yaweza kuwa kuhusu swala hilo dogo?"

"Haya, tuahirishe somo hadi kesho, nasi twende nyumbani mwangu." Walipotokea ugani mwa Kaaba Maulawii Nuruddin akiashiria kwenye Kaaba akauliza: "Bwana, kwa sababu gani watu wanaelekea Nyumba (Kaaba) wanaposujudu katika sala?"

"Ndivyo alivyoagiza Mtume Mtukufu s.a.w."

"Bwana, U mjuzi sana wa Maandiko ya Kiyahudi nawe wajua pia ya kwamba Jerusalemu ilikuwa *Kibla* sawa na *Ijmai* ya manabii wote wa Wana wa Israeli. Mbona mliachana na ijmai ya manabii wote kwa sababu ya Nabii mmoja? Kama nilihitilafiana juu ya jambo dogo kabisa katika kueleza hadithi moja nimedhuru nini?"

"Moyo wangu huona mashaka."

"Lakini wasemaje kumhusu yule mtu ambaye moyo wake

hauoni mashaka?"

"Vema, nilikuombea kwa Sheikh na kumtuliza. Waweza kuendelea bila kizuizi kusoma kwake."

Halafu Maulawii Nuruddin akamaliza masomo yake ya *Nasai* na *Ibni Majah* zaidi ya *Abu Dawud* kwa Sheikh Muhammad Khazrajii.

Wakati huo huo Hadhrat Shah Abdul Ghanii Mujaddidii akawasili Makkah kutoka Madina. Ujaji wake ulitangazwa sana huko Makkah na akapokelewa kwa shauku na furaha. Maulawii Nuruddin naye akaenda kumsalimu. Akakalishwa uwanjani mwa Kaaba akizungukwa na wasifu wake wengi. Maulawii Nuruddin baada ya kumsalimu akamwuliza pasipo kusema lolote: "Bwana, *Itikafu* yaanzia lini?"

Bila kusita kasema: "Asubuhi ya tarehe 20."

Maulawii Nuruddin akapendezwa sana na kuathirika kwa adhama yake na daraja lake kubwa. Kisha akathubutu kusema: "Bwana, nimepata kusikia ya kwamba hiyo itakuwa kinyume cha *Ijmai*."

Bwana Shah akajibu kwa sauti ngeni: "Ukosefu wa elimu ni taabu kubwa;" naye akataja majina ya wataalamu wengi wa fik'hi wa madhehebu ya *Hanafi, Maliki, Shafii* na *Hambali* waliokuwa na rai hiyo.

Ujuzi huo mkubwa na fikira pana ya Bwana Shah ikamtilia Maulawii Nuruddin moyoni mwake huba na upendo wake, naye wakati wa kuagana naye akamwandikia akiomba ruhusa ya kufuatana naye kwenda Madina kwa ajili ya kusoma kwake. Bwana Shah akisoma barua yake akamwambia aende Madina baada ya kuhitimu kozi ya

masomo yake katika Makkah.

Maulawii Nuruddin akaeleza hayo yote kwa Maulawii Rahmatullahi na akasema: "Huu ndio utaalamu wa kweli. Sheikh wetu alikuwa mwoga, lakini Bwana Shah akatangaza maoni yake uwanjani mwa Kaaba mbele ya maelfu ya watu, wala hakuna hata mmoja aliyedakiza."

Maulawii Rahmatullahi akasema tu: "Bwana Shah ni mtaalamu mkubwa mwenye maarifa ya dini."

Safari moja mama mzazi wa mwalimu mmojawapo wa Maulawii Nuruddin alipatwa na maradhi, na maradhi yakafuliza sana. Matabibu wengi wakajaribiwa lakini hakuna kilichofaa. Hapo mwalimu akamwambia Maulawii Nuruddin aende kuonana na tabibu anayemjua. Pasipo kudhihirisha ya kuwa Yeye mwenyewe ndiye tabibu, akatayarisha dawa iliyomponya mgonjwa katika siku mbili au tatu. Mwalimu mpaka mwisho hakumtambua tabibu alikuwa ni nani.

Alipokuwa tayari kuondoka kwenda Madina, Maulawii Nuruddin akaweka amana fedha nyingi na mizigo yake kwa mwanafunzi mwenzake aliyetoka Bhera ambaye aliishi Makkah. Akamwambia kutumia fedha katika biashara yake, na kwamba atakaporudi kutoka Madina atachukua mizigo na fedha zake akimwachia faida yoyote anayoweza kupata kwa kutumia fedha hizo. Huko Madina akahudhuria mbele ya Hadhrat Shah Abdul Ghanii aliyempatia makazi ya kuishi. Baada ya siku chache akajitolea kufanya baiati ya Bwana Shah kama mwalimu wake wa kiroho. Bwana Shah akakubali, sharti atakaa nayy kwa uchache kwa muda wa miezi sita. Yeye akamwagiza kukaza fikira yake kwenye aya hii ya Kurani Tukufu: "Tu karibu naye (mtu) kuliko halkumu yake" (50:17). Baada ya muda kidogo akaongeza aya hii: "Naye Yu pamoja nanyi popote mlipo" (57:5). Matokeo ya kuzifikiria sana aya hizo ni kwamba akajaliwa heshima ya kumwona Mtume

Mtukufu s.a.w. mara kwa mara katika ndoto zake na akatambua tija ya unyofu wake wa kiroho kwa jiha fulani. Akajinufaisha kikamilifu kwa kukaa na Bwana Shah aliyekuwa mwangalifu, mwenye maneno machache, mwenye busara kali na mwenye ujuzi mwingi. Akatoa darasa la *Bukhari*, *Tirmidhi, Mathnawi cha Maulana Rumi* na *Qushairiyyah.* Alikuwa stahifu sana.

Safari moja Maulawii Nuruddin alimwuliza anayathaminije madhehebu manne ya fik'hi ya Kisunni. Kaitikia: "Yanayojulikana sana ni madhehebu ya Abu Hanifah, yaliyo mapana zaidi ni madhehebu ya Malik, yaliyo imara zaidi ni madhehebu ya Shafii na yaliyojikusanyia yote ni madhehebu ya Ahmad bin Hambal."

Kurani Tukufu nzima ilikuwa inasomwa nyumbani mwake, na baadhi ya wanafunzi wake wakakariri mara elfu kumi na tisa kila siku: "Hakuna apasaye kuabudiwa isipokuwa Allah." Mmojawapo katika hao akamwambia Bwana Shah: Nuruddini si mwangalifu katika mazoezi ya kiroho. Aidha husoma sura *Fatiha* katika zile sala pia ambamo Imam huisoma kwa sauti ya juu. Vile vile anaidhinisha kuinua mikono mahali fulani fulani ndani ya sala. Hapo Bwana Shah akajibu vikali: "Haya, chukua, basi, kisu ukakate na kutupilia mbali yale marejeo katika *Bukhari* yanayoeleza kusoma *Fatiha* pindi Imam anapoisoma kwa sauti ya juu, na yale yanayosema kuinua mikono katika sehemu fulani za sala. Aidha, mwonyeshe ushuhuda wa kukariri 'Hakuna apasaye kuabudiwa isipokuwa Allah' mara kumi na tisa elfu kila siku, nami nina hakika ataitikia." Hilo likawanyamazisha wakinzani.

Mtu mmoja, Maulawii Nabi Bakhsh Chishti wa Jampur alikuwa anakaa katika chumba jirani ya chumba cha Maulawii Nuruddin. Shabaha ya huyo bwana kukaa Madina ilikuwa ni kwamba alikuwa na shauku kubwa ya kumwona Mtume Mtukufu s.a.w. akiwa macho.

Bwana huyo alikuwa na maoni ya kwamba hairuhusiwi kusali rakaa moja ya witri. Maulawii Nuruddin akamhakikishia kinyume chake na kumtuliza. Halafu Maulawii Nuruddin akamwona katika ndoto Mtume Mtukufu s.a.w. aliyemwambia: "Wewe unakaribishwa kula nyumbani mwangu, lakini ninamhofia Nabi Bakhsh." Ndipo Maulawii Nuruddin akaendelea kumtafuta Bwana Nabi Bakhsh kwa muda mrefu, lakini bwana huyo hakufika chumbani kwake. Mwishowe alipokutana naye, akamwuliza je umepatwa na shida yoyote? Na akamtolea fedha. Bwana huyo akakiri kwamba kweli alipatwa na dhiki kubwa lakini sasa amekwisha pata kazi na amepata hela kidogo iliyomwondolea taabu, hivyo hahitaji sasa msaada.

Mturuki mmoja, mkazi wa Madina, aliyemiliki maktaba kubwa, akawa mpenzi wa Maulawii Nuruddin na kwa kuathirika na mapenzi yake ya Kurani Tukufu akampa uhuru wa kuazima kitabu chochote alichotaka kukisoma. Ndipo akamwomba ampatie kitabu kitakachotilia mwanga swala la idadi ya aya za Kurani Tukufu zilizotanguka. Akamletea kitabu ambamo ilihakikishwa kwamba aya mia sita zilitanguliwa. Hilo likamtatanisha. Rafikiye akamletea tena *Itqan* (utungo wa Bwana Suyuti). Kutokana na hicho akafahamu kwamba aya kumi na tisa tu zilitanguliwa. Akafurahi sana na akapata mawazo ya kukisoma kitabu cha Shah Waliyyullahi alichonunua huko Bombay lakini alikuwa hajapata kukisoma. Akafurahika mno kwa kugundua ya kwamba sawa na maoni ya Shah Waliyyullahi aya tano pekee ndizo zilizotanguliwa. Hiyo ikamhakikishia kwamba swala la kutanguliwa aya kwa hakika ni jambo la fahamu na utambuzi tu. Halafu yeye mwenyewe akaweza kutatua tatizo hilo na akatulia kabisa ya kwamba hata aya moja ya Kurani Tukufu haikutanguka.

Huko Madina yeye aliudhika kugundua ukosefu wa maadili na uaminifu wa watumishi wa serikali. Rafiki yake mmoja aliazimu

kujenga hoteli moja kubwa ya wasafiri kwa ajili ya wale wanaokuja Madina kuitembelea, na akatumia fedha nyingi kwa hiyo kazi. Kadhi akamtaka amkopeshe pauni mia. Bwana huyo akamtaka Shah Abdul Ghanii shauri yake ambaye alimwambia hatarudishiwa fedha zake. Basi akakataa kumpatia fedha. Kesho yake akapokea notisi kutoka kwa idara ya Kadhi ya kwamba hoteli yake itazuia njia ya watu wote, jambo ambalo ni kinyume cha agizo la Mtume Mtukufu s.a.w. na kwa hiyo kazi ya ujenzi isimamishwe. Hilo likamharibia mpango wake. Akataka ushauri wa rafiki yake mmoja aliyemshauri aende Jeddah na kupata msaada wa balozi wa Uingereza. Balozi akamwandikia Kadhi ambaye kwa kupokea barua ya balozi akatoa notisi nyingine iliyomaanisha kwamba kwa kuwa uchunguzi umehakikisha ya kuwa njia hiyo haitumiwi na watu, hivyo hakuna swala la kizuizi, basi ujenzi wa hoteli unaruhusiwa.

Safari moja mtu fulani alimjia Bwana Shah na kulalamika kwamba yeye amehamia Madina, lakini ameyakuta mambo ya Madina yenye kusikitisha. Bwana Shah akaudhika sana na akasema: "Mimi nami nimehamia hapa. Kama kuhamia kwako kuliongozwa na hamu yako ya kuwa karibu na Mtume Mtukufu s.a.w., basi shabaha hiyo mepakitana tayari. Lakini kama umekuja hapa kutafuta kukaa na Abu Bakr, Umar, Uthman na Ali, hutawakuta hapa. Afadhali uende na kuwatafuta pengine."

Maulawii Nuruddin safari moja hakuweza kusali sala ya adhuhuri kama kawaida pamoja na jamaa. Akasumbuka mno kwamba ametenda dhambi kubwa isiyoweza kusamehewa. Katika hali hiyo ya wasiwasi mkubwa akaingia msikitini kutoka katika 'Mlango wa Rehema' ambao juu yake aya hii ilikuwa imeandikwa: "Enyi watumishi wangu mliojidhulumu wenyewe, msikate tamaa katika rehema za Mwenyezi Mungu; bila shaka Mwenyezi Mungu Husamehe

dhambi zote; hakika Yeye ni Msamehevu, Mrehemevu" (39:54). Hata uhakikisho huo wa Mungu haukumtuliza. Akaanza kusali mahali fulani palipo baina ya mimbari na chumba cha Mtume Mtukufu s.a.w. alipoinama (katika rukuu) akakumbuka kuwa Mtume Mtukufu s.a.w. aliwahi kusema ya kwamba nafasi baina ya mimbari na chumba chake ni sehemu ya bustani za Peponi. Hivyo yeye alikuwa Peponi ambako chochote akiomba atapokelewa. Basi akaomba kusamehewa kosa lake.

Katika safari yake kutoka Makkah kwenda Madina aliona kwamba mara kwa mara mabishano yalizuka baina ya mabedui waendeshaji wa ngamia na Wahindi wale waliowaajiri, jambo ambalo likasababisha ugomvi baina yao. Alipofikiri akaona mambo mawili yalisababisha hali hiyo. La kwanza, kukosekana njia ya mawasiliano. Mahaji kutoka India hawajui Kiarabu, na mabedui hawajui Kihindi.

La pili, desturi ya Waarabu ya kwamba kila mmoja hukaribishwa kwenye chakula. Basi hutokea mara nyingi ya kwamba chakula anachopewa mwendeshaji wa ngamia, wengi hushirikiana kula hicho na matokeo yake ni kwamba hakuna hata mmoja anayepata kushiba, bali wote hubaki na njaa na huwa wanakasirika haraka.

Sababu ile ya kwanza haikuhusikana na Maulawii Nuruddin (maana alijua Kiarabu). Kwa kujikinga na ile ya pili akawa na hadhari ya kwamba kabla ya kuondoka Madina kwa safari ya kurejea Makkah akachukua tende nyingi sana. Na kila usiku, usiku wa manane, akampatia mwendeshaji wa ngamia wake magao mawili ya tende zilizomshibisha vizuri na kumweka mchangamfu, naye akamhudumia kwa moyo kwa kuangalia raha yake na mahitaji yake.

Alipokurubia Makkah akakumbuka ya kwamba imesimuliwa katika Hadithi moja ya kuwa Mtume Mtukufu s.a.w. aliingia kwa kupitia Kadaa. Lakini kwa kuona kwamba ngamia na punda waliobeba

mizigo hawawezi kupitia njia hiyo, akateremka kutoka ngamia wake, kidogo baada ya Dhi Tuwaa na akaingia Makkah kwa njia ya Kadaa. Akaona kwamba wachache tu walifanya hivyo.

Huko Makkah, wakati wowote alipotaka kufanya *Umra* (hija ndogo), alivaa ihramu (shuka za mhaji) nyumbani mwake. Kuona hivyo, mwenyeji wake mheshimiwa Makhdum akamshauri aende Tan‘imu na kuvaa Ihramu pale. Ndipo akamweleza ya kwamba hakuna haja ya kwenda maili sita au saba nje ya mji ambapo katika Hadithi za Mtume s.a.w. ipo ruhusa kwa wakazi wa Makkah kuvaa Ihramu mjini Makkah. Bwana Makhdum akahangaika, akasema: “Unatenda kinyume cha mazoea ya wanamji na unapingana nao.” Kajibu ya kwamba hapingani na wanamji bali na waendeshaji punda wanaopungukiwa mapato yao. Hayo yakamfanya Makhdum atabasamu na akatulia.

Baada ya kuhiji akamwendea mwanafunzi mwenzake wa Bhera na kumtaka amrudishie mzigo wake na fedha zake. Bwana huyo akakawilisha mara moja au mara mbili, lakini alipong’ang’ania sana akakubali na kumpeleka kwenye nyumba moja kubwa ambayo mlango wake ulikuwa umetiwa kufuli, akasema: “Niliweka mzigo wako na fedha zako kwa mwenye nyumba hii. Sielewi amekwenda wapi.” Walipokuwa wakiongea akaja Mwarabu mmoja na akauliza: “Kuna nini?” Maulawii Nuruddin akasema: “Mzigo wangu uliwekwa kwa mwenye nyumba hii, na ni la ajabu ya kuwa nyumba kubwa hii imetiwa kufuli.” Mwarabu akauliza: “Kwa nini Mhindi huyu amesimama hapa?”

“Huyu ndiye aliyeweka mzigo wangu humu.”

Akisikia hayo akashikwa na hasira kali, akasema kwa kupaza sauti: “Mtu huyu ni mwongo na mlaghai. Amekwisha tumia fedha zako na mzigo wako. Mwenye nyumba hii ni mwanamji mwenye

heshima sana. Yeye pamwe na watu wa nyumbani wamekwenda Jeddah kuwaaga marafiki zao wala hawatarudi hadi wahaji wote wameondoka kwenda makwao."

Mwarabu huyo akaongea na Maulawii Nuruddin kwa adabu na mahaba, lakini akamtusi mwanafuzi mwenzake vikali sana ambaye akakaa kimya akiinamisha kichwa chake kwa fedheha. Kapaza sauti: "Ndivyo ilivyo hapa Makkah. Wahindi hawa wametupatia jina baya, tena hawajali kujirekebisha. Bwana, mtu huyu amekwisha mpa mwanamke mmoja M'bengali fedha zako zote na mzigo pia. Ndiyo mambo ya watu hawa. Hutapata katu chochote katika vitu vyako."

Baadaye, mwalimu wa Maulawii Nuruddin, ambaye wote hao wawili walikuwa wanafunzi wake, alipotaka kuondoka kwenda kuhiji akamtanabaisha kuhifadhi mwenyewe vitu vyake wala asimwamini yeyote awaye. Aliporudi baada ya kuhiji akamshukuru sana Maulawii Nuruddin kwa nasaha yake ambayo ilimlinda asidangaywe na mwanafunzi wake wa zamani.

Bwana Makhdum alikuwa mzee sana, mkewe alikuwa bado kijana na mzuri wa sura. Siku moja Maulawii Nuruddin akamwambia: Nataka kukuuliza maswali mawili. La kwanza: "Je unajitambua barabara kwamba u mzuri sana?"

"Kabisa, ni mzuri miye. Nalifahamu jambo hili sana hata kwamba ni mimi mwanamke wa pekee katika mji mzima wa Makkah nisiyetumia rangi na unga wa kujirembesha."

"Swali langu la pili: Nimeona unajibidiisha sana kumpa kila raha Bwana Makhdum. Yu mzee sana, nawe u kijana kabisa. Kujitolea kwako hivyo kwa ajili yake hunishangaza."

"Asingekuwa mzee nisingejitahidi sana. Kwa kuwa Mungu amenijalia huyo kuwa mume wangu, basi ni wajibu wangu kumtendea

vizuri kabisa na kumpatia kila raha."

Maulawii Nuruddin akawa na hakika kabisa kwamba mama huyo mwenye umri mdogo amefikia upeo wa wema na uzuri. Akamwuliza Bwana Makhdum: "Je, umeridhika kabisa na mkeo?" Kajibu: "Naweza kushuhudia uaminifu wake. Yu mwangalifu sana kunipatia raha; yeye anathibitisha kabisa kuitwa jina Sadiqa (mkweli) kuwa ni sawa hasa."

Maulawii Nuruddin akawasili Bombay pamoja na mzigo mkubwa wa vitabu. Akatuma hivyo kwa rejista katika masanduku kwenda Lahore, shehena itakayolipwa ushuru wake wakati wa kupokelewa. Akakawia kidogo mjini Delhi ambako aliambiwa kwamba mwalimu wake wa utabibu pia yuko Delhi. Akaenda kumsalimu na akaulizwa: "Umeleta nini kutoka Hijazi (Uarabuni)?" Akataja baadhi ya vitabu alivyoleta. Mwalimu wake akasema: "Niletee hivyo."

"Bwana, ningefurahi kufanya hivyo, lakini vimekwisha tumwa kupelekwa Lahore. Baada ya kufika Lahore nitakuletea."

Ningependa kutembelea Lahore. Hebu tuende pamoja leo hii hii.

Hivyo basi, akafuatana naye kwenda Lahore na kumtembeza huko. Vitabu vikaletwa; basi mwalimu mkarimu akalipa gharama ya mzigo kutoka Bombay na kumpatia mwanafuzi wake wa zamani akieleza: "Nimepanga hivyo ili niweze kushiriki katika kukupatia vitabu hivyo."

Kwa hakika Maulawii Nuruddin hakuwa na fedha wakati huo za kulipia gharama. Sasa alipokwisha kumuaga mwalimu wake, Baniani mmoja wa Bhera aliyemiliki malori kadha akajitolea kupeleka mizigo yake yote huko Bhera akisema uichukue mizigo hiyo kutoka kwangu mjini Bhera.

# V

# TABIBU MJINI BHERA

Alipofika Bhera, Maulawii Nuruddin alipokelewa na watu wengi wa mjini, Waislamu kwa Mabaniani. Haraka sana akagundua kwamba hali iliyoenea mjini ilikuwa ni ushupavu wa dini pasipo kutumia akili, fitina na kutokuaminiana. Baina ya Waislamu kulipatikana maelekeo ya kukazania mambo madogo madogo kuhusu ibada na utaratibu wa sala, na kukosekana kabisa jazba ya kukuza khulka njema na kuendeleza mbele hali ya kiroho. Mara kwa mara aliingizwa katika majadiliano yasiyofaa kuhusu mambo madogo ya dini, na maoni yake ya kiakili yenye utu mwema yakasababisha chuki ya hatari. Akaonywa kwamba asipoafikiana na maoni ya kawaida kuhusu mambo hayo maisha yake yatafanywa kuwa magumu. Mara nyingi akaingizwa kwa hila katika hali ya hatari sana ambamo akaweza kujitoa kwa kutumia akili, mbinu, ushupavu na busara aliyojaaliwa na Mungu. Bado wengi walimkimbilia kwa masomo ya dini naye akawafunza vizuri sana alivyoweza, lakini mabishano na hila ikaendelea kupata nguvu.

Hatimaye akaamua kuanza shughuli za utabibu. Akashauriana na tabibu mmoja aliyekuwa ameimarika, naye akamtahadharisha: “Mimi nawatoza ada wagonjwa, hata hivyo kwa shida napata riziki kidogo. Najua hutamwomba mgonjwa atoe ada; na watakayotoa kwa hiari yao itakuwa kidogo sana. Aidha, yaelekea utawaandikia dawa za kawaida zisizo ghali, tena hutawarejesha wagonjwa kwa madaktari wa upasuaji wala kwa wauza dawa za kizungu. Masheikh nao hawakupendi. Hivyo kwa jumla hali inayoelekea kuwa si ya kutia moyo.”

Alikuwa ameoa hivi karibuni na akaona huu ndio wakati kwamba ajichagulie kazi ya kuchuma riziki. Mazoea yake ya utabibu

ijapokuwa si mengi sana tena ya kubahatisha, lakini yeye alithibitisha ustadi wake. Uchunguzi wake wa maradhi na kuvumbua haraka bila vifaa malumu ndiyo ikathibithisha ukweli wa jambo hili. Aliimarishwa na imani madhubuti na kumtegemea Mungu kikamilifu. Babake pia akamtia moyo na kumshauri aanzishe hospitali katika jengo kubwa lenye wasaa ambalo akampatia. Utabibu wake wa kawaida uliwavutia haraka sana wagonjwa. Maisha mazima hakumwambia mgonjwa yeyote kutoa ada na akaridhika na chochote Alichompatia Mungu. Hakuwabagua wagonjwa. Kila mmoja akatibiwa kwa uangalifu. Wenye hali ndogo na maskini wakatunzwa naye sana. Ikihitajika akawasaidia kwa fedha pia.

Babake akafa na baada ya muda si mrefu kaka yake akamwambia ya kwamba jengo ambamo anaendesha hospitali yake lilinunuliwa na kurekebishwa kwa fedha zake, na kwa sababu fulani anahitaji aandikiwe hati ya kujulisha habari hii. Mara moja yeye akaandika kwa furaha na ili kumhakikishia zaidi akawaagiza wanafunzi wake kuhamisha vyombo na vifaa vyake katika chumba kilichoungana na msikiti fulani, nao wakatekeleza mara moja. Mamake alipopata habari hii akamwambia kwamba kakake hakuwa na maana ahamishe vifaa vyake na akajaribu kueleza sababu ya kuandikisha hati hiyo, lakini yeye alikwisha hama tayari.

Baada ya kukuta kiwanja kimoja cha kufaa kilichomilikiwa na Baraza la Mji wa Bhera, akamwagiza mjenzi kujenga hapo jengo lifaalo. Akamwomba Baniani mmoja aliyejuana naye amkopeshe fedha zinazohitajika kwa ujenzi. Kazi ikaanza; ndipo mkuu wa tarafa akamletea habari ya kwamba jengo lolote haliwezi kujengwa katika kiwaja kilichomilikiwa na Baraza la Mji, na tena pasipo ramani iliyotolewa kibali. Akaongeza ya kwamba kwa sababu nakuheshimu sitapinga wala wanakamati wengine wa Baraza la Mji pia hawatapinga

kwa sababu hiyo; lakini jambo hili limekwisha ripotiwa kwa Mkuu wa Wilaya, ambaye akiwa mwenyekiti wa kamati ya Baraza la Mji, hana budi ataagiza kulibomoa jengo. Mjenzi naye alikuwa na maoni yayo hayo, lakini akaambiwa kuendelea kujenga. Akipokea taarifa hiyo, Mkuu wa Wilaya akaleta habari kwamba katika muda si mrefu atatafuta nafasi ya kuhudhuria hapo na kuangalia mambo yalivyo.

Mkuu wa Wilaya akaja na akaagiza kusimamisha kazi ya ujenzi mpaka atakapotoa uamuzi wa mwisho. Maulawii Nuruddin alipofika hapo kumwona Mkuu wa Wilaya, yeye alikuwa ameondoka, lakini alipoambiwa ujaji wake akarejea na kamwuliza:

"Je, unajua mahali hapa ni milki ya serikali?"

"Ndiyo, naelewa; lakini mji mzima ni milki ya serikali."

"Vipi?"

"Serikali ikitaka kujenga makazi ya maaskari popote pale mjini, je, mtu yeyote aweza kupinga?"

Bila shaka, hapana!"

"Basi mji mzima ni milki ya serikali."

Bila kusema lolote, Mkuu wa Wilaya akauliza: «Kiasi gani cha eneo hili unahitaji kwa shabaha uliyonuia?"

"Sehemu hii ni baina ya barabara na njia ya kupitika sana. Ningehitaji hii yote."

Mkuu wa Wilaya akaelekea kwa Mkuu wa tarafa na wanakamati wa Baraza la Mji na kuwauliza: "Je, mna ubishi wowote?"

Wakasema: "Jengo linalokusudiwa kujengwa litatumika kwa manufaa ya watu wote. Hatuna upingamizi."

Mkuu wa Wilaya akaagiza kupigiliwa vijiti kuonyesha mipaka ya eneo hili, na akaondoka.

Mkuu wa Tarafa akamwambia Maulawii Nuruddin: Mkuu wa Wilaya hana mamlaka ya kutoa milki ya serikali haraka bila kufikiria.

Mkuu wa Wilaya aliyekwisha kwenda mbali kiasi fulani akarudi na akamwambia Maulawii Nuruddin: "Nimeona mfereji wa maji machafu unapita kando kando ya njia ya kupitwa na watu wote. Huo utakusumbua."

"U mtu mwenye busara. Labda utaweza kutatua tatizo hili."

"Nafikiri Baraza la Mji linapaswa kujenga ukuta kutazamana na ukuta wa jengo lako upande ule." Na akiwageukia wajumbe wa mji akawauliza: "Je, mnao ubishi wowote?"

Walikuwa hawanao. Kamwambia Maulawii Nuruddin: «Basi hili limekwisha amuliwa tayari. Waweza kuendelea na kazi ya ujenzi."

Akiisha ondoka, mjumbe mmoja wa Baraza la Mji akanung'unika: "Huu ni utaratibu wa ajabu. Siyo tu kwamba kamati ya Baraza la Mji imenyimwa kiwanja chenye thamani kilichokuwa chake, bali zaidi ya hayo imetozwa Rupia elfu moja kwa kujenga ukuta."

Maulawii Nuruddin akasema: "Haya ni mambo usiyoweza kuyafahamu."

Gharama ya ujenzi ikawa Rupia elfu moja mia mbili. Alipokuwa anafikiria atailipaje, akaja rafiki yake, Malik Fateh Khan, siku moja na kumwambia nipo safarini kwenda Rawalpindi kuhudhuria Baraza la Mkoa, na kwamba mjini Delhi kutakuwa na Baraza la mtawala wa kikoloni wa India wakati huo huo. Maulawii Nuruddin

akataka kufuatana naye; akakaribishwa kupanda farasi pamoja naye. Akapanda alivyokuwa, akiacha nyuma wagonjwa wake, tena pasipo kumwarifu mkewe. Mjini Jhelum, Malik Fateh Khan akapanda gari moshi kuelekea Rawalpindi, lakini Maulawii Nuruddin akaamua kwenda Delhi. Akahitaji kubadilisha mavazi naye akaazima koti, kilemba na teitei kwa Mkuu wa Tarafa, Malik Hakim Khan. Kisha akaelekea kituo cha gari moshi akitembea polepole ili kupanda gari kuelekea Lahore. Akapata kujua kwamba nauli ya kwenda Lahore kutoka Jhelum katika daraja la tatu ni Anna kumi na tano. Alipotia mkono mfukoni mwa koti aliloazima akakuta humo sawasawa Anna kumi na tano. Basi akafika Lahore ambako stesheni ilijaa abiria wenye kuelekea Delhi ili kuhudhuria Baraza. Yeye hakuwa na fedha. Hata kama angelikuwa nayo asingeliweza kufika dirishani kununua tiketi. Muda si muda akaja hapo padre Rev. Golak Nath, aliyejuana naye, na akamwamkia. Na alipoelewa kwamba yeye anakwenda Delhi, akaenda na kumletea tiketi. Alipomwona Maulawii Nuruddin akitia mkono mfukoni, mheshimiwa huyo akasema hatakubali abadan kupokea pesa za tiketi.

Aliwasili Delhi jioni. Tabia yake ya utafiti ikamwongoza upande wa kambi la machifu watawala. Akiisha tembea maili kadha akaona jua ni karibu kuchwa na alikuwa akifikiri kurejea mjini, mara mfuasi mmoja wa Munshi Jamaluddin wa Bhopal akaja akimkimbilia na kumwambia ya kwamba Bwana Munshi alikuona ukitembea naye akanituma kukuchukua. Lakini yeye akasema, “Nitachelewa, hivyo afadhali nionane naye asubuhi.” Lakini mtu huyo akang’ang’ania na kusema kambi la Bwana Munshi lipo karibu sana, basi wewe mwenyewe uende kumtolea udhuru. Bwana Munshi akampokea kwa ukarimu kama ilivyokuwa kawaida yake na akasema: “Mwanaye binti yangu, Muhammad Umar, anaugua. Ningependa umwone.” Akasema, naona nije asubuhi na kumwona mgonjwa. Bwana Munshi

akakazania alale kwake; na alikwisha mpigilia hema ambamo alilala vizuri. Kesho ilikuwa siku ya Ijumaa, Bwana Munshi akashonesha mavazi kwa ajili yake wakati wa usiku.

Kesho yake, baada ya sala ya Ijumaa, Bwana Munshi akajitolea kufuatana naye katika gari lake kwenda makazini kwake ili kuchukua mzigo wake na akamwuliza upande gani aelekee. Akaashiria kwenye mtaa mwembamba ambamo gari halikuweza kuingia. Bwana Munshi akawatuma wafuasi wake wawili pamoja naye ili kuchukua mzigo. Akifuatana nao, akaingia katika njia nyembamba. Akaendelea kutembea makusudi hadi akaona jengo ambamo watu walikuwa wanaingia na kutoka walivyotaka. Yeye naye akaingia humo. Akiona watu wengi wanakwenda kwenye ghorofa ya kwanza, akawaambia wenzake wale wawili kusubiri chini na mwenyewe akaenda juu ghorofani. Hakutambua asilani yuko wapi; isipokuwa akahisi anaendeshwa na nguvu ya ndani ambayo akaitii. Juu ghorofani, baina ya watu wengi akamtambua Maulawii Ubaidullah, mwandishi wa Tuhfatul Hind, ambaye akaonekana amefurahi kumwona na akasema: «Ujaji wako ni bahati njema. Ninao hapa vijana kadha waliosilimu hivi karibuni, napenda sana kuwatafutia makazi yafaayo kwa ajili yao. Tafadhali wachukue na kuwaangalia.” Akadhihirisha furaha yake kufanya hivyo. Mizigo yao ikachukuliwa na wafuasi wa Bwana Munshi, na wote hao wakafuatana na Bwana Munshi hadi kambi lake.

Baada ya kumchunguza Muhammad Umar, Hakim (tabibu) Nuruddin akagundua kwamba kijana ana tezi ambayo itachukua muda mrefu kutibiwa. Bwana Munshi akamsisitizia afuatane naye mpaka Bhopal, lakini yeye akasema kwamba alipata kuondoka nyumbani ghafla, kwa hiyo hawezi kukawia zaidi. Bwana Munshi akampa Rupia mia tano ili kuzituma nyumbani na akasisitiza aende naye Bhopal. Akamtumia mdai yule Baniani fedha na akamwandikia mkewe asiwe

na wasiwasi kumhusu yeye. Baada ya siku chache Bwana Munshi akampa tena Rupia mia saba ambazo nazo akamtumia mdai wake, na akiisha tulia akaenda na Bwana Munshi huko Bhopal kwa furaha.

Huko Bhopal nako akaikabili husuda na fitina, na katika wakati wa mashaka na hatari akasaidiwa sana na Pir Ali Ahmad Mujaddidi, ambaye alimtendea vizuri sana hata mara ya kwanza alipokaa Bhopal. Hatimaye Muhammad Umar akapona na ndipo tabibu wake akarejea kwao Bhera.

Kazi yake ya utabibu ikaanza kufana, umahiri na ubingwa wake ukatambuliwa. Hilo nalo likachochea husuda ya kikazi. Mgonjwa wake mmoja aliyekuwa tajiri sana alipatwa na homa ya matumbo. Akamtibu kwa uangalifu sana. Akiangalia mwendo wa homa siku ya saba akakisia ya kwamba homa ipo karibu kufikia upeo wake na kisha itapata kupona. Jioni hiyo dalili zake zikaonekana na tabibu akapata tumaini. Ahali zake mgonjwa wakiwa na mahangaiko wakamleta tabibu mwingine mahiri kutoka Pind Dadan Khan ambaye aliwasili usiku sana. Akigundua hali ilivyo (ya homa kupona haraka) akatangaza mgonjwa hana shida sana, maana anayo tiba sawasawa kwa ajili yake. Akampa dawa ya unga-unga pamoja na dawa ya kawaida ya kunywa, akimtazama Hakim Nuruddin kwa dharau. Keshoye mgongjwa akapata ahueni. Tabibu mgeni akapata sifa ya hali ya juu sana, bali Nuruddin akafedheheshwa machoni mwa watu wa nyumbani ambao kwa furaha wakampatia mganga mpya ada kubwa sana aliyodai.

Malik Fateh Khan, mwenye umri wa miaka themanini aliyekuwa rafikiye Hakim Nuruddin na aliyempenda sana na kumfanyia hisani nyingi, alikuwa hana kizazi. Akamsihi kuoa; akakataa kwani amekwisha zidi umri wa kuoa. Nuruddin akamtia moyo, bali akamtengenezea dawa iliyo mchanganyiko wa zarniki,

zebaki na afyuni ambayo ikaleta matokeo yaliyotakikana. Akaoa alivyoshauriwa na rafikiye. Katika muda wa mwaka mmoja mke na mume wakabarikiwa mtoto wa kike na mwaka mmoja baadaye wakajaliwa mwana. Nuruddin alitazamia kupata zawadi kubwa, lakini matumaini yake hayakutimia, ingawaje bwana huyo akamtolea shukurani tele na urafiki wao ukaimarika kuliko hapo zamani.

Matukio hayo yakaimarisha imani yake kwamba Mungu pekee ndiye Mpaji na kwamba matamanio ya mtu yasimtegetemee binadamu. Akawa na hakika ya kwamba toka sasa Mungu ndiye Atakayempatia riziki; akafunga nia ya kuwa hatamshauri mgonjwa au kumpatia dawa ili kupata fedha badala yake. Hilo likamfungulia milango ya ufanisi.

Siku hizo alikuwa na shauku sana ya kusoma kitabu cha Ibn Khaldun juu ya Historia. Mwuza vitabu mmoja akawa tayari kumwuzia hicho kwa Rupia sabini. Akasema hawezi kutoa bei yote mara moja bali angelipa kidogo kidogo; mwuza vitabu hakukubali. Jioni hiyo alipoingia katika kliniki yake akakikuta kitabu hicho juu ya dawati lake. Udadisi wake kujua kitabu kimekujaje mezani pake haukufana. Siku moja, mgonjwa mmoja akamwambia kwamba yeye alimwona Singasinga mmoja akikiweka juu ya dawati lake. Akasema hajui jina lake, lakini anaweza kumtambua. Baada ya siku kadha, akamleta Singasinga huyo mbele yake ambaye akaeleza ya kwamba: "Baada ya kujua yaliyotendeka baina yako na mwuza vitabu, haraka sana nikanunua kile kitabu na kukiweka juu ya dawati lako." Akaongeza: "Nami nimekwisha lipwa tayari fedha hizo na tajiri wangu ambaye alikuwa ameniagiza tangu zamani kwamba sikuzote chochote akihitaji Maulawii Nuruddin umpatie nami nitalipa." Sasa Maulawii Nuruddin aliweza kulipa Rupia sabini, basi akamtumia fedha hizo mhisani wake. Lakini Bwana huyo akachukizwa na kumlalamikia kakake Maulawii Nuruddin ambaye akakubali kupokea hizo fedha na kumlaumu yeye.

Siku karibu hizo hizo akaitwa kutibu kiharusi kisicho cha kawaida ambacho hakumbuki mfano wake. Akatumia kanuni za kawaida na kufanyiza papo hapo matengenezo na mgonjwa akaanza kupata ahueni na hatimaye akapona kabisa. Tiba hii ya ajabu ikazungumzwa sana na watu na ikafanikisha sana utabibu wake.

Aliwahi kupata habari ya mjane mmoja ambaye kutokana na hali yake alifikiri itafaa amwoe. Akamwendea na nia ya kumposa. Huyo naye akaonyesha radhi yake lakini akachelea kwamba mlezi wake hatapenda wala hatatoa kibali chake kwa sababu wajane kuolewa huchukizwa kwa kawaida. Hata hivyo yule mama akashauri ndoa itangazwe rasmi asaa yaweza kumhimiza mlezi kutoa kibali chake. Maulawii Nuruddin akaona ya kwamba kupinga mjane kuolewa kwaonyesha mwenendo ulio kinyume cha Islam, hivyo yafaa kupuuziliwa mbali. Basi ndoa ikafungwa rasmi, lakini mke kuenda kwa mumewe ikaahirishwa mpaka mlezi wake aonyeshe badiliko la kufaa katika fikara yake.

Katika hali kama hiyo, Maulawii Nuruddin akamwona Mtume Mtukufu s.a.w. katika ndoto kwamba amenyoa ndevu zake na rangi yake imefifia. Akaagua kwamba kufunga ndoa yake hiyo rasmi ndiyo kinyume cha suna ya Mtume Mtukufu s.a.w. lakini ili kuihakikisha akawaandikia Mian Nazir Husain wa Delhi na Maulawii Muhammad Husain wa Batala habari hiyo yote na kutaka shauri lao. Akapata majibu kutoka kwa mmoja wao kwamba katika hali kama hiyo mjane anaweza asimjali mlezi wake na kuolewa pasipo kibali chake. Akaongeza kwamba kwa vyovyote Hadithi isemayo 'Mwanamke hawezi kuolewa pasipo kibali cha msimamizi' ina ushuhuda wenye shaka. Majibu hayo yaliafikiana na matakwa yake, basi akafanya matayarisho kumleta bi arusi nyumbaini kwake. Akaondoka na mpango wake, lakini langoni pa nyumba yake akakabiliana na mtu aliyekuwa ameshika

kitabu cha Hadithi mkononi mwake. Yeye bwana huyo akamwomba kufafanua muradi wa Hadithi isemayo: Kile kinachokutatiza moyoni ni dhambi ingawaje wanasheria wakitangaze kinajuzu. Lo, akashikwa na bumbuazi; akamkawisha mwulizaji. Akawa na hakika kwamba Mungu amechagua njia hii ili kumtanabahisha asithamini maoni ya wanasheria. Akafunga mlango, akarudi chumbani mwake kutafakari mambo yalivyo, akififikiri kwamba Hadithi hiyo ilikuwa na ushuhuda wenye shaka wala haikuthibitishwa na wanasheria. Akajiona ana usingizi na akapata kulala. Akamwona tena Mtume Mtukufu s.a.w. aliyeonekana mwenye umri wa miaka ishirini na mitano, ndevu zake zilikuwa fupi upande wa kushoto, na nyingi na kamilifu upande wa kuume. Akafikiri moyoni: Angeonekana mzuri sana namna gani kama pande zote mbili za ndevu zake zingekuwa sawa. Akahisi kwamba ndevu za Mtume Mtukufu s.a.w. zilionyesha picha ya shaka yake kuhusu ushuhuda wa Hadithi hiyo, basi pale pale akasema kwa uthabiti moyoni kwamba hata kama wote wakiwa na shaka katika ushuhuda wa hadithi hiyo, lakini yeye ataikubali kuwa ni kweli kabisa. Papo hapo ndevu za Mtume Mtukufu s.a.w. zikawa sawasawa pande zote mbili, na akatabasamu na kumwuliza: “Je, utapenda kuiona Kashmir?” Akasema: “Ndiyo, Ewe Mjumbe wa Mungu.” Na wote wawili wakafunga safari ya kwenda Kashmir kwa njia ya Banihal. Hiyo ilidokeza kwamba yeye ataondoka Bhera kwenda Kashmir.

Ikawa hivi kwamba jirani yake mmoja mjini Bhera, Lala Mathra Das, aliyekuwa afisa wa polisi katika serikali ya Jammu na Kashmir akaanza kuugua kifua kikuu. Yeye akamjia ili kutibiwa. Akapona haraka. Wakati huo huo Diwan Kirpa Ram, Waziri Mkuu katika serikali ya Kashmir, akipitia Pind Dadan Khan, akapata habari ya umashuhuri wa Hakim Nuruddin na akamwambia Maharaja (Mtawala) wa Kashmir habari zake, ndipo akapewa kazi ya kuwa makamu wa Mganga kwa Maharaja.

# VI

# MGANGA WA MAHARAJA

Mganga Mkuu wa Maharaja alikuwa Hakim Fidaa Muhammad Khan ambaye baada ya muda si mrefu alistaafu na Hakim Nuruddin akafanywa Mganga Mkuu badala yake. Akiwa na madaraka haya akawa pia msimamizi wa hospitali zote za nchini. Alikuwa mwenye umri wa miaka thelathini na sita wakati huo, na aliendelea na kazi hii kwa miaka kumi na mitano.

Aliyoyakabili mwanzoni katika Kashmir hayakuwa ya kutia moyo sana. Fitina ilienea kote na akafikiri kwamba lazima ajihadhari. Maofisa wakubwa wawili hata hawakujali kuficha ukinzani wao.

Alipanga ghorofa ndogo ya nyumba ifaayo kwa kukaa iliyomilikiwa na serikali. Alionywa ya kuwa ofisa wa mali ya serikali aliye mzee si mtu wa kutegemewa, hivyo apate hati iliyosajiliwa ya kodi kutoka kwake. Kwa kufuata ushauri huo akapata hati ya kodi iliyosajiliwa kwa mwaka mmoja. Katika muda wa siku chache tu ofisa huyo wa mali akamwita na kumwambia aondoke ghorofani, kwani mtu mwingine yuko tayari kutoa kodi maradufu. Alimkumbusha hati iliyosajiliwa ya kodi, lakini akaipuuzilia mbali kama kitu kisichofaa na akakazania aondoke ghorofani. Basi mwenye hati ya kodi isiyofaa akalazimika kukubali kutoa kodi mara mbili kuliko iliyoandikwa kwenye hati. Lakini mambo hayakuishia hapo. Haraka sana ofisa wa Mali akarudi na kung'ang'ania aondoke ghorofani akidai kwamba mtu mwingine wa tatu amekubali kutoa kodi yake mara nne kuliko iliyoelezwa katika hati ya mapatano. Mpangaji kwa kusumbuliwa hivyo akakubali kutozwa kwa lazima ingawaje alilalamikia madai ya kutoa kodi mara nne kuliko iliyoelezwa katika hati ya mapatano ya kodi. Lakini hilo likazidisha tu tamaa ya ofisa wa mali; akarejea

baada ya siku moja au mbili na kueleza kwamba ameahidiwa kupewa kodi yake mara kumi na mbili. Mpangaji akachukizwa sana na akafunga nia kuondoka pale ambako uaminifu na mwenendo mwema hauna thamani. Akamwambia mfanyakazi wake kufunga virago kwa kuhama na kupeleka vitu vyote chini nje ya ghorofa.

Vitu vyake vilipokwisha rundikwa mtaani, mwananchi mmoja mwenye heshima Sheikh Fateh Muhammad akawahi kupitia hapo na kumwuliza yule mfanyakazi kwamba vitu hivi ni vya nani. Wakati huo mwenye mali pia akaja chini na akamweleza kwamba anahama mji huu.

"Lakini umekaa hapa siku chache tu, kwa nini waondoka haraka hivyo."

"Kwa sababu sipendi kukaa mahali ambapo uaminifu hauna thamani yoyote."

Sheikh Fateh Muhammad aliposikia kilichokuwa kimetendeka akasema: "Ofisa wa mali anajulikana kwa ulaghai wake. Nakuomba uje kukaa kwangu."

"Nakushukuru sana, lakini sina moyo wa kuishi hapa."

"Ee, hapana, hapana; sitakubali kukataa kwako."

Akawaagiza watumishi wake kuchukua vitu vya Bwana Mganga na kuvipeleka nyumbani kwake. Hapo aliyekirimiwa akajaribu tena kumzuia akisema kwamba ukarimu wako utakutia katika shida, kwani maofisa wakubwa wawili wa serikali wana uhasama mkali nami, hivyo waweza kupata uadui wao kwa sababu ya kunikirimu. Lakini udhuru huu ukaondolewa mbali, na mganga wa Maharja akaanza kukaa kwa Sheikh Fateh Muhammad. Akakaa kwake kwa miaka kumi. Katika muda huo wote alikaa kwa raha na utulivu. Si mwenyeji wake tu

bali kila mmoja wa familia yake akajaribu kumtangulia mwenzake kutafuta njia ya kumpatia raha na kujua kila alichotaka. Yeye, wala wageni wake wala wanafunzi waliomjia hawakupungukiwa chochote wakati wowote. Ukunjufu huo wa moyo kwa kweli hupatikana kwa nadra. Mwenyeji alistahili kweli kuwa na mgeni wake huyo. Kama mjini humo kulikuwa na watu haini kama ofisa wa mali, basi na walikuwapo pia Sheikh Fateh Muhammad na watu wa familia yake.

Wagonjwa kadha walipona kwa kutibiwa naye. Jambo hili likamnyakulia umashuhuri wa hali ya juu sana akiwa mganga. Binti mmoja wa Lall Din, tajiri mmoja aliyekuwa mwananchi mheshimiwa wa Jammu, akaugua tumbo la kuhara damu. Ijapokuwa alitibiwa kwa bidii na madaktari aliowaleta babake, hali yake ikazidi kuwa mbaya. Baba hakupenda kumwita Hakim Nuruddin kwa sababu alihitilafiana naye kuhusu baadhi ya masaala za kidini. Lakini maradhi ya bintiye yalipomtia wasiwasi akamwomba aje kumtibu. Akatumia elimu yake ya utabibu wa kizungu na kampatia mgonjwa dawa. Mgonjwa akapata nafuu haraka sana na akapona kabisa katika siku mbili au tatu. Baba mwenye shukrani akampa mganga zawadi ya vazi la heshima na farasi wa aina ya Yarkandi pamoja na lijamu na kigwe cha kuongozea farasi.

Mkuu mmoja wa idara ya ushuru akamwita usiku wa manane. Alipatwa na maumivu makali sana ya msokoto wa tumbo. Mganga akampatia mchanganyiko wa dawa naye akapona haraka.

Kipindupindu kikalipuka nchini. Maharaja akahamia kwa muda Bahu Fort kubadilisha hewa. Hakim Nuruddin alitakiwa kufuatana anaye. Jamaa mmoja wa karibu wa Maharaja, Raja Moti Singh, ambaye pia alifuatana naye, akaanza kuugua tumbo la kuhara sana. Akatibiwa na Mganga wa mfalme na akapona na akawa rafiki yake. Akampatia zawadi ya fedha nyingi sana na akaendelea kumpa

hiyo zawadi kwa miaka mingi. Uhusiano wa Maharaja na Raja Moti Singh haukuwa mzuri. Arusi ya mwana mmoja wa Maharaja ilikuwa karibu na Raja Moti Singh alishauriana na Hakim Nuruddin ahudhurie sherehe hiyo ama hapana. Akamshauri ahudhurie tu, kwani hiyo yaweza kurudisha uhusiano mwema baina yake na Maharaja. Sherehe hiyo ya arusi ilitazamiwa kuwa ya fahari kubwa. Raja Moti Singh akamwarifu Maharaja ya kwamba atahudhuria sherehe ya arusi, na hiyo ikamfurahisha sana Maharaja na suluhi ikapatikana baina yao.

Safari ya arusi, kwenda na kurudi, ilikuwa safari ya kifalme iliyotazamiwa kuchukua mwezi mzima. Hakim Nuruddin alitakiwa kusafiri juu ya ndovu. Kiti cha kukalia juu ya ndovu kilitosha sana kwa watu wawili. Lakini springi moja ambayo haikufungwa vizuri ikamchubua, na akasafiri mpaka kituo cha kwanza kwa taabu. Katika safari ya kituo cha pili akaumia vibaya sana hata kwamba akaona hataweza kuendelea kusafiri kesho. Ilikuwa ni usiku sana, akamwita daktari mstadi wa kupasua aliyekuwa katika msafara, maana alifikiri amepata jipu. Akamwambia alipasue jipu na kusafisha vizuri. Daktari akasita, kwani alikwisha funga vyombo vyake kwa vile ilikuwa usiku; akasema ataweza kupasua asubuhi. Lakini kwa sababu ya mgonjwa kung’ang’aniaakalipasuajipuhovyohovyokwakisukidogochakawaida na kuondoa mbali usaha. Asubuhi jeraha ikaonekana imeungunika na kuanza kupona. Mgonjwa akaona ataweza kumpanda farasi kama ajiangalie asitie uzito zaidi kwenye jeraha. Lakini alipokwenda tu maili chache akasikia maumivu makali yasiyoweza kuvumilika. Akateremka na akaanza kumngojea yeyote atakayeweza kumsaidia. Muda si muda akawasili hapo mwana wa Mahraja aliyetakiwa kurithi ufalme, akamwamkia na kumwuliza kwa nini anakawia. Akamweleza kwamba hajisikii vizuri wala hawezi kumpanda farasi. Yule Mwana-Maharaja akampa pole na akamshauri kujaribu kusafiri hadi kituo kijacho kilicho maili mbili au tatu ambako mpango wote wa kumtibu

utafanywa, na akaendesha farasi na akaondoka. Wana wengine wawili wa Maharaja nao wakatenda vivyo hivyo, mmoja wao akiwa rafiki yake mkubwa sana. Akaja Raja Moti Singh pia aliyeeleza tu huruma yake kwa maneno ya kupendeza. Mwishowe akapita msimamizi wa kambi naye akasema yayo hayo kama ya waliopita kabla yake. Hakim Nurudddin akaona kwamba ameishiwa njia zote za kupata msaada wa mwanadamu na kwamba alikosea kuwategemea watu. Mungu tu ndiye Awezaye kuleta msaada.

Hakukawia sana hata Dewan Lachman Das aliyekuwa zamani ofisa katika jeshi akaja akipanda farasi. Alipomwona tu akateremka haraka na kuuliza: "Shida gani?" Akajibu: "Ninalo jipu linalonizuia nisiweze kupanda farasi. Lakini waweza kuendelea na safari yako."

"Nawezaje kukuacha katika shida?"

Akaketi naye na wakaongea kwa kitambo. Kisha ikawasili machela yake na akawapa watu wake maagizo na akaondoka. Wabebaji machela wakamletea machela Hakim Nuruddin na kumwomba aingie humo wakisema: Hii itakuwa chini ya amri yako mpaka urejee Jammu. Akaikuta machela imeandaliwa vizuri. Akalala humo kwa raha. Na akimshukuru Mwenyezi Mungu akaanza kusoma Kurani Tukufu. Jeraha lake likapona haraka na akataka aache kutumia machela. Lakini wale wabebaji wakasisitiza kwamba waliagizwa kuendelea naye mpaka wote warejee Jammu.

Katika safari ya mwezi mzima yeye alikumbuka kwa ghaibu nusu nzima ya Kurani Tukufu, naye akaendelea baadaye pia na kazi hii kwa bidii hadi akahifadhi Kurani Tukufu nzima. Basi Maulawii, Hakim, Alhaj Nuruddini akawa Hafidh pia.

Aliporejea Jammu baada ya safari ya kwenda kushiriki sherehe ya arusi akawashukuru wabebaji machela kwa kumwangalia vizuri

na akataka kuwapa bakshishi ya kutosha, lakini wakakataa kupokea wakieleza ya kwamba Diwan Singh alikwisha tupatia fedha za kutosha kwa matumizi yote pamoja na zawadi na akatukataza tusipokee chochote kutoka kwako. Akajaribu kuwashawishi akiwahakikishia kwamba Bwana Diwan hatapata habari; lakini wakatoa fedha na kuweka mbele yake na kusema: Katika fedha alizotupatia Bwana Diwan Singh hizi hazijatumika. Twakuomba kuzipokea, kwani hatuwezi kuthubutu kumrudishia hizi. Akaathirika sana na moyo wao wa kutekeleza wajibu wao na uaminifu wao kwa Bwana wao na unyofu wao. Baadaye pia akafadhiliwa sana na Diwan Lachman Das.

Baada ya muda fulani Diwan Lachman Das akapewa madaraka ya kuwa Waziri Mkuu wa Serikali. Yeye alipenda sana lugha ya Kipashto na wafanyakazi wake wote walikuwa Ma-patani waliozungumza lugha ya Kipashto. Akaagiza kwamba mtu yeyote asije nyumbani mwangu kuonana nami. Kama mtu alikuja akafukuzwa na Mapatani hao pasipo heshima. Jioni moja Sheikh Fateh Muhammad akasema kwamba anataka kuonana na Waziri Mkuu kwa kazi fulani. Mgeni wake akamsisitizia aende haraka kuonana na Waziri Mkuu. Lakini yeye akasema hawezi kuthubutu kwa sababu ya wale Mapatani walindao nyumba yake. Hapo akasema Maulawii Nuruddin ya kwamba sasa hivi yeye atamwandikia Waziri Mkuu. Mwenyeji wake akajaribu kumzuia, lakini yeye akachukua kalamu na karatasi na akaandika kama yafuatayo:

> “Nimepata habari ya kwamba umeweka ulinzi mkali wa Mapatani nyumbani kwako ili kufukuza wajao kuonana nawe nyumbani. Raia wamezoea kuonana na wakuu wa nchi nyumbani kwao. Tafadhali teua chumba kimoja kikubwa kilichotandazwa zulia la Ki-Irani liwafaalo wageni. Waweza

> kuonana nao sawa na nafasi yako na kukataa kuonana na wale usiowataka. Lakini hailingani na heshima yako ya kwamba wajao kukuona wafukuzwe kwa kufedheheshwa na walinzi wako Mapatani."

Barua ikatumwa mara moja. Baada ya kitambo kidogo Katibu Shakhsiya wa Bwana Diwan akaja na taa ya mkono na kumwambia Hakim Nuruddin ya kwamba yeye ametumwa na Bwana Diwan ili kumchukua. Sheikh Fateh Muhammad akihisi hatari kutokana na mwito huo wa haraka usioweza kukatalika akamshauri asiende saa hizo za usiku sana; lakini yeye akaenda tu. Akakuta hamna walinzi huko nje. Bwana Diwan akampokea vizuri sana na akasema: "Pengine umekwisha ona kwamba hakuna walinzi nje. Nimewaondoa. Chumba fulani na fulani kimetandaziwa zulia la Ki-Irani na kimetengwa mahususi kwa wageni."

Mgeni wake akamshukuru sana kwa sababu ya kutekeleza haraka hivyo aliyomshauri. Mwenyeji akasema: "Nchi inahitaji watu wanyofu kama wewe. Nakuheshimu sana mno. Tangu sasa hakuna atakayefukuzwa. Kwako wewe hamna kizuizi chochote. Una uhuru wa kufika wakati wowote upendapo.»

Shughuli zake hazikuhusikana na utabibu pekee. Yeye alikuwa mtumishi mwaminifu wa Islam na akatumia kila nafasi ili kuondolea mbali makosa yaliyoenea baina ya mawaziri na wakuu wa serikali kuhusu Islam. Safari moja Gavana wa Jammu, Pandit Radha Krishna, alimwambia ya kwamba upinzani kadha wa kadha aliotoa Pandit Lekh Ram dhidi ya Islam ni madhubuti sana usioweza kukanushika. Akamwambia Gavana kueleza upinzani mmoja aliofikiria ndio madhubuti kabisa kuliko upinzani wake wote. Gavana akataja Maktaba maarufu ya Alexandria (Iskandaria) iliyochomwa moto kwa amri ya Hadhrat Umar r.a., Khalifa wa Pili wa Mtume Mtukufu

s.a.w. Hakim Nuruddin akamwuliza kwamba ataje jina la kitabu kinachotegemewa zaidi cha historia ya siku za mwanzo wa Islam. Gavana akataja kitabu cha Gibbon kiitwacho *'Decline and Fall of the Roman Empire.'* Kitabu hicho kiliagizwa, na Gavana akaonyeshwa ile sehemu alimoeleza mwandishi kuchomwa kwa Maktaba ya Iskandaria ambayo ilihakikisha ya kwamba Hadhrat Umar r.a. hakuhusikana na habari hii hata kidogo. Gavana akapatwa na soni na akasema, "Kwa kuwa tumekulia katika mazingira yenye uhasama dhidi ya Islam hivyo tunaamini haraka kila kinachoelezwa dhidi ya Islam."

Alikuwa na fursa ya kuwatolea mafunzo ya Kurani Tukufu watumishi wa Maharaja ambao wakayasifu sana. Raja Amar Singh, nduguye Maharaja, akajifunza Kurani Tukufu kwake na alikuwa anamheshimu mno. Maharaja mwenyewe akajifunza kwake tafsiri ya nusu ya Kurani Tukufu.

Akapata sifa nzuri sana katika utibabu. Baadhi ya maponyo yake yalikuwa kweli ya kushangaza, lakini hakujisifu kwa sababu hiyo. Alitambua saa zote kwamba ufaulu wowote hauwezi kupatikana isipokuwa kwa fadhili za Mwenyezi Mungu, na kwamba kiumbe wa Mungu awe mwangalifu isije akachochea ghera ya Mungu kwa sababu ya wazo au neno au tendo fulani na akapata kughadhibikiwa na Mungu.

Katika utabibu wake hakujilazimisha kutumia utaratibu wa dawa za Kiyunani (Dawa za miti-shamba) tu. Akajipatia vitabu vingi vya dawa za kizungu kwa lugha ya Kiarabu kutoka Misri na kuvitaali kwa uangalifu. Akajifunza pia utabibu ya Kihindi kutoka kwa mganga mmoja wa Kihindi, Pandit Harnam Das, na kusoma kwake vitabu *Amrit Sagar* na *Sasrat*. Akamstahi sana mwalimu wake mheshimiwa na kumtumikia kwa njia mbalimbali na kumtii ijapokuwa alikuwa mfanyakazi mdogo mahakamani. Mtu fulani akamwambia Maharaja

kwamba Nuruddin hawezi kuhesabiwa mganga, kwani bado anajifunza kutoka kwa mtu mdogo Pandit Harnam Das. Siku moja Maharaja akamwuliza: “Mbona unamheshimu sana Pandit Harnam Das?” Akajibu; “Namheshimu akiwa mwalimu wangu.” Maharaja akaathirika sana, na yeye akazidi kuheshimika machoni mwake.

Alikuwa anampenda sana Firuzuddin, mwanaye Mian Lal Din, kwa sababu ya sifa zake bora, na kijana pia akajitolea kwake. Yeye alisumbuliwa na ndui. Rafikiye mheshimiwa akatumia njia zote za kumtibu lakini bure, na mgonjwa akafa kwa maradhi mbele ya mganga maarufu ambaye akahuzunika mno kwa msiba huu na akatambua mara nyingine tena kwamba kila kitu chaitegemea rehema na huruma ya Mungu.

Mpwawe mmoja alifariki huko Bhera kwa ugonjwa wa kuhara damu. Muda kidogo baadaye yeye akawasili Bhera kutoka Jammu. Dadake akiona kwamba mtu mwingine aliyekuwa anaugua kwa kuhara damu amepona kwa utibabu wake akamwambia, “Kama ungelikuwa hapa mwanangu alipougua, asingelikufa.” Akashtuka na kumsihi, “Utapata mwana mwingine atakayeugua kwa kuhara damu, naye atakufa ingawaje nitakuwa nimemtibu.” Halafu akapata mwana mmoja mzuri sana ambaye akapatwa na ugonjwa wa kuhara damu. Nduguye alikuwa hapo Bhera na akajishughulisha kumtibu mpwawe mdogo. Dadake akakumbuka ile nasaha yake na akamng’ang’ania amwombee mtoto apate kupona. Akafanya hivyo, na akamwambia kwamba mtoto atakufa; lakini yeye atabarikiwa na mwana mwingine tena ambaye atakua na kuendelea vizuri. Na ndivyo ilivyotendeka.

Maharaja alikuwa anamsifu sana Hakim Nuruddin vipawa vyake na khulka zake bora na sifa zake za kiroho, na mara nyingi akadhihirisha kwamba anamheshimu. Jioni moja alipokea ujumbe kwamba haraka sana amwendee Maharaja. Alipokuwa karibu aondoke,

akaja mke wa topasi kwake katika mahangaiko sana na akamwomba aende kumtazama mumewe ambaye yuko taabani. Yeye akamwambia mjumbe wa Maharaja aende na kumhakikishia Maharaja ya kwamba atafika kwake baada ya kitambo kidogo. Mjumbe huyo hakupendezwa, na akasema kwa mshangao: "Topasi mmoja anatangulizwa juu ya Maharaja."

Mganga hakuwa na shaka kwamba mjumbe huyo atamweleza Maharaja habari hii kubwa kupita kiasi; lakini huruma yake isingeliweza kumpuuza topasi mnyonge aliyekuwa taabani. Akamchunguza na kuelewa kwamba anaugua kwa yabisi kali sana ya tumbo na hapati choo. Akamtibu kwa dawa ya kuingizwa katika njia ya haja kubwa naye akapata choo akapona papo hapo. Akapumua kwa kuondolewa taabu na kumshukuru akisema. "Mungu Akubariki sana wewe na yule pia aliyekupatia nafasi ya kuja hapa kwangu." Alisema hayo kwa moyo wenye bidii sana hata mganga akawa na imani kabisa ya kwamba Maharaja aliyeingizwa katika dua hiyo amekwisha ondolewa tayari shida yake yoyote aliyokuwa nayo.

Alipowasili jumba la Maharja akakuta kweli ilikuwa alivyofikiri; Maharaja hakuwa na haja ya kusaidiwa. Akaulizwa nini ilimcheleweshа. Akamweleza Maharaja yote yaliyotokea na pia kwamba alikuwa na hakika kabisa ya kwamba ombi la topasi limekwisha ondolea mbali shida yako. Maharaja akausifu mwenendo wake unaomfaa mganga mnyofu na kumtuza bangili mbili nzito za dhahabu. Kabla hajaondoka jumbani akamwita yule mjumbe na kumpa bangili mojawapo. Yeye akashangaa sana na akataka kujua sababu ya kutuzwa zawadi. Jawabu lilikuwa: "Kama usingalinishtaki kwa Maharaja nisingalituzwa hizi bangili; hivyo unastahiki kupata sehemu yako."

Safari moja Maharaja akawaagiza wakuu wote wa serikali

kuvaa mavazi rasmi ambayo thamani yake isipungue mshahara wa mwezi mmoja. Wakuu wote wakatekeleza amri isipokuwa Mganga Mkuu hakuleta badiliko lolote katika nguo zake zisizo za thamani. Mtu mmoja akamwambia Maharaja habari hii, ambaye akasema: "Amefanya vizuri. Nguo rasmi zingekuwa kizuizi kutimiza wajibu wake. Isitoshe, yeye mara nyingi hutakiwa kuingia katika jumba ambamo kuna akina mama, na mavazi ya kawaida yafaa sana kwa mtu wa aina hii."

Maharaja alipofanya baraza kwa watu wote, kila Mkuu wa serikali alitakiwa kuonyesha uaminifu wake kwa kumpa zawadi ya sarafu moja ya fedha ambayo Maharaja akaigusa kwa vidole viwili kama alama ya kuipokea. Mganga Mkuu akaona haya kuonyesha uaminifu wake kwa njia hiyo, lakini hakuweza kutafuta njia ya kuhepa. Zamu yake ilipokurubia, Maharaja akaona kwamba yeye anaitazama sarafu iliyokuwa katika kiganja cha mkono wake. Aliposogelea karibu, Maharaja akamwuliza: "Unafikiria kuonyesha uaminifu ama waifikiria sarafu?" Akajibu: "Bwana, naifikiria sarafu iliyo alama ya kuonyesha uaminifu wangu."

Maharaja akatabasamu, akasema: "Wewe hulazimiki kuonyesha uaminifu hivyo. Agizo hilo halikuhusu wewe."

Mtu fulani alimwarifu Maharaja kwamba Hakim Nuruddin ni wa nasaba ya yule (Hadhrat Umar r.a.) aliyejitwalia Ukhalifa wa Mtume s.a.w. pasipo haki. Basi siku moja Maharaja akamwuliza: "Kwa nini mtoto wa Mtume s.a.w. hakufanywa Khalifa baada ya kifo chake?" Akajibu kwamba Ukhalifa hauhusikani na mambo ya kidunia, tena Mtume s.a.w. hakuacha nyuma yake mtoto wake wa kiume, na wajukuu wake wa kiume walikuwa bado watoto wadogo sana. Hapo Maharaja akakazania kusema: "Lakini Maula Murtadha (Hadhrat Ali r.a.) alikuwa mwanaye na Hadhrat Umar r.a. akamnyanganya Ukhalifa

wake."

Akajibu: "Hadhrat Ali r.a. hakuwa mwanaye bali alikuwa mume wa bintiye. Tena Hadhrat Umar r.a. hakumfuata Mtume s.a.w. bali yeye alikuwa Khalifa wa Pili."

"Yaani Hadhrat Ali r.a. hakuwa mwanaye?"

"Hapana, alikuwa mume wa bintiye, jinsi alivyo huyu Raja (akiashiria kwake) mume wa binti yako."

"Enhee, nimekwisha elewa sasa. Hatuwaozi binti zetu kwa mtu, wala hatumfanyi kuwa waziri yeyote anayeweza kudai kuwa Maharaja baadaye. Familia ya huyu mume wa binti yangu iliwapinga Waingereza katika Uasi wa mwaka 1857 nao wakafukuzwa nchini na kupelekwa visiwa vya Andaman. Sisi tuliwasaidia Waingereza nao wakatupatia eneo zaidi la ardhi kwa kutambua msaada wetu mwaminifu. Lakini sisi hatukukubali kupata ardhi zaidi, bali badala yake tukawarudisha huyu Raja na babake kutoka Port Blair, tukawarudishia mashamba yao na mali yao na kumwoza binti yetu kwa huyu Raja. Sasa wakijaribu kufanya chochote dhidi yetu, bado port Blair ipo tu. Ama Waziri Mkuu, nikimfukuza kesho, atalazimika kuanzisha duka la vyakula na vitu kama sabuni."

Safari moja Hakim Nuruddin alipata shauku kubwa ya kusoma kitabu *'Abakatul-Anwari,'* maelezo ya Hadithi hii ya Mtume s.a.w.: "Yule aliye rafiki yangu, na awe rafiki ya Ali," utungo wa Mir Hamid Husain, wenye kurasa zaidi ya mia saba. Alipata kusikia kwamba kitabu hiki anacho Mir Nawab wa Laknau, Mshia, aliyekuwa mganga katika Jammu. Akamwomba amwazime hicho. Akakubali kwa sharti kwamba akichukue saa 4 za usiku na kukirudisha baada ya masaa sita yaani saa 10 asubuhi. Hakim Nuruddin akakisoma chuo kizima saa za usiku, akaandika sehemu zake za muhimu na kukirudisha katika muda

uliowekwa. Baadaye akataali hayo maneno aliyoandika na kutafakari juu yake, ijapokuwa hakujua kwamba kazi hiyo yote ya kuchosha aliifanya kwa shabaha gani.

Baada ya siku chache aliambiwa na Sheikh Fateh Muhammad kwamba leo watakula chakula cha usiku nyumbani kwa Mian Ilahi Bakhsh, mwanamji mashuhuri. Walipokuwa wanakwenda kwa mwenyeji wao, Sheikh Fateh Muhammad akamwarifu kwamba mwenyeji wao ni Mshia mshupavu aliyemkaribisha Mujtahid (mtaalamu wa Kishia) ili kujadiliana naye kuhusu itikadi za Kishia, kwa sharti kwamba kama yeye (Hakim Nuruddin) hataweza kubatilisha hoja za Mujtahid, hapo Masunni wote waliopo hapo watakubali itikadi za Kishia kuwa sahihi. Hakim Nuruddin hakuambiwa mapema, kwani ilionelewa kwamba akijadili papo hapo bila kujitayarisha itavutia sana. Akamlaumu Sheikh Fateh Muhammad kwa kukubali sharti ya kipuuzi, lakini bwana huyo hakujali kukaripiwa.

Walipofika nyumbani kwa Mian Ilahi Bakhsh, mara Sheikh Fateh Muhammad akadai kwa nguvu kwamba mshindani Mshia ajitokeze. Na Hakim Nuruddin akapatiwa kitabu kimoja, akashangaa na kufurahi kujua kwamba hicho kilikuwa *'Abakatul-Anwar.'* Akazipindua pindua kurasa zake haraka na kukiweka mbele ya Mian Ilahi Bakhsh, akauliza yashauriwa nini? Akaambiwa kukisoma vizuri sana kitabu hicho. Kasema, amekwisha kisoma tayari; na kama wakipenda angeweza kueleza muhutasari wake na pia kuzivunjilia mbali hoja zilizomo humo. Wataalamu wengi wa Kishia walikuwapo ambao wote hao walitaka awaelezee muhutasari wake naye akaeleza. Walipokwisha sikiliza, wakaenda kando na kunong'onezana wao kwa wao kwamba hawatamweza kitu katika kujadiliana naye. Mian Ilahi Bakhsh akawaagiza watumishi wake wapakue chakula; lakini Sheikh Fateh Muhammad akaendelea kupiga kelele: "Hatutaki chakula,

twataka kusikiliza mjadala; leteni Mujtahid wenu." Lakini wapi! Hakuna aliyejitokeza, hivyo mjadala haukufanyika katu.

Kama ilivyoelezwa, Mian Lal Din alikuwa tajiri sana na mwanamji mheshimiwa wa Jammu, ijapokuwa hakusoma sana. Yeye hakuwa na uhusiano mzuri na Hakim Nuruddin. Hata hivyo siku moja Hakim Nuruddin alichukua hatua kinyume cha kawaida ya kwenda kuonana naye nyumbani kwake. Akamkuta ameketi mahali palipoinuka karibu na dirisha katika chumba kikubwa kilichojaa watu wenye haja zao. Akamsikiliza kila mmoja kwa zamu na kumwandikishia karani maagizo yake. Hakim Nuruddin akangoja kwa subira mpaka kila mmoja akapata kusikilizwa na kuondoka. Karani pia akaondoka akifikiri kwamba yeye Hakim Nuruddin pengine anataka kuongea na Bwana wake faraghani ndiyo maana amesubiri bila kusema. Hapo Hakim Nuruddin akamwambia Mian Lal Din: Wewe una heshima kubwa sana hata kwamba mtaalamu wa wasitani wa kidini hawezi kuthubutu kukutolea nasaha. Hata hivyo kila mmoja anamhitaji mtu wa kumsihi. Nimekuja kutafiti nani ni mwenye kukusihi.

Akajibu: "Bwana Maulawii, unajua sijui kusoma na kuandika, nami sitambui madokezo mepesi."

"Haya, basi kueleza kwa uwazi ni kwamba karibu na kila mji kuna magofu ya mji wa zamani, na karibu na nyumba ya tajiri kuna nyumba ya maskini pengine aliyekuwa tajiri zamani ambayo yaweza kuwa mwonyaji kwake."

"Sasa, kwa kuwa umesema hayo, tafadhali inama ukatazame kutoka dirishani. Kule waona nafasi ya mlango iliyojengewa tao. Hii inafanya kazi kama mwonyaji kwangu. Nakaa karibu na dirisha ili niweze kuiona. Mwenye nyumba hiyo alikuwa tajiri mkubwa sana na mwenye cheo cha juu kiasi hiki kwamba mbele ya Maharaja yeye alikuwa na haki ya kuwekewa mwavuli mwekundu, ilhali mimi sina

ruhusa ya hata mwavuli mweusi. Lakini sasa huyo amefilisika kiasi hiki kwamba mkewe anaosha vyombo jikoni kwetu."

"Hakika huhitaji mwonyaji mwingine."

Hakim Nuruddin akamweleza habari hiyo Maharaja aliyesema: "Ninao waonyaji wengi. Mahali sherehe ya kidini ya kumpaka mafuta Maharaja inapofanywa pamezungukwa na nyumba duni za watu walio wazao wa watawala wa nchi hii. Hao hawalazimiki kuonyesha uaminifu kwetu. Kulikuwa na mji maarufu wa Dharnagar mbele ya mahali ninapobarizi. Huo sasa ni magofu. Tena Bahu Fort ilikuwa ni makao ya watawala wenye nguvu. Siwezi kuwa na waonyaji bora zaidi. Kwa hakika wale tuliochukua utawala kutoka kwao nao ndio waonyaji bora sana kwetu."

# VII

# MTAFUTA NA MTAFUTWA

Mpaka sasa Maulawii Nuruddin alikuwa amekwisha pata umaarufu kama mganga mahiri kabisa, mtaalamu mtawa, sufii mjuzi na mwaminio bora. Tangu muda mrefu yeye alikuwa anamtafuta mwongozi mkamilifu wa kiroho na mwalimu wa mambo ya kiroho. Alikuwa na fursa ya kuonana na watu wenye utaalamu wa hali ya juu walioishi maisha mema na manyofu ambao walikuwa wenye akili nzuri na wapaji lakini hawakushughulikia kuitetea Islam na kuhakikisha ubora wake juu ya dini nyinginezo. Alikuwa anamwomba sana Mungu ili adhihiri shujaa wa aina hiyo wa Kiislamu. Baadaye alifafanua jiha hii ya maisha yake katika kijitabu kwa Kiarabu ambayo tafsiri yake ni kama ifuatavyo:

> “Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu. Sifa zote njema zamhusu Mungu, Mola wa walimwengu, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu, Mmliki wa siku ya Malipo. Baraka na amani ziwe kwa Mkuu wa wanadamu, Mbora wa Wajumbe na Manabii, wa Mungu Mteule wa wateule, Muhammad s.a.w., Muhuri wa Manabii, na kwa ahali zake na Masahaba zake wote. Mtumishi huyu mnyonge na maskini wa Mungu Mwenye nguvu na Mwenye kutegemewa, Nuruddin (Mungu amlinde na taabu zote na amwingize katika watumishi Wake ambao Amewaweka chini ya ulinzi Wake na kumfanya kwelikweli nuru ya dini kama ilivyo tafsiri ya jina lake) anaeleza yafuatayo: Tangu nipate habari ya maovu ambayo watu wa zama hizi wamekuwa nayo, na kushuhudia mabadiliko yaliyopatikana katika dini na wafuasi wa dini, nina shauku, na ninaendelea kuomba, kwamba

Mungu Mtukufu aniongoze kwenye mtu atakayehuisha imani ya Kiislamu na kuwashambulia kiroho maadui zake na watu waovu. Nilitumai kabisa kwamba matamanio yangu haya yatatimia, kwani Mungu Mtukufu Aliye Mkweli kabisa kuliko wote Alitoa habari njema kwa waaminio katika Kitabu Bayana: "Mwenyezi Mungu Amewaahidi wale waaminio miongoni mwenu na kufanya vitendo vizuri, bila shaka Atawafanya makhalifa katika ardhi kama Alivyowafanya makhalifa wale wa kabla yao, na kwa yakini Atawaimarishia dini yao Aliyowapendelea, na Atawabadilishia amani baada ya hofu yao. Wataniabudu, hawatanishirikisha na chochote." (24:56)

"Pia Alisema kumhusu Mtume Mtukufu s.a.w.: Wala hasemi kwa tamaa (ya nafsi yake). Siyo haya ila ni ufunuo uliofunuliwa. (53:4,5). Mtume Mtukufu s.a.w. alikuwa mkweli kabisa na mwaminifu sana. Alisema kwamba Mungu Atamwinua mwanzoni mwa kila karne yule atakayejadidisha dini. Basi mimi nilikuwa miongoni mwa wale walioingojea Rehema yake hiyo; na kwa shabaha hiyo nikasafiri kwenda mahali pa kudhihirikia nuru za ukweli na yakini – Nyumba Takatifu ya Mungu. Nikapitia maporini na majangwani nikimtafuta huyo baina ya waja wa Mungu.

"Katika mji wa Makkah uliobarikiwa, nikakutana na Seyyid Husain aliyekuwa mtu mwema sana na mcha-Mungu, na nikaonana na mheshimiwa Sheikh Muhammad Khazraji. Mjini Madina nikapata heshima ya kuwa pamoja na mwalimu wangu mtukufu Sheikh Abdul Ghani Mujaddidii. Nawaheshimu wote hao kwamba ni wanyofu. Mungu Awapatie ujira kwa sababu ya kunifanyia wema. Amin. Walikuwa na

daraja kubwa wakiwa wataalamu na waja watukufu, lakini hawakuwakabili maadui wa Islam, wala hawakujibidiisha kuwaondolea mbali wasiwasi wao. Walishughulikia ibada faraghani na kumwomba Mola wao upwekeni.

"Sikumkuta mtaalamu yeyote wa dini akishughulikia kuwaeleza ujumbe wa Islam Wakristo, Waaria, Mabrahmu, Madaharia, Wanafalsafa, Wasidikio na wapinzani wengine wa Islam. Upande mwingine nikagundua kwamba nchini India zaidi ya milioni moja ya wanafunzi wa Kiislamu wameachilia mbali masomo ya kidini na wamechagua masomo na lugha za Kimagharibi, na wamependelea kukaa na wasiokuwa Waislamu kuliko Waislamu.

"Zaidi ya milioni sita za vikaratasi, majarida na vitabu vimekwisha enezwa dhidi ya Islam, hata hivyo twasikia kwamba masheikh wa zama hizi na wafuasi wao wako imara kusema kwamba ni kinyume cha desturi ya wakuu wa dini kuwaita watu wasilimu na kufanya mijadala na wapinzani wa Islam. Masheikh wetu wengi hawana habari ya mambo yalivyo. Jitihada ya mwisho ya wataalamu wetu wachunguzi ni kwamba wakati wao wote unatumika katika kujadiliana maswala yasiyofaa na yenye kumnenea Mungu kama vile, je, Mungu Anao uwezo wa kuongopa au hanao. Matokeo ni kwamba hawabakiwi na nafasi ya kuwanyamazisha wapinzani wa Islam na kuvunjilia mbali mipango yao dhidi ya Islam.

"Hata hivyo twapaswa kutambua kwa shukurani kubwa kazi iliyofanywa katika uwanja huo na waheshimiwa Sheikh Rahmatullahi, Dkt. Wazir Khan, Imam Abdul Mansur wa Delhi, Seyyid Muhammad Ali wa Kanpur, mwandishi wa *Tanzihul Kuran*, na wengineo. Mungu Azibariki bidii zao,

naye ndiye Mbora wa kuthamini uzuri wa kazi yoyote. Lakini bidii zao zote zilihusikana na sehemu moja tu ya wapinzani wa Islam, tena kazi yao haikutiliwa nguvu na Ishara za kimbinguni na bishara zitokazo kwa Mungu. Mimi nilikuwa na shauku ya kuonana na mtu mkamilifu ambaye awe wa pekee baina ya watu wa zama zake, na ajitokeze uwanjani ilhali amejiandaa vizuri kabisa kuisaidia dini na kuwanyamazisha wapinzani. Niliporudi kutoka Hijazi, nilihangaika sana. Nikazunguka nikiwa na kiherehere kutafuta na kungoja mwito wa mtu mwema huyo.

"Katika hali hiyo nikapata habari ya ujaji wa mtu mtukufu wa hali ya juu, mataalamu mkubwa, mja wa Mungu, Mjaddidi wa karne, Mahdi na Masihi wa zama hizi, mwandishi wa *Barahine Ahmadiyya*. Nikafanya haraka kumwendea ili nimwone mwenyewe. Nikatambua mara moja ya kwamba huyu ndiye Mwamuzi Aliyeahidiwa, naye ndiye aliyetumwa na Mungu Mtukufu kwa kuhuisha imani. Mimi mara moja nikauitikia mwito wa Mungu, nikaanguka katika sujuda kumshukuru kwa neema hii kubwa. Sifa zote njema ni Zako Uliye Mwingi wa ukarimu, nakushukuru kwa unyenyekevu kwa rehema Yako. Nikajitolea kwa Mahdi wa zama hizi na kufanya baiati kwa uaminifu kabisa. Wema wake na ukarimu wake ukanifunika kikamilifu na nikampenda kabisa kabisa kwa moyo wote. Nikampenda kuliko vyote nilivyo navyo, na mke wangu na watoto wangu na wazazi wangu na jamaa zangu wote na hata uhai wangu. Ujuzi wake, maarifa yake na ufahamu wake wa kiroho ukaufanya moyo wangu kumstahi na kumheshimu. Namshukuru Mungu sana mno kwani Aliniongoza kwake. Ni bahati yangu njema ya kwamba nikampenda zaidi kuliko kila kitu na nikajitolea kwa kumhudumia kama mtumishi

mwaminifu asiyepungukiwa kwa jiha yoyote. Shukurani zote kwa Mungu, Mwingi wa rehema, Aliyenifanyia ukarimu wa hali ya juu."

Ikawa hivi: Mwislamu mmoja aliyejipatia masomo ya Kizungu ambaye alikuwa ofisa mkubwa alijadiliana kirefu na Maulawii Nuruddin kuhusu utume, itikadi aliyokatalia mbali kwa dharau. Mwishowe, siku moja akatangaza kwamba amekuwa na yakini ya kuwa Mtume Mtukufu s.a.w. kweli alikuwa *Khatamun Nabiyyin* (Muhuri wa Manabii) na kwamba yeye hataki kuendelea kujadili. Maulawii Nuruddin akafikiri kwamba kwa kweli kutangaza huko ni rahisi, na akamwambia kuleta hoja ya kumsaidia. Akaitika: "Mtume Mtukufu s.a.w. alikuwa mwenye akili na busara. Alikwisha tambua kwamba akili ya mtu yaendelea kukua haraka na kwamba wazo la Utume na ufunuo tangu sasa halitakubaliwa, hivyo, basi, akatangaza kwamba yu *Khatamun Nabiyyin*." Maulawii Nuruddin akashtuka na kuchukia sana kipeo cha upumbavu na ujinga wa kupita kiasi. Kitambo kidogo tu baadaye Waziri Mkuu wa serikali akampatia tangazo la Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad wa Qadian ambamo wazo bovu la huyo ofisa mkubwa lililokuwa limemwudhi sana lilikuwa limebatilishwa. Haraka sana akalichukua na kumwendea, akasema: "Hapa pana mfano wa mtu anayedai kwamba anapokea wahyi na anayakinisha kwamba Mungu Anazungumza naye." Akalijibu tu: "Iliyobaki ni kujionea mwenyewe."

Maulawii Nuruddin akataharuki mno na tangazo hilo la mheshimiwa Hadhrat Mirza hata kwamba mara moja akaondoka kwenda Qadian ili kuonana naye na kumchunguza mwenyewe. Katika hali ya safari akashughulikia maombi kwa moyo wote kwa kupata mwongozo. Ameeleza katika maneno yafuatayo ilivyokuwa hali yake mara alipomwona: "Pindi nilipomwona, moyo wangu ukashuhudia

kwamba huyu ndiye Mirza, nami nitajitolea uhai wangu kwake." Hapo ndipo paliishia utafiti wake. Alikwisha mpata aliyekuwa anamtafuta. Wakati huo alikuwa mwenye umri wa miaka arobaini na mitatu.

Akamwomba Hadhrat Mirza apokee baiati yake, ambaye akajibu: "Sina idhini kupokea baiati. Siwezi kuchukua hatua yoyote pasipo kuamriwa na Mungu."

"Basi, je, naweza kuhakikishiwa kwamba pindi upatapo agizo hilo nitakuwa wa kwanza kuitwa kufanya baiati?"

"Uwe na yakini."

"Je, kuna jitihada maalumu ambayo napaswa kufanya ili kujipatia mapenzi ya Mungu?"

"Andika kitabu kimoja kuhakikisha uwongo wa lawama za Wakristo dhidi ya Islam."

Akafunga nia kutekeleza agizo hilo, ingawaje hakujua sana kuhusu Ukristo wala hakuelewa namna za upinzani wanazoleta Wakristo dhidi ya Islam. Isitoshe alishughulishwa sana huko Jammu na akashangaa atawezaje kupata wasaa kwa kutaali, kuchunguza na kuandika.

Aliondoka Qadian akaenda kwao Bhera kabla hajarudi Jammu. Huko katika msikiti Imam aliyekuwa Hafidh (Yaani alikuwa amekumbuka Kurani nzima kwa ghaibu), naye alikuwa zamani mwanafunzi mwenzake shuleni, akaanza kubishana naye kuhusu hiari ya mtu na kadiri ya Mungu kwa maneno ya ujasiri. Watu wengine walipokwisha ondoka na akajikuta yuko peke yake pamoja na Imam akamwuliza: "Bwana Hafidh, nafikiri umeathirika na Ukristo." Akajibu: "Kuna ubaya gani katika Ukristo?" Akatoa shauri kwamba yeye na Imam wamwendee mhubiri wa Kikristo ambaye Imam

anahubiriwa naye, na huko Maulawii Nuruddin aongee naye. Imam akakubali shauri hilo na kumpeleka kwa mhubiri huyo Mzungu huko Pind Dadan Khan. Akawapokea kwa heshima na kuwakirimu, lakini haikuwezekana kumwingiza katika majadiliano. Hatimaye akasema kwamba atawapelekea upinzani wake dhidi ya Islam kwa sura ya maandishi. Maulawii Nuruddin akamwambia Imam: "Bwana Hafidh, je, waweza kusubiri usibatizwe mpaka upate kusoma upinzani huo na hoja za kuubatilisha?" Imam akasema hiyo ni sawa, na mwungwana mheshimiwa akaridhika.

Baada ya mhubiri kuondoka hapo, Maulawii Nuruddin akamwuliza Imam: "Je, wamjua yeyote mwingine ambaye yumo katika hali uliyomo wewe?" Akaambiwa kwamba mkuu wa stesheni anayo nia hiyo. Basi wote hao wakamwendea mkuu wa stesheni moja kwa moja ambaye akasema kwamba hakuna dini yoyote inayoweza kuukabili Ukristo. Hata hivyo akashangaa kujua ya kwamba mhubiri alikataa kujadiliana. Huyo naye akakubali kusubiri kabla hajasoma upinzani ule na majibu yake. Maswali hayo ya kuipinga Islam yalikuwa mengi na ya aina tofauti na ikafahamika kwamba itachukua mwaka mzima kutayarisha majibu na kuyachapisha.

Mwaka huo nchi ilifululiza kupata matetemeko ya ardhi ambayo yakamtisha sana mno mwanawe Raja wa Punch hadi akapatwa na wazimu. Raja huyo akamwomba Maharaja wa Jammu kumpelekea tabibu mmoja aliyeelimika sana kwa kumtibu mwanaye. Maharaja akampendekeza Hakim Nuruddin naye akaenda Punch. Akapatiwa huko makazi mazuri nje ya mji. Alikuwa na mgonjwa mmoja tu kutibu, hivyo akawa na nafasi nyingi kwa kutaali kwa bidii akilinganisha Biblia na Kurani Tukufu na kuandika mambo ya muhimu kwa kutayarisha majibu ya maswali ya mhubiri wa Kikristo. Akiisha kujiandaa vizuri akaandika majalada manne kwa kufutilia mbali upinzani wote ule

wa Kikristo, ambayo majalada hayo yakaitwa *Faslul-Khitabi*. Pindi muswada ulipokamilika mwana-Raja alikuwa amepona kabisa. Raja wa Punch akampa tabibu zawadi ya pochi ambamo mna elfu kadha za Rupia kama alama ya shukrani yake. Aliporudi Jammu, Mahraja akamwuliza: "Ni kiasi gani alichokupa Raja?" Naye akaliweka pochi hilo mbele yake. Maharaja akaudhika kwamba amelipa kidogo sana, na akaamuru kwamba apatiwe pia mshahara wa mwaka mzima na marupurupu kutoka katika hazina ya serikali. Yeye akatuma fedha na majalada mawili ya kitabu chake kwa mpiga chapa mmoja huko Delhi. Kitabu kilipokwisha chapishwa akatuma nakala zake kwa watu mbalimbali pamwe na yule mkuu wa stesheni na Imam mjini Bhera, ambao wakarudisha majibu kwamba baada ya kukisoma kitabu kwa makini sana wasiwasi wao wote umeondolewa na sasa wanaamini kwa moyo wote katika Islam na hakuna chochote zaidi ya hayo kinachohitajika.

Maulawii Nuruddin akawasiliana mara kwa mara na Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. na akaendelea kuongozwa na kuangazwa na barua zake na maandiko yake. Akamwomba ushauri wake kuhusu kila alilotaka kufanya. Watoto wake wengi walifariki utotoni, mmoja baada ya mwingine. Kila mara Hadhrat Mirza Ghulam Ahmd a.s. akamwandikia kumpa pole na kumfariji kiroho na kuimarisha imani yake kwa Mwenyezi Mungu na kumfanya amtegemee kabisa Mungu. Katika barua mojawapo miongoni mwa barua alizomwandikia mwanzoni alimsihi sana kuomba hivi katika ibada yake ya tahajjudi: E Mungu wangu, Mfadhili wangu, mimi ni kiumbe wako duni mwenye dhambi nyingi na ni mzembe. Umeona kwangu kosa baada ya kosa, nawe ukanijaalia neema baada ya neema. Umeniona nikifanya dhambi baada ya dhambi, nawe ukanifanyia ukarimu baada ya ukarimu. Siku zote umefunika daima makosa yangu na kuniongezea zawadi nyingi zisizohesabika. Nakuomba sana unihurumie tena niliye kiumbe

wako mbovu na mwenye dhambi, na unisamehe usafihi wangu na kutokushukuru kwangu. Niokoe kwa hisani yako katika huzuni yangu, kwani hakuna Mwokozi minghairi yako Wewe.

Maulawii Nuruddin alikuwa amejitolea kikamilifu kwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. wala hakumzuilia chochote. Safari moja yeye akapata agizo kutoka kwake lililoelezwa kama hivi:

> "Pandit Lekh Ram ametoa hivi karibuni kitabu kwa kujibu kitabu changu *Barahine Ahmadiyya* ambamo yeye amejaza upuuzi mwingi, ambacho amekiita *Takdhib Barahine Ahmadiyya*. Hakuna budi uwongo huo na ulaghai huo mwingi sana utobolewe wazi upesi iwezekanavyo. Ninashughulikia kikamilifu kutunga kitabu cha *Siraje Munir* wala sina nafasi kabisa. Sipigi chuku wala sikusukumwa na matilaba kukusifu nisemapo kwamba Mungu Amenitilia moyoni ya kuwa hakuna mwingine ambaye Yeye Amemjazia shauku kubwa sana ya kuitumikia dini na kunisaidia. Kwa hiyo mimi nakuambia uchukue jukumu la kukisoma kitabu hicho tangu mwanzo hadi mwisho na kuorodhesha mateto yake aliyoleta mwandishi dhidi ya Islam. Halafu ratibu majibu kama Atakavyokuelimisha Mungu, moja baada ya jingine na kuniletea. Lile linalonihusu mimi binafsi nitalifafanua mwenyewe nipatapo nafasi. Hii ni kazi ya muhimu sana nami nakuambia kwa kusisitiza kwamba ianze kwa mkazo wa fikara na jazba na kwa kujitolea kwa uwezo wako wote. Na jinsi ulivyonisaidia kwa mali kwa uwezo wako wote, basi na ufanye hivyo barabara kabisa kwa vipawa ulivyojaliwa na Mungu.
>
> "Wapinzani wetu wote wameungana dhidi yetu na wanafanya kila juhudi kuiadhiri Islam. Nionavyo mimi, yule anayeingia uwanjani wakati huu na kujitahidi kwa ajili ya

> Islam, hufanya kazi inayohusiana na Manabii. Nangoja majibu yako. Mungu Awe pamoja nawe na Akusaidie.»

Maulawii Nuruddin akatekeleza kazi hiyo ya muhimu kwa njia bora sana kwa kutunga kitabu chake *'Tasdiq Barahine Ahmadiyya.'*

Safari moja yeye akapatwa na homa kali sana na kuumwa kichwa. Maradhi yake yaliendelea muda mrefu. Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. alipopata habari hiyo akamwandikia kwamba ninafika Jammu kukutembelea na kwamba nilipokuombea afya njema Mungu akipokea ombi langu Ameniambia kwamba nitakapofika nitakukuta umekwisha pona. Na ndivyo ilivyotokea. Hadhrat Mirza Sahib akashinda Jammu kwa siku tatu.

Baada ya kukaa miaka mingi huko Jammu na Kashmir, Maulawii Nuruddin akawa na uhusiano mkubwa sana na Maharaja na Raja wa Punch. Pia akatambua kuhusu fitina zilizoendelea ndani kwa ndani katika Jumba la Maharaja, na akajihadhari asijiingize humo. Kila mara alipofikiwa na mtu fulani ili atoe habari kumhusu Maharaja, akakataa katakata. Uaminifu wake kwa Maharaja, aliueleza kwa kifupi hivi: "Yeye aniamini; sitasaliti imani yake."

Raja wa Punch akaanza kumtolea kila mwaka fedha za posho, naye alikuwa anamwendea kumwangalia kila alipofika Jammu. Safari moja Raja alipofika Jammu alikuwa anaugua na Maulawii Nuruddin akamtembelea na kumwandikia dawa. Alipokuwa anaondoka mtu fulani akampasha habari ya kwamba mtumishi fulani wa Raja anakutaka umtembelee. Akajibu: "Makazi yangu yako njiani mwake, arudipo nyumbani aweza kuonana nami." Mtumishi huyo alipopata ujumbe huu, akakasirika na akasema: "Yaonekana Nuruddin ameanza kujivuna. Sitampa nafasi tena kumtazama Raja." Tangu hapo, yeye hakuitwa kumwona Raja kwa miezi mingi.

Kisha ikawa hivi kwamba Maharaja alilazimika kwenda Lahore, na Raja wa Punch aliyekuwa pamoja naye akawa mgonjwa huko Lahore. Kwa kuwa mganga yeyote mwingine hakuwa pamoja nao, hivyo akamwita Maulawii Nuruddin saa za adhuhuri wakati alipokuwa peke yake. Alipofika, Raja akamwambia: "Posho yako kwa mwaka huu haijatolewa kwako. Nitaagiza upewe posho kwa miaka miwili mara moja." Maulawii Nuruddin akajasiri kusema: "Labda umeniita saa hizi kinyume na kawaida ili yule mtumishi aliyenikasirikia kwa sababu sikumtembelea asipate kujua kwamba nimekuja kukutazama. Kama ni hivi, basi yeye anaweza kuchukia mimi kukutibu na huenda akakudhuru kwa namna fulani." Raja akakubali: "Sisi twapaswa kujitahadhari kwao. Waovu hao hata hawawezi kukosa kulisha sumu."

Aliendelea kumtibu Raja, lakini afya yake ilizidi kuharibika kidogo kidogo na muda kidogo baada ya kurejea Punch akafariki. Maulawii Nuruddin akaonywa na mtu fulani kwamba mwanaye Raja marehemu aliyemrithi Uraja ambaye yeye alimtibu katika maradhi yake kwa muda mrefu na ambaye siku zote alidhihirisha maoni mazuri kwake, sasa ananuia kumshtaki kwa kusababisha kifo cha baba yake kwa kumtibu vibaya na kwa nia mbaya, pengine hata kumlisha sumu. Akafikiri kwamba mwana wa Raja alichochewa na yule mtumishi mkorofi. Lakini habari hiyo haikuendelea mbele.

Maulawii Nuruddin alikuwa mkarimu sana katika kuwasaidia wanafunzi waliostahaki ili kukuza vipawa vyao vya kiakili. Safari moja akafanya mpango wa kuwatayarisha wanafuzni dazeni moja ili kuhudumia Islam na akawapangia wajipatie ubingwa katika lugha moja au mbili miongoni mwa lugha kadhaa za muhimu kama vile Kiarabu, Kiebrania, Kigiriki, Kisansikriti na Kiingereza. Akatumia fedha nyingi sana kwa azimio hili. Lakini wanafunzi

waliochaguliwa kwa uangalifu sana walipohitimu mafunzo, hata mmoja kati yao hakujishughulisha katika kazi aliyonuia mfadhili wao. Akavunjika moyo, lakini hakuwachukia, wala hakukata tamaa.

Tarehe 20 Februari 1886, Hadhrat Mirza Sahib a.s. alitoa tangazo la bishara moja kubwa kuhusu kuzaliwa kwa mwana ambaye kwa fadhili ya Mwenyezi Mungu atakuwa na sifa na vipawa bora mno vya ajabu; sehemu moja ya maneno ya ufunuo ndiyo hii:

> "Mwana, furaha ya moyo, aliyenyanyuliwa, mtukufu, dhihirisho la yule Wa Kwanza na Wa Mwisho, alama ya Yule Aliye Mkweli na Mkuu, kana kwamba Mungu Ameteremka kutoka mbinguni."

Mwana huyo akazaliwa 12 Januari, 1889. Mwaka huo ukathibitika kuwa wa muhimu kabisa katika historia ya dini na ya Islam, na katika maisha ya Maulawii Nuruddin. Jumuiya ya Ahmadiyya ilianza mwaka huo, na matukio fulani ya maana yalitukia mwaka huo yaliyomwathiri Maulawii Nuruddin, ambayo baadhi yake yaelezwa kwa kifupi hapa chini.

Yeye alipata kuoa mara mbili, lakini watoto wake wote wa kiume wakafa utotoni. Hadhrat Mirza Sahib alipenda sana aoe mara ya tatu na akafanya maombi kwa kupata mwongozo na akafanya utafiti kuhusu mke atakayemfaa. Hatimaye katika barua yake ya tarehe 23 Januari, 1889, akapendekeza ya kwamba Maulawii Nuruddin afikirie kwa kumposa Sughra Begum bintiye marehemu Sufi Ahmad Jan aliyekuwa mtaalamu mtawa wa Ludhiana, lakini wa Delhi kwa asili. Likapelekwa ombi la kuposa, likakubaliwa. Ndoa ikatangazwa rasmi mnamo Februari na arusi ilifanyika Machi 1889. Ndoa hiyo ikafana na ikabarikiwa, kwa rehema ya Mungu. Na miongoni mwa watoto wa kiume waliopata mke na mume wanne wakapata kubalahe, ambao

kati yao watatu wakaoa na wakapata kizazi. Binti yao, Amatul Hai, alipovunja ungo akaolewa na Mwana Aliyeahidiwa wa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s., ambaye alizaliwa tarehe 12 Januari, 1889.

Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. alikuwa ametangaza sawa na maagizo ya Mungu kuanzisha Jumuiya yake, na tarehe 12 Januari 1889 akaweka masharti ya kuungana naye. Kisha akaweka tarehe 23 Machi, 1889 ili wafuasi wake waje mjini Ludhiana kufanya baiati yake. Maulawii Nuruddin akawa wa kwanza kufanya ahadi ya kufungamana kiroho na Mwanzilishi Mtukufu wa Mwendeleo huu. Hiyo ilimaanisha kufungamana naye kikamilifu na kwa kudumu dawamu, na akaitekeleza ahadi hiyo barabara kabisa kwa njia bora sana. Maisha yake yote ya hapo baadaye yalikuwa kielelezo cha maana ya kweli ya ahadi hiyo ya baiati. Akiisha funga ahadi ya baiati ya kiroho akarejea Jammu, lakini daima akawasiliana na mwalimu wake wa kiroho kwa kuandikiana naye na kutembelea Qadian mara kwa mara ambako akajenga nyumba ndogo ya matofali ya kuchomwa kwa kukaa humo kwa muda.

Mnamo Mei 1889 mamake akafariki huko Bhera ilhali yeye alikuwa hayuko kule. Miaka kumi na minane hapo kabla ambapo magazeti yalikuwa yanatangaza vifo vya watu wengi katika vita vya Urusi na Uturuki, yeye alimshauri mamake akisema: “Mama, una wana wanane na mabinti wawili ambao wote hao wamekwisha oa au kuolewa isipokuwa mimi; basi waweza kuniruhusu nijitolee wakfu kwa ajili ya Mungu.” Mamake akatishika na akapata kutamka: “Yewezekanaje hiyo ilhali niko hai!” Yeye hakung’ang’ania. Hapo baadaye nduguze wakafa, mmoja baada ya mwingine, katika vipindi vidogo. Kila ndugu alipofariki, mjane wake akafunga virago vyake na kuhama jumba la kifamilia ambalo hatimaye likagubikwa na ukiwa. Safari moja alirejea kwao kutoka Jammu ili kumtembelea mamake wakati wa kiangazi.

Baada ya chakula cha mchana alipokuwa amelala usingizi kidogo mara akaamshwa na kilio cha mamake kilichosikika kutoka katika chumba cha pili: "Sisi ni wa Mungu na kwake tutarejea" (2:157). Yeye akamwendea na kumshauri ya kwamba maneno ya kuonyesha kujitolea kwa imara kwa radhi ya Mungu hayafai kutamkwa kwa sauti ya kulalamika. Kisha akamwuliza: "Je watambua kwa nini jumba hili kubwa limekuwa kiwa sasa?" Akajibu: "Naam, nakumbuka uliyosema zamani sana. Niliyakumbuka kila alipofariki mwanangu miongoni mwa wanangu." Akauliza: "Je, watambua habari nyingine yoyote?" Mama akajibu: "Naam, najua ya kwamba ijapokuwa napenda uwe karibu nami pindi nifapo na kuangalia mambo yote, nitafariki wakati hupo kwangu." Na ndivyo ilivyotokea. Yeye alikuwa huko Jammu wala hakuweza kufika kwake alipofariki.

# VIII

# KUHAMA

Maulawii Nuruddin akaendelea kuwa tabibu wa Maharaja kwa miaka mingine mitatu. Akaridhika na hali yake aliyokuwa nayo wala hakuona sababu ya kuleta mabadiliko. Kulikuwa na vipindi vya fitina na pia vipindi vya utulivu, lakini maadamu Maharaja alimtegemea na kumwamini hakujali mambo mengine yoyote.

Mnamo mwaka 1892, Rajah Suraj Kaul alikuwa mwanachama wa daraja la juu wa halmashauri ya nchi. Alikuwa anaugua kwa maumivu ya figo. Alimtaka Maulawii Nuruddin amtibu. Akamchunguza kikamilifu na akagundua kuna kijiwe figoni mwake na akamwarifu. Mgonjwa akashtuka na kufoka: "Je, hujui kwamba madaktari saba wa kizungu wamefanya kazi chini yangu?"

"Hilo halihusiani na kijiwe figoni"

"Hata mwanangu mmoja ni daktari"

"Babake daktari hana kinga dhidi ya kijiwe figoni mwake."

Raja akahangaika na akamwondosha. Baada ya kitambo Colonel Perry wa Chuo cha utabibu, Lahore, pamoja na daktari mwingine Mzungu aliye fundi wa upasuaji walitembelea Jammu. Maharaja akawaomba kumchunguza Raja Suraj Kaul na kumwandikia dawa. Wakati alipokuwa anachunguzwa, Raja akasema ya kwamba tabibu mmoja aliniambia ya kuwa ninacho kijiwe figoni mwangu. Hapo Bwana Perry akamwagiza mwenzake afanye mkato kidogo ili kutazama kijiwe; lakini kijiwe chochote hakikuonekana. Ndipo Col. Perry mwenyewe akashika kisu kile cha kazi ya udaktari na kupanua mkato huo na kukuta kijiwe kipo ambacho akakitoa nje. Madaktari wote wawili wakafurahi sana na kumsifu tabibu huyo umahiri wake.

Baada ya kupona Raja Suraj Kaul akamwita Maulawii Nuruddin mara nyingine, lakini alikataa kwenda. Alitambua kwamba Raja hampendi na kwamba kumtembelea mara moja hakutatengeneza mambo. Ikaonekana kwamba Raja amemshawishi Maharaja amwondoe kazini Maulawii Nuruddin na pengine Raja alikwisha waeleza habari hii wenzake katika Baraza ambao mmojawapo katika hao, Bwana Bag Ram, akamshauri kwamba itakuwa busara ampelekee Maharaja hati ya kujiuzulu. Maulawii Nuruddin akamwambia kwamba Islam haipendi mtu aiache njia ya kujichumia riziki pasipo kulazimika. Isitoshe, kutuma hati ya kujiuzulu kwaweza kuwa dalili ya utovu wa shukurani kwa Maharaja. Muda si muda, akapata hati ya kuondolewa kazini.

Haraka sana akamwarifu mwalimu wake wa kiroho ambaye akimjibu alisema:

> "Njia mojawapo ya Mungu kuonyesha upendo wake kwa mtumishi wake ni kumtia katika majaribio. Hilo ni jaribio tu la aina hii wala si kitu cha kuogopwa. Mungu Anajua vizuri kadri niliyokuombea sana na tena kwa moyo wote na bidii. Nitaendelea kuomba nikitumai kupokea majibu ya kuchangamsha. Maombi yangu kwa ajili yako ni ya aina maalumu ambayo huwa kwa rafiki aliyejitolea. Haiyumkiniki kufafanua kinaganaga kiasi na kadiri tunavyoamini nguvu na rehema na neema za Mwenye Enzi, Mzima wa milele, Mfalme Mwenye nguvu na Bwana ambaye twasujudia daima kizingitini pake."

Maulawii Nuruddin akapata mshahara mnono, na mara kwa mara akapewa zawadi zenye thamani kubwa kwa sura mbalimbali. Kwa hiyo akawa na mapato makubwa sana ambayo yote hayo akatolea kusogeza mbele miradi bora pamoja na kuwatunza mayatima, wajane,

wanafunzi na wenye haja. Mchuuzi mmoja Baniani sikuzote alimsihi kuweka akiba sehemu moja ya mshahara wake kwa siku za shida zisizoepukika. Lakini yeye akamwambia hiyo hailingani na imani yake ya kumtegemea Mungu kikamilifu, na kwamba Mungu daima Humtimizia mahitaji yake. Siku aliyopokea hati ya kuondolewa kazini, huyo mchuuzi akamjia na kuuliza, "Mheshimiwa Maulawii, je, unakumbuka nasaha yangu niliyokutolea?" Akajibu: "Naibeza nasaha yako nilivyoibeza sikuzote."

Yule mchuuzi alipokuwa bado anaongea naye, tarishi mmoja wa Hazina ya serikali akamletea barua ambamo mlikuwa na Rupia mia nne na themanini zikiwa ni mshahara wa siku zile alizofanya kazi mwezi huo. Hiyo ikamhangaisha mchuuzi; akaona ni upumbavu wa hali ya juu wa maafisa wa ofisi ya bwana fedha ya serikali. Alikuwa bado hajatulia mara mjumbe wa Rani (mkewe Maharaja) akaja na fedha nyingi zilizotumwa na Rani pamoja na kuomba radhi kwani wakati huo hakuweza kupata fedha nyingi zaidi kuliko hizo. Jambo hili likamduwaza mchuuzi moja kwa moja. Lakini kwa kuficha mahangaiko yake akasema huku ameshika tama: "Hiyo yote ni sawa, lakini unadaiwa Rupia laki mbili takriban na mwia fulani ambaye huenda hatakuacha uondoke pasipo kufanya mpango wa kumridhisha kwa kulipa deni lake." Papo hapo akawasili wakili wa huyo mwia naye akifunga mikono yake kifuani kwa heshima sana akasema: "Nimeagizwa na Bwana mkubwa nije kufanya mpango wa safari yako na kutuma mizigo yako yote na kukukopesha kiasi chochote cha fedha unachotaka." Mheshimiwa Nuruddin akasema, "Umfikishie Bwana wako ahsante nyingi kwa niaba yangu." Akaongeza: "Nimekwisha pata kutoka Hazina ya serikali na kutoka kwa njia nyinginezo zaidi kuliko ninayohitaji, nami nitachukua mizigo yangu pamoja nami."

Mchuuzi akainuka, akatikisa kichwa chake huku akisema:

"Yaonekana Mungu pia Anapendelea. Sisi tunalazimika kufanya kazi kwa bidii tangu asubuhi hata jioni ili kujichumia Rupia chache, na hapa pana mwia mpumbavu ambaye badala ya kudai deni lake yuko tayari kukopesha zaidi."

Bwana Maulawii Nuruddin kajibu: "Mungu anao ujuzi wa nyoyo za viumbe vyake. Mimi, Mungu Akijalia, nitalipa deni hili katika muda mfupi. Haya ni mambo usiyoweza kufahamu."

Kutoka Jammu akaenda Bhera ambako akanuia kujenga jengo kubwa litakalotumika kama makazi yake na pia kliniki yake. Ujenzi ulipokuwa unaendelea alipaswa kwenda Lahore kununua vifaa vya ujenzi. Akiisha maliza kazi yake hiyo mjini Lahore, akaonelea aende mara moja Qadian kuonana na Hadhrat Ahmad a.s. kwa siku moja kabla hajarejea Bhera. Wakati wa kuongea na Hadhrat Ahmad a.s. akaulizwa: "Je huna shughuli sasa?" Kaitika kwamba hana, na akaonelea si vizuri kuomba ruhusa ya kuondoka siku iyo hiyo. Kafikiri kuahirisha safari ya kurudi kwa siku mbili tatu. Keshoye Hadhrat Ahmad a.s. akamwambia: "Ungehitaji mtu yeyote wa kukutunza, hivyo waweza kumwagiza mkeo aje hapa." Basi akamwandikia mkewe kuja, na pia akaagiza kusimamisha ujenzi kwani aweza kukaa Qadian kwa muda fulani. Mkewe akiisha wasili Qadian, siku moja Hadhrat Ahmad a.s. akasema: "Maulawii Sahib, kwa kuwa unapenda sana vitabu, hivyo ungeweza kuagiza vitabu vyako kutoka Bhera." Basi akafanya mpango wa kuleta vitabu. Baada ya siku kadha akaambiwa asifikirie Bhera kuwa ni kwao tena. Hapo akawa na hofu kidogo. Hataenda tena Bhera; lakini haiyumkiniki kukoma kuwaza kwamba Bhera ndiyo kwao. Mara nyingi, hapo baadaye, akaeleza kwamba Mungu kwa fadhili zake Akazuia mawazo yake hata kwamba fikara ya Bhera kuwa kwao haikupitia moyo wake kabisa.

Qadian ilikuwa ni mji mdogo wenye wakazi mia chache, maili kumi na moja kutoka kituo cha gari moshi na ofisi ya simu ya maandishi. Barabara ielekeayo kituo cha gari moshi na ofisi ya simu ilikuwa ya mchanga yenye mashimo mashimo. Njia pekee ya kupeleka habari nje ilikuwa ofisi ndogo ya posta. Urahisi na raha yote inayopatikana katika mji wowote ilikosekana kabisa. Hata maji ya kunywa yalikuwa shida kupatikana. Maulawii Nuruddin akachagua kukaa katika nyumba ya matofali isiyo ya fahari iliyopigwa na jua kali, akiwa na furaha kwa sababu ya ndoto yake kutimia ya kuipendeza roho yake. Shabaha yake ya pekee ilikuwa kujipatia radhi ya Mungu kwa kujitolea kwa mwongozi wake wa kiroho aliyetumwa na Mungu kuijadidisha Islam.

Mkazi mmoja mashuhuri wa Bhera alimwandikia kwamba anaugua na anapenda yeye aje kumtazama na kumtibu kwani yeye alikuwa mganga wa familia yake. Akamwandikia jawabu kwamba yeye amekwisha hama Bhera na atakaa Qadian kwa kudumu wala hawezi kuondoka kwenda nje pasipo kuruhusiwa na Bwana wake. Hapo mgonjwa akamwandikia Hadhrat Ahmad a.s. akimwomba amwagize Maulawii Nuruddin kumtembelea na kumwandikia dawa. Akiagizwa hivyo, Maulawii Nuruddin akaenda Bhera, akamtazama mgonjwa nyumbani mwake mpakani mwa mji, akamchunguza, na kumwandikia dawa pasipo kuingia mjini wala kuonana na rafiki yake yeyote, wala kuona jumba la zamani la familia yake au kutazama jengo lililojengwa nusu, akarejea Qadian kana kwamba Bhera haikuwa kwao kabisa.

Mkazi mmoja tajiri wa Rawalapindi aliwasili Qadian na akamwomba Hadhrat Ahmad a.s. amwagize Maulawii Nuruddin r.a. aende Rawalpindi akamtibu mgonjwa mmoja wa familia yake. Hadhrat Ahmad a.s. akamwambia: “Ninayo yakini kabisa kwamba

kama ningemwambia Maulawii Sahib ajitupe baharini ama kuingia mara moja motoni, atafanya hivyo bila kusita hata kidogo. Lakini sina budi kufikiria furaha na raha yake. Mkewe anatazamia kujifungua, basi siwezi kumwambia aende nje ya Qadian." Maulawii Nuruddin r.a. aliposikia hayo akaathirika mno na akaona ni vigumu kueleza furaha yake kwamba Bwana wake anamwamini sana.

Chifu mmoja mashuhuri, alifika Qadian naye alikuwa anatibiwa na Maulawii Nuruddin r.a. Siku moja wafuasi wawili wa huyo chifu wakamjia Maulawii Nuruddin r.a. na kumwambia Leftinanti Gavana wa Mkoa atatembelea hivi karibuni ile sehemu ya Mkoa iliyo chini ya Chifu, naye amependa kwamba Maulawii Nuruddin r.a. aende naye na awepo hapo wakati huo. Lakini yeye akamwambia kwamba hawezi kutoka nje ya Qadian hata kidogo bila idhini ya Bwana wake. Hapo wakamsubiri Hadhrat Ahmad a.s. atoke, ndipo ombi la Bwana chifu likapelekwa kwake. Yeye akawaambia: "Shughuli za Maulawii Nuruddin hapa ndizo njia za manufaa ya kimwili na ya kiroho kwa watu wengi sana; sionelei kwamba hayo yasimamishwe kwa ajili ya shabaha tupu ya kidunia."

Baniani mmoja wa Batala alimwomba amtazame mkewe mgonjwa na kumwambia afanye nini. Hadhrat Ahmad a.s. akamruhusu kwenda Batala kwa shabaha hiyo na akasema, "Natumai utarudi leo hii hii usiku." Akaenda Batala, akamchunguza mama na kamwandikia dawa fulani apewe. Wakati alipokuwa tayari kufunga safari ya kurudi kulikuwa na giza totoro na mara ikaanza kunyesha mvua kubwa. Kila mmoja akamshauri na kujaribu kumzuia asifunge safari ya hatari ya kurudi Qadian, wakati wa usiku; lakini hakukubali. Bwana wake alimtaka arudi usiku huo huo, basi hawezi kukosa kutekeleza kama alivyotazamiwa. Akajikakamua dhidi ya dhoruba kali ya mvua kubwa na kushindana na hatari zote na akarejea Qadian katika sehemu ya

mwisho ya usiku. Hadhrat Ahmad a.s. akapitisha usiku akitaharuki na baada ya sala ya alfajiri akauliza kwamba Maulawii Nuruddin amewasili salama? Maulawii Nuruddin akaja mbele na kumwarifu kwamba amekwisha rudi.

Baada ya yeye kukaa Qadian kwa mwaka mmoja, akaja mtu mmoja kutoka Jammu na kumkabidhi Maulawii Nuruddin Rupia 195,000 taslimu. Kiasi hicho hicho kabisa alikuwa anadaiwa na mdeni wa Jammu. Alipouliza fedha hizo anapewa kwa nini, mtu huyo akamweleza kwamba Maharaja aliweka sharti mwaka jana kwamba yeyote atakayepewa kandarasi kuhusu misitu ya serikali, mtu huyo atampa nusu nzima ya faida Maulawii Nurudddin. Tenda zilitakiwa kutolewa kwa sharti hilo, nami nikapewa kazi hiyo; basi nimekuletea nusu ya faida niliyopata. Maulawii Nuruddin r.a. akamwagiza kuchukua fedha hizo zote na kumlipa mdai wake huko Jammu. Mwaka uliofuata akaja tena mtu huyo na kumletea nusu ya manufaa aliyopata, lakini Maulawii Nuruddin r.a. alikataa kupokea. Huyo bwana akamsisitizia achukue fedha kwani sawa na sharti alilokubali analazimika kuzitoa, lakini Bwana Maulawii r.a. hakukubali.

“Ulipokea mwaka jana,” kasema.

“Hiyo ilikuwa fadhili ya Mungu ili niweze kulipa deni langu. Sasa sina haja hiyo.”

# IX

# MFUASI BORA HALISI

Maulawii Nuruddin r.a. alifanya baiati kwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. akimwamini yu mkweli katika madai yake ya kwamba anafunuliwa wahyi na Mwenyezi Mungu na kwamba ametumwa ili kuhuisha Islam. Cheo chake cha kuwa Masihi Aliyeahidiwa na Mahdi kiliposisitizwa katika funuo alizofunuliwa, dhoruba kali ya kumpinga ilizuka, na baadhi ya wale waliokuwa wamempokea kwa shangwe kama mtetezi mkubwa wa Islam ambaye mfano wake hamna katika miaka elfu iliyopita wakageuka kuwa wapinzani wake; wakamlaumu kwamba si mwaminio tena, na wakamkufuruisha na kumtolea matusi machafu sana. Maulawii Nuruddin r.a. akasimama imara kama mwamba kumwunga mkono na kujibidiisha kushindisha shabaha yake ambayo aliamini kwa moyo mkunjufu kwamba ndiyo shabaha ya Islam.

Upande wake Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. ambaye tangu sasa tutamtaja kuwa Masihi Aliyeahidiwa, alimheshimu sana mfuasi wake wa kwanza na akamsifu mno. Kwa mfano:

> "Tangu nitumwe na Mwenyezi Mungu na kufufuliwa na Mzima wa milele Aliye Mkwasi, nilikuwa na shauku ya kupata wasaidizi bora wa dini, na shauku yangu hiyo ilizidi kuliko tamaa ya mwenye kiu kupata maji. Nikafanya maombi mchana na usiku: 'Mola wangu, nipo peke yangu pasipo msaada, nani atakuwa msaidizi wangu, nani ataniauni? 'Mikono yangu ilipoinuka mara kwa mara kwa kuomba, na anga lilipojaa maombi yangu, Mungu Mwenyezi Akasikiliza malalamiko yangu, na rehema ya Mola wa walimwengu ikataharuki kwa ajili yangu naye Akanijalia rafiki mmoja mnyofu na mwaminifu

ambaye ndiye mboni ya wasaidizi wangu na kiini cha wale walio marafiki zangu waaminifu katika njia ya dini. Jina lake, kama zilivyo sifa zake zing'aazo, ni Nuruddin (Nuru ya Dini). Yu mzaliwa wa Bhera, na kinasaba yu Mqureishi, Hashimi, na kwa hiyo ni Mudiri mmojawapo wa Islam. Yu mwungwana. Furaha yangu nilipoonana naye ilikuwa kana kwamba mkono wangu uliokatika, nimerudishiwa. Moyo wangu ulijaa furaha kubwa jinsi alivyofurahika Mtume Mtukufu s.a.w. kwa kumpata Hadhrat Umar r.a. Aliponijia na kuonana nami, nikamtazama, nikahisi kwamba yu ishara mojawapo miongoni mwa ishara za Mola wangu. Nami nikatambua kwamba yeye ndiye matokeo ya maombi yangu niliyofululiza kuomba, na nikahisi kwamba yu mtumishi mmojawapo mteule wa Mungu. Naona maneno ya hekima yatoka midomoni mwake na mwanga wa kimbinguni wamteremkia. Anapojishughulisha na kueleza Kitabu cha Mungu, huwa anafichua machimbuko ya siri na kububujisha chemchemi za busara na kufunua hazina za hekima zilizofichikana hata sasa. Anachungua kila upande wa maarifa barabara na akichimba mpaka vyanzo hakika anafunua mianga ing'aayo. Wenye hekima humnyoshea shingo zao ikiwa alama ya kuthibitisha athari ya kimwujiza ya maongezi yake. Anafafanua ukweli kama kipande cha dhahabu ing'aayo, na anang'olea mbali upinzani wa wapinzani."

"Sifa zote njema ni za Mungu Mwenye Enzi, Aliyenijalia rafiki huyu pindi nilipomhitaji sana. Namwomba Mungu Atie baraka katika umri wake, afya yake na heshima yake. Mungu ni Shahidi wangu kwamba naona adhama isiyo ya kawaida katika maneno yake, na ninamheshimu akiwa wa mstari wa mbele kwa kufafanua mafumbo ya Kurani Tukufu na kuingia ndani kabisa ya maana yake na muradi wake. Namwona

kama yu milima miwili inayotazamana, mmoja wa ujuzi na mwingine wa hekima, nami sielewi upi waupita mwingine. Yu bustani mojawapo ya imani ing'aayo. E Mola, mteremshie baraka kutoka mbinguni, na Umlinde na fitina za maadui zake, na Uwe pamoja naye popote alipo na Umrehemu hapa duniani na huko akhera, E Mwingi wa Rehema. Amin.

Namshukuru kwa unyenyekevu Mungu Mwenye Enzi kwamba Amenijalia rafiki huyu bora mwaminifu aliye mwema na mtaalamu wa hali ya juu sana. Yu mwenye busara na akili nyingi. Anajibidiisha katika njia ya Mungu na amewapita marika zake katika kumpenda Mungu kwa uhalisi wa moyo."

"Yu mwenye kuafikiana kikamilifu nami jinsi mpwito unavyoafikiana na pumzi."

Safari moja mkewe Maulawii Abdul Karim r.a. na mkewe Maulawii Nuruddin r.a. walijadiliana; kila mmoja akakazania kwamba mumewe ndiye mpenzi zaidi wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. Wakamwomba Hadhrat Ummul Muminin r.a., mkewe Hadhrat Ahmad a.s., kuwaamulia. Mama huyu akasema hamna shida; swala hilo laweza kuamuliwa mara moja. Akamwendea Masihi Aliyeadhidiwa a.s. na akaanza kusema: "Sahaba wako mpendwa kuliko wote......" Akamkatiza na kuuliza akishtuka: "Imetokea nini kwa Maulawii Nuruddin?"

Muda fulani baada ya kufariki Maulawii Abdul Karim, Maulawii Nuruddini akapata kuugua. Masihi Aliyeahidiwa akamtembelea kila siku kumjulia hali, na safari moja akamshughulikia kumtengenezea dawa. Hadhrat Ummul Muminin r.a. akiona mahangaiko yake akasema: Maulawii Burhanuddin amekwisha fariki, Maulawii Abdul Karim naye ameaga dunia; Mungu amponye haraka Maulawii Nuruddin. Hapo Masihi Aliyeahidiwa a.s. akasema: "Huyu ni sawasawa na

Ma-Abdul Karim elfu moja."

Jambo fulani dogo lilitokea lililomwudhi Masihi Aliyeahidiwa ndipo akawasihi wafuasi wake akisema:

> "Baadhi yenu wameshuhudia ishara nyingi, hata hivyo imani yao yapungukiwa yakini. Lakini wapo wengine ambao hawakuhitaji ishara. Yupo Maulawii Nuruddin aliyeamini mara moja; na akiwa dhuria ya Hadhrat Umar r.a, akafuata mfano wa Hadhrat Abu Bakr r.a. Akisikia hayo, Maulawii Nuruddin r.a. akainuka na kusema: 'Hadhrat Umar r.a. akathibitisha imani yake kwa kusema: 'Tu radhi na Mungu kuwa Mola wetu, na Muhammad kuwa Mtume wake s.a.w.' Sikukaribisha katu shaka yoyote kuhusu madai yako. Nami pia nahakikisha: Namridhia Mungu kuwa Mola wangu, nawe kuwa Masihi na Mahdi a.s."

Masihi Aliyeahidiwa akachangamka sana mno hata kwamba uso wake ukang'aa na akaacha kuendelea kusihi zaidi.

Mpinzani mmoja wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. aliandika ya kwamba Bwana Mirza amepata Jumuiya kwa kuwapoteza Waislamu wachache; kama angelifaulu kuwasilimisha watu kadha wasiokuwa Waislamu, hapo bila shaka kungelikuwa na sababu ya kuchunguza madai yake kwa makini. Masihi Aliyeahidiwa a.s. alipojulishwa habari hii akamwagiza Maulawii Nuruddin r.a. kutayarisha orodha ya wasiokuwa Waislamu ambao walisilimishwa na Masihi Aliyeahidiwa a.s. Akitekeleza agizo hilo akaandika kwanza jina lake mwenyewe pamwe na maelezo ya habari zake. Rafiki yake mmoja alipostaajabia habari hii, akajibu: "Nina heshima ya kujifunza Islam ya kweli kwa Masihi Aliyeahidiwa a.s. tu."

Mwanajumuiya mmoja alipomwomba Masihi Aliyeahidiwa

a.s. kumshauri amwoze binti yake kwa nani? Aliposhauriwa, baba huyo akaona mashaka kuhusu shauri hilo. Maulawii Nuruddin r.a. aliposikia habari hii akasikia uchungu sana na akasema: "Kama Bwana Mirza angeniagiza kumwoza Amatul Hai (bintiye) kwa mwanaye Nihali (mwanamke topasi) nisingesita kutekeleza agizo lake."

Mtu wa kidunia mwenye busara, pasipo kuhoji uaminifu wa uhakikisho wake, anaweza kuuona uaminifu huo kuwa imani ya kijinga. Lakini imani ya Maulawii Nuruddin r.a. iliimarika kabisa katika mwamba imara wa hoja za kweli (12:109) na kwa hiyo alikuwa mwenye maarifa kamili. Hii ndiyo hadhi ya imani hiyo kwamba wanaobarikiwa na Mungu hujaliwa hisia za ufahamu zaidi ya kawaida inayowawezesha sikuzote kupambanua baina ya sahihi na isiyo sahihi, na kutambua kipi chafaa na na kipi chadhuru. Ndiyo sababu ni kweli kabisa kwamba kama Masihi Aliyeadhidiwa a.s. angelimtaka kutenda lililo sawa na kujitupa katika bahari ama moto, angelitekeleza tu bila kusita akiwa na yakini kamili kwamba lotole aliloambiwa ni la kumnufaisha tu. Hii ndiyo yalingana na mafundisho haya ya Kurani Tukufu:

> "Huenda mchukie kitu nacho ni heri kwenu, na huenda mpende kitu nacho ni shari kwenu. Na Mwenyezi Mungu Anajua, lakini ninyi hamjui." (2:217)
>
> "Huenda mchukie kitu na Mwenyezi Mungu Ametia heri nyingi ndani yake." (4:20)

Yafaa kuzingatia ya kwamba Bi Amatul Hai, bintiye Maulawii Nuruddin, alipobalehe akaolewa na Hadhrat Sahibzada Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad r.a., Mwana Aliyeahidiwa, na Khalifa wa Pili wa Masihi Aliyeahidiwa a.s.

Safari moja Maulawii Nuruddin r.a. alipokuwa anasali alisikia

Masihi Aliyeahidiwa anamwita. Akavunja sala yake na haraka kamwendea Masihi Aliyeahidiwa a.s.  Washikiliao vikali utaratibu wa sala uliowekwa, pengine waweza kupinga kitendo chake hicho, lakini tendo kama hilo la mfuasi wake mwingine alilowahi Masihi Aliyeahidiwa kuona, likapata kibali chake. Maulawii Seyyid Sarwar Shah r.a., mtaalamu mwingine mashuhuri, alipata kuchelewa kidogo kwa sala ya jamaa. Alipoingia msikitini ilhali sala ilikuwa imekwisha anza tayari, akapata nafasi upande wa kuume kabisa katika safu ya mwisho ya wasalio. Sala ilipokwisha yeye akainuka akiendelea kusali sehemu aliyokosa pamoja na jamaa. Ndugu wengine wakamsubiri Masihi Aliyeahidiwa a.s. aondoke kabla hawajatawanyika. Njia ya kuendea nyumbani kwake ilikuwa inapitia pale alipokuwa anasali Seyyid Sarwar Shah r.a., hivyo akasimama hapo. Asaliye alipohisi kwamba amemzuia njia akavunja sala yake ili kumpa nafasi ya kupita. Hapo mtu aliyekaa karibu naye akamnong'oneza: "Kwa nini umevunja sala?" Masihi Aliyeahidiwa a.s. akapata kusikia mnong'ono huo na akasema: "Maulawii Sahib amefanya sawa. Hakika mema huyaondoa maovu." (11:115).

Ilikuwa desturi ya Maulawii Nuruddin r.a. ya kwamba hata kama akishughulikia nini, apatapo tu habari Masihi Aliyeahidiwa aweza kufika, huaacha shughuli yake papo hapo, akainuka na kukimbilia kumngojea akikokota viatu vyake na kuburuta kilemba chake katika mchakato wa kukipiga kichwani.

Katika ziara mojawapo ya Masihi Aliyeahidiwa huko mjini Delhi, mkwewe Hadhrat Mir Nasir Nawab r.a. aliyekuwa mmojawapo wa waliofuatana naye akapata kuugua. Akaamua kumwita Maulawii Nuruddin r.a. kutoka Qadian kumtibu. Akaagiza apigiwe simu ya maadishi kwamba afike Delhi. Yule aliyepeleka simu hiyo akaandika tu: "Njoo mara moja." Maulawii Nuruddin r.a. alipopokea ujumbe huo

alikuwa katika kliniki yake. Papo hapo akainuka, akampelekea mkewe ujumbe kwamba ameitwa na Hudhur a.s. afike Delhi, akaondoka akielekea Batala mara moja bila kuwa na fedha yoyote mfukoni. Kwenye kituo cha gari moshi cha Batala, tajiri mmoja Baniani wa hapo akamwomba afuatane naye mpaka nyumbani kwake kwa kumtazama mkewe aliye mgonjwa. Akamjibu, yeye analazimika kupanda gari moshi liendalo Amritsar, kwani yuko safarini kuelekea Delhi, hivyo hana nafasi ya kwenda mjini. Mume mwenye kiherehere akamwomba kumleta mkewe hapo stesheni na akafanya hivyo. Maulawii Nuruddin r.a. akamchunguza na kumwandikia dawa. Mume akawa na shukurani kubwa ajabu, akaenda haraka na kumletea tiketi ya kwenda Delhi na akampa fedha nyingi kama ada yake. Keshoye asubuhi akahudhuria mbele ya Bwana wake mjini Delhi.

Yesu a.s. kuzaliwa bila baba ilikuwa ni swala la kujadiliwa. Maulawii Nuruddin r.a. alikuwa na rai ya kwamba Yesu alikuwa na baba. Masihi Aliyeahidiwa a.s. katika kitabu cake *Mawahibur Rahman* alitangaza ya kuwa ni sehemu ya imani yake kwamba Yesu alizaliwa bila baba. Maulawii Nuruddin r.a. aliposoma tu hiyo, akatupilia mbali rai yake na akawa na itikadi iliyoelezwa na Masihi Aliyeahidiwa r.a. Akakiri kubadili rai yake hiyo kwa unyofu bila kusita, katika kitabu chake Nuruddin.

Aidha, alikuwa na maoni kwamba moto uliotajwa katika sura 21:70 unamaanisha moto wa upinzani. Lakini Masihi Aliyeahidiwa a.s. alinena: "Hamna haja ya kukimbilia maana hiyo. Mimi nami nimeitwa na Mwenyezi Mungu kuwa Ibrahimu. Wale wasioweza kutambua jinsi moto ulivyopozwa kwa Ibrahimu a.s. wanakaribishwa wanitupe katika moto, wakaone natoka salama kutoka humo ama hapana. Basi Maulawii Nuruddin r.a. akiondolea mbali upinzani wa Dharampal, akaandika ndani ya Nuruddin: "Waweza kumtupa kiongozi wetu

katika moto, nawe utaona kwamba Mungu Mwenye enzi sawa na ahadi yake atamlinda na moto jinsi Alivyomlinda Ibrahimu a.s.”

Masihi Aliyeahidiwa a.s. alipofafanua kinaganaga madai yake ya kupata Unabii ulio kivuli cha Unabii wa Mtume s.a.w., mtu fulani akamwuliza Maulawii Nuruddin r.a.: “Je, baada ya Mtume Mtukufu s.a.w. nabii aweza kutokea?”

“Hapana”, akajibiwa.

“Utasemaje, basi, kumhusu yule adaiye kuwa Nabii”?

“Nitaona kama yu mtu mkweli na mwema. Kama kweli yu mkweli na mwema nitaangalia madai yake sawa na ustahili wake.”

Hivyo ndivyo alivyokuwa Nuruddin r.a., na ndiyo maana Masihi Aliyeahidiwa akamteua kutoa mfano wake katika ubeti wake wa kiajemi:

> Ingekuwa vizuri sana kama kila mmoja wa umati ungekuwa Nuruddin,
>
> Na hiyo itakuwa kama kila moyo utajaa mwanga wa yakini katika imani.

## X

## MTAALAMU MTUKUFU

Maulawii Nuruddin r.a. alijulikana kuwa mganga mashuhuri wa zama zake. Katika utambuzi wa maradhi kulikuwa hakuna aliye sawa naye. Uchunguzi wake aliofanya papo hapo bila matayarisho yoyote, ulitokea kuwa sawa kila mara. Hakubagua wagonjwa wake; tajiri na maskini walipokea huduma kwa usawa pamoja na maombi yake kwa moyo mkunjufu. Usiku mmoja alifikiwa na mtu aliyefadhaika kwa sababu ya mkewe aliyekuwa na uchungu mkali sana wa kuzaa. Alikuwa na wasiwasi kwamba atakufa usiku huo. Maulawii Nuruddin r.a. akampatia dawa na kumwagiza namna ya kumtibu. Kasema ataendelea kumwombea mama huyo, na kwamba aendelee kuarifiwa kuhusu hali yake. Usiku kucha hakupata habari yoyote. Asubuhi mapema alipomwita kuleta habari ya mkewe, mume akaja akifurahi na kuchangamka na kamwambia kwamba mkewe alijifungua salama katika muda wa saa moja baada ya yeye kurudi na akalala vizuri usiku.

"Kwa nini hukunipasha habari?"

"Bwana, kwa kuwa kulikuwa hamna wasiwasi tena, nikaonelea hamna haja ya kukusumbua wakati wa usiku."

"Kunisumbua! Je, wajua kwamba ninyi nyote mlipolala vizuri usiku, Nuruddin alikesha kucha akiomba kwa unyenyekevu bila kupata usingizi hata kidogo?"

Safari moja alipokuwa mjini Lahore, aliitwa kutoa shauri kumhusu mama mmoja wa Kibaniani wa ukoo wenye heshima aliyesimama pamoja na wanawake wengi waliokuwa wanamwomboleza jamaa mmoja aliyefariki, mama huyo katika hali ya

huzuni kali kabisa akainua juu mikono yake mara kwa mara. Akaiinua mara moja kwa kupita kiasi. Matokeo yake ni kwamba mikono yake ikawa migumu isiweze kushushwa chini. Madaktari wakashindwa wasiweze kutafuta mbinu za kuilegeza misuli ya mikono yake hadi ishuke chini. Alipojulishwa kuhusu hali yake hiyo, yeye pasipo kutaka kumwona na pasipo kutaka kuingia katika chumba kile kikubwa alimosimama bila kutikisika, akashauri kwamba kijana mmoja mzuri sana wa sura na umbo wa sehemu za jirani, aletwe. Alipokwisha wasili, akamwambia kuingia katika chumba hicho na kumwendea mama huyo na ajifanye kana kwamba anataka kuvua nguo zake huyo mama. Kijana akatekeleza sawasawa alivyoagizwa. Mama huyo alipotambua shabaha yake, akatoa kilio kwa sababu ya wasiwasi na papo hapo mikono ikashuka chini. Kishindo hicho kikashtua mfumo wa neva nao ukaanza kufanya kazi kama kawaida.

Lakini yeye hakuwa tu na ujuzi wa tiba za kimwili na kiakili; bali alishughulika kwa bidii nyingi katika tiba ya kiroho. Alijitolea kutaali kuponya roho. Kwa muradi huo kitabu chake cha sayansi ya sifa za dawa, kitabu chake zilimoorodheshwa dawa za maradhi na kitabu chake cha maelezo kumhusu yeye alichokuwa nacho wakati wote kilikuwa ni Kurani Tukufu. Akaikumbuka nzima kwa ghaibu na maana zake za ndani akazijua sana. Hakuacha nafasi yoyote ya kufafanua kinaganaga hazina zisizomalizika za hekima zilizomo humo. Akadumu kuifundisha mpaka dakika ya mwisho ya uhai wake. Alizoea kusema:

> "Kurani ni riziki yangu na ndiyo kiburudisho cha roho yangu. Naisoma mara nyingi kila siku, lakini roho yangu haikinai. Hiyo ni ponyo, ni rehema, ni mwanga, ni mwongozo."

Alipoulizwa namna ambavyo Kurani isomwe, akajibu:

> "Kurani ni kitabu kilicho rahisi sana kabisa duniani kusoma

kwa anayependa hasa kuisoma. Sharti la kwanza na muhimu zaidi kuitaali ni wema. Mungu Ameahidi kwamba Atamfundisha Kurani yule aliye mwema. Mwanafunzi wa Kurani anahitaji faragha na kwamba asiwe na wasiwasi kuhusu kujichumia riziki. Kama akifuata njia za wema, Mungu Humruzuku kutoka katika mahali asipotazamia na Mwenyewe anakuwa Msimamizi wake.

"Sharti la pili la kutaali Kurani ni kujitahidi ipasavyo kwa kujitolea kwa Mungu kikamilifu, hapo Mungu Ameahidi kutatua matatizo yote.

"Nija ya kusoma Kurani ni kuwa mwanafunzi kwanza aisome tangu mwanzo hadi mwisho kana kwamba inafunuliwa kwake na kila aya inamhusu yeye. Kwa mfano, pale anapotajwa Adamu a.s. na Iblisi, yeye ajichunguze hapo kwamba yu Adam ama Iblisi, na kadhalika afanye kwa kila aya. Popote akabilipo mushkili apazingatie. Na akisoma mara ya pili awaingize mkewe na watoto wake pia. Ataona kwamba matatizo yake mengi yatatatuliwa. Asomapo mara ya tatu awaingize marafiki zake pia. Mara ya nne asome akipanua eneo lake. Anapaswa kudumu kuomba ili matatizo yake yatatuliwe."

Mafafanusi yake ya Kurani yalikuwa bora kabisa. Alialikwa kuhutubia Mkutano wa Mwaka wa *Anjuman Himayati Islam* mjini Lahore mnamo mwaka 1893. Akachagua aya hii kwa mazungumzo yake:

"Mwenyezi Mungu ni nuru ya mbingu na ardhi; mfano wa nuru Yake ni kama kishubaka kilichomo taa: taa ile imo katika tungi: tungi lile ni kama nyota ing'aayo, inayowashwa katika mti uliobarikiwa wa mzeituni, usio wa mashariki wala wa magharibi; ni karibu mafuta yake kung'aa ingawa moto haujayagusa – nuru juu nuru – Mwenyezi Mungu

Humwongoza kwenye nuru yake Amtakaye. (24:36)"

Akaanza kueleza:

"Baadhi ya wasikilizaji hujilazimisha kufuata desturi za kimashariki, na baadhi ya vijana ndio husifu utamaduni wa kimagharibi. Ninalopenda kulieleza – kwa maneno ya Kurani Tukufu – si la kimashariki wala si la kimagharibi. Kurani Tukufu yatoa nafasi kwa watu wote kustawi."

Kisha akaendelea kufafanua kiini cha habari kulingana na aya aliyosoma kabla na akawashangaza wasikilizaji hadi mwisho wa maongezi.

Miongoni mwa waliohudhuria maongezi hayo alikuwepo mbashiri wa Islam pia aliyejulikana sana, Maulawii Hasan Ali wa Bhagalpur katika Bihar. Yeye aliandika kumbukumbu kuhusu maoni yake juu ya hotuba hiyo kama ifuatavyo:

"Mnamo 1893 nilipata nafasi ya kuhudhuria Mkutano wa Mwaka wa *Anjuman Himayati Islam*, ambako nilikutana na mfasiri wa Kurani mwenye ujuzi wa hali ya juu sana, Maulawii Hakim Nuruddin, ambaye hana mwenzake, si katika India tu bali katika eneo kubwa zaidi. Nilipata kusikia sifa zake kubwa katika ziara yangu ya Panjab mnamo 1887 pia. Katika Mkutano huo yeye alisoma baadhi ya aya za Kurani na akaanza kutoa maelezo yake. Nashindwa kujieleza, sipati maneno ya kufafanua jinsi nilivyoathirika sana mno na maongezi yake. Alipomaliza, nikainuka na kusema: 'Naona fahari kwamba macho yangu yamepata kumwona mtaalamu mkubwa na mjuzi wa hali ya juu wa maelezo ya Kurani. Na Waislamu wanapaswa kuona fahari kwamba kati yao yupo mtu mwenye elimu nyingi ajabu.'

"Nilikuwa na shauku ya kuonana na Maulawii Hakim Nuruddin, lakini akanipa heshima kufika hapa na kuonana nami. Katika maongezi yetu nikamwuliza: 'Umefanya baiati ya Hadhart Mirza Sahib, je, waweza kuniambia umefaidikaje na baiati yake?' Akajibu: Nilijaribu kuepukana na dhambi, lakini nikashindwa kufaulu. Lakini baada ya kufanya baiati ya Hadhrat Mirza Sahib a.s., si tu kwamba nikaepukana na dhambi, bali naichukia sasa.'"

"Kama angelinieleza baadhi ya miujiza ya Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad, pengine nisingeliitia sana maanani, lakini niliathirika mno na yale aliyoniambia."

Baadaye Maulawii Hasan Ali alitembelea Qadian, akaonana na Masihi Aliyeahidiwa a.s., akakaa naye kwa muda fulani na akajiunga naye. Akajithibitisha kuwa mwanajumuiya wa Kiahmadiyya mwaminifu na mwenye kujitolea sana. Idadi kubwa ya watu walijiunga katika Ahmadiyya kwa sababu ya mawaidha yake.

Safari moja mnamo Februari 1901 alipokuwa anapitia Lahore, Maulawii Nuruddin r.a. akaombwa kuhutubia hafla ya watu wengi sana. Akaongea juu ya kuwepo kwa Mungu sawa na kanuni zilizowekwa ndani ya Kurani Tukufu. Mwahmadiyya mmoja alimleta mtu mmoja Bwana Jalaluddin pamoja naye ili kusikiliza hotuba hiyo. Bwana huyo alikuwa karani katika ofisi za Relwe na alikuwa daharia mgumu, asiyemwamini Mungu. Hotuba ilikwisha saa 7:30 adhuhuri, wasikilizaji wakaondoka. Keshoye jioni akirudi kutoka ofisini Bwana Jalaluddin akakiri mbele ya rafikiye kwamba baada ya kusikiliza hotuba ya Maulawii Nuruddin r.a. alitubu na sasa anamwamini Mungu kwa unyofu sana. Akawa na yakini kwamba hakuna awezaye kuvunja hoja zake.

Mnamo Juni 1902, Baniani mmoja akaja Qadian na akasilimu. Masihi Aliyeahidiwa a.s. akamwagiza Maulawii Nuruddin kumfundisha mafundisho ya Kiislamu. Haya ndiyo aliyomwambia:

> "Islam yamaanisha mambo matatu. Kwanza, kumwamini Mwumbaji Anayetawala kila kitu na kukisimamia ni Mmoja. Hakuna minghairi Yake, ambaye mtu anapaswa kusujudia mbele Yake au kufunga saumu kwa ajili Yake au kumchinja mnyama kwa jina Lake (kwani yu pekee ndiye Bwana wa viumbe wenye uhai) au kufanya mzunguko kwa yeyote mwingine. Hofu yote na matumaini yote yapaswa kuwa kwa ajili Yake. Hii ndiyo maana ya: Hakuna Mungu minghairi ya Allah. Tabu zote, raha zote na kutimiza haja zote ziko chini ya amri Yake. Maombi yote yapaswa Aombwe Yeye. Kuamini hayo yote kwa unyofu ndiyo kuwa Mwislamu. Na kwa hilo hakuna haja ya sherehe ama ubatizo wowote.
>
> Hatua ya pili ni kumwamini Muhammad s.a.w. kuwa Nabii na Mtume wa Mungu. Alitumwa duniani kutangaza adhama na utukufu na sifa njema za Mungu, na kuwafundisha watu hizo. Hivyo, kitu cha pili cha muhimu cha Islam ni: Muhammad s.a.w. ni Mjumbe wa Mungu.
>
> Kitu cha tatu cha msingi wa Islam ni kuendeleza mbele ustawi wa viumbe vyote vya Mungu.
>
> Aidha, Mwislamu anapaswa kuwaamini Malaika, Mitume wote na Vitabu vyote vya Mungu, na kwamba kuna malipo ya kila tendo. Hilo la mwisho ni Uamuzi.
>
> Hayo ndiyo mambo ya kuaminiwa. Pia hakuna budi Mwislamu kusali, kufunga saumu ya Ramadhani, kutoa zaka ili kuinua hali ya maskini na mwenye mahitaji, kwenda

Makkah kuhiji akiweza.

Kwa ufupi, Islam humaanisha imani nyofu; aaminiye kwa unyofu na kutenda kuthibitisha imani yake ndiye Mwislamu. Basi watakiwa kuamimi kwa moyo mweupe: Hakuna apasaye kuabudiwa isipokuwa Allah, na Muhammad s.a.w. ni Mjumbe Wake. Hakuna haja ya sherehe yoyote. Naam, wapaswa kuoga ili uweze kuomba: Allah, nasafisha mwili wangu; Wewe Usafishe roho yangu. Pia badilisha nguo zako kama alama kwamba umeondosha uzembe."

Masihi Aliyeahidiwa akampatia kijana huyo jina Abdullah. Yeye akatumikia kwa bidii kwa miaka mingi katika Nur Hospital na akawa akijulikana kama Daktari Abdullah. Akaweka mfano bora wa kuishi maisha ya kiutawa na akapendwa na watu wote.

Sawa na agizo la Masihi Aliyeahidiwa a.s. maelezo mafupi ya sura 103 (Al-'Asr) ya Kurani Tukufu yaliyotolewa na Maulawii Nuruddin r.a. yalinaswa mnamo Oktoba 1902 katika sahani ya fonografi (aina ya santuri ya zama hizo) ambayo ndiyo yafuatayo:

"Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu. Naapa kwa alasiri, kwa hakika mtu yumo hasarani, isipokuwa wale walioamini na wakafanya vitendo vizuri, na wakausiana (kushika) haki na wakausiana (kushika) subira (103:1-4). Katika sura hii fupi Allah, Mwenye enzi, Mola wa walimwengu, Mwingi wa Rehema, Mwingi wa Ukarimu, Mmiliki wa siku ya malipo, Amefafanua kwa hisani Yake njia mbalimbali za kupata ukaribu Wake, kupata utulivu, kupata sifa njema na kupata maendeleo. Kwanza Amedokeza kwamba zama za ujaji wa Mjumbe wa Mungu, na zama za ufahamu mkamilifu wa mtu na tajiriba zifaazo, ni kama sehemu ya mwisho ya mchana ambapo jua hufifia. Kwa kuwa

baada ya wakati huo haibaki nafasi ya sala ya pamoja iliyo chanzo cha kunyanyuka kiroho kwa mwaminio na kumkurubia Mungu na ndiyo nafasi ya kufanya maombi, hivyo baada ya zama za Mjumbe wa Mungu ambazo ndizo zama za utambuzi kamili wa mtu na tajiriba zifaazo haibaki nafasi kwa mtu kuondoa hasara yake na mapungufu yake. Kwa hiyo, katika zama za Mjumbe wa Mungu, ambapo mtu hujaaliwa ufahamu mkamilifu, yeye mtu huyo anapaswa kujishughulisha ili (a) Kujipatia elimu ya kweli na sahihi na itikadi katika kuwepo kwa Mungu, umoja Wake, kuwa Kwake wa pekee, Ambaye Hana mshirika katika sifa Zake na utukufu Wake; akitekeleza mashauri mema ya Malaika wa Mungu, akiwa na imani katika Vitabu vya Mungu, Mitume Wake, uamuzi Wake na kanuni Zake nyinginezo; (b) Atekeleze kwa uaminifu kabisa kanuni hizo; (c) Adumu hadi pumzi yake ya mwisho kueneza Ukweli na (d) Ajibidiishe kuwashawishi wengine kutekeleza kanuni hizo zote ili awe imara kuepukana na maovu na kufungamana na wema."

Mgeni mmoja aliyefika Qadian mnamo February 1903, alieleza maoni yake hivi:

"Mwenzangu na mimi tuliwasili Qadian kama saa za sala ya adhuhuri. Tulielekezwa kwenye Masjid Aqsa. Baada ya sala waabudu wakajipanga katika duara, Kurani Tukufu mikononi, ili kusikiliza darasa litolewalo na mtu mashuhuri mheshimiwa wa sura. Akaanzia kwa kusoma sehemu ya Kitabu Kitukufu kwa namna iliyowavutia wasikilizaji wake na kuwaathiri sana. Kisha akaanza kutoa maelezo ya aya alizokuwa amesoma na kufafanua falsafa na hekima iliyofundishwa humo. Nilikuwa sijawahi kusikiliza mfano wake hapo kabla. Moyo wangu

> ukaathirikia sana, nami nikamwuliza aliyekaa karibu, 'Je, huyu ndiye Masihi Aliyeahidiwa?' Akasema: 'La, huyu ndiye Maulawii Nuruddin'. Nikashikwa na mshangao. Kama huyu asiye na kifani ndiye mwanafunzi tu, basi mwalimu wake aliye mtukufu na mkubwa zaidi, atakuwaje?"

Mhariri wa *Badr,* mtaalamu mashuhuri, akiwa na haki akatoa maoni yake kuhusu darasa la kila siku la Kurani Tukufu litolewalo na Maulawii Nuruddin r.a. hivi:

> "Hakuanza kutoa darasa katika Qadian tu. Aliendelea kuitumikia Kurani Tukufu kwa njia hiyo tangu kitambo kirefu. Nilikuwa kijana nilipoanza kuhudhuria katika darasa lake la Kurani Tukufu huko Jammu na pia Kashmir. Ni darasa lake hilo lililonifanya Mwislamu wa kweli, na ndilo darasa lililonifanya baadaye Mwahmadiyya. Nimelikuta lenye kufaa kiasi hiki hata kwamba baada ya kulihudhuria kila siku kwa miaka mingi, bado nanufaika nalo upya kila siku. Katika darasa lake tu nimegundua sifa ambayo kutoka hiyo vijana, watu wa makamu na wazee wanafaidika sawa na uwezo wao. Asiye na ujuzi anajipatia elimu kiasi fulani, na mwenye elimu anajiongezea elimu kulisikiliza. Miongoni mwa baraka nyingi wanaopata wale walioshika Qadian kuwa makazi yao, baraka mojawapo ni darasa hili. Mungu naye Alidumishe ili nasi tuendelee kupata baraka na rehema kutokana nalo."

Maulawii Nuruddin r.a. mara nyingi alisema, kama Mungu angeniuliza ni kitu gani nikipendacho sana, ningemwomba kupatiwa Kurani.

Babake mwandishi wa kitabu hiki alikumbuka Kurani nzima kwa ghaibu mnamo miaka ya mwisho ya kazi yake ya uwakili. Alipomweleza Maulawii Nuruddin r.a. habari hii, akafurahi sana na

akawaambia waliokuwapo: "Bwana Nasrullah Khan anampenda sana Nuruddin hata kwamba kwa kujipatia mapenzi yake amekikumbuka kwa ghaibu kitu anachokipenda sana Nuruddin, na akajihakikishia kujinyakulia upendo wake."

Hafidh Raoshan Ali r.a., mwanfunzi wake mmojawapo ameeleza:

> "Nilipokuwa naikumbuka kwa ghaibu Kurani Tukufu huko Wazirabad, chini ya usimamizi wa babangu mdogo Hafidh Ghulam Rasul, nikaota usiku mmoja kwamba mtu mmoja mtukufu amenipa kikombe kilichojaa maziwa na akasema: 'Kunywa haya.' Nikanywa sehemu yake kubwa, naye akasema: 'Kunywa zaidi.' Nikanywa zaidi. Sikuzingatia muradi wake wakati huo, lakini nilipofika Qadian nikatambua kwamba huyo mtukufu niliyemwona ndotoni alikuwa Maulawii Nuruddin r.a. Wakati mwingi nilikaa naye usiku nikijifunza kwake, lakini yeye hakuchoka kabisa."

Miongoni mwa waliohudhuria darasa lake la Kurani Tukufu kila siku, baadhi yao waliandika muhtasari wa maelezo na katika hayo yakachapishwa madondoo yake, lakini yeye mwenyewe hakuchapisha maelezo yake ya Kurani. Sababu aliyotoa ni hii:

> "Kurani Tukufu ni Neno la Mungu; jinsi Mungu Asivyo na mwisho, ndivyo lilivyo Neno Lake. Hivyo hatuwezi kuyawekea mipaka maelezo yake kwamba ni hayo tu basi. Kaongeza, Kurani Tukufu ikiwa Neno la Mungu, ilitazamiwa kwamba Mungu Mwenyewe Angeliieleza, lakini Hakufanya hivyo; wala Mtume Mtukufu s.a.w. hakuchukua jukumu hili. Baada yake, Makhalifa waliomfuata wangeliweza kufanya hivyo, lakini hawakufanya. Hata mmojawapo miongoni mwa maimamu watukufu wa Fik'hi, Abu Hanifa, Malik, Shafii

na Ahmad bin Hambal, hawakuandika maelezo ya Kurani Tukufu, ingawa huyo wa kwanza hakuishi katika zama zilizo mbali sana na zama za uhai wa Mtume Mtukufu s.a.w., na akapata kuonana na baadhi ya Masahaba zake. Miongoni mwa wakusanyaji wa Hadithi za Mtume s.a.w., *Bukhari, Tirmidhi*, na *Abu Dawud* walikuwa watu mashuhuri watukufu, lakini hata mmoja wao hakuandika maelezo ya Kurani Tukufu. Miongoni mwa masufii, Muinuddin Chishti rh., Shah Nakshbandi rh., Seyyid Abdul Qadir Jilani rh. na wengeneo walikuwa watu wakubwa waliojaliwa ujuzi wa ndani na wa dhahiri, hata hivyo hawakuandika maelezo ya Kurani. Shihabuddin Suharwardi rh. akaandika maelezo, lakini hayana lolote jipya.

"Masihi Aliyeahidiwa a.s. aliyetumwa kuhudumia Kurani Tukufu hakutoa tafsiri au maelezo ya Kurani Tukufu. Watu wamefaidika na baadhi ya tafsiri na maelezo ya Kurani Tukufu yaliyochapishwa na kuenezwa, lakini wengi huelekea kuyachukua ni ya mwisho na kwa kuyategemea hayo hukoma kufikiria wenyewe, jambo ambalo huleta hasara kubwa.

"Niliandika maelezo, na marafiki zangu wakasisitiza kwamba niyachapishe. Kisha nikafikiria kwamba watakaokuja nyuma yangu pengine watafikiria kwamba hayo ni ya mwisho kabisa na watajifungia mlango wa kujielimisha kwa kweli zile za Kurani Tukufu na hekima zake. Hiki ni Kitabu cha Mungu, kinatatua matatizo ya kila zama na ni tiba kwa magonjwa ya roho katika kila hali. Manufaa yake yasiwekewe mipaka. Hivyo nikaachilia mbali kujaribu kutia bahari isiyo na mipaka ndani ya mtungi."

Kiu yake ya kujiongezea elimu haikuwa ya kuzimika. Alijitengenezea maktaba kubwa iliyo na vitabu vingi vya muhimu vinavyopatikana

kwa nadra ambavyo alivikusanya kutoka mahali pa mbali na karibu kwa sura ya miswada ama akavinukuu. Safari moja yeye alimtuma mwanafunzi mmojawapo, Maulawii Ghulam Nabii, aende Bhopal kunukuu *Shaukani,* maelezo ya Kurani Tukufu, ambacho kilihifadhiwa katika maktaba ya Nurul Hasan Khan, mwanaye Nawab Siddik Hasan Khan. Hicho kilikuwa na majalada sita na kazi hiyo ya kunukuu ilichukua muda wa mwaka mzima.

Aliporejea kutoka Bhopal, akaambiwa kuondoka kwenda Misri na kunukulu kitabu cha Imam Ibni Qayyim rh. kiitwacho *Shifa-ul-'Alil Fi Masa'ilil Kadhai Wal-Kadri Watta'lil,* kutoka kwenye maktaba za Chuo cha Al-Azhar na Serikali ya Misri. Kilikuwa na kurasa 800 na kazi ya kukinukulu ikamshughulisha Maulawii Ghulam Nabii kwa miezi kumi na minane. Kitabu kingine tena alichonakili ni cha Imam Suyuti, *Ham'ul Hawami' Fi Sharhi Jam'il Jawami',* chenye kurasa 700.

Mtaala wa Maulawii Nuruddin r.a. ulikuwa mpana sana. Aliwahi kusoma vitabu vyote vya Shakespeare kwa Kiarabu.

Mimi mwandishi nakumbuka hotuba ya Jaji Bwana Shah Din, Jaji wa Mahakama kuu ya Panjab, aliyoitoa huko Abbotabad juu ya elimu, mnamo Septemba 1910, ambayo alimalizia kusema. "Sawa na msingi nilioweka mbele yenu mtu wa pekee miongoni mwa marafiki zangu wengi na wale ninaojuana nao, ni Maulawii Nuruddin wa Qadian aliyeelimika sawasawa kabisa."

Nawab wa Bahawalpur alipata kuugua katika Agosti 1894, na akashauriwa na mwalimu wake wa dini, Khwaja Ghulam Farid wa Chachran, kumwita Maulawii Nuruddin kutoka Qadian. Bwana Nawab akamwandikia Masihi Aliyeahidiwa akimwomba kumtuma Maulawii Nuruddin afike Bhahawalpur kwa siku chache ili kumchunguza na kumtibu. Basi akaenda na baada ya kumtibu Bwana Nawab, ilivyopasa

akawa tayari kurejea Qadian. Hapo Bwana Khwaja Ghulam Farid kwa njia ya simu ya maandishi akapata ruhusa kutoka kwa Masihi Aliyeahidiwa kwamba Maulawii Nuruddin akawie zaidi kidogo huko Bhahawalpur. Akamwambia Maulawii Nuruddin r.a. kwamba shabaha hasa ya kumwita ilikuwa kwamba nijuane nawe na nisikilize maelezo yako ya Kurani Tukufu; ugonjwa wa Bwana Nawab ulitupatia nafasi hiyo. Na maadamu upo hapa Bhahawalpur, tuna shauku ya kujifunza kwako Kurani Tukufu. Ndipo Maulawii Nuruddin r.a. akaanzisha kozi ya masomo ya Kurani Tukufu huko Bhahawalpur. Muda wake wa kukaa huko ulipokurubia kwisha, Khwaja Ghulam Farid akamshauri Bwana Nawab amshawishi kukaa Bhahawalpur kwa kudumu. Bwana Nawab akamwendea kumshauri, ingawaje matokeo yalitazamiwa ya kuchukiza, hata hivyo kwa kumhakikishia ubovu wa shauri lake, akamwuliza Bwana Nawab: "Kama nikikubali shauri lako, kutakuwa na mpango gani kwa posho yangu?"

"Nitakupa eka elfu sitini za ardhi inayolimika."

"Nitaifanyaje hiyo?"

"Waweza kuistawisha ukawa tajiri sana."

"Nilivyo wakati huu, wewe huja kwangu kupata nasaha na mwongozo. Nikiwa tajiri sana, je, utanijia hata hivyo?"

"La, hasha!"

"Basi, nimenufaikaje?"

Bwana Nawab hakuwa na habari ya utawala wa khulka ulioratibisha maisha yake.

Mnamo 1896, Nawab Muhammad Ali Khan r.a. alimwandikia Masihi Aliyeahidiwa a.s. kwamba ana shauku ya kujifunza Kurani Tukufu, na akamwomba amtume Maulawii Nuruddin r.a. kufika

Malir Kotla na kumfundisha Kurani Tukufu. Akiagizwa na Masihi Aliyeahidiwa a.s. akaenda Malir Kotla na kukaa huko kwa miezi mingi. Kwanza alipewa makazi mjini, na baadaye akahama kwenda kukaa nyumbani mwa Mheshimiwa Nawab katika Shairwani Kut. Bwana Nawab kila siku akahudhuria mbele yake kujifunza Kurani na akala naye chakula cha mchana. Baadhi ya wanafunzi wake kutoka Qadian wakamfuata na kufika Shairwani Kut. Bwana Nawab akawafanyia mpango wa makazi yao na chakula chao. Masomo yake ya Kurani Tukufu yakakamilika katika miezi sita.

Siku hizo, huko kulikuwa na dakatari mmoja jina lake Bhagat Ram Sahni, aliyekuwa mtu wa Bhera na alipata kufanya kazi huko Kashmir. Yeye alikuwa anamheshimu sana Maulawii Nuruddin r.a., na alimtembelea mara kwa mara. Siku moja dakatari huyo alimweleza kwamba yeye anapata Rupia elfu moja kila mwezi bila ya kwenda nje ya Malir Kotla. Maulawii Nuruddin akasema hata yeye naye anapata kiasi hicho pasipo kwenda popote.

Wakati mwingine akamwandikia Nawab Muhammad Ali Khan katika barua yake:

> «Zingatia vizuri aya hizi za Kurani Tukufu: Yule aliye mwangalifu kutekeleza wajibu wake Aliomwajibikia Mungu, Mungu Humtengenezea njia ya kujiokoa katika shida zake, na Humpa riziki kwa mahali asipotazamia (65:3-4). Mimi mwenye dhambi si mwangalifu sana, hata hivyo Mungu Ananiruzuku kwa mahali nisipotazamia. Katika muda niliokaa Malir Kotla nilitakiwa kutimiza haja zangu nyingi ambazo zilihitaji Rupia elfu mbili mia tano takriban. Huwezi kukisia toka wapi ikaja sehemu yake kubwa. Mungu pekee Anajua mahali zilipokuja hizo fedha. Hata mke wangu hajui."

Yeye mwenyewe hakutaka kuingia katika mjadala na mtu yeyote, lakini

alipolazimika akamwomba Mungu msaada na wongofu na kila mara akaongozwa barabara. Pindi alipokuwa matembezini Lahore, wakili mmoja Baniani akaja kuonana naye, ambaye alikuwa amekwisha waambia marafiki zake kwamba atamhangaisha Maulawii Nuruddin r.a. katika mjadala kuhusu imani ya Kibaniani kwamba mtu afapo, roho yake huingia katika mwili mwingine. Hoja yake ilikuwa ya kwamba hali tofauti za watu mbalimbali, utajiri na umaskini, neema na shida, cheo kikubwa na unyonge, siha na ugonjwa na kadhalika, zaweza kuelezwa kwa njia hii tu ya kwamba mienendo ya mtu katika kipindi cha kuishi kwake humfanya azaliwe mara ya pili katika hali fulani, na kwamba Mungu hana nguvu katika habari hii. Kabla hajaanza mazungumzo, Maulawii Nuruddin r.a. akatoa rupia mbili za fedha toka mfukoni mwake na akiziweka mbele ya wakili akamtaka achukue mojawapo katika hizo mbili. Wakili akakaa kimya akizifikiria hizo sarafu na hakufanya lolote kwa nusu saa hivi. Waliokuwapo wakashangaa kwa kukaa kwake kimya, na mmoja wao akamwuliza wakili ni kitu gani kilichomzuia asiichukue sarafu mojawapo?

Akajibu: “Sina budi kuchagua mojawapo. Pindi nichukuapo sarafu moja katika hizi, naweza kuulizwa sababu ya kuipendelea kuliko ile nyingine. Hapo nitalikabili tatizo kwamba kama ninao uhuru wa kutumia hiari yangu, je, Mungu Hana hiari ya kuumba wanadamu katika hali mbalimbali zinazotofautiana sana? Hivi sasa siwezi kufikiria jawabu. Nitarudi baada ya kupata nafasi ya kufikiria zaidi.”

Hakurejea tena.

Mkristo mmoja Mzungu aliyejitetea akijikuta ametiwa mashakani kuhusu imani ya Utatu akatafuta kuepa kwa kusema kwa uthabiti na dharau ya kwamba akili ya Ki-Asia haina uwezo wa kufahamu siri ya Utatu, na akachochea kutolewa jawabu kali: “Ala!

Hiyo yatoboa. Ndiyo maana Yesu, Petro na Paulo, wote watatu walio Wa-Asia, pia hawakuufahamu!"

Mhubiri mmoja Mkristo akampa Maulawii Nuruddin r.a. zawadi ya kitabu chake *'Quran Dispensable*,' na akamwambia akisome kwa uangalifu. Madhumuni yake ilikuwa kwamba Kurani Tukufu si Neno la Mungu, bali ni mkusanyiko wa itikadi na mafundisho kwa Kiarabu yaliyochukuliwa kutoka katika vitabu vilivyofunuliwa zamani kama vile *Torati, Injili, Maveda, Zand, Avita* na kadhalika. Mwandishi akachagua aya kadha za Kurani Tukufu na kujaribu kuonyesha kwamba kila moja katika hizo imechukuliwa kutoka katika kitabu miongoni mwa vitabu hivyo. Mheshimiwa Maulawii Sahib hakuchukuwa muda mwingi kukisoma na akakirudisha kwa mwandishi akieleza maoni yake haya yafuatayo:

> "Nakushukuru kunipatia nafasi ya kukisoma kitabu chako. Kukisoma hicho kumeimarisha zaidi imani yangu na kutia nguvu katika itikadi yangu kwamba Kurani Tukufu kweli ni Neno la Mungu. Kujipatia na kuvisoma vitabu hivyo mbalimbali katika lugha tofauti kama vile *Kisanskrit, Kiajemi, Kiebrania, Kiarami, Kipali* na kadhalika, (yasemekana kutaali Ma-Veda pekee kunahitaji miaka arobaini) na kuyalinganisha maandiko hayo na kuyapanga lilikuwa ni jambo lililo zaidi ya uwezo na njia za Mwarabu mmoja asiyejua kusoma na kuandika aliyeishi mwanzoni mwa karne ya saba ya kalenda ya Kikristo. Aidha, ni Kurani Tukufu pekee inayoeleza hekima za kanuni hizo kubwa na kupatanisha baina ya hoja za kiakili na kanuni zinazofanya kazi ulimwenguni. Kabla haijaja Kurani Tukufu, wafalme na watwala walikuwa wanatumia nguvu kuwalazimisha watu kukubali maoni yao ya kidini na itikadi zao; viongozi wa dini hawakuruhusu kuhoji maelezo yao ya

> matatizo ya kidini; waalimu wa dini hawakuvumilia uhuru wa wanafunzi wao. Kurani Tukufu ikatangaza zama za uhuru wa kutumia akili ikisihi: Mbona hamtumii akili; mbona hamtumii ubongo; kwa nini hamtafakari katika Kurani?"

Mzee mmoja mjuzi wa elimu ya falsafa aliyependa kufafanua kila kitu alizoea kumwuliza kila mmoja kutoa ufafanuzi wa hiki au kile. Kisha akachambua aliyoambiwa na kutoa makosa yake, na kwa njia hii akajikuza mbele ya watu kwamba ana ujuzi mwingi sana. Safari moja bwana huyo akamwuliza Maulawii Nuruddin r.a.: "Hekima ni nini?" Akajibu: "Hekima ndiyo kuepukana na uovu wa kila namna, kuanzia kumshirikisha Mungu na chochote hadi ufidhuli." Mjuzi huyo wa falsafa akashikwa na butaa kwa hilo jawabu na akauliza: "Una ushahidi gani juu yake?" Maulawii Nuruddin r.a. akaelekea kwa mtu mmoja aliyekuwa amekumbuka Kurani nzima kwa ghaibu ambaye alikuwapo hapo, na kumwambia: Tafadhali soma na tafsiri fungu la tatu na nne la sura ya 17 ya Kurani Tukufu, naye akafanya hivyo. Tafsiri yake ni kama hivi.

> "Na Mola wako Ameagiza kuwa msimwabudu yeyote ila Yeye tu, na kufanya wema kwa wazazi; kama mmoja wao akifikia uzee pamoja nawe, au wote wawili, basi usiwaambie hata Akh! wala usiwakemee na useme nao kwa masemo ya heshima. Na uwainikie bawa la unyenyekevu kwa huruma. Na useme: Mola wangu, Uwarehemu kama walivyonilea katika utoto. Mola wenu Anajua sana yaliyomo mioyoni mwenu; kama mkiwa wema, basi hakika Yeye ndiye Mwenye kughofiria waelekeao. Na umpe ndugu haki yake, na maskini na msafiri, wala usitapanye (mali yako) kwa ubadhirifu. Hakika wabadhirifu ni ndugu za mashetani; na shetani ndiye asiyemshukuru Mola wake. Na kama unatengana nao kwa

kutafuta rehema ya Mola wako unayoitumai, basi sema nao kwa maneno laini. Wala usifanye mkono wako ufungiwe shingoni mwako. Wala usiukunjue mkunjuo wa kabisa, usije ukakaa hali ya kulaumiwa na kufilisika. Hakika Mola wako Humkunjulia riziki Amtakaye na Hudhikisha. Hakika Yeye kwa watumishi wake ni Mwenye habari, Aonaye. Wala msiwaue watoto wenu kwa kuogopa umaskini. Sisi ndio Tunaowaruzuku wao na nyinyi pia. Kwa yakini kuwaua ni hatia kubwa. Wala msikaribie zinaa. Hakika hiyo ni kinyaa na ni njia mbaya. Wala msiue nafsi ambayo Mwenyezi Mungu Amekataza isipokuwa kwa haki. Na mwenye kuuawa kwa kudhulumiwa, basi Tumeweka mamlaka kwa mrithi wake, hivyo asipite kiasi katika kuua; hakika yeye atasaidiwa. Wala msikaribie mali ya yatima, isipokuwa kwa njia iliyo bora, mpaka afike balehe yake, na timizeni ahadi. Kwa hakika ahadi itaulizwa. Na timizeni kipimo mpimapo, na pimeni kwa mizani iliyo sawa. Hayo ni wema na bora mwishoni. Wala usifuate usiyo na elimu nayo. Hakika masikio na macho na moyo – hivyo vyote vitaulizwa. Wala usitembee katika ardhi kwa maringo; hakika wewe huwezi kuipasua ardhi, wala huwezi kufikia urefu wa milima. Hayo yote ubaya wake mbele ya Mola wako ni uchukizao. Hayo ni katika yale Aliyokufunulia Mola wako katika hekima. Wala usiweke pamoja na Mwenyezi Mungu, mungu mwingine, usije kutupwa katika Jahanamu hali ya kulaumiwa (na) kufukuzwa (17:24-40).”

Mtaalamu huyo wa falsafa akanyamazishwa moja kwa moja!

# XI

## MSHAURI MWENYE BUSARA

Uasi nchini India mnamo mwaka 1857, ulioitwa baadaye Vita ya India kujinyakulia Uhuru, uliwaacha Waislamu wa Bara Hindi kuhangaika bila msaada katika hali ya taabu na kukata tamaa. Kampuni ya India ya Mashariki (East India Company), ambayo kwa kweli ilitawala India, iliwadhania Waislamu kuhusika sana na maafa ya Uasi na ikawa kali kulipiza kisasi. Mfalme wa mwisho tena dhaifu kabisa wa Kimoghuli ambaye alikuwa anapata pensheni kutoka kwa Kampuni hiyo, na alikuwa kibaraka tu asiye na madaraka ya aina yoyote, akalazimishwa na waasi kujifanya kuwaunga mkono maono yao katika shabaha yao. Katika hali alimojikuta hakuwa na hiari yoyote iwayo. Naye akapatilizwa vikali kwa njia ya kuhuzunisha kwa bahati yake mbaya. Akafukuzwa nchini na kupelekwa Burma, akamalizia maisha yake ya taabu huko Rangoon alikozikwa.

Alipokuwa mjini Delhi, akawa kwa akali kwa Waislamu ukumbusho usikitishao wa adhama yao ya zamani na kuwasaidia kudumisha wazo la kukusanyika kijamii na kiutamaduni. Akiisha ondoka, hakukubakia kitu isipokuwa hakika tupu yenye kutia huzuni. Dini na utamaduni, vyote viwili, vilianza kurudi nyuma. Masheikh wa Kiislamu kwa jumla walikuwa hawana ujuzi, walitaka kurudi nyuma na kupenda giza.

Malkia wa Kiingereza alipochukua utawala wa Bara Hindi, hali ikaanza kuwa nzuri polepole na kwa wasiwasi, lakini Waislamu wakaendelea kubaki nyuma kabisa wala hawakuweza kunufaika na maendeleo; ndivyo ilivyokuwa. Sawa na agizo la Lord Macaulay, Kiingereza kilifanywa njia ya kufundisha katika shule za sekondari

katika India. Kwa bahati mbaya Masheikh wa Kiislamu wakatangaza kwamba kujifunza Kiingereza ni kinyume na Islam. Hicho kikawa kizingiti kingine tena kwa Waislamu. Matokeo ni kwamba wasiokuwa Waislamu walipojinufaisha kikamilifu na njia hizo za kupata mafunzo ya sekondari, Waislamu wakaanza kurudi nyuma hatua kwa hatua. Matokeo yake ni kwamba kwa sababu ya kukosa kujua Kiingereza Waislamu hawakupewa kazi katika ofisi na idara za serikali ambazo zote hizo wakazitumikia wasiokuwa Waislamu.

Utovu wa uongozi wenye busara ulikuwa ni shida kubwa zaidi ya Waislamu. Katika robo ya mwisho ya karne ya kumi na tisa, Sir Seyyid Ahmad Khan, aliyejulikana zaidi na kwa upendo kwa jina Sir Seyyid, akatambua kwamba mafunzo ya kisasa ni mahitaji ya muhimu sana ya Waislamu, akajitolea kutimiza hayo kadri alivyoweza. Akapata kundi la wenzake waliojitolea kama yeye ambao walitiliwa fikara hizo nyoyoni mwao, na akaanzisha chuo cha masomo ya sekondari kule Aligarh alichokiita Muhammadan Anglo-Oriental College. Kikapata wanafunzi kutoka sehemu zote za Bara Hindi, na kikawa idara kuu ya kielimu ya Waislamu nchini. Hicho kilishirikiana na Chuo Kikuu cha Alahabad lakini baadaye kikawa chenyewe Chuo Kikuu cha Waislamu cha Aligharh. Mwamsho alioleta Sir Seyyid ukaenea hadi sehemu nyingine za nchi na wanafunzi wa Kiislamu wakaaza kunufaika na idara za kutoa mafunzo ya sekondari za mahali pao.

Maulawii Nuruddin r.a. alithamini juhudi za kweli za Sir Seyyid kwa ajili ya kuwaelimisha Waislamu, na akatoa mchango kwa ukarimu sana. Sir Seyyid naye akamheshimu sana na kuthamini msaada wake. Sir Seyyid aliulizwa na mtu mmoja: "Asiyejua kusoma na kuandika anapokuwa bingwa wa kusoma na kuandika huitawa mwenye kuelimika; aendeleapo zaidi kujipatia elimu huitwa mjuzi wa falsafa; anapojifunza hulka na mambo ya kiroho huwa Sufi; na Sufi

apatapo maendeleo ya hali juu huwa nani?" Sir Seyyid akamwandikia jawabu: "Huwa Nuruddin."

Maulawii Inayatur Rasul Chiryakuti alikuwa mtaalamu wa dini aliyekuwa bingwa wa Kiebrania na Kigiriki na alikuwa amesoma sana Maandiko Matakatifu ya Wayahudi na Wakristo. Yeye alimshauri Sir Seyyid kwamba kwa mtaala wa Taurati na Kurani Tukufu ili kuvilinganisha hivyo viwili, yanahitajika maelezo ya Taurati sawa na maoni ya Kiislamu, na akajitolea kuyaandika. Sir Seyyid akatoa kibali cha azimio hili na akamwandikia Maulawii Nuruddin r.a. akimwomba asaidiane naye kutekeleza kazi hii kubwa. Yeye akakubali mara moja, lakini kwa bahati mbaya Maulawii Inayatur Rasul kwa sababu fulani hakuweza kuanza kazi hii na habari hii ikaishia tu hapo.

Sir Seyyid alikuwa mtu ashikiliaye mawazo yake mwenyewe katika mambo ya dini. Akashikilia kwamba kumwomba Mungu ili kufaulu kupata shabaha fulani ni namna fulani ya ibada tena ni mazoezi ya kiroho lakini hakumsaidii mtu kupata shabaha yake hiyo anayonuia kuipata. Pia hakuamini kwamba maneno maalum huweza kufunuliwa katika wahyi. Sawa na maoni yake wahyi huwa baadhi ya mawazo anayotiliwa mtu moyoni mwake na mtu anayaeleza hayo kwa maneno yake mwenyewe. Masihi Aliyeahidiwa a.s., kwa kushauriwa na Maulawii Nuruddin r.a., akakanusha dhana hizo mbili ndani ya kijitabu chake *'Barakatud-Duaa.'* Humo alisema kwamba kwa kueleza mawazo hayo, Sir Seyyid amejaribu kuvunjilia mbali kabisa uhusiano baina ya Mwumbaji na viumbe Wake. Yeye akajitolea kumhakikishia Sir Seyyid kwamba maombi hupokelewa. Akamwelekeza kwenye utabiri wake kumhusu Pandit Lekh Ram uliofanywa ukiwa ni matokeo ya maombi. Kutimia kwake kutahakikisha kwa uwazi kwamba maombi hupokelewa na pia wahyi hufunuliwa ukiwa ni maneno maalum. Isitoshe, akaeleza ushuhuda wake mwenyewe

kuhusu hayo mawili. Akampelekea Sir Seyyid nakala moja ya *'Barakatud-Duaa'* na ya kitabu chake *'Izalah Auham*,' naye akamletea barua ya kumshukuru na kutaka aombewe.

Mwishoni mwishoni mwa uhai wake Sir Seyyid alipata kuudhika mno kwa uhaini na ulaghai wa mfanyakazi mmoja asiyekuwa Mwislamu aliyemsaliti na kumwibia fedha nyingi sana alizokusanya kwa kuendeleza mbele mipango yake yenye kufaa. Msiba huo, sawa na maoni ya mwanaye, Bwana Mahmud, Jaji wa Korti Kuu ya Alahabad, huenda uliharakisha kifo chake kutokea. Kabla hajafariki alimwandikia Maulawii Nuruddin r.a. kwamba anahisi ya kuwa katika jambo lolote ufaulu hauwezi kupatikana bila maombi.

Mkutano mkuu wa Dini ulioandaliwa na wawikilishi kadha wasiokuwa Waislamu ulifanyika mjini Lahore tarehe 26-29 Desemba 1896. Maswali matano yalipendekezwa kujadiliwa. Masihi Aliyeahidiwa a.s. naye alikaribishwa kusoma makala yake kujibu maswali hayo. Hakuhudhuria mwenyewe, lakini aliandika makala iliyosomwa mkutanoni na Maulawii Abdul Karim r.a., Maulawii Nuruddin r.a. alikuwa mwamuzi mmojawapo miongoni mwa waamuzi sita wa mkutano. Yeye aliombwa awe mwenyekiti wa Mkutano siku ya pili. Akafungua kikao kwa maneno yafuatayo:

> "Kama huruma ya Mungu, na hisani Yake, na utunzaji Wake unaojumlisha yote, na upaji Wake wanaojaliwa watumishi Wake wateule, visingemsaidia mtu, bila shaka angekoma kuwepo. Miongoni mwa hisani Zake Alizotujaalia katika zama hizi ni njia mbalimbali za kujipaita elimu, na kutupatia hazina kubwa za elimu. Karatasi nyingi na mitambo mingi ya uchapaji, idara za posta ambazo kwa njia hizo twaweza kupeleka maoni yetu mahali pa mbali sana kwa gharama ndogo kabisa, mfumo wa simu, magari ya moshi, meli na njia

nyinginezo za usafirishaji, hivyo vyote ni neema za Mungu. Kama mtu hatumii neema hizo kwa njia njema bali anazitumia vibaya ataulizwa na kuadhibiwa. Na kama akizitumia vizuri ataongezewa hizo. Katika ujana wangu vitabu vilipatikana kwa shida; waliokuwa navyo walisita kuviazima. Baadaye vitabu vizuri sana vya Constantionple, Misri, Tripoli, Tunisia na Moroko vikaanza kupatikana bila shida yoyote. Basi yambidi kila mmoja kufaidika sawasawa na neema hizo katika zama hizi za amani.

Haja ya dini yatiliwa nguvu kwa sababu maisha ya binadamu huhitaji sheria. Shabaha ya kanuni ni kuzilinda haki za bindadamu. Sheria inayowahusu watu kwa jumla huishia tu kutoa adhabu kama hatia zimekwisha fanyika, haina nguvu ya kufutulia mbali sababu zao. Kwa mfano, sheria yaweza kutoa adhabu kwa kumbaka mwanamke kwa nguvu, lakini haimo katika uwezo wa sheria kukomesha tamaa mbaya za nafsi, au kuwatenga marafiki waovu, au kuzuia macho yatazamayo huko na huko yanayomshawishi mtu kutenda dhambi hiyo. Ni dini tu inayotuzuia kufanya hivyo. Inachukia uovu. Machoni mwa dini mwema na mwovu hawalingani. Hawako sawa katika imani na mienendo; wala matendo yao hayaleti matokeo ya namna moja. Ni dini pekee imzuiayo mtu kutenda mabaya yasiyoingia katika eneo la sheria ya serikali, kwa kuyatangaza kuwa ni miiko. Yapo maovu mengine yanayolaumiwa na akili na maono ya umma, na serikali na jamii pia inayaona ni mabaya, lakini serikali wala jamii haina uwezo wa kuyang'olea mbali kwa nguvu, kama vile kutumia ulevi ama uzinzi kwa ridhaa baina ya wanaohusika. Ni dini pekee inayoweza kuyakomesha maovu hayo, si tu kwa kuyalaumu, bali kwa kuzuia mwelekeo wa fikira na mawazo yanayoyachochea maovu hayo yatendwe.

> Basi mtu aliye kiumbe aishiye katika jamii huhitaji sheria – sheria ambayo yatimiza shabaha yake barabara ni sheria tukufu ya dini. Na hii tu ndiyo sheria ambayo ina nguvu na ambayo ina uwezo juu ya utashi na mwelekeo wa mtu, na uwezo huo haupatikani kwa sheria yoyote iwayo iliyoundwa na serikali yenye amri zote na ya kidikteta.
>
> Basi, kutaali dini ingekuwa ni shughuli yetu kubwa kabisa, si tu kwa kuhifadhi sheria ya umma inayohakikisha kuleta amani na umoja, bali na kwa kujilinda na aina nyingine yoyote ya uovu. Twapaswa kutafakari sana namna tunavyoweza kufaidika nayo. Sasa kwa kuwa Mungu Ametujaalia njia mbalimbali na urahisi katika mambo yetu ili kutusaidia katika kazi yetu hii kubwa, basi itakuwa utovu wa shukurani tusiponufaika na njia hizo kwa kutafakari juu ya sheria na kanuni za mienendo ambazo, chini ya mwongozo wa Mungu, dini imeziunda na kuzifanya zitawale mienendo yetu. Hivyo, tunalazimika kuwa macho kuhusu dini. Na hiyo ndiyo shabaha ya mkutano huu."

Dondoo ya mwisho ya kikao cha siku hiyo ilikuwa ni kusomwa kwa makala ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. ambayo baadaye ilitolewa kwa sura ya kitabu *'Hekima ya Mafundisho ya Kiislamu.'* Alitangulia kutangaza mapema ya kwamba yeye amehakikishiwa na Mungu ya kuwa makala yake itakubaliwa kwamba imezishinda makala zote zitakazosomwa mkutanoni. Tangu mwanzo ilisikilizwa kwa makini kabisa. Kikao kilipoishia, jibu la swali la kwanza tu lilipata kujibiwa miongoni mwa maswali matano yaliyotakiwa kujibiwa mkutanoni. Waskilizaji waliosikiliza wakishangaa na kulishangilia kila neno wakakazania kwamba mkutano uendelee kwa siku moja nyingine baada ya siku tatu zilizokuwa zimewekwa mwanzoni, ili makala

nzima iweze kusomwa kikamilifu. Kwa hiyo kamati ya utendaji ya mkutano ikiungwa mkono na wasimamizi, ikachukua ruhusa ya *Anjuman Himayat-e-Islam* kutumia ukumbi kwa siku nyingine moja na kumwomba mwenyekiti wa kikao kutangaza habari hiyo. Maulawii Nuruddin r.a. akafunga kikao kwa kusema haya:

> "Marafiki zangu, mmeskiliza jibu la Hadharat Mirza Sahib kwa swali la kwanza. Twamshukuru sana mno Maulawii Abdul Karim kwa usomaji wake mzuri sana. Mimi, sasa, nawapasheni habri hii njema kwamba kwa sababu ya jazaba na upendo mliodhihirisha mliposikiliza makala hiyo na kwa kupendekezwa hasa na wasimamizi wa mkutano na wasikilizaji watukufu, kamati ya utendaji imetoa uamuzi kwamba mkutano utaendelea kwa siku moja zaidi ili makala ya Hadhrat Mirza Sahib ipate kusomwa kikamilifu."

Makala iliyobakia ikasomwa tarehe 29 Desemba.

Mkutano ulipokwisha, kamati ya utendaji ikawaomba wasimamizi kutoa maoni yao. Kwa kukubali ombi hilo, Maulawii Nuruddin r.a. akasema kwa uthabiti:

> "Nashuhudia kwamba hakuna Mungu isipokuwa Allah, Aliye Mmoja, Asiye na mshirika; na ninashuhudia kwamba Muhammad s.a.w. ni mtumishi wake na Mjumbe wake Na akasoma:
>
> Sema: Ninajikinga kwa Mola wa watu, Mfalme wa watu, Mwabudiwa wa watu, katika shari ya wasiwasi wa (Shetani) aendaye kisirisiri kwa hila, atiaye wasiwasi mioyoni mwa watu, miongoni mwa waliofichikana machoni na pia watu wa kawaida (sura 114: 2-7). Na akatoa hotuba fupi ambayo kwa kifupi ni kama ifuatayo:

Mtume Mtukufu s.a.w. alithibitisha kwamba yu mtumishi wa Mungu – sehemu isiyoweza kutengana na kanuni ya imani – ili Waislamu wazingatie daima dawamu kwamba washuhudiapo Umoja wa Mungu wasiangukie kosa la kumshirikisha Mungu na chochote.

Sifa tatu za Mungu zilizoelezwa katika aya nilizosoma, yaani Mola wa watu, Mfalme wa watu, Mungu wa watu zalingana na hali za maumbile, huluka na roho za mtu. Yule Dhati Anayelea na kuruzuku mwili, vipawa na roho za mtu Ameitwa jina Mola (*Rabb*) wa watu; Yule Anayemhukumu mtu kwa itikadi, matamshi na vitendo vya mwili, khulka na roho ndiye huitwa Mfalme wa watu, na Yule Aliye lengo na shabaha ya kweli na utashi wa mtu, ndiye aliyeitwa Mungu wa watu.

Basi Mungu Akimkumbusha mtu kwamba kwa kuwa Yu Mola, Mfalme na lengo na shabaha ya kweli na Mpendwa, Anamsihi ya kwamba akiwa mtumishi wake anapaswa kujikinga kwa Mkamilifu na Mtukufu kuhusu mambo yote ya riziki, utawala na upendo, Akiwa Mola wa watu, Mfalme wa watu na Mungu wa watu katika manong'onezo ya kila mnong'onezi msiri awaye yeyote.

Mmesikiliza katika siku nne zilizopita maongezi mengi ya aina tofauti. Baadhi yake msingi wake waweza kuwa ni ukweli na wema, na mengine yaweza kuwa uwongo mtupu, ujanja na udanganyifu. Basi kwa kufuata nasaha hiyo ya Kurani Tukufu mwapaswa kujikinga kwa Mola wa watu, Mfalme wa watu, Mungu wa watu katika makosa na wasiwasi unaoweza kuchochewa na muongezi au mnong'onezi mfitini. Wasiwasi wa aina hiyo na mashaka ni kama mbwa msumbufu ambaye

> saa zote yuko tayari kuuma. Kwa kuwa, ili kujikinga katika shari ya mnyama kama huyo, twalazimika kupata ulinzi wa bwana wake, kwani kama bwana wake akitaka kutulinda na kumkaripia vikali, hawezi tena yeye kumdhuru yeyote, hivyo kujikinga kwa mtu katika mashambulio ya wasiwasi wa Kishetani ni lazima kupatikane kwa kumwomba ulinzi Yule Aliye Mola na Mfalme na Mpenzi wa kweli wa viumbe vyote."

*'Hekima ya Mafundisho ya Kiislamu'* kilileta athari kubwa ajabu baina ya wale waliopenda kulinganisha mafundisho ya dini mbalimbali, na kimekubaliwa kuwa andiko bora.

Mnamo 1897 kijana mmoja, Abdul Hamid, alifika Qadian na akaonana na Maulawii Nuruddin r.a.; akaeleza kwamba yu mtoto wa nduguye Maulawii Burhanuddin r.a. wa Jhelum, mwanajumuiya wa Kiahmadiyya mwenye heshima sana. Akapokelewa kwa heshima na kukaribishwa kwa ukarimu. Akaarifu kwamba anamwamini Masihi Aliyeahidiwa na anataka sana kufanya baiati yake. Lakini Masihi Aliyeahidiwa a.s. akahisi kwamba huyo si mwaminifu na akakataa kumpokea katika Jumuiya. Yeye hakupendezwa na habari hiyo na akaondoka kuelekea Batala ambako alionana na wahubiri kadha wa Kikristo, ambao walimpeleka kwa Dkt. Henry Martyn Clarke wa Amritsar aliyekuwa adui mkali wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. Bwana padre akamshawishi kutoa maelezo kwa kula kiapo mbele ya Jaji wa Wilaya ya Amritsar ya kwamba Mirza Ghulam Ahmad amenituma nije Amritsar na kumwua Dkt. Clarke kwa kumtupia jiwe zito ghafla. Jaji wa Wilaya akapeleka maelezo hayo ya kiapo ya Abdul Hamid kwa Jaji wa Wilaya ya Gurdaspur, Captain W. Douglas, kwa kuchukua hatua ifaayo, ambaye aliwaamuru waliohusika kuhudhuria kortini Batala tarehe 10 Agosti ili kuandisha maelezo ya mashahidi,

Maulawii Nuruddin r.a. akiwa mmojawapo. Yeye alitoa maelezo yake kwa njia iliyo safi na nyofu ambayo ilimwathiri Jaji wa Wilaya, ambaye alivutika sana na sura ya mzee mhashamu, na alipoondoka baada ya kutoa ushahidi, Jaji akamwambia mwandishi (karani) wake, "Kama mtu huyo angesema yu Masihi Aliyeahidiwa, ningefikiri kwa makini sana madai yake."

Shahidi mwingine aliyehojiwa siku hiyo alikuwa Maulawii Muhammad Husain wa Batala ambaye uhasimu wake mkali dhidi ya Masihi Aliyeahidiwa ulijulikana sana. Ukaidi wake wa kuendelea kutoa maelezo ya uwongo waziwazi wakati wa kuhojiwa ukamlazimisha Jaji wa Wilaya kurekodi kumbukumbu ambayo ilifanya maelezo yake kuwa chapwa. Maulawii huyo alipoondoka chumba cha mahakama, kila mmoja aliyefikiwa naye akampa kisogo kwa kumchukia hata kwamba akashindwa kupata mahali pa kukaa. Maulawii Nuruddin r.a. akiona fedheha yake akamwonea huruma, akamwendea na kwa kumshika mkono wake akasema: "Bwana Sheikh, njoo ukakae pamoja nasi."

Katika kikao kingine cha kusikiliza kesi Abdul Hamid hakujiweza na akaungama ya kwamba maelezo yake ya kwanza yalikuwa ya uwongo ambayo yalitolewa kwa sababu ya kuchochewa na Dkt. Clarke na baadhi ya wenzake. Masihi Aliyeahidiwa a.s. akaachiliwa huru kwa heshima. Na ingawaje, Jaji wa Wilaya alimpa ruhusa ya kuwashitaki sawa na sheria mashahidi wakubwa dhidi yake kwa sababu ya kutoa ushahidi wa uwongo kwa nia mbaya ya kumdhuru, lakini yeye akakataa kutumia ruhusa hiyo akisema: "Kesi yangu inangojea kusikilizwa mbinguni, sitaki kupoteza wakati wangu kuwasaka wapinzani wangu mbele ya majaji wa kidunia!"

Zaidi ya robo karne baadaye, muda mrefu baada ya Captain Douglas kustaafu, mimi mwandishi nilikwenda kuonana naye kujua

maoni yake kumhusu Masihi Aliyeahidiwa a.s. Yeye alikuwa mwenye afya njema sana na hali nzuri kabisa. Tukaongea sana. Kwa jumla akasema: "Pindi alipoingia Bwana Mirza katika chumba changu cha mahakama nilimwona na kutambua kwamba mtu huyo si wa dunia hii. Roho yake ilionekana inaongea na Mungu. Ingawaje alikuwa ameshtakiwa kwa kosa kubwa, lakini nikahisi yeye hawezi kutenda kitu kama hiki. Nikampatia kiti na kumwambia akae jukwaani. Nikaathirika na ubora wake na utu mwema wake. Nikasadikisha ukweli wa madai yake kwamba alikuwa Nabii, na kwa sababu hiyo niliamini tangu wakati huo kwamba Muhammad s.a.w. alikuwa Mjumbe mkweli wa Mungu."

Yastahili kukumbukwa kwamba yule Abdul Hamid baada ya miaka michache akatubu kwa moyo kwa kosa kubwa alilowahi kutenda na akajiunga katika Jumuiya ya Ahmadiyya.

Kulikuwa na mtu mmoja jina lake Sa'dullah wa Ludhiana ambaye alikuwa Baniani lakini alisilimu. Yeye alikuwa adui mkali sana wa Masihi Aliyeahidiwa ambaye alidhihirisha uadui wake kwa mdomo mchafu sana. Alitabiri kwamba Masihi Aliyeahidiwa atakufa pasipo kupata kizazi na Jumuiya aliyoanzisha itatoweka taratibu baada ya kufa kwake. Masihi Aliyeahidiwa akamjibu kwamba yeye amefunuliwa wahyi ya kwamba Sa'dullah mwenyewe atakuwa mkiwa. Hapo baadaye Masihi Aliyeahidiwa akabarikiwa na kuongezewa wazao, lakini Sa'dullah akabakiwa na mwana yule yule mmoja aliyekuwa kijana wakati Masihi Aliyeahidiwa a.s. alipopokea wahyi huo.

Mwishoni mwishoni mwa mwaka 1906, Masihi Aliyeahidiwa akaandika utabiri wake kumhusu Sa'dullah pamoja na ishara na bishara nyingine ndani ya kitabu alichokuwa anaandika, na akasisitiza kwamba Sa'dullah wala mwanaye aliyekuwa wakati huo mwishoni

mwa kumi la pili la umri wake, hawatapata kizazi. Wakili mmoja mashuhuri aliyekuwa mwanajumuiya maarufu wa Kiahmadiyya alijaribu kumzuia Masihi Aliyeahidiwa asiueneze utabiri huu kwa kuchapisha. Kwani alichelea kwamba utangazwapo utabiri huu, isije Sa'dullah au mwanaye ama wote hao wawili wakamshtaki kwa hatia ya jinai ya kuwakashifu. Masihi Aliyeahidiwa a.s. akimjibu alisema:

> "Nafikiri njia iliyo sawa ni kuthibitisha Neno la Mungu; kulificha ni dhambi tena haifai. Hakuna awezaye kunidhuru isipokuwa Mungu, sina hofu ya kudhuriwa na serikali. Naam, nitamwomba Mungu Mwenye Enzi Aliye chanzo cha fadhili na rehema zote, kwamba Anilinde na madhara na taabu zote. Hata hivyo kama imekadiriwa nisumbuke kwa njia hii, naridhika tu."

Kisha akipaza sauti yake akaongeza: "Naapa kwa jina la Mungu, Mwenye nguvu, ya kwamba Yeye Hatamfanya habithi huyo kuniweza, na Atamlinda mtumishi wake huyu aombaye ulinzi Wake dhidi ya ukorofi wake kwa kumwadhibu kwa namna fulani."

Kusikia hayo, Maulawii Nuruddin r.a. akainuka na katangaza:

"Itakuwa tu hivyo: Kwani Mtume Mtukufu s.a.w. amesema: Mara nyingi mtu mwenye nywele timtimu na vumbi usoni akiapa, na Mungu humtimizia kiapo chake."

Baadaye Masihi Aliyeahidiwa akaendelea na maombi yake na katika siku mbili au tatu akafunuliwa maneno yayo hayo ya Hadithi aliyokuwa ameitaja Maulawii Nuruddin r.a. Siku chache baadaye Sa'dullah akafa kwa ugonjwa wa tauni tarehe 3 Januari 1907. Mwanaye baada ya kufiwa na babake aliishi karibu nusu karne, na ingawaje akapata kuoa mara mbili lakini hakupata kizazi. Na ndipo ukaishia ukoo wa Sa'dullah.

Bangal iligawanywa mwanzoni mwa karne ya ishirini katika zama za Ukaimu wa Lord Curzon. Hatua hii ya kiserikali ilielezwa na Mabaniani kwamba ilichukuliwa kwa kuwadhoofisha katika Bangal na kuwaimarisha Waislamu katika Bangal ya mashariki, nayo ikawachukiza sana. Msukosuko wao dhidi yake ukaenea nchi nzima na ikawa hatari sana. Ikawa tishio kwa hali ya amani katika majimbo mengi. Mnamo Mei 1907, Masihi Aliyeahidiwa a.s. alitoa tangazo hadharani kuwasihi wanajumuiya wa Jumuiya yake wasishiriki katu katika fitina hiyo ya Mabaniani. Kwa kutangaza habari hiyo hadharani mkutano mmoja wa watu wote uliitishwa mjini Qadian ambao pia ulihutubiwa na Maulawii Nuruddin r.a. Akikazania umuhimu wa kuimarisha nchini sheria na hali ya amani akasema:

> “Walionufaika zaidi na serikali ya Kiingereza ni Mabaniani. Wanayo nguvu kila mahali. Kila mwaka mali ya Waislamu kiasi kama rupia milioni kumi inaingia mikononi mwa Mabaniani. Kazi zote kubwa zaidi za serikali zimeshikwa na Mabaniani, na Waislamu wameachiwa kazi ndogo ndogo. Katika hali kama hii Mabaniani walipaswa kuwa wenye shukurani sana kati ya umma na kuwa waaminifu. Lakini kwa bahati mbaya wamejithibitisha kuwa wasio na shukurani kabisa. Hata hivyo hilo si la kustaajabisha. Wanamshirikisha Mungu na vitu vingine. Basi yule anayempa kisogo Mwumbaji Mhisani wake wa kweli na akainama mbele ya sanamu la jiwe hawezi asilani kutazamiwa kuwa mwenye shukurani kwa binadamu mhisani.”

Mnamo Februari 11, 1906, Masihi Aliyeahidiwa alipokea wahyi (tafsiri):

> “Watafarijiwa kuhusu hukumu iliyotolewa juu ya Bangal.”

Ufunuo huo ulichapishwa na kutangazwa mara moja, nao ukachekwa

na kufanyiwa dhihaka na wapinzani. Lakini ukashtusha ulipotimia mnamo 1911, ambapo mgawanyiko wa Bangal ulitangazwa kufutiliwa mbali kwenye Baraza la kumvisha Mfalme George V taji alipotawazwa, mjini Delhi.

Katika Juni 1907, mtu fulani alimwandikia Maulawii Nuruddin r.a. baadhi ya maswali:

1. Je, wasiomwamini Masihi Aliyeahidiwa ni kama wale wasiomwamini Mtume Mtukufu s.a.w.?
2. Hadithi hii itafafanuliwaje: "Hakuna Nabii baada yangu."
3. Kama Nabii anaweza kutokea katika Islam, kwa nini Abu Bakr na wengineo hawakuwa manabii?

Akarudisha majibu yafuatayo:

1. Kurani Tukufu inahakikisha ya kwamba waaminio hawatofautishi baina ya mmoja wa Mitume wa Mungu katika kuwaamini (2:286). Lakini wewe unataka kutofautisha baina ya wale wasiomwamini Mtume mwenye sheria mpya na wale wasiomwamini Mtume asiyeleta sheria mpya. Sifahamu sababu ya kutofautisha huku. Tumeongozwa kumwamini Masihi Alieyeahidiwa kwa dalili zile zile ambazo kwazo tumeongozwa kuiamini Kurani Tukufu. Kukataa dalili ni sawasawa na kukataa Islam. Hebu tafakari: Na wanapoambiwa: Amininі Aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, husema: Tunaamini yaliyoteremshwa juu yetu; na huyakataa yaliyo nyuma yake, nayo ndiyo haki inayosadikisha yale yaliyo pamoja nao (2:92). Kwa nini ulinganifu wa hoja hizo usilete matokeo ya

aina moja katika kadhia hizo mbili?

2. Mtume Mtukufu s.a.w. ameeleza Masihi aliyetakiwa kuja kwamba atakuwa Nabii wa Mungu na Masihi Aliyeahidiwa mwenyewe aliitwa kuwa Nabii katika funuo zake alizofunuliwa na Mungu. Hadithi za Mtume s.a.w. zinatofautisha baina ya habari za kawaida na habari maalum. Hebu fikiria mifano ifuatayo iliyo ya mambo ya kawaida yasiyoacha nje yale yaliyo maalum: "Asiye mnyofu hana imani, avunjaye ahadi hana dini; hakuna *sala* pasipo kusoma sura *Fatiha*; hakuna ndoa bila kibali cha mlezi (msimamizi) wa Bi arusi; husuda haisihi isipokuwa kuhusu watu wawili." Kisha ndani ya Kurani Tukufu, Mtume Mtukufu s.a.w. ameitwa *Khatamun Nabiyyin* (Muhuri wa Manabii) siyo *Khatimun Nabiyyin* (Mwisho wa Manabii). Kurani Tukufu inathibitisa ya kwamba Mayahudi walitaka kuwaua manabii. Je hiyo yamaanisha manabii wote, au baadhi yao?

3. Abu Bakr r.a. hakuitwa Nabii na Mwenyezi Mungu, na Masihi Aliyeahidiwa aliitwa hivyo.

Tawi la Wachuwali la dhehebu la Arya Samaj mjini Lahore liliitisha mkutano wa dini zote uliotakiwa kufanyika tarehe 2,3 na 4 Desemba, 1907, ambamo makala zilitakiwa kusomwa kuhusu sifa za Kitabu kilichofunuliwa na Mungu. Masihi Aliyeahidiwa pia aliombwa kuandika makala. Akielewa ujeuri wa Arya Samaj, alichelea kidogo, lakini alipohakikishiwa na wasimamizi wa mkutano kwamba Waanzilishi wa Dini zote watapewa heshima, wala halitasemwa lolote linaloweza kuelekea kuumiza maono ya kidini, akakubali kuandika makala. Makala yake ilisomwa katika mkutano, nusu ya kwanza, na

Maulawii Nuruddin r.a. na nusu nyingine na Dkt. Mirza Yakub Beig, kutokea saa 12 jioni hadi saa 4 za usiku, tarehe 3 Desemba.

Akimalizia makala yake akaandika funuo zake nyingi alizokuwa amefunuliwa kwa Kiarabu. Maulawii Nuruddin r.a. akaombwa kuzifasiri hizo kwa Kiurdu. Kwa heshima na staha aliyokuwa nayo Maulawii Sahib kwa Bwana wake, akatamka:

> «Kwa kuwa mpokeaji wa funuo hizi hakuzifasiri mwenyewe, naona sina haki ya kuzifasiri. Hata hivyo, kwa kuwa wasikilizaji wanafikiri kwamba tafsiri itawasaidia, nazifasiri kwa kueleza wazi wazi kwamba tafsiri yangu itakuwa jinsi ninavyofahamu mimi binafsi maana zake wala haitamlazimu mpokeaji funuo kuafikiana na hizi maana. Yeye peke yake anayo haki ya kueleza muradi wake wa kweli.”

Mjumbe wa Arya Samaj alisoma makala yake tarehe 4 Desemba ambamo aliishutumu Islam na Mwanazilishi wake Mtukufu s.a.w. pasipo kuona haya. Kitendo hicho kilikuwa cha kikatili na kikorofi kilichowachukiza na kuwakasirisha sio Waislamu tu bali na pia wasikilizaji wote wenye heshima. Mwenyekiti wa kikao hakukawia kueleza masikitiko yake kwa sababu ya makala kama hiyo iliyosomwa mkutanoni. Akahakikisha kwamba kama angelijua yaliyomo humo asingaliiruhusu kusomwa, lakini hakufanya bidii kumkemea msomaji wala kumzuia wakati makala ilipokuwa inasomwa na ukorofi ukafanyika tayari.

Wajumbe kutoka Qadian waliporejea kwao na Masihi Aliyeahidiwa akaambiwa habari hiyo, yeye alikasirika sana mno. Akawakemea vikali wajumbe hao tena mara nyingi kwa nini hawakuondoka hapo walipokwisha tambua mwendo wa makala ya msomaji wa Arya Samaj. Akawakumbusha agizo la Kurani Tukufu:

> "Naye Amekwisha wateremshieni katika Kitabu ya kwamba mnaposikia Aya za Mwenyezi Mungu zinakataliwa na kufanyiwa mzaha, basi msikae pamoja nao, hata waingie katika mazungumzo ghairi ya hayo; (maana mtakapokaa) hakika ndipo mtakuwa kama wao (4:141)."

Ni baada ya kuombwa sana radhi kwa unyenyekevu ndipo hasira yake ikapoa na akasamehe kosa hilo kubwa. Hata hivyo akathamini kujizuia kwao katika hali ngumu kabisa na ya uchokozi. Basi akaandika:

> "Kama Waislamu hao wema wasingalizingatia ustaarabu wao na kukaa imara katika hali ya kukasirishwa sana, sawa na mafunzo ya Kurani Tukufu, na kuzuia ghadhabu yao, mkutano huo, bila shaka, ungeishia maangamizi kwa sababu ya uchokozi mbaya sana uliofanywa na watu wakorofi. Wanajumuiya wa Jumuiya yangu waliohusika wanastahili kusifiwa mara elfu kwani waliweka mfano bora sana wa kujizuia, na waliposikia maneno ya Ma-Arya yakiwachoma yaliyokuwa makali kuliko risasi, hawakutamka hata neno moja. Kama nisingalikuwa nimeitayarisha Jumuiya yangu kwa kuisihi mara kwa mara na kwa kudumu kwamba hawana budi kusubiri hata wakitukanwa vikali sana, mkutano ungelichovywa damu. Ni mafundisho yangu tu aliyowawezesha kuzuia hasira yao."

Sardar Mihar Singh, kijana mmoja aliyetokana na familia moja yenye heshima ya Kisingasinga, alipata kusilimu na akajiunga katika Jumuiya ya Ahmadiyya. Familia yake ilitengana naye na kuwa mpinzani wake. Akajipatia jina Abdur Rahman. Maulawii Nuruddin r.a. alimsaidia katika masomo yake na kumtunza. Tangu mwanzo akahakikisha uaminifu wake, bidii na jitihada yake, na Maulawii Nuruddin r.a. akamridhia sana. Ghauri Patan mmoja wa Jammu, jina lake Khalifa Nuruddin aliyekuwa rafiki wa Maulawii Nuruddin

r.a. tangu siku zake za kukaa huko Jammu, alimtaka shauri kuhusu kumwoza bintiye. Akampendekezea Abdur Rahman. Wazazi wa msichana walipopata habari kamili za kijana wakamwambia Maulawii Nuruddin r.a. kwamba kijana kweli ni mwaminifu na mwema, lakini hana jamaa wala hana matumaini kwa siku za mbele. Alicho nacho ni mkeka mmoja, kopo kubwa la maji, kitanda kimoja na mshahara mdogo akiwa mwalimu. Atawezaje kumlisha mkewe? Maulawii Nuruddin r.a. kajibu: "Kama binti yako amebarikiwa kuwa na bahati njema, ataijaza nyumba iliyotupu, na kama akiondolewa bahati njema ataifanya tupu nyumba iliyojaa."

Wazazi wa binti wakakubali nasaha yake kwa moyo, msichana akatoa kibali na ndoa ikafungwa. Ikathibitika kuwa nzuri na yenye baraka kwa kila jiha. Wazao wao wengi ni ushahidi wa jambo hili.

Maulawii Nuruddin r.a. alikuwa na kiherehere kwamba wale wanaofika Qadian wajipatie faida kamili kwa kukaa karibu na mhashamu mtukufu Masihi Aliyeahidiwa a.s. Katika hotuba yake moja akasema:

> "Ni shabaha gani iliyonileta hapa? Ninayo nyumba iliyojengwa vizuri huko Bhera, na nilikuwa na wasaa na raha kule. Hapa ninakaa katika nyumba ndogo ya matofali ya udongo yasiyochomwa, nami nimetupilia mbali raha zote. Kwa nini? Kwa sababu nilijiona ni mgonjwa, mgonjwa sana; nilikuwa fukara, fukara kabisa; nilikuwa taabani, taabani moja kwa moja. Basi nikaja hapa kujitafutia tiba ya maradhi yangu. Kama mtu akija hapa kuniona na kujifunza kutokana na mfano wangu, ama anakuja kutusuta sisi tunaoishi hapa, anakosea sana. Anajidanganya kwa kuwadhania wagonjwa kuwa wazima na kuwatolea hukumu. Urafiki wote na udugu wote hapa, wajao wote hapa na waondokao hapa, kuja kukaa

hapa na kuishi hapa, yote hayo yawe chini ya, na maelezo ya: Hakuna Mungu isipokuwa Allah. Kama hiyo siyo shabaha ya kuja hapa, kwa nini uje? Unacho chakula bora na starehe zaidi kwenu kuliko utakavyopata hapa. Ujaji wako hapa utathibitika kuwa wa haki hapo tu ambapo katika yote ufanyayo lengo lako ni kujinyakulia radhi ya Allah."

## XII

## KHALIFATUL MASIHI

Alipopata ruhusa ya Masihi Aliyeahidiwa a.s., Maulawii Nuruddin r.a. akaandika yafuatayo tarehe 19 Machi 1908 chini ya kichwa cha maneno: "Marafiki na Ndugu wanaombwa," kama ifuatavyo:

> "Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.
>
> Twamsifu Yeye na kumwombea baraka Mjumbe wake mtukufu.
>
> Amani iwe kwenu na rehema ya Allah na baraka Zake. Usiku mmoja nilipata kufikiria umri wangu na wakati mrefu zaidi unaofuata mwanzo wa dini ya Kiislamu na nikasumbuka kutafakari yale yanayotakiwa kufanyika kabla haijaisha nafasi ya kuishi. Mawazo yangu yakaelekea kwenye muradi wa maombi yanayoombwa katika hali ya kukaa ndani ya *Sala* na kuishia kwenye kisa cha kasuku kilichoelezwa na Maulana Jalaluddin Rumi katika *Mathnawi* yake (Shairi lenye mistari miwili katika kila ubeti). Kisa chenyewe ni kwamba kasuku huyo alimwagiza bwana wake mfanya biashara awasalimie kasuku wenzake huko India pindi atakapowahi kupitia huko. Shabaha ya kasuku ilikuwa kupata mwongozo kwao ili kujipatia uhuru. Kasuku wenzake wakarudisha jibu kwamba barabara ielekeayo uhuru hupitia bonde la kifo.
>
> Njia hii ya kutafakari ikanielekeza kwenye kasuku wa Mungu, yaani roho za wale waliopata kuuawa katika njia ya Mungu. Nami nikaanza kutafakari maombi yanayoombwa

katika hali ya kukaa ndani ya *sala*: Amani iwe kwako, ewe Nabii, na rehema ya Mungu na baraka Zake. Na: Amani iwe kwetu sisi na kwa watumishi wote wema wa Mungu. Nami katika hali ya jazba yangu nikafanya biashara na Mungu kama Alivyosema: Hakika Mungu Amenunua kwa waaminio nafsi zao na mali zao ili wapate Pepo (9:111). Katika aya hii Mungu Anajieleza kuwa mnunuzi, mfanya biashara. Mwaminio akiishajitolea kwa Mungu kikamilifu hana budi kujitahadhari asitumie maisha yake wala mali yake pasipo kuruhusiwa na Mungu. Na kwa kupata shabaha hii nikajibidiisha kumsalia sana Mtume Mtukufu s.a.w.

Kisha nikaonelea kwamba nifanye urafiki na watu wengi ambao niwawekee alama maalum ya kupambanua, ili tuweze kumtukuza Mungu sana na kumkumbuka mno. Basi, Mungu Asifiwe, sawa na busara yangu kidogo na kutendeana na watu nikafanya urafiki na wanajumuiya wa Kiahmadiyya – Jumuiya inayochukia sana ushirikina na bidaa katika dini na inaamini kwa uaminifu katika: Hakuna Mungu isipokuwa Allah na Muhammad s.a.w. ni Mjumbe wake; na kwa sababu ya kumfuata Mtume Mtukufu s.a.w. suna yake inastahili kuhesabiwa Masunni, na kwa kuungana na Imam a.s. haina budi kuwa *Jumuiya* – wale walio wakarimu, imara, wastahimilivu na wenye imani katika maombi. Kwa haya yote shabaha yangu ilikuwa:

1. Kwamba hao wawe mashahidi wangu juu ya ardhi kwa ajili ya Mungu, wakishuhudia imani yangu; kwani Mtume Mtukufu s.a.w. alisema kwamba yule anayethibitishwa kuwa mwema na kundi la watu wema, atastahili kuingia katika Pepo za radhi ya Mungu; na anayehesabiwa nao kwamba hafai, atahukumiwa

kutupwa Motoni. Kwa kushuhudiwa na mashahidi hao juu ya ardhi kwa ajili ya Mungu nitajaaliwa na Mungu yale ayapendayo.

2. Kwamba kwa ushirika wetu huo tutaweza kusaidiana kuendeleza maadili na wema tukawa marafiki na wasaidizi.

3. Kuna baadhi ya baraka maalum za Mungu linazozipata kundi tu la watu wenye umoja. Kwa hiyo umoja wa marafiki waweza kuundwa kwa kuvutia rehema ya Mungu, ili Mungu Atuwie radhi na Akatufanye watumishi wa kweli wa Islam na Waislamu.

4. Imesimuliwa ya kwamba Mtume Mtukufu s.a.w. alisema: Siku ya Kiama watu wa aina saba watajaaliwa kivuli cha Mungu ambapo kutakuwa hakuna kivuli kingine. Aina moja katika hizo ni marafiki wawili wanaopendana kwa ajili ya Mungu, huungana kwa ajili Yake na huachana kwa ajili Yake. Basi nikapenda tuwe kundi la aina hii, na tukiwa hivyo tupate ufanisi chini ya himaya ya Arshi ya Mungu, himaya tunayoweza kuishuhudia hapa duniani na huko Akhera.

5. Baadhi ya njia zitafutwe kueneza ujuzi wa lugha ya Kiarabu baina ya Waislamu na hususan baina ya Jumuiya ya Ahmadiyya, kwani hiyo ndiyo njia ya pekee inayoweza kuimarisha umoja na maafikiano kati yao. Aidha, ujuzi wa Kurani Tukufu na Hadihti za Mtume s.a.w. hutegemea ujuzi wa Kiarabu. Twapaswa kujibidiisha sana kwa ajili hii na kutafuta njia za kupata lengo hili, kama kwa mfano, njia mojawapo ya kusafiri nchini ni garimoshi.

6. Popote panapokuwa na utovu wa maelewano au pana chuki, marafiki hao wanapaswa kuwa njia ya kurudisha kuelewana kwema na upendo, kama Asemavyo Mungu: Suluhisheni mambo baina yenu (8:2); Fanyeni suluhu baina ya ndugu zenu (49:11); Suluhu ni bora (4:129).

7. Hamna budi kukimbilia sala katika hali zote, za raha na taabu. Lakini ni uzembe wa hali ya juu kwamba hata waishio Qadian pia hawajali. Nimetayarisha majibu ya maswali kuhusu azimio hilo na kutuma nakili zake, lakini nimepokea maoni ya ndugu kutoka Sialkot na Peshawar tu. Wa Lahore hawakuitika. Isitoshe, nimewaandikia Waislamu walio watalamu wa hali ya juu wa nchi za mbali kutoa shauri kuendeleza mbele ujuzi wa lugha ya Kiarabu na kuhimiza kueneza khulka za Kiislamu. Nilitoa pia shauri ya kuchapisha vjitabu vidogo kueneza mafunzo ya Kiislamu na kutoa majibu ya upinzani ulioletwa dhidi yake na wasiokuwa Waislamu. Kwa njia hii twaweza kutimiza wajibu wetu wa kuamrisha mema na kukataza maovu, na marafiki zetu kutahadharishwa kuhusu hasara kubwa inayoweza kuletwa na mawazo mabovu."

Azimio hilo lilitangazwa katika *Al-Hakam*, *Badr* na *Tash-hidhul Adhhan,* na Maulawii Nuruddin r.a. akachapisha kadi 1400 ambazo lengo lake lilipangwa kwa kifupi. Alinuia kwamba akiisha pata marafiki 1400 kwa mpango huo, Masihi Aliyeahidiwa ataombwa aiombee shabaha hiyo maombi maalum ili yapatikane mafanikio katika hiyo, lakini ikashindikana kwa sababu ya mambo kusogea mbele haraka sana.

Hadhrat Ummul Muminin (mkewe Masihi Aliyahidwa a.s.) alikuwa anaugua na akamshauri Masihi Aliyeahidiwa a.s. kwamba waende Lahore ili kupata mashauri yafaayo ya kitabibu. Yeye alisita kidogo kwa sababu alikuwa amepashwa habari kwa njia ya wahyi kuhusu kifo chake kilichokwisha sogea karibu. Karibu na mwisho wa mwaka 1905, akafunuliwa tena habari kama hii kwamba muda kidogo, kama miaka miwili au mitatu, imebaki katika umri wake, akachapisha Wasia wake akiwafariji kwamba baada yeye kuwaacha mkono, Mungu Atawasaidia kwa Dhihirisho la Kudra yake ya pili, jinsi ilivyofanyika alipofariki Mtume Mtukufu s.a.w. ambapo Mungu Akamwinua Hadhrat Abu Bakr r.a. kuwakusanya tena Waislamu, naye akachukua hatua zifaazo kuwalinda dhidi ya hatari kubwa zilizowakabili kutoka kila upande. Yeye a.s. akaanzisha *Sadr Anjuman Ahmadiyya* (Jumuiya Kuu ya Kiahmadiyya), kwa kusimamia uendeshaji wa shughuli za Jumuiya, na akamfanya Maulawii Nuruddin r.a. kuwa Mwenyekiti wake.

Sasa kabla hajafunga safari ya kwenda Lahore, akashughulikia maombi ili kupata mwongozo kuhusu safari yake aliyonuia kufunga na akawaomba marafiki zake kumsaidia kwa maombi yao. Akamwambia bintiye mkubwa, Nawab Mubaraka Begum, kwamba anataka kuamua jambo moja la muhimu sana, basi atafurahi kwamba amsaidie kwa maombi. Keshoye akamwambia kwamba aliomba kwa bidii sana na ndipo akamwona Maulawii Nuruddin katika ruya akikaa katika ghorofa na ameshika kitabu kimoja mkononi mwake. Akamwambia: Kitabu hiki kina funuo alizofunuliwa Hadhrat Sahib (Masihi Aliyeahidiwa). Mimi ni Abu Bakr r.a.

Masihi Aliyeahidiwa akamwambia asimweleze mamake ruya hii, na akafanya matayarisho kwa safari ya kwenda Lahore. Msafara ukaondoka Qadian tarehe 27 Aprili 1908, na wakashinda njiani mjini

Batala kwa siku mbili hivi wakawasili Lahore tarehe 29 Aprili. Masihi Aliyeahidiwa akakaa nyumbani mwa Khwaja Kamaluddin ndani ya Ahmadiyya Buildings kwenye Barabara ya Brandreth, lakini baada ya siku chache akahamia nyumba iliyo jirani yake ya Dkt. Seyyid Muhammad Husain katika jengo hilo hilo. Kwa kuwa muda wa kukaa Lahore ulikuwa mrefu kidogo, basi akamwita Maulawii Nuruddin r.a. na baadhi wa wataalamu wengine waje Lahore kutoka Qadian.

Tarehe 17 Mei, baadhi ya Waislamu mashuhuri walikaribishwa kuonana na Masihi Aliyeahidiwa kwenye chakula cha mchana, ambapo yeye aliwahutubia akieleza msingi na uhakika wa madai yake, na akaondolea mbali makosa walimoangukia watu kuhusu habari hiyo. Akasikilizwa kwa makini sana, na baadhi ya wasikilizaji wakamsisitizia kutoa hotuba moja hadharani ili watu wafaidike na hekima zake. Sawa na shauri hilo akaanza kuandika hotuba moja iitwayo *'Paighame Sulh'* (Ujumbe wa Suluhu) ambamo alieleza mpango wa kuleta maelewano mema baina ya Mabaniani na Waislamu. Katika muda huo huo funuo zikafululiza kumtahadharisha kuhusu ukaribu wa kifo chake, lakini akaendelea na shughuli hii kwa makini kabisa. Akamaliza kuandika hotuba yake tarehe 25 Mei Jioni na akaenda nje kidogo kupunga hewa katika gari la farasi.

Aliporudi baada ya kupunga hewa akahudhuria katika sala za Magharibi na Isha kwa kuzikusanya. Akala kidogo, na kwa kuwa alisikia uchovu akaenda kitandani mapema. Usiku wa manane hivi akaenda haja mara mbili katika kitambo kidogo, jambo lililomdhoofisha sana na akasema Maulawii Nuruddin aitwe kutoka nyumba ya jirani, ambaye alikuja haraka na akajaribu pamoja na Dkt. Seyyid Muhammad Husain na Mirza Yakub Beig kila njia bila kufanikiwa. Mgonjwa wao mtukufu akaenda haja tena na hali yake ikawa mbaya haraka sana. Akasali sala ya alfajiri katika hali ya kizimia kidogo, kisha akaonekana

kuzimia. Mara moja moja akasikika kunong'ona: Allah, mpendwa wangu Allah. Saa 4:00 za asubuhi akazirai kabisa, akikokota pumzi, na saa 4:30 akakoma kupumua. Maiti yake ikapelekwa Qadian ambako ilifika saa 2 za asubuhi tarehe 27 Mei. Ikawekwa katika nyumba yake iliyomo bustanini mwake ambako masaa mengi ya mchana wafuasi wake waaminifu waliofika kutoka mbali na karibu wakapata nafasi ya kutazama mara ya mwisho uso uliotakata wa bwana wao mtukufu na mpendwa.

Habari ya kifo cha Masihi Aliyeahidiwa ikawa pigo kali sana kwa wanajumuiya wa Kiahmadiyya. Wakafadhaika na katika hali ya msiba huu mkubwa wakakimbilia kuomba kuongozwa kwa unyenyekevu na bidii. Labda Maulawii Nuruddin r.a. aliathirika sana ambaye mara kwa mara alinena: Baada ya kifo cha Hadhrat ulimwengu unaonekana hauna uhai tena.

Tufanyeje? Tuelekee wapi?

Viongozi pamwe na wana-*Sadr Anjuman Ahmadiyya* wakakusanyika katika nyumba ya Nawab Muhammad Ali Khan aliyekuwa amemwoa bintiye Masihi Aliyeahidiwa. Na wanajumuiya wengine wote waliowasili Qadian kutoka kila upande wakangojea katika bustani kubwa, jirani ya nyumba ambamo mwili wa kiongozi mkuu mtukufu ulikuwa umewekwa. Waliokusanyika mjini wakasihiwa na Khwaja Kamaluddin kwa maneno yenye kuathiri sana: "Mja mmoja alidhihirika ardhini akiwa Mjumbe wa Mungu na akawaita watu kwa jina lake. Tukamwitikia mwito wake na kukasanyika pembeni mwake. Sasa ametuacha mkono na amerejea kwa Mungu. Katika hali kama hii tufanye nini?"

Wasikilizaji wake wakashikwa na butwaa; ikawa kimya kabisa. Baada ya kitambo kidogo, Shaikh Rahmatullah, mwana-*Sadr Anjuman Ahmadiyya* akainuka na kwa nguvu akaagiza kwa sauti ya

kuvutia: "Pindi tulipokuwa safarini toka Lahore kuelekea Qadian nilisema moyoni mwangu na sasa nawaambieni kwamba tunalazimika kumwomba mzee wetu mhashamu (yaani Maulawii Nuruddin r.a.) kujitokeza mbele. Pasipo yeye tutapotea njia." Hakuna aliyepinga maoni hayo, na ikafahamika kwamba shauri hilo limeungwa mkono na kila mmoja aliyekuwapo. Kati yao alikuwepo Sahibzada Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad r.a. ambaye alipoulizwa akaeleza haraka kibali chake na ndivyo alivyofanya Mir Nasir Nawab, mkwewe Masihi Aliyeahidiwa, ambaye wakati huo alikuwa huko bustanini. Baadaye Khwaja Kamaluddin akaambiwa kwenda kumngojea Hadhrat Ummul Muminin na kujua maoni yake. Yeye naye akasema kwamba Maulawii Nuruddin r.a. ndiye mwenye heshima kuliko wote katika Jumuiya na apaswa kuwa *Khalifa.*

Ndipo taarifa fupi iliandikwa na waliokuwepo wakamwendea Hadhrat Maulawii Nuruddin r.a. nayo na kumpa. Akaipokea bila kusema neno na kisha akawaambia kwamba atatoa majibu baada ya kwisha kuomba mwongozo. Akasema: Twende pale palipo mwili wa bwana wetu na wanapotusubiri ndugu zetu. Alipofika bustanini, Mufti Muhammd Sadiq akasoma ombi lifuatalo sawa na matakwa ya waliokuwepo:

> "Kwa jina la Allah, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.
>
> Twamsifu Yeye na kumsalia Mtume wake Mkarimu. Sifa zote zamhusu Allah, Mola wa walimwengu, na baraka na amani zimwie *Khatamun Nabiyyin*, Muhammad s.a.w., Mteule, na zimwie Masihi Aliyeahidiwa, *Khatamul Auliya*.
>
> Sawa na agizo la Masihi Aliyeahidiwa lililomo katika *Al-Wasiyyat* (kijitabu cha Wasia), sisi Waahmadiyya ambao sahihi zao zimetiwa chini twakubali kwa unyofu kwamba

wanajumuiya wote wa Kiahmadiyya wa hivi sasa na wale watakaojiunga katika Jumuiya baadaye walazimika kufanya baiat, kwa jina la Ahmad a.s, kwa Mhamiaji wa kwanza Hadharat Haji Hakim Nuruddin r.a., ambaye ndiye mtaalamu zaidi na mwema zaidi kuliko sisi sote na rafiki mwaminifu zaidi tena wa zamani sana wa Hadhrat Imam a.s. kama alivyosema (katika ubeti wake mmoja wa Kiajemi):

Ingekuwa vizuri sana kama kila mmoja wa umati angekuwa Nuruddin. Ingekuwa hivyo kama kila moyo ungejaa mwanga wa yakini.

Amri za Hadhrat Maulawii Sahib zitalazimika kutekelezwa nasi kama zilivyokuwa amri za Masihi Aliyeahidiwa a.s."

Akijibu, Hadhrat Maulawii Sahib akatamka:

"Yaangalieni maisha yangu yaliyopita. Sikutamani uongozi hata kidogo. Najijua vizuri, na Mola wangu Ananijua vizuri zaidi. Sitamani chochote cha dunia. Nitakacho ni kwamba Bwana wangu Aniwie radhi. Kwa ajili hii nafanya maombi, na kwa hiyo nimekaa na nitaendelea kukaa Qadian. Kwa muda fulani nikatafakari kwamba baada ya Hadhrat Sahib tutakuwaje. Ndiyo maana nilifanya bidii sana kumwelimisha Mian Mahmud.

Kuna watu watatu wafaao miongoni mwa jamaa wa karibu wa Hadhrat Sahib a.s. Kuna Mian Mahmud Ahmad ambaye ni ndugu yangu na pia mwanagu. Ninao uhusiano naye maalum. Kisha kuna Mir Nasir Nawab, mkwewe Hadhrat Sahib a.s, anayestahaki heshima yake na kuheshimiwa nasi pia. Wa tatu ndiye Nawab Muhammad Ali Khan aliyemwoa bintiye Hadhrat Sahib a.s. Na miongoni mwa watumishi wa dini

waliojitolea sana ni Seyyid Muhammad Ahsan ambaye ana ustadi wa kuvutia sana. Yu miongoni mwa nasaba za Mtume Mtukufu s.a.w. Amepata kutumikia dini vizuri kabisa hata mtu kama mimi anaona haya. Katika uzee wake ametunga vitabu vingi kuhakikisha ukweli wa Hadhrat Sahib, na kwa njia hii ametoa huduma ya pekee. Tena kuna Maulawii Muahmmad Ali anayehudumia kwa njia ambazo siwezi kuwaza. Hao wote wapo Qadian. Miongoni mwa ndugu wa nje kuna Seyyid Hamid Shah. Maulawii Ghulam Hasan Khan na wengine wengi.

“Hili ni jukumu zito lenye hatari linaloweza kuchukuliwa na yule tu anayeamriwa na Mungu, ambaye ameahidiwa msaada wa Mungu unaomhifadhi akibeba mizigo mizito inayomlemea mgongo wake. Wakati huu hakuna budi kwamba wanaume kwa wanawake waungane pamoja. Na ili kupata shabaha hii fanyeni baiati kwa mheshimiwa mmojawapo kati ya wale niliowataja; mimi nami nitafanya hivyo pamoja nanyi. Mimi ni dhaifu, sina afya nzuri na tabia yangu hailingani na kazi hii iliyo nzito na si rahisi kutekeleza.

“Hadhrat Sahib r.a. alitekeleza kazi nne. (a) Kutimiza wajibu wake binafsi akiwa mtumishi wa Mungu. (b) Kusimamia ahali zake. (c) Kukaribisha wageni. (d) Kueneza Islam, na ndiyo ilikuwa shabaha yake hasa. Katika hizo ile (a) imekwenda pamoja naye. Alivyotekeleza hapa ndivyo atakavyotekeleza huko akhera. Hiyo mmeondolewa. Katika zile tatu zilizosalia, kueneza Islam ndiyo ya muhimu zaidi tena ngumu sana. Zaidi ya udahria (kutokumwamini Mungu), Islam inakabiliana na mafarakano na hitilafu za ndani. Waweza kuifikiria rahisi, lakini kwa yule anayebeba huo mzigo ni kazi nzito moja kwa moja.

Nawaahidi kwa makini kwamba mkimchagua mmojawapo wa wale niliowataja, nitafanya baiati kwake pamoja nanyi.

Lakini mking'ang'ania kufanya baiati kwangu, basi zingatieni kwamba baiati hii yamaanisha kujiuza kabisa. Safari moja Hadhrat Sahib a.s. alinidokezea, japo si waziwazi, kwamba nisiwaze tena habari za kwetu. Tangu hapo utii wangu na fikara yangu yote imekuwa kwa ajili yake tu, nami sikuwaza katu tena habari za kwetu. Basi kufanya baiati ndiyo jambo la uaminifu sana tena la muhimu kabisa. Yule anayefanya baiati huweka uhuru wake na fikara zake chini ya mwingine, ndiyo maana Mungu Mtukufu Kamwita mtu kuwa mtumishi Wake. Ni vigumu kwa mtu kutimiza wajibu wake binafsi akiwa chini ya utumwa huo; namna gani na kadiri gani aweza kujitwalia wajibu kama huo na kuutekeleza kwa niaba ya mwingine? Tukizingatia hitilafu za tabia mbalimbali, uthabiti wa hali ya juu sana hutakiwa kuleta mapatano. Sikuzote nilishangaa kwa kazi nyingi za Hadhrat Sahib a.s. Alikuwa na afya isiyo nzuri, hata hivyo alitekeleza kazi hizo nzito za aina mbalimbali. Lakini alifululiza kusaidiwa na Mungu; nami mwenye umri kama wake najiona mtu mtupu. Ni fadhili tu ya Mungu iliyotufanya tuwe ndugu sisi kwa sisi. Hamwezi kufaulu kupata lolote pasipo rehema Yake.

Ningependa kuwakumbusheni tukio moja kubwa la historia ya Kiislamu. Katika zama za *Ukhalifa* wa Hadhrat Abu Bakr r.a. bara zima la Uarabu, ukiacha Makkah, Madina na mahali pamoja au pawili pengine, likaasi. Wamakkah pia wakawa na mashaka na kusitasita, lakini yeye akawapa moyo kwa kuwasihi: 'Nyinyi mlikuwa wa mwisho kuamini, kwa nini mwapenda kuwa wa kwanza kukufuru?' Bintiye

Bi Aisha r.a. alisema: 'Kama mlima uliomwangukia baba yangu ungelimwangukia mwingine yeyote, yeye mtu huyo angelisagika kabisa.' Katika Madina watu elfu ishirini wenye nguvu na afya ya mwili walikuwapo, lakini kama alivyokuwa amenuia Mtume Mtukufu s.a.w. kutuma jeshi upande wa kaskazini, Abu Bakr r.a. akawatuma hao wote. Katika hali ngumu kama hiyo Mungu Mwenye nguvu Akaonyesha nguvu yake na Akadhihirisha ahadi yake hii kutimia: Hakika Atawaimarishia dini yao Aliyoridhia kwao. (24:56). Leo tunaikabili hali kama hiyo. Ninapenda kwamba kabla hatujazika mwili wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. kuimarike umoja baina yetu.

Baada ya kufariki Mtume Mtukufu s.a.w., masahaba zake walitakiwa chini ya uongozi wa Abu Bakr r.a. kutekeleza kazi kubwa nyingi, kubwa zaidi katika hizo ikiwa kukusanya Kurani Tukufu kwa sura ya Kitabu. Shughuli inayolingana na kazi hiyo leo hii ni kufanya matendo sawa na Kurani Tukufu. Kisha Abu Bakr r.a. akasimamia kukusanya zaka. Hii ni kazi kubwa sana inayohitaji utii wa hali ya juu; na kuna wajibu mwingine mwingi na faradhi zinazopaswa kutimizwa. Sasa mtalazimika kutii amri zangu bila kujali mwelekeo wenu binafsi ni nini. Kama mkikubali hii, nitachukua jukumu hili nikipenda nisipende.

Masharti kumi yaliyowekwa na Masihi Aliyeahidiwa yataendelea kutimizwa. Naongeza katika hayo na kusisitiza kufundisha Kuran Tukufu na kukusanya zaka, kutayarisha wahubiri na kazi nyingine ambazo Mungu Akipenda Aweza kutilia moyoni mwangu. Mafunzo ya dini na kozi za masomo katika chuo cha dini vitahitaji kibali changu. Nachukua

jukumu hili kwa ajili ya Mungu peke yake Aliyeagiza: Liwepo miongoni mwenu kundi liitalo kwenye heri na kuamuru kutenda mema na kukataza maovu (3:105).

Kumbukeni wema wote huanzia umoja. Watu wasio na kiongozi ni sawa na maiti."

Pindi alipomaliza kusema, wote waliokuwa wamewasili toka mbali na karibu wapatao 1200 wakasisitiza kwa neno moja: "Twafanya baiati kwako. Tutatii amri zako. U kiongozi wetu na *Khalifa* wa Masihi wetu a.s."

Walikuwa wameshughulikia maombi na kutiririsha machozi ili kupata mwongozo, sasa wakapata utulivu kuona kwamba wamejaaliwa mara nyingine tena kiongozi wa kiroho kwa sura ya Hadhrat Maulawii Nuruddin r.a. Wote wakafanya baiati kwake kwa kuapa kama Khalifatul Masih I. Maneno ya baiati yalikuwa haya:

"Nashuhudia kwamba hakuna apasaye kuabudiwa isipokuwa Mungu, Aliye Mmoja, Asiye na mshirika; nami nashuhudia kwamba Muhammad s.a.w. ni mtumishi wake na Mjumbe wake (yalikaririwa mara tatu).

Leo ninafanya baiati kwa mkono wa Nuruddin nikikubali masharti yote yaliyowekwa na Masihi Aliyeahidiwa a.s. kwa baiati; na ninaahidi hususan ya kwamba nitajibidiisha kusoma na kusikiliza Kurani Tukufu, Suna na Hadithi Sahihi na kutenda sawa nazo; na nitajiweka tayari kujitolea nafsi yangu na mali zangu kwa kueneza Islam sawa na uwezo wangu na njia zangu; na nitakuwa mwangalifu kutoa zaka; na nitafanya bidii kuimarisha uhusiano wa kirafiki baina ya ndugu.

Namwomba Mungu, Bwana wangu, msamaha wa makosa yangu, na ninaelekea Kwake nikitubu (yakarudiwa mara tatu).

> Mola wangu, nimejidhulumu nafsi yangu na ninakiri dhambi zangu. Nisamehe dhambi zangu, kwani hakuna awezaye kusamehe dhambi isipokuwa Wewe."

Wote walipokwisha fanya baiat, Khalifatul Masihi r.a. akaongoza sala ya jeneza ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. na kisha akaongoza sala ya alasiri. Ndipo kila mmoja akakimbilia kujionea mwenyewe mara ya mwisho sura yenye kupendeza ya marehemu wao Mtukufu. Mazishi yalimalizika saa 12:00 jioni. Sisi ni wa Mungu na kwake tutarejea.

Keshoye Khwaja Kamaluddin, mwana-*Sadr Anjuman Ahmadiyya* aliyekuwa katibu wake akachapisha na kueneza taarifa ifuatayo:

> "Kabla ya sala ya jeneza ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. wanajumuiya wote waliokuwepo Qadian ambao idadi yao ilikuwa 1200 wakamkubali Hadhrat Haji Hakim Nuruddin, Mungu Amlinde, kuwa naibu na *Khalifa* wake sawa na maagizo yaliyoandikwa katika *Al-wasiyyat* (Wasia) na kwa kuafikiana na mapendekezo ya wana-*Sadr Anjuman Ahmadiyya* waliokuwapo Qadian wakati huo na jamaa wa karibu wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. na kwa idhini ya Hadhrat Ummul Muminin; na wakafanya baiati kwake. Miongoni mwa wana-*Sadr Anjuman Ahmadiyya* waliokuwapo ni Maulawii Seyyid Muhammad Ahsan, Sahibzada Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad, Nawab Muhammad Ali Khan, Shaikh Rahmatullah, Maulawii Muhammad Ali, Dkt. Mirza Yakub Beig, Dkt. Seyyid Muhammad Husain Shah na Dkt. Khalifa Rashiduddin.
>
> Ingawaje kifo kilikuwa cha ghafla na nafasi ilikuwa kidogo, hata hivyo idadi kubwa ya ndugu waheshimiwa waliwasili kutoka Ambala, Jalandar, Kapurthala, Amritsar,

> Lahore, Gujranwala, Wazirabad, Sialkot, Jummu, Gujrat, Batala, Gurdaspur na penginepo, na wakamkubali kwa shauri moja Hadhrat Qibla Hakimul Ummat, Mungu Amlinde, na wakasali sala ya jeneza ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. Taarifa hii inatolewa kwa wanajumuiya wote kwamba pindi waipatapo, haraka sana wafanye baiati kwa Hadhrat Hakimul Ummat, Khalifatul Masihi wal Mahdi, wakija kwake binafsi au kwa njia ya barua."

Walipopokea taarifa hii, wanajumuiya wote haraka sana na kwa jazba wakafanya baiati, na katika muda usio mrefu Jumuiya nzima ikajumuika chini ya bendera moja.

Basi jahazi la Uahmadiyya lililoshushwa baharini miaka kumi na tisa hapo kabla likatoka salama katika tufani kali iliyolipata ghafla sana. Lakini muda si muda milio na ngurumo zikaanza kusikika. Dalili ya kwanza ya ufa ilidhihirika kabla wiki moja haijamalizika. Siku ya sita baada ya kufanya baiati ya *Khalifa* ambaye amri zake zilikuwa zitekelezwe kama zile za Masihi Aliyeadhidiwa a.s., Khwaja Kamaluddin akawasili Qadian. Akiongea na Sahibzada Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad akasema hivi: "Mian, tumeangukia katika kosa moja ambalo laweza kusahihishwa tukiweka mipaka madaraka ya *Khalifa*. Yeye achukue baiati ya wanajumuiya wapya, aongoze katika sala, atangaze ndoa za watu na aongoze sala za jeneza tu basi."

Hili lilikuwa wazo ambalo Sahibzada alilipinga akisema: "Fikira hii imechelewa sana kupendekezwa. Ungefikiria hiyo kabla ya kufanya baiati. *Khalifa* alifafanua kinaganaga kwamba baiati humaanisha utii mkamilifu. Tulifanya baiati kwa kufahamu hivyo. Uhusiano wetu na *Khalifa* sasa ni ule wa Bwana na watumishi. Hatuna madaraka ya kumwekea Bwana wetu mipaka ya madaraka yake."

Bw. Khwaja akatambua kwamba hakuweza kueleweka, kwa hiyo hakulifuatia jambo hili.

Kwa idhini ya Khalifatul Masihi, *'Ujumbe wa Suluhi'* yaliyo maneno ya mwisho ya Masihi Aliyeahidiwa, ulisomwa na Khwaja Kamaluddin, tarehe 21 Juni 1908, mbele ya hadhara ya watu maelfu kadha katika Ukumbi wa Chuo Kikuu, Lahore. Mwenyekiti alikuwa Justice Pratul Chandra Chattarji, Jaji wa Panjab Chief Court.

# XIII

## CHEO CHA KHALIFA

*Ukhalifa* ulipoanza, papo hapo na fikira hii ilianza kuenezwa kwamba cheo cha *Khalifa* ni cha Kiroho tu pekee, na kwamba kwa kusimamia Jumuiya na kuendesha mambo yake mengine *Sadr Anjuman Ahmadiyya* ndiyo mrithi wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. *Sadr Anjuman Ahmadiyya* ni chombo kinachojifanya upya mara kwa mara. Sawa na kawaida zake, zilizokubaliwa kwa kupendekezwa na Khwaja Kamaluddin, nafasi baina ya wana-*Anjuman* ikipatikana kwa sababu ya kifo au kujiuzulu kwa mmojawapo, ilijazwa kwa mchaguo wa wengi wa wana-*Anjuman* waliobakia. Basi kama wana-*Anjuman* wanane kwa akali miongoni mwa kumi na wanne wakiafikiana wakawa 'wengi' na wakaweza daima kuchagua mtu wa aina yao. Alipofariki Masihi Aliyeahidiwa a.s. kulikuwepo kikundi cha aina hii katika *Anjuman*, walio mashuhuri kati yao ni Maulawii Muhammad Ali, Khwaja Kamaluddin, Sheikh Rahmatullah, Dkt. Seyyid Muhammad Husain na Dkt. Mirza Yakub Beig, wanne wa mwisho wakiwa wakazi wa Lahore. Mwenyekiti alikuwa Maulawii Nuruddin r.a. na baadhi ya wanachama wengine walikuwa Seyyid Muhammad Ahsan, Sahibzada Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad, Nawab Muhammad Ali Khan na Khalifa Rashiduddin, Khwaja Kamaluddin alikuwa katibu.

Pindi Maulawii Nuruddin alipokuwa Khalifatul Masihi, hali ngeni ikapatikana, kwa sababu sasa yeye alikuwa *Khalifa* na kwa hiyo Kiongozi Mkuu wa Jumuiya nzima na pia Mwenyekiti wa *Sadr Anjuman Ahmadiyya*. Kile kikundi cha 'wengi' kilitumia hali hiyo ya aina ya pekee ya mkusanyiko usio wa kawaida wa vyeo viwili katika mtu mmoja kwa kuvuruga mambo. Wakaanza kukuza cheo cha kuwa

Mwenyekiti wa *Anjuman* kana kwamba cheo hicho kina madaraka makuu sio *Ukhalifa*. Mapema sana mnamo Desemba 1908, katika Mkutano wa Mwaka baadhi yao walisisitiza haja ya utii mkamilifu kwa *Sadr-e-A'la* (Mwenyekiti Mkuu) na kuafikiana na matakwa yake. Katika taarifa ya vikao vya *Anjuman*, maagizo ya Khalifatul Masihi yalielezwa kuwa ya Mwenyekiti. Tatizo hili la hali hii ngeni liliondolewa mnamo mwaka 1910 *Khalifa*-Mwenyekiti akajiuzulu kuwa Mwenyekiti kwa sababu vyeo hivi viwili havichanganyiki, na akaagiza kwamba Sahibzada Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad atakuwa Mwenyekiti wa *Anjuman*. Lakini mpaka wakati huo swala la nani ana uwezo zaidi baina ya *Khalifa* na *Anjuman* lilikwisha pata kuibuka.

Baada ya maelezo hayo yaliyokwenda upande mwingine kidogo, tutarejea kwenye mfululizo wa habari yenyewe. Maulawii Muhammad Ali ambaye akawa *Amiri* wa kikundi kisichokubaliana na wengine hakuwa na maoni ya kwamba Masihi Aliyeahidiwa alipofariki ilimlazimu kufanya baiati kwa Hadhrat Khalifatul Masihi, kama alivyoandika baadaye:

> "Masihi Aliyeahidiwa a.s. alifariki Lahore. Maiti yake ilipowasili Qadian, Khwaja Kamaluddin akaniambia katika bustani kwamba imependekezwa Hadhrat Maulawii Nuruddin awe *Khalifa*. Kisha akaniambia pia kwamba imependekezwa ya kuwa wanajumuiya wote wafanye baiati yake. Hapo nikasema hiyo siyo ya lazima. Waahmaiyya wapya tu wanapaswa kufanya baiati, na hiyo ndiyo iliyoandikwa katika *Al-Wasiyyat* (Wasia). Bado ninayo maoni haya kwamba waliokwisha fanya baiati ya Masihi Aliyeahidiwa hawalazimiki kufanya baiati kwa mwingine yeyote. Hata hivyo nilifanya baiati ili kudumisha umoja katika Jumuiya."

Kama ndiyo hivyo, anaonekana – kwa uchache wakati huo –

aliongozwa na nguvu ya moyo wa utii, kama inavyosadikishwa na maneno yake yafuatayo yaliyoandikwa katika kijitabu chake *'Tangazo Moja la Muhimu:'*

> "Kuna desturi nyingine ya baiati inayoendelea baina ya *Masufii* inayoitwa Baiati ya Toba. Mtu anayefanya baiati ya aina hiyo huwa chini ya amri za Mwalimu wake kama ilivyokuwa shabaha ya baiati kwa Mtume Mtukufu s.a.w. au kwa Masihi Aliyeahidiwa a.s. Lakini baiati hiyo hailingani na *Ukhalifa* wa mmojawapo katika hao. Baiati hii ndiyo tuliyofanya sisi wanajumuiya kwa mkono wa Khalifatul Masihi r.a., na kwa sababu ya baiati hii sisi sote twalazimika kutii amri zote za Hadhrat Khalifatul Masihi pamoja na zile zilizohusu imani. Baiati hii ilikuwa kwa shabaha ya kuimarisha uhusiano wetu wa kiroho na Mungu, na kujinufaisha kukaa na waja watukufu kama Hadhrat Khalifatul Masihi, na kuinamisha vichwa vyetu mbele ya utaalamu wake wa hali ya juu na mvuto wake. Kwa shabaha hii haina budi mwanafunzi ajitupe mbele ya mwalimu wake kama maiti na kusalimisha kwake matamanio yake yote; siyo kwamba mwalimu akisema jambo fulani ni sawa na linafaa, lakini mwanafunzi aseme kwamba mwalimu hakuelewa hilo vizuri bali nalielewa vyema. Baada ya kufanya baiati mwendo huo utaheshabiwa kuwa ni kumfanyia ufidhuli Hadhrat Khalifatul Masihi na kuifanyia dhihaka shabaha ya baiati."

Sawa na maneno hayo, yaonekana wazi kwamba Maulawii Muhammad Ali alikubaliana kabisa na maneno thabiti yafuatayo ya Hadhrat Khalifatul Masihi r.a.:

1. Naapa kwa jina la Allah kwamba Yeye ndiye Aliyenifanya *Khalifa.*

2. Nani awezaye sasa kuninyanganya joho la *Ukhalifa?*
3. Allah Amenifanya *Khalifa* kwa upendo wake na busara yake.
4. Waweza kunitolea makosa elfu, lakini kwa hakika mtakuwa mnamtolea kosa Mungu shauri Yake Aliyenifanya *Khalifa*.
5. Jinsi Abu Bakr r.a. na Umar r.a. – Mungu Awawie radhi – wakawa *Makhalifa*, ndivyo Mungu Mtukufu Alivyonifanya *Khalifa* baada ya Hadhrat Mirza Sahib.

Katika *'Tangazo Moja la Muhimu'* Maulawii Muhammad Ali alisema:

> "Mtukufu huyu Maulawii Nuruddin anayeitwa Khalifatul Masihi ndiye peke yake anayestahili kuitwa hivyo katika muradi wa kweli wa neno hili."

Kwa hayo Maulawii Muhammad Ali anaweza kumaanisha kwamba hata kama Maulawii Nuruddin akikubaliwa kuwa Khalifatul Masihi katika maana ya kweli ya neno hili, hiyo haina maana kwamba *Ukhalifa* utaendelea baada yake pia. Lakini shaka yoyote kuhusu habari hii ikaondolewa na Khalifatul Masihi kwa kutangza:

> "Hamwezi kufaidika na mabishano hayo. Hakuna yeyote atakayewafanyeni *Khalifa,* wala yeyote hawezi kuwa *Khalifa* katika uhai wangu. Nikifa, yule tu ataibuka ambaye Mungu Atamchagua na kumwinua."

Basi itambulikane ya kwamba kiini cha mabishano hayo yaliyojitokeza kilikuwa ni *Ukhalifa*. Hitilafu nyinginezo za kiitikadi zilizushwa na wapinzani wa *Ukhalifa* kuusaidia msimamo wao na kuupa nguvu.

Hata hivyo kuhusu swala hasa walikuwa tayari, shingo upande, kumtambua Hadhrat Maulawii Nuruddin r.a. kuwa Khalifatul Masihi. Kwa sababu ya kishindo cha kufadhaisha cha kifo cha ghafla cha Masihi Aliyeadhidiwa a.s. walikwisha jifunga sana pasipo kuacha nafasi ya kurudi nyuma bila kuona haya. Wenyewe walifumba mikono yao kwa nguvu sana. Haraka wakatambua kwamba walifanya kosa, na wakaanza kutafuta hila zitakazowasaidia kujitoa katika hali ngumu kwa fedheha kidogo zaidi. Kumpinga *Khalifa* moja kwa moja kusingeliweza kuvumiliwa na sehemu kubwa ya Jumuiya na kwa hiyo hakungelikuwa na busara. Khalifatul Masihi r.a. alikuwa anakurubia miaka sabini, na hakuwa na afya nzuri sana. Katika muda usio mrefu swala la uchaguzi wa *Khalifa* litajitokeza. Wakataka kuelekeza fikira ya Jumuiya kwenye jambo hili ya kwamba *Sadr Anjuman* inayo madaraka makubwa zaidi, na kwamba *Khalifa* ni mwalimu tu wa kiroho kama alama anayestahili kupewa heshima na taadhima kwa sababu ya cheo hiki lakini hana madaraka yoyote. Wakachelea kwamba Sahibzada Mirza Bashiruddin Mahumd Ahmad anaweza kuwa Khalifa ambaye alikuwa mwenye umri wa karibu miaka ishirini, kijana tu ambaye Khalifatul Masihi alimpendelea na alionekana kumheshimu sana mno. Kwa sababu hiyo walikuwa na kiherehere kwamba ukuu wa *Sadr Anjuman* kwa kulinganishwa na *Khalifa* uimarishwe wazi wazi.

Kwa kupata shabaha hiyo, baadhi yao hawakuwa na huruma hata kugeuza mafunzo imara ya dini. Wakahoji kwamba kutaja aya 24:56 ya Kurani Tukufu na kutoa mfano wa Hadhrat Abu Bakr r.a. ili kuupa nguvu *Ukhalifa* ni bure. Kwani Mtume Mtukufu kweli alikuwa na *Makhalifa* waliomfuata nyuma yake, lakini Masihi Aliyeahidiwa ambaye mwenyewe alikuwa *Khalifa* wa Mtume Mtukufu s.a.w., na hakuwa Nabii wa kujitegetemea, hangeweza kuwa na *Khalifa*. Kwa mfano, Dkt. Basharat Ahmad aliyekuwa mmojawapo wa wale waliotia sahihi chini ya ombi lililoandikwa alilopelekewa Hadhrat Maulawii

Nuruddin r.a. tarehe 27 Mei 1908 ili akubali kuwa Khalifatul Masihi, akajasiri kuandika:

> "Tulikuwa tumesema wazi wazi kwa uthabiti ya kwamba Mirza Sahib hakuwa Nabii bali alikuwa *Khalifa* wa Mtume Mtukufu s.a.w. *Ukhalifa* huufuata Unabii tu, *Ukhalifa* wa *Khalifa* hauna maana."

Maneno hayo yalipingana moja kwa moja na maneno thabiti yaliyosemwa mara kwa mara na viongozi wa kundi la Dkt. Basharat Ahmad, bali kwa hakika mwenyewe alihusika na maneno thabiti yafuatayo:

> "Kwa kifupi, kutakuwa na Manabii na wajumbe lakini watakuwa wafuasi wa Mtume Mtukufu s.a.w., na kwa hiyo Ujumbe wao na Unabii wao hautakuwa dhidi ya Muhuri wa Manabii."

Mifano mingine yaweza kutolewa pia ili kufafanua jambo hili. Mnamo 1903, Maulawii Muhammad Ali akitoa ushahidi kwa kula kiapo katika kesi ya jinai ya kashfa ambapo Maulawii Karam Din alimshtaki Masihi Aliyeahidiwa a.s., alihakikisha:

> "Mshtakiwa Mirza Sahib ni mdai wa kuwa Nabii. Alieleza madai yake katika vitabu vyake. Madai yake ni kwamba yu Nabii lakini hakuleta sheria."

Akitoa hotuba iliyoripotiwa katika *Al-Hakam* la Julai 18, 1908, alitamka:

> "Mpinzani anaweza kueleza aya (4:70) kwa njia yoyote, lakini sisi twaona kwa yakini kabisa kwamba Mungu Anaweza kumfanya mtu kuwa Nabii, Siddiki, Shahidi na Mwema. Kinachohitajika ni mtafutaji. Yule ambaye tulifanya baiati

> ndiye Mteule wa Mungu na Mjumbe Mtukufu. Amejaa roho takatifu kikamilifu kabisa."

Akihutubia mkutano mjini Batala, Khwaja Kamaluddin alisema:

> "Nabii na Mjumbe mmoja ametokea karibu yenu. Ni juu yenu kumpokea au la."

Dkt. Seyyid Husain akanena kwa nguvu:

> "Tunamshukuru sana mno Mungu kwamba kutimia kwa utabiri wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. kwahakikisha ya kuwa wahyi aliofunuliwa ni Neno la Mungu na kwamba aliyefunuliwa huo ndiye Mjumbe wa Mungu. Allah Ameleta uthibitisho usio na shaka."

Dkt. Mirza Yakub Beig alisema: "Ni fadhili ya Mungu kwamba ili kuwaelimisha watu wenye busara ya wasitani kama sisi Yeye huwainua Manabii, Mawalii na watu wema katika zama zote."

Maulawii Umaruddin wa Simla akatamka:

> "Wapinzani wetu wameghadhibika juu ya maelezo ya Hadithi: 'Hakuna Nabii baada yangu.' Wanaisoma mara kwa mara kila wakati na kwa sababu hiyo wanatangaza madai ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. kuwa Nabii kwamba ni ukafiri na ulaghai. Wamekuwa kama mafakihi wa Kiyahudi. Muradi wa Hadithi hiyo ni kwamba hakuna Nabii mwenye kuleta Sheria baada ya Mtume Mtukufu s.a.w., lakini anaweza kutokea Nabii aliye mtumishi wake."

*'Paighame Sulh,'* gazeti la kundi la wapinzani litolewalao mjini Lahore lilitangaza katika toleo lake la tarehe 16 Oktoba 1913:

> "Tumepata habari ya kwamba baadhi ya marafiki zetu wameongozwa vibaya kwa kufikiria kwamba wale

wanaohusikana na gazeti hili, au baadhi yao, wanadunisha daraja tukufu la bwana wetu na mwongozi wetu Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad, Masihi Aliyeahidiwa na Mahdi a.s. Sisi Waahmadiyya wote tunaohusikana na *Paighame Sulh* kwa njia yoyote twamfanya Mungu Ajuaye sana siri za mioyoni kuwa shahidi na kutangaza ya kuwa kulinasibisha hilo kwetu ni masingizio makubwa sana. Twamwamini Masihi Aliyeahidiwa na Mahdi a.s. kuwa Nabii, Mjumbe na Mwokozi wa zama hizi."

Basi kujitetea kwamba kwa kuwa Masihi Aliyeahidiwa a.s. hakuwa Nabii, basi hakuna *Khalifa* baada yake ni ujanja tu; wala hauna maana. Lakini wakiisha tumia njia hii ya hila katika majibizano, hiyo ikawa ni sehemu ya imani ya wapinzani wa *Ukhalifa*. Wakaona faida nyingine tena katika kukataa Unabii wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. Wakafikiri kwamba wakiacha kukazania habari hii, kizingiti kilichopo katika njia ya Waislamu wengi wa kawaida wanaoitambua Jumuiya Ahmadiyya kitaondolewa na wao pamoja na wale wanaofikiria namna moja watapokelewa kwa shangwe kuwa viongozi waliokuwa mbele katika juhudi za kujadidisha Islam kiroho na kiutambuzi. Msingi wao utakuwa mafundisho na hekima ya Islam jinsi alivyoeleza Masihi Aliyeahidiwa, lakini hawatakazania madai yake yakubaliwe. Baadhi yao, hususan Khwaja Kamluddin, wakaanza kuhutubia mikutano ya hadhara kwa njia hiyo na wakafikiria kwamba wanafanikiwa sana. Ikawachukua muda kugundua kwa masikitiko kwamba walikosea sana.

Kuhusu *Ukhalifa* ingeliwatosha kwamba Masihi Aliyeahidiwa alipata kutaja wazi wazi *Ukhalifa* mara kwa mara katika maandiko yake na hotuba zake. Kwa mfano, wiki sita tu kabla hajafariki alisisitiza katika hotuba yake moja:

> "Masufii wamesema ya kwamba yule mtu anyekadiriwa kuwa *Khalifa* baada ya Sheikh, Mjumbe au Nabii, ndiye wa kwanza anayetiliwa moyoni uwezo wa kupokea haki. Kifo cha Mjumbe au Sheikh ni tetemeko kali na ni wakati wa hatari kubwa. Lakini Mungu Anaondolea mbali mashaka kwa njia ya *Khalifa*, na *Khalifa* anaitilia nguvu upya shabaha ya ujaji wa marehemu. Kwa nini Mtume Mtukufu s.a.w. hakumteua *Khalifa* kumfuata yeye? Kwa sababu alijua sana kwamba Mungu Mwenyewe atamleta *Khalifa*; kwa sababu kuweka *Khalifa* ni kazi yake, na uchaguzi wake ni safi kabisa. Basi Yeye Akamfanya Abu Bakr r.a. kuwa *Khalifa* kwa kumfanya wa kwanza kabisa kumtilia moyoni mwake uwezo wa kupokea haki."

Huo ulikuwa uthibitisho wazi wazi kwamba yeye mwenyewe atafuatwa na *Khalifa*, na kwamba huenda akawa Maulawii Nuruddin r.a. aliyekuwa wa kwanza ambaye alitiliwa moyoni uwezo wa kupokea haki. Kumhusu yeye, aliwahi kuhakikisha mapema:

> "Yeye alinipokea bila kusita wakati nilipokuwa karibu kukufurishwa kutoka kila upande, na wengi waliofanya baiati wakaitupilia mbali, au wakateleza na kuangukia katika shaka. Tena ni Maulawii Sahib ambaye barua yake ilinifikia kwanza kabisa katika Qadian akipokea madai yangu ya kuwa Masihi Aliyeahidiwa, ambamo akaandika: 'Tunaamini na tunakubali, basi tuandike miongoni mwa mashahidi."

Basi hilo lilikuwa agizo la Mungu lililosukuma nyoyo za wote waliohudhuria katika ushirika wa kiroho mjini Qadian jioni ya 27 Mei 1908, kutangaza kwa sauti moja kumpokea Maulawii Nuruddin r.a. kuwa Khalifatul Masihi na kufanya baiati kwake, wa kwanza miongoni mwao wakiwa wana-*Sadr Anjuman* ambao mara baadaye

wakadai kwamba *Anjuman* ina madaraka makubwa zaidi kuliko *Khalifa*. Katika saa ya upeo wa hatari kwa kulazimika na hali ya kiroho wakapata kusema kwa uthabiti: "Amri zake hatuna budi kuzitekeleza kama zile za Masihi Aliyeahidiwa a.s. Walikuwa hawakujiachia nafasi ya kukimbia. Ni dhahiri, hiyo ilikuwa kazi ya Mungu. Lakini muda si muda wakaanza kujitafutia nafasi ya kukimbia. Ujanja ukachukua mahali pa uharara na unyofu. Maenezi yao yalipoibuka, wale wenye busara ya kiroho wakajitahadhari.

Mmoja wao, Mir Muhammad Is'haq, mdogo wa Hadhrat Ummul Mumini, mtaalamu mwenye busara na mtawa, mtu aliyekuwa mfano katika utakaso na unyofu, akapanga maswali kadha mwanzoni mwa Januari 1909 kuhusu madhumuni ya uhusiano baina ya *Khalifa* na *Sadr Anjuman* na kumletea Hadhrat Khalifatul Masihi r.a., akimwomba kuyafafanua akipenda. Khalifatul Masihi r.a. akampelekea Maulawii Muhammad Ali hayo maswali na kumwagiza kuleta majibu sawa na maoni yake. Khalifatul Masihi r.a. alipopokea maoni yake, akashtuka kwa maoni hayo ambayo yalidhihirisha kwamba mwandishi anaafikiana na waliohitilafiana ambao wanatafuta kukomesha *Ukhalifa*. Kwa mfano aliandika:

> "Haionekani kutoka kwa agizo la Wasia wa Masihi Aliyeahidiwa a.s kwamba *Khalifa* lazima awe mtu mmoja, ijapokuwa yaweza kuwa hivyo katika baadhi ya hali mahususi kama iliovyo hivi sasa. Kwa hakika Hadhrat Sahib alifanya *Anjuman* kuwa *Khalifa*. Siyo lazima kwamba mtu mmoja pekee awe *Khalifa*."

Hapo ndipo Khalifatul Masihi r.a. akaagiza nakala nyingi za maswali hayo zitayarishwe na viongozi wa Jumuiya wapelekewe hizo ambao watapaswa kuleta majibu yao ifikapo tarehe fulani, na wajumbe kutoka matawi yote wajumuike Qadian tarehe 31 Januari kwa kushauriana.

Maswali yalipomfikia Khwaja Kamaluddin huko Lahore, akaitisha kikao cha Jumuiya nyumbani mwake na kuwatolea hotuba kali kwamba Jumuiya inakabili hatari kubwa ambayo yaweza kuangamiza Jumuiya kama hawatakuwa waangalifu, na kwamba *Khalifa* hasa wa Masihi Aliyeahidiwa ni *Anjuman*, na kwamba kama hiyo haitaimarishwa, Jumuiya itatupwa katika hatari na mwendeleo utaangamia. Akawataka kuunga mkono maoni yake hayo. Wawili tu miongoni mwao, Hakim Muhammad Husain Qureshi, Katibu wa Anjuman wa hapo, na Babu Ghulam Muhammad, msimamizi wa Idara ya Reli, wakakataa kuunga mkono, juu ya msingi huu kwamba baada ya kwisha kufanya baiati kwa mheshimiwa aliye mtaalamu zaidi na mcha-Mungu kuliko hao wote, ambaye alimheshimu Masihi Aliyeahidiwa a.s. kuliko yeyote miongoni mwao, watamtii yeye katika yote atakayoamuru.

Habari ya kikao hicho ilipofika Qadian Sheikh Yakub Ali Irfani, Mhariri wa *Al-Hakam*, akaitisha kikao nyumbani mwake ambamo hotuba zilitolewa kuunga mkono *Ukhalifa* na cheo chake cha hali ya juu kabisa, na wakakubali azimio la kuthibitisha kujitolea kwa unyofu kwa *Khalifa*. Miongoni mwa waliokuwapo wawili tu wakakataa kuliunga mkono azimio hilo.

Mpaka jioni ya tarehe 30 Januari, wajumbe wote wa Jumuiya wakajumuika Qadian. Wengi wao wakapitisha usiku katika sala na maombi katika Masjid Mubarak, wengine wakaungana nao kabla ya kupambazuka. Kulikuwa na vilio vya kwikwi kwa Mungu na maombi yenye uchungu ili kupata mwongozo kana kwamba asubuhi itakuwa Siku ya Kiyama. Adhana ya sala ya alfajiri ilipotolewa na wote wakahudhuria msikitini, wenye kutetea mamlaka makuu ya *Sadr Anjuman* Ahmadiyya wakifaidika na nafasi kabla ya ujaji wa Khalifatul Masihi r.a. wakawasisitizia waliokuwa wanangojea sala

usahihi wa maoni yao. Sheikh Rahmatullah akasikika akisema kwa nguvu: "Msiba kweli huu kwamba wakorofi wachache wanataka kumfanya kijana mmoja kuwa *Khalifa* na kuiangamiza Jumuiya."

Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akaja kuongoza sala na kimya kikawashika waliofika kusali. Baada ya kusoma sura *Fatiha*, akasoma sura ya 85 ya Kurani Tukufu. Alipofikia aya ya 11:

> "Hakika wale wanaowafitini waaminio wanaume na waaminio wanawake, kisha hawakutubu, basi itakuwa kwao adhabu ya Jahanamu, na watapata adhabu ya kuungua."

Sauti yake ikakatika na waabuduo wakatawaliwa na kishindo cha maono. Akakariri aya hiyo kwa sauti iliyokatika-katika na msikiti ukajaa kelele za vilio na maombolezo ya waabuduo walioshtushwa. Nyoyo zote zikaonekana zimetakaswa na kujazwa huba ya Mungu. Imani halisi ikawatawala wote. Kila mmoja akahisi kwamba ameshuhudia ishara ya kimbinguni. Sala ikaisha na Khalifatul Masihi r.a. akaenda nyumbani.

Wapinzani wakafaidika na hali ya majonzi ya waabuduo, na Khwaja Kamaluddin akaliambia kundi lao moja ya kwamba kwa kukariri mara kwa mara aya 85:11 kwa uchungu, Khalifatul Masihi amethibitisha ya kwamba wale wanaoipuuza *Anjuman* ambayo Masihi Aliyeahidiwa aliifanya *Khalifa* wake, na kuufikiria *Ukhalifa* kuwa bora zaidi wamefanya kosa la kuihangaisha Jumuiya na watapata adhabu kali sana. Ni masikitiko makubwa kufikiria kwake visivyo! Yeye na wenzake wakafumbuliwa macho. Akifuata shauri yake, Dkt. Mirza Yakub Beig akamwendea Khalifatul Masihi na akasema kwa nguvu: "Hongera sana! Kila mmoja amebainishiwa kwamba *Anjuman* ndiyo *Khalifa*."

Akajibiwa: "*Anjuman* ipi? *Anjuman* unayodhania kuwa

*Khalifa* si chochote."

Mjumbe akarudi na majonzi. Mambo yakaanza kuwa magumu! Lakini yeye pamwe na wale aliowawakilisha walikuwa hawajajua kitu gani kipo tayari kujitokeza haraka.

Kikao cha kushauriana kiliitishwa kufanyika juu ya sakafu ya paa la msikiti iliyokuwa wazi; walikuwa watu wapatao mia mbili na hamsini. Walipokwisha wasili wote Hadhrat Khalifatul Masihi akafika na akakaribishwa kukaa mahali alipotayarishiwa katikati ya paa. Lakini alikataa na akaenda upande wa kaskazini na kusimama katika sehemu iliyokuwa imejengwa kwa agizo la Masihi Aliyeahidiwa a.s. paa la matofali lilikuwa wazi.

Miaka michache baadaye, Hadhrat Khalifatul Masihi II r.a. akaeleza habari hii kama ifuatavyo:

> "Machoni mwa mtu wa dunia, mkutano huo wa watu mia mbili na hamsini waliokaa kwenye sakafu wazi ni kitu hafifu kisicho na maana, lakini nyoyo zao zilikuwa zimejaa imani na waliamini kabisa katika ahadi za Mungu. Walihisi kwamba wamejumuika kuamua hali ya Jumuiya katika siku zijazo itakuwaje ambayo kwayo amani na maendeleo ya dunia yategemea. Siku hiyo itahakikisha kwamba Ahmadiyya ni Jumuiya mojawapo ya kidunia ama ni Jumuiya ya wafuasi wakweli wa Mtume Mtukufu s.a.w. ambayo kwa njia yake Islam itapata kujadidishwa. Siku hiyo hatima ya binadamu ilitakiwa kuamuliwa. Leo habari hii pengine haiwezi kuzingatiwa, lakini katika muda usio mrefu itatambuliwa kwamba mwendeleo huu hafifu wa kidini utakuwa na nguvu sana kuleta mapinduzi matakatifu ya amani duniani kuliko miendeleo mikubwa ya kisiasa."

Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. alianza kusema. Kwa sauti nzito na ya taratibu akaainisha ya kwamba *Ukhalifa* ni itikadi ya kidini na ni kitu cha lazima kwa Jumuiya kupata maendeleo. Akasema:

> "Mungu Ameniambia kwamba kama mmoja wenu akiniacha, Yeye Atanipatia kundi kubwa badala yake. Basi siwategemeeni nyinyi. Namtegemea Mungu kwa rehema yake kikamilifu kwamba Atanisaidia."

Kisha kuhusu majibu yaliyotolewa na Maulawii Muhammad Ali na Khwaja Kamaluddin, akasema:

> "Nimeambiwa kwamba kazi pekee ya *Khalifa* ni kuongoza sala za kila siku na sala za jeneza, kufunga ndoa za watu na kuchukua baiati. Yeyote asemaye hayo ni mjinga na mshupavu. Mtu kama huyo apaswa kutubu, la sivyo atajidhuru."

Akasihi:

> "Mmeniudhi sana mno kwa mwenendo wenu na mmefanya hatia ya kubeza *Ukhalifa*."

Akaongea kuhusu cheo cha *Khalifa*, na sifa na ubora wa utii anaostahili kufanyiwa, hata kwamba kusiwe na shaka moyoni mwa mtu kuhusu matokeo ya baiati. Akawalaumu waliofanya hatia ya kutokuwa waaminifu kwa *Khalifa*, na akaeleza kwamba amewakasirikia wale walioitisha mkutano kuupendelea *Ukhalifa* pasipo ruhusa yake. Mwishowe akawaita baadhi ya watu kueleza maoni yao. Sahibazada Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad r.a. na Nawab Muhammad Ali Khan wakaeleza kuafikiana naye kabisa na kwamba wakati wowote hawakuwa na hitilafu yoyote. Khwaja Kamaluddin akatoa maelezo yasiyo wazi sana lakini yalikuwa ya kutuliza.

Hapo Khalifatul Masihi r.a. akawataka Maulawii Muhammad

Ali na Khwaja Kamaluddin kufanya baiati upya. Akawashauri waende faraghani na kushauriana wao kwa wao kwamba wako tayari kufanya hivyo. Akamwita pia Sheikh Yakub Ali Irfani aliyekuwa ameitisha mkutano kuunga mkono *Ukhalifa* na kujadidisha baiati. Wote watatu wakaitikia na kikao kikamalizika. Wote wakapata kutulia kwamba hatari kubwa imetoweka na Jumuiya imesalimika katika hatari kubwa ya mfarakano.

Lakini Maulawii Muhammad Ali na Khwaja Kamaluddin walifura kwa hasira iliyofochwa. Mara waliposhuka chini kutoka kwenye paa la msikiti, Maulawii Muhammad Ali alisikika akimwambia Khwaja Kamaluddin kwa hamaki: "Tumefedheheshwa sana na kudhalilishwa na mtu anayedai kuongoza Jumuiya. Siwezi kuvumilia hayo."

Baada ya siku mbili au tatu, Khalifa Rashiduddin r.a., mwenyewe mwaminifu sana na mtiiifu, tena mnyofu, aliyemheshimu sana Maulawii Muhammad Ali na kumfikiria kuwa nguzo madhubuti ya nguvu ya Jumuiya, akaja kwa Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akihangaika mno kana kwamba mbingu iko tayari kuanguka chini, na kusema ghafla: "Msiba mkubwa unataka kutokea. Tafadhali chukua hatua haraka kuuzuia." Alipoambiwa afafanue usemi wake akasema akitweta: "Maulawii Muhammad Ali anasema amefedheheshwa vibaya sana, basi hawezi kuendelea kukaa Qadian. Tafadhali, fanya chochote haraka kumzuia isije akaondoka Qadian." Hapo Hadhrat Khalifatul Masihi akasema: "Nenda ukamwambie Maulawii Muhammad Ali nimesema kwamba hana haja ya kuchelewa kuondoka. Yu huru kwenda mara moja." Bwana Khalifa akaduwaa na kuguna: "Hapo naogopa fitina itaibuka." Khalifatul Masihi r.a. akarudisha: "Bwana Daktari, nimekwisha toa kauli yangu. Fitina ikitokea, itaelekezwa kwangu. Wahangaikia nini? Mwambie akitaka kuondoka Qadian,

anaweza kuondoka sasa hivi."

Basi ni dhahiri kwamba katika kujadidisha baiati yao Maulawii Muhammad Ali na Khwaja Kamaluddin waliinama tu mbele ya dhoruba lakini hawakuwa na nia ya kugeuza mwenendo wao. Muda si muda jambo fulani likatokea kuutahini uaminifu wao. Hakim Fadhl Din r.a. wa Bhera, jamaa wa karibu wa Hadhrat Khalifatul Masihi r.a, alikuwa ameiachia *Sadr Anjuman* sawa na wasia wake milki fulani huko Bhera ambayo aliinunua kutoka kwa Mshia mmoja aliyeiuza kwa sababu ya shida yake fulani ya muda. *Anjuman* ikaamua kuiuza milki hiyo. Mwuzaji wake wa kwanza alipopata habari hii, akamwandikia Khalifatul Masihi akieleza sababu zilizomfanya kuiuza milki hiyo kwa Hakim Fadhl Din, na akamwomba auziwe hiyo milki tena, kwa masharti ya kufaa. Khalifatul Masihi r.a. akalipeleka ombi lake kwa *Sadr Anjuman* na kuagiza lifikiriwe kukubaliwa. Anjuman ikajibu hivi kwamba milki hiyo inadiwe na bwana huyo aliyeimiliki zamani ataweza kuizabuni. *Anjuman* haikutaka kumsaidia isije Anjuman ikapata hasara. Hadhrat Khalifatul Masihi akaona kwamba moyo huu sio tu unakosa ukarimu bali ni wa kumchukiza yeye, na akaeleza kutokuridhika kwake kwa kuandika: "Fanyeni mpendavyo; sijihusishi tena na jambo hili."

Swala hilo lilipokuja tena katika kikao cha wadhamini wa *Anjuman*, Katibu akawakumbusha wadhamini wajibu wao kwa Mungu na kuwauliza ifanywe nini. Sahibzada Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad akatoa maoni yake kwamba Hadhrat Khalifatul Masihi alitaka kumfanyia hisani yule mmiliki wa kwanza wa milki hiyo, basi matakwa yake yatekelezwe. Katibu akasema ya kwamba Khalifatul Masihi aliwaachia kuliamulia jambo hili, na akasoma maneno yake; ndipo Sahibzada Sahib akafafanua kwamba maneno hayo yalieleza kuchukia kwake siyo kuwapa ruhusa, hivyo hakuna

budi kufanya alivyotaka. Majadiliano marefu yakafuata na Sahibzada Sahib akasihiwa mara kwa mara kuzingatia wajibu wake kwa Mungu, akiwa mdhamini, lakini yeye akang'ang'ania rai yake aliyokwisha ieleza. Hatimaye uamuzi ukafanywa na wengi wao kinyume cha hoja yake.

Taarifa hiyo alipopelekewa Hadhrat Khalifatul Masihi r.a., yeye akawaita wadhamini waliokuwa wamesisitiza ya kwamba uamuzi huo umefanywa baada ya kujadiliana kikamilifu na kushauriana ambamo Sahibazada Sahib vilevile akashiriki. Sahibzada Sahib akaitwa. Alipowasili, Hadhrat Khalifatul Masihi akamwuliza: "Imekuwaje, Mian; maagizo yangu bayana yamehalifiwa?"

Akajibu: "Hudhur, sikumbuki kufanya ukosefu wa aina hii."

"Niliwaagiza kuhusu uuzaji wa milki ya Hakim Fadhl Din katika Bhera. Kwa nini imefanywa kinyume chake?"

"Hudhur, sikushirikiana nao kuhalifu. Niliwasisitizia mara kwa mara kufanya sawa na maagizo yako, na kukazania kwamba maneno yako yalimaanisha kukasirika kwako siyo kuidhinisha wafanye wapendavyo."

Kisha Khalifatul Masihi r.a. akaelekea kwa wengine na kasema: "Mwasema huyu ni kijana tu mdogo, hata hivyo yeye alifahamu barabara maneno yangu, lakini ninyi mlishindwa kuyaelewa."

Akawasihi kwa muda fulani akifafanua kwamba utii ni chanzo cha baraka, na kwamba wanapaswa kujirekebisha, la sivyo watajinyima rehema ya Mungu.

Mdogo wa Hakim Fadhl Din r.a. alikuwa tayari kutoa bei nzuri kwa milki hiyo, lakini alipoelewa hitilafu baina ya Khalifatul Masihi r.a. na *Anjuman* akajitoa na *Anjuman* haikubakiwa na njia isipokuwa

kutekeleza alivyotaka Khalifatul Masihi. Wadhamini wakaidi wakamwomba Khalifatul Masihi r.a radhi sana, lakini hayakutokea mabadiliko katika mwenendo wao na propaganda yao dhidi yake ikaendelea mbele kwa kasi. Mnamo Septemba 1909, akatangaza ya kwamba kama haitaonekana tofuti katika mwenendo wao mpaka *Idil-Fitri,* wataondolewa katika Jumuiya. Hapo viongozi wa kundi hilo wakaomba radhi, lakini mwenendo wao haukuonyesha tofauti yoyote hasa.

Katika hotuba ya Idi, tarehe 19 Oktoba 1909, Hadhrat Khalifatul Masihi akawasihi mara nyingine kwa kirefu. Miongoni mwa mambo mengine akaeleza:

> "Jumuiya yoyote haiwi bila umoja na mapatano. Hamwezi kupata maendeleo pasipokuwa na umoja."

Akiwataja Adam a.s, Daudi a.s. na Abu Bakr r.a. wakiwa Makhalifa na wale waliowapinga, akasema kwa uthabiti:

> "Sasa mimi ni *Khalifa* wenu, kama mtu akisema kwamba jina Nuruddin halikutajwa katika Wasia wa Hadhrat Sahib a.s., nitamjibu: Wala majina ya wale niliowataja hayakutajwa katika tabiri za zamani.
>
> Jumuiya nzima kwa shauri moja imenikubali kuwa *Khalifa*. Atendaye kinyume cha shauri hilo la pamoja anampinga Mungu, kama ilivyosemwa katika Kurani Tukufu: Atakayefuata njia isiyo ya waaminio, Tutamwingiza katika Jahanamu (4:116). Tena sikilizeni kwa makini ya kwamba kama mkitenda kinyume cha ahadi yenu mioyo yenu itajazwa unafiki (9:77). Kwa nini nawasihini hivyo? Kwa sababu baadhi yenu wana upungufu wa elimu na mara kwa mara wanaonyesha udhaifu. Sidhani kwamba wanajua vizuri kuliko mimi.

Nahakikisha na kukazania kwa nguvu zangu zote na ninamfanya Mungu kuwa Shahidi kwamba sitavua joho hili Alilonivika. Amenichagua kwa shabaha fulani. Kama nyinyi na dunia nzima ikinipinga, sijali. Timizeni ahadi zenu, muone mnasonga sana mbele namna gani na jinsi mnavyofaulu. Nalazimika kusema hayo kwani hakuna budi yasemwe hayo. Yeye Amenihakikishia kwamba Ataniauni. Siwatakini kufanya baiati upya. Shikamaneni kwa imara na baiati yenu ya kwanza, isije mkaangukia unafiki. Kama mkiona nimepotea, nirekebisheni kwa kuniombea. Lakini msiwaze kunifundisha maana ya kweli ya aya fulani ya Kurani Tukufu, au ya Hadithi, au ya maandiko ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. Kama mmoja wenu anafikiri kwamba mimi ni mpotovu, amwombe Mungu Aniondoe katika dunia, kisha aone maombi hayo yanamrudia nani.

Kosa jingine linahusu neno *Ma'ruf* (mema). Inasemwa kwamba baiati inawalazimisha katika mambo wanayofikiria ni mema. Kurani Tukufu inatumia neno hilo kuhusu utiifu mbele ya Mtume Mtukufu s.a.w. pia (60:130). Je, basi, wamekwisha orodhesha makosa yake? Kadhalika, Masihi Aliyeahidiwa a.s. naye ameweka kumtii katika *Ma'ruf* (mema) kuwa sharti mojawapo ya baiati. Ninafafanua hayo yote ili kuwalindeni msiangukie kosa.

"Tena ilisemwa kwamba ninaonana na kila mtu bila kujali kitu. Jibu langu kwa kifupi kwa waliofanya baiati kwangu ni: Ninyi mnalazimika kufuata maagizo yangu; lakini mimi silazimiki kufuata maagizo yenu. Mimi nahofia isije mkajaribiwa. Jambo hili kwamba mkome kuwa na umoja linatisha zaidi kuliko kupasuka kombora au tetemeko kali la ardhi.

> Ni rahisi kutamka maneno, lakini ni vigumu kuyatangua. Baadhi yenu wanasema kwamba hawataki kutia mipaka madaraka yangu, bali wanapenda kufafanua na kueleza madaraka ya *Khalifa* atakayenifuata. Lakini hawafikiri kwamba huyo anaweza kuwa mkubwa kuliko Abu Bar r.a. na Hadhrat Mirza Sahib a.s.
>
> "Nilinuia kuchukua hatua fulani leo, lakini nimezuiwa na Mungu. Sina nguvu mbele ya hekima na uamuzi wake. Wale miongoni mwenu walio na udhaifu kadha wanapaswa kuuondoa. Siwafukuzeni katika Jumuiya kwani ipo nafasi kwa ajili yao kuondolea mbali makosa yao, nami sitawanyima hiyo nafasi. Nawasihini nyote kutupilia mbali chuki na husuda. Kama linatokea jambo fulani la amani au hofu msilieneze, lakini likiisha amuliwa mwaweza kulitangaza.
>
> Nawaambieni mwatakiwa kuyafuata hayo yote, mkipenda msipende. Kama mkitii kwa furaha, itakuwa bora kwenu. Nawasihini kwa manufaa yenu. Mungu Mtukufu awasaidieni nyinyi na mimi kuendelea kukanyaga njia ya  mwongozo na Atufikishe hadi mwisho mwema."

Sasa bidii yote ya wakaidi ilikuwa na lengo la kupendwa na Waislamu wa kawaida kwa kueneza hekima za huluka za Kiislamu kama zilivyofafanuliwa na Masihi Aliyeahidiwa bila kutaja jina lake na kuzimua hitilafu zinazowapambanua Waahamadiyya na wasiokuwa Waahmadiyya. Baadhi ya wanajumuiya wakaanza kuathirika na njia hiyo waliyoishika. Sahibzada Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad akitambua uzito wa hasara inayoweza kutokea, akachukua hatua ya kudhihirisha upuuzi wa hoja ya uwongo iliyowavutia, na kwa njia hii akaikomesha ili isipate kufuatwa na wanajumuiya wengine.

Siku ya Ijumaa, Novemba 18, 1910, Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. alianguka kutoka juu ya farasi aliyekuwa amempanda, na akapata majeraha ambayo katika hayo lile lililokuwa kwenye paja lake la kuume lilikuwa la hatari. Kwa siku chache hali yake ilionekana mbaya mno. Katika hali hiyo, siku moja akamwambia Dkt. Mirza Yakub Beig, mganga wake mkuu, "Siogopi mauti. Kama hali yangu ni mbaya sana, waweza kuniambia wazi wazi ili niweze kuandika maagizo fulani." Yeye akamhakikishia kwamba hayuko katika hatari, lakini maradhi yake yakigeuka kuwa mbaya zaidi atamtahadharisha. Hata hivyo alipoondoka tu na kuungana na wenzake katika makazi ya Maulawii Muhammad Ali wakashuriana na kumtuma aende kumwita Sahibzada Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad kushirikiana nao. Alipowasili, Khwaja Kamaluddin akamweleza hali iliyokuwa kwa maneno haya:

> "Tumekusumbua kufika hapa kwani tumeambiwa kwamba Hadhrat Maulawii Sahib r.a. ni mgonjwa na dhaifu sana. Miongoni mwetu waliotoka Lahore hawana nafasi ya kukaa hapa zaidi, kwani hatuna budi kurudi Lahore. Twapenda tushauriane na kukubaliana njia fulani itakayoondoa hatari au shida, likitokea jambo la ghafla. Twakuhakikishia kwamba yeyote kati yetu hataki kuwa *Khalifa*, kadhalika Maulawii Muhammad Ali pia hataki."

Hapo Maulawii Muhammad Ali akathibitisha usemi huo, na Khwaja Kamaluddin akaendelea:

> "Hatumwoni yeyote minghairi yako astahili kuwa *Khalifa*; lakini twaomba kwamba lisiamuliwe lolote mpaka tuwasili kutoka Lahore, isije mtu mmoja akachukua hatua fulani kwa haraka inayoweza kuleta shida. Lazima tungojewe tufike."

Sahibzada Sahib akamsikiliza bila kumdakiza ijapokuwa akaudhika kwa kudokezwa kwamba ikiwa wote hao hawataki kuwa *Khalifa* yeye ndiye ana shauku ya kuwa *Khalifa*, na alipomaliza akasema:

> "Nafikiri hata kuzungumzia tu swala hili katika uhai wa *Khalifa* mmoja kwamba nani atakuwa *Khalifa* baada yake ni dhambi, licha ya kumweka mtu fulani maalum kuwa *Khalifa* baada yake."

Akiisha sema hayo akaondoka akiwaacha wafuate matakwa yao.

Jeraha la panja la Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. likakawia kupona, likawa kidonda. Usiku wa tarehe 19 Januari 1911, akahisi shinikizo moyoni mwake akaagiza karatasi na vifaa vya kuandikia na akaandika: 'Mahmud Ahmad' juu ya kipande cha karatasi na kukitia ndani ya bahasha, na baada ya kuifunga akaandika juu yake:

> "Kwa kufuata mfano wa Abu Bakr r.a." kwa Kiarabu, na chini yake kwa Kiurdu, "Fanyeni baiati ya yule ambaye jina lake limeandikwa juu ya kile kilichomo ndani."

Akamkabidhi bahasha hiyo mwanafunzi wake aliyempenda, Sheikh Muhammad Taimur, na kumwambia: Nikifa, lifuatwe agizo lililomo ndani yake. Baaada ya siku chache, alipopata ahueni akaagiza ile bahasha na kuipasua. Habari hii kwamba yeye alitoa agizo hilo imehakikishwa na Maulawii Muhammad Ali katika taarifa ya matukio hayo kwa maneno haya:

"Nimepata habari za kuaminika sana ya kwamba katika Wasia wake alitaja jina la Mian Sahib kuwa *Khalifa* baada yake."

# XIV

# UKHALIFA

Kazi ya *Khalifa* imefafanuliwa na Masihi Aliyeahidiwa a.s. katika 'Wasia' wake kwa maneno haya:

> "Ni suna ya Mwenyezi Mungu ambayo suna hii tangu Alipomwumba binadamu katika ardhi Aliendelea kudhihirisha ya kwamba Yeye Huwasaidia manabii na mitume wake, na Huwapa ushindi kama Asemavyo, 'Mungu Amekwisha andika ya kwamba: Mimi na mitume wangu tutashinda.' Na ushindi muradi wake ni kwamba kama yanavyokuwa matakwa ya mitume na manabii ya kuwa hoja ya Mungu ikamilike ardhini na asiweze yeyote awaye kushindana naye, ndivyo Mwenyezi Mungu Anavyodhihirisha ukweli wao kwa ishara zenye nguvu, na kweli ile wanayotaka kuizagaza kote duniani Anapanda mbegu zake kwa mikono yao. Lakini Haitimizi kazi hii kikamilifu kwa mikono yao, bali kwa kuwafisha katika wakati ambao kidhadhiri huwa na hofu ya ushindi, Huwapa wapinzani nafasi ya kucheka na kudhihaki na kufanya masihara na kuaibisha. Na pindi wanapokwisha kudhihaki, hapo Huonyesha mkono wa pili wa kudra yake na Huleta sababu ambazo kwa njia ya hizo hutimia miradi iliyobakia kadri fulani kutimia. Ndiyo kusema kwamba Hudhihirisha kudra ya namna mbili. (1) Kwanza, kwa mkono wa manabii wenyewe huonyesha mkono wa kudra yake. (2) Pili, katika wakati ambapo matatizo yanazuka baada ya kifo cha manabii na maadui hupata nguvu na hudhani mambo yameharibika na huwa na yakini kwamba sasa Jumuiya hii

itafutika, bali na wanajumuiya nao huhangaika na kuvunjika moyo, na baadhi yao wenye bahati mbaya wanashika njia ya kuritadi, hapo Mwenyezi Mungu Hudhihirisha mara ya pili kudra yake yenye nguvu na kuimarisha Jumuiya iliyokuwa inaanguka. Basi yule anayesubiri mpaka mwisho, huona mwujiza wa Mwenyezi Mungu, kama ilivyotendeka katika enzi ya Hadhrat Abu Bakr r.a. Wakati huo kifo cha Mtume s.a.w. kilipofikiriwa kutokea wakati usiofaa na mabedui wengi wakaritadi na masahaba kwa sababu ya huzuni kubwa wakawa kana kwamba wameshikwa na wazimu, hapo Mwenyezi Mungu kwa kumsimamisha imara Hadhrat Abu Bakr Siddiq r.a., Akaonyesha mara ya pili onyesho la kudra yake na Akanusuru Islam iliyokurubia kufutika na Akatimiza Aliyoahidi ya kwamba: 'Baada ya hofu Tutawaimarisha' (24:56). Ndivyo ilivyofanyika katika zama za Hadhrat Musa a.s., ambapo yeye Hadhrat Musa a.s. kabla ya kuwafikisha wana wa Israeli huko Misri na Kanani sawa na ahadi yake akafariki njiani. Kifo chake kilizusha maombolezo makubwa ilivyoelezwa katika *Torati*. Wana wa Israeli waliendelea kuomboleza siku arobaini kwa huzuni ya kifo kilichotokea wakati usiofaa na kuaga kwa Hadhrat Musa a.s. ghafla. Kadhalika ikatokea kwa Hadhrat Isa a.s. Wakati wa tukio la msalaba, wanafunzi wote wakatawanyika na mmojawapo akaritadi pia.

Basi enyi wapenzi, kwa kuwa hii ndiyo suna ya Allah tangu kale ya kwamba Mwenyezi Mungu Huonyesha kudra mbili ili kuzikanyagilia mbali furaha mbili za bandia za wapinzani, hivyo haiwezekani sasa ya kuwa Mwenyezi Mungu Aiache suna yake ya zamani. Kwa hiyo msihuzunike kwa habari niliyowaambieni wala nyoyo zenu zisifadhaike, kwani hamna budi kuiona kudra ya pili vilevile. Na kuja kwake ni bora kwenu

> kwa sababu hiyo itadumu nayo itaendelea bila kukoma mpaka Kiyama. Na hiyo kudra ya pili haiwezi kuja mpaka niondoke. Lakini niondokapo, hapo Mwenyezi Mungu Atakutumieni hiyo kudra ya pili itakayodumu nanyi milele."

Basi kazi ya *Khalifa* ni kutia bidii kutimiza miradi ya Bwana wake. Hivyo, Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akaziangalia shughuli zisizokuwa zimekamilika au zilikuwa zimefikiriwa wakati alipofariki Masihi Aliyeahidiwa a.s.

Chuo kimoja cha mafunzo ya dini kiitwacho Madrasa Ahmadiyya kilianzishwa na Masihi Aliyeahidiwa a.s. mnamo 1906, ili kutoa mafunzo ya juu ya dini, na kutayarisha na kuwafunza wataalamu na wenye elimu ya hali ya juu ya dini watakaoweza kukabidhiwa kazi ya kufikisha ujumbe wa Jumuiya na kueneza itikadi zake na mifano yake bora huko na huko; lakini kwa upungufu wa fedha shughuli hii haikuendelea mbele zaidi ya hatua ya mwanzo. Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akateua kamati mnamo Juni 1908, wanakamati wakiwa: Sahibzada Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad r.a., Maulawii Muhammad Ali, Nawab Muhammad Ali Khan r.a. na Dkt. Khalifa Rashiduddin. Walitakiwa kuchukua hatua kukiimarisha chuo hicho juu ya msingi imara sana. Kamati ikatayarisha mpango na ikapendekeza kwamba baadhi ya sehemu zake zitekelezwe mara moja na ikaiomba Jumuiya kuchanga kwa kutimiza mpango huo. Chuo hicho sasa kimekwisha kuwa *Jamia* ambayo waliohitimu masomo katika hiyo wanaendelea kufanya kazi nzuri sana ya kueneza ujumbe wa Islam ya kweli katika sehemu mbalimbali za dunia.

Masihi Aliyeahidiwa a.s. alipenda wawepo kwa uchache watu mia moja katika Jumuiya wenye sifa bora sana na vipawa ambao wawe na ujuzi wa ishara zote na sababu na hoja zote thabiti ambazo Mungu Amedhihirisha kuisaidia Jumuiya na madai yake, ili waweze

kuwajibu kwa njia bora sana wakinzani wenye uhasama. Pia waweze kuwaondolea watafuta ukweli wasiwasi wao uliozushwa na wapinzani Wakristo na Ma-Arya dhidi ya Islam, na waweze kufafanua kinaganaga ubora wa Islam na kuwatuliza. Kwa shabaha hii akatangaza tarehe 9 Septemba 1901 kwamba kundi la watu wenye akili na busara na wataalamu mara moja waanze kuvisoma kwa uangalifu vitabu vyake na maandiko yake na wajitokeze kutahiniwa tarehe 24 Desemba hapo Qadian. Mtaala huu na mtihani utarudiwa kila mwaka. Mpango huo haukufuatiwa wakati huo. Mnamo Julai 1908, Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akaona sana haja ya kuwepo kundi la wabashiri wenye ujuzi mwingi wa dini watakaozagaza ujumbe wa Islam duniani kote. Alipokuwa akifikiria habari hiyo akapata kuona tangazo la Masihi Aliyeahidiwa a.s. la tarehe 9 Septemba 1901, na akaathirika sana moyoni. Mara moja akaagiza kwamba tangazo hilo lienezwe katika Jumuiya nzima na kwamba kila mwaka mtihani wa vitabu fulani maalum vya Masihi Aliyeahidiwa a.s ufanywe mnamo mwezi Disemba, kuanzia tarehe 24 Disemba 1908. Tangu hapo desturi ya kutaali vitabu vya Masihi Aliyeahidiwa a.s. inaendelea kufuatwa zaidi sana katika kila sehemu ya Jumuiya.

Baada ya kufariki Masihi Aliyeahidiwa a.s. wapinzani wakapinga na kukinza sana madai yake. Wataalamu na masheikh wengi wakaandika vijitabu na makala kujibu ukinzani huo. Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. naye akaandika kijitabu juu ya kichwa cha maneno: *'Kifo Cha Masihi Aliyeahidiwa a.s.'* Akaanzia madhumuni haya kwa kuandika aya hii kama msingi: 'Masihi bin Mariamu siye ila ni Mtume tu; bila shaka Mitume wamekwisha fariki kabla yake (5:76);' na: 'Siye Muhammad ila yu Mtume. Bila shaka wamekwisha fariki kabla yake Mitume. Je, akifa au akiuawa mtarudi nyuma kwa visigino vyenu (3:145)?'

Katika kijitabu hicho akamtukuza Mungu kwa fadhili yake wakati alipofariki Masihi Aliyeahidiwa a.s. Akaihifadhi Jumuiya isipate kuvunjika, kwa kuleta umoja ndani yake. Akasema:

> "Wapenzi, fikirini namna Mungu Mwenye nguvu na Mkuu Alivyopuliza roho ya umoja na mwafaka katika Jumuiya nzima, kutoka kaskazini mpaka kusini, na kutoka mashariki hadi magharibi. Mola wangu, najitolea kwako kwa ajili ya fadhili yako kubwa. Si mmoja bali wana wanne na mjukuu mmoja wa Hadhrat Mirza Sahib a.s. walikuwepo, kadhalika na yule mstadi mheshimiwa aliyemwoa bintiye ambaye jina lake lakusanya 'Muhammad' na 'Ali,' na pia alikuwepo kati yao mkwewe mhashamu kama baba, na hata hivyo Jumuiya yote pamoja na wale niliowataja wakafanya baiati kwa yule aliye nje ya familia ya Hadhrat Sahib a.s.
>
> Sasa wapinzani wake na wafanye mikutano na kupiga mbiu kuonyesha furaha yao. Wamekwisha ona onyesho imara la kwanza la nguvu ya Mungu na msaada Wake, na sasa washuhudie onyesho la pili la nguvu Yake. Mti huu ambao hadi sasa umehifadhiwa na huruma halisi ya Mungu utakua sasa na kustawi kwa njia hizo hizo ijapokuwa idadi yetu ni ndogo na wafanyakazi wetu ni wachache.
>
> Enyi wapinzani wetu wenye haraka, mngefanya subira kidogo. Mmeshuhudia onyesho la kwanza la nguvu ya Mungu, mngetuliza roho zenu ili kushuhudia lile la pili; lakini Mungu Mwenye nguvu Ametuwekea sisi ujira wa subira vilevile. Sifa zote njema zamhusu Mungu, Mola wa walimwengu.
>
> Hamkuona Imam wetu amefariki, nasi tumevumilia msiba kwa uthabiti? Lakini nyinyi mkadhihirisha masikitiko yenu

> juu ya huzuni yetu kwa kutembeza jeneza za bandia na vitendo vya upuuzi. Profesa na Sufii wenu akawapa walioshiriki katika maandamano hayo lakabu ya heshima ya kuwa Watumishi wa Imani. Wema na wabaya wanakufa kote duniani. Je, mmesoma popote tangu lini njia hiyo ya kuonyesha masikitiko imeshikwa na Waislamu, na nani akianzisha njia hiyo akajipatia lakabu: Yule aanzishaye kitendo kiovu? Waislamu wengi wa Lahore wakaleta ghasia wakati huo nisiyowaza mapema, na nikadhani hatutaweza kufika kituo cha gari la moshi, lakini ghafla Mungu Mwenye nguvu Akaleta polisi kama alama ya huruma yake kutuhifadhi nasi tukaweza kupanda gari moshi bila taabu tukiishukuru serikali nyoyoni mwetu.
>
> Hadhrat Mirza Sahib ameacha nyuma yake watoto sita; sifa zote njema zamhusu Mungu, Mola wa walimwengu. Kama mmoja wao au mzao wao akithibitika kuwa thabiti na Immanueli mkuu ambaye ametabiriwa kuzaliwa, hapo wakati ule nyinyi au wazao wenu wataikabilije dunia?"

Sahibzada Mirza Mahmud Ahmad r.a., ambaye alikuwa hajawa mwenye umri wa miaka ishirini, naye akaandika kijitabu wakati huo kiitwacho: *Nani Awezaye Kuzima Nuru ya Watu Wema?* Baada ya kukisoma hicho Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akamwambia Maulawii Muhammad Ali: Wewe na mimi sote wawili tumeandika kuvunjilia mbali upinzani wa wapinzani dhidi ya Masihi Aliyeahidiwa a.s., lakini Mian Mahmud ametuacha sote wawili nyuma. Kisha akampelekea Maulawii Muhammad Husain wa Batala nakala yake moja kwa rejista na akamwandikia: Wewe umesema wazao wa Mirza Sahib sio wema. Nimekutumia nakala moja ya kijitabu kilichoandikwa na mmoja wao. Kama mmojawapo kati ya wazao wako amepata kuandika chochote, niletee nakala yake. Miongoni mwa sifa nyingi za pekee za Hadhrat

Khalifatul Masihi r.a., ningependa kueleza hapa mbili tu. Yeye alikuwa msimulizi mmojawapo wa Hadithi arobaini za Mtume Mtukufu s.a.w. zilizosimuliwa kwa midomo tangu karne nyingi na mnyororo usiokatika wa wasimulizi. Yeye naye akazipeleka mbele kwa Hafidh Raoshan Ali r.a. na Mir Muhammad Is'haq r.a. pamoja na wengineo.

Pia alipata nafasi ya kuzunguka Kaaba wakati ambapo hakuna yeyote aliyekuwa anaizunguka.

Wakati vijana watatu, miongoni mwao wawili wakiwa wanafunzi wa utabibu, walipofanya baiati kwa Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akawatolea mawaidha:

> "Afanyaye baiati anakuwa mtumwa kwa hiari yake na kwa furaha yake. Wamagharibi husema mtu huzaliwa huru na utumwa ni jambo ovu. Lakini hebu niwaambie habari moja. Mwalimu wangu mmojawapo katika mambo ya dini alikuwa mheshimiwa sana Sheikh Abdul Ghanii Mujaddidi aliyeselea Madina. Watu kutoka sehemu za mbali kama vile Shamu, Misri, nchi za Magharibi, Urusi na kadhalika wakafanya baiati kwake. Nilikuwa namtembelea mara kwa mara, lakini nilifikiri kwamba mema na mabaya yamekwisha elezwa katika vitabu, nami nimekwisha hitimu masomo yangu, hivyo sina haja ya kufanya baiati kwa mtu yoyote; na nikashangaa kwamba watu wengi sana walikuwa wamefanya baiati kwake. Kisha wakati fulani nikafikiri naweza kufanya baiati kwake kwa kujaribia. Nisipofaidika kwake nitaivunja. Basi nikamwendea kwa mpango huo, lakini dhamiri yangu ikanilaumu juu ya uwezekano wa kuvunja baiati, nami nikarudi pasipo kufanya baiati. Baadaye tena nikaamua kufanya baiati kwake, na nilipomtembelea nikamwuliza nitanufaika nini nikifanya baiati kwako. Akajibu kwamba kwa njia ya kufanya baiati ya

> kiroho kitu kinachosemwa kinaonekana ni hakika kabisa; na kile ukisikiacho unakiona. Nilijifunza mengi kutoka kwake na nikapata maendeleo mengi ya kiroho chini ya uongozi wake."

Katika kumi la mwisho la Ramadhani (Oktoba 1908), Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. alikaa *Itikafu* msikitini pamoja na watu wengi, miongoni mwao akiwa Sahibzada Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad. Kwa kuacha nafasi ya sala tano, akajishughulisha tangu asubuhi mpaka usiku kuwafundisha wenzake Kurani Tukufu. Akawafafanulia sehemu zilizo ngumu kueleweka, akawabainishia maana za ndani sana na kuwajibu maswali yao. Kwa njia hii akawasomesha sehemu ya kumi ya Kurani Tukufu kila siku na kumaliza maelezo ya Kitabu Kitakatifu kizima mpaka mwisho wa Ramadhani. Shughuli hiyo ikiangaliwa kidhahiri, kwa kuzingatia umri na afya yake na uchovu wa saumu, ni kazi kubwa ya ubingwa. Hiyo ilibainisha mapenzi yake kamili na kujitolea kwake kwa moyo wote kwa Neno Takatifu la Mungu.

Katika msimu wa kharifu (msimu baina ya kiangazi na kipupwe) wa mwaka 1908, mji wa Hyderabad ukapatwa na mafuriko makubwa ajabu yaliyowaletea watu taabu nyingi moja kwa moja. Makazi yote ya mji yakaanguka na maelfu ya watu wakanaswa chini na kuangamia. Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akatuma barua nyingi za rejista na simu za maandishi za haraka sana ili kujua habari za wanajumuiya wa mji uliosibiwa, lakini kwa sababu ya hali ilivyokuwa ya mahangaiko hata barua moja haikufika, kwa hiyo hakupata majibu. Hapo akamtuma Hafidh Abu Saidi Mwarabu akiwa mjumbe wake ili kuleta habari. Barua aliyopokea kutoka kwa Jumuiya ya mji wa Hyderabad kwa kumshukuru kwa sababu ya kuwafikiria wanajumuiya na kuwahurumia katika shida zao yaonyesha jinsi alivyowapenda sana wanajumuiya na jinsi alivyowahangaikia kuhusu usalama wao

na ustawi wao. Barua yenyewe ilikuwa hivi:

> “Kwa jina la Mungu, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.
>
> Twamsifu Yeye na kumsalia Mjumbe Wake Mtakatifu. Kwa mtukufu Khalifatul Masihi-wal-Mahdi, Kiongozi wa Waaminio, Hadhrat Mkuu Nuruddin, Mungu Atufululuzie hisani yake na baraka zake.
>
> Amani iwe kwako na huruma ya Mungu na baraka zake. Wanajumuiya wa Jumuiya ya Hyderabad hawapati maneno yafaayo kwa kumtolea Khalifatul Masihi shukurani kwa kutuma barua nyingi za rejista na simu za karatasi kwa hisani yake na mapenzi yake ili kujua hali zao wakati ambapo wakazi wa Daccan wakapatwa na shida namna ilivyoelezwa katika Kurani Tukufu: Siku ambayo mtu atamkimbia nduguye, na mamaye na babaye, na mkewe na wanawe (80:35-37). Kwa bahati mbaya risala hizo karimu hazikutufikia katika hali ilivyokuwa ya machafuko, na kwa hiyo upokeaji wa hizo haukujulishwa. Lakini moyo wa huruma na mahaba wa kiongozi wa waaminio haukuridhika pasipo kumtuma kwa gharama yake binafsi rafiki yake mwaminifu, Hafidh Saidi Mwarabu, afunge safari ndefu sana ili kuwajulia hali waliokaa mbali na kupatwa na msiba. Baada ya kuwasili hapa, bwana Mwarabu, ijapokuwa yu mgonjwa, anajibidiisha kutimiza wajibu wake na kwa kumtoa mashaka na wasiwasi kila ndugu Ahmadiyya amehakikisha kwamba anazo khulka bora za Kiahmadiyya.
>
> Bwana Mwarabu pia amefikisha ujumbe mkarimu wa Hadhrat Khalifatul Masihi ya kwamba kama watu wa familia ya Ahmadiyya fulani wameachwa pasipo kitu, basi

wakipenda waweza kuletwa Qadian ambako wataangaliwa vizuri na gharama ya safari yao pia itatolewa. Tulitazamia, na tutatazamia, hayo kutoka kwa mbarikiwa Hadhrat Khalifatul Masihi, lakini yeye pamwe na waheshimiwa wengine wa Jumuuiya kwa yakini watafurahi kujua ya kwamba ingawaje ni hakika ya kuwa nyumba za wanajumuiya wengi zaidi zilikuwa katikati ya sehemu za hatari zilizoangamia na zikawa magofu na maelfu ya maiti zilipatikana huko, lakini hata Ahmadiyya mmoja, wala jamaa ya Ahmadiyya hakufa katika maafa hayo makubwa. Sifa zote njema zamhusu Mungu kwa kutuhurmia.

Mwishoni, wanajumuiya wote wa Jumuiya ya Ahmadiyya mjini Hyderabad wanamwomba kwa adabu Hadhrat Khalifatul Masihi, tafadhali waombee wanyonge walio mbali kwamba Mungu Mpaji Akamilishe imani yao na kuwaimarisha katika nyakati za majaribio na kurekibisha mienendo yao. Atujalie tulete mabadiliko mema katika nafsi zetu na kuweka mfano bora kwa wengine. Na tutakapoondoka makazi haya ya muda tuhesabiwe waaminio wa kweli, watii na watumishi wanyofu wa Jumuiya ya Ahmadiyya, Amin."

Mapema tarehe 30 Oktoba 1908, Sheikh Yakub Ali Irfani akaandika gazetini *Al-Hakam:* Hadhrat Khalifatul Masihi hupitisha wakati wake katika mambo mawili: Katika kufikisha maamrisho ya Mungu, na kuwahurumia viumbe.

"Katika zama za uhai wa Masihi Aliyeahidiwa a.s., Maulawii Nuruddin r.a. alikuwa anaongoza sala ndani ya Masjid Mubarak. Maulawii Abdul Karim r.a. alipohamia Qadian akaombwa kuongoza sala katika msikiti huo, lakini alipofariki yeye, Maulawii Nuruddin akalazimika, shingo upande, kuanza

tena kuwaongoza watu katika sala katika Masjid Mubarak. Tangu awe *Khalifa*, anaendelea kuongoza ibada ijapokuwa yu dhaifu na mwenye afya isiyo nzuri.

Baada ya sala ya alfajiri huwafunza kina mama Kurani Tukufu. Kisha kwa saa nzima huwatibu wagonjwa wanaofika Qadian kutoka nje. Baadaye huwafundisha Sahibzada Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad r.a. na Mir Muhammad Is'haq r.a. Aidha, kuna masomo ya Kurani Tukufu, Hadithi na Kanuni za Fik'hi ambayo mtu yeyote anaweza kuhudhuria.

Saa zote anadumu kuomba dua kwa sauti ndogo. Nimejionea mwenyewe ya kwamba anapopokea barua zake, huwa anaishika kila barua mkononi mwake na kumwombea mwandikaji. Desturi hii imepanuka sana hata kwamba baada ya kila sala na masomo ya Kurani Tukufu yeye anakuwa na makumi ya barua za maombi ya watu mkononi mwake. Kila barua anaposoma huwa anamwombea mwandishi wake kuhusu jambo aliloandika. Kabla hajawa *Khalifa*, uhusiano wake na wanajumuiya ulikuwa na kidugu, na akawaomba akiwa ndugu yao. Sasa yu baba yao kiroho, na kila mmoja anaweza kuzingatia kwamba baba anawaonea huruma sana namna gani watoto wake na kuwa na jazba ya kuwatunza. Katika Jumuiya ya watu wapatao laki nne kuna wengi walio wagonjwa, wenye mahitaji, na wengi wanakufa. Nani aweza kujua kwamba moyo wake wenye huruma waathirika vipi kwa shida za hao wote?

Tangu Mungu Ampandishe kwenye cheo hiki kitukufu amejaaliwa kuwa mwangalifu sana ajabu. Anapata habari ya afya na hali za kila mmoja aishiye Qadian na kutenda

kama baba mwenye huruma katika hali ya shida na huzuni ya kila mmoja. Mimi binafasi nina deni kwake kwa sababu ya hisani zake nyingi. Nilipougua, yeye alinitembelea bila kuombwa na kuendelea kunitibu. Mke wangu akapata kuugua alipokuwa katika *Itikafu*, naye akamwekea watu wawili au watatu kumtumikia na kumpasha habari ya hali yake. Nayakini kila mmoja anajiona kwamba yeye anaangaliwa na kutunzwa naye hasa kama ilivyokuwa hali kwa marehemu Imam a.s.

Ingawaje anashughulikia saa zote mambo ya Jumuiya na kutetea Islam, anatafuta nafasi ya kumtazama na kumwandikia dawa kila mgonjwa anayemjia; kuandika majibu ya barua za muhimu; kuitolea *Sadr Anjuman Ahmadiyya* maagizo ya lazima kuhusu shughuli zake; kuonana na wageni wanaowasili kutoka nje, kusikiliza shida zao na haja zao, kuwapa mashauri na mauidha, na kufikiria maazimio na mipango kwa kueneza Islam na Jumuiya na kuwaelekeza wanajumuiya kwenye mambo hayo. Nyakati za sala ni nyakati maalum, mengine yote yanapangwa sawa na hizo.

Jinsi alivyokuwa mwenye huruma nyingi mno na kamilifu yaweza kupimwa kwa kuzingatia tukio moja. Mafuriko ya ajabu yalileta maangamio mengi sana huko Hyderabad mbali sana kutoka Qadian. Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. alihuzunika sana hata kwamba barua na simu za karatasi ziliposhindwa kuleta habari, yeye akamtuma mjumbe maalum aende mbali sana huko Hyderabad kuwasaidia pamoja na risala za kuwapa pole na kuwafariji wanajumuiya. Kwa hayo yote Jumuiya kwa jumla ikamaizi kwamba baada ya Mwanzilishi wa Jumuiya kutuacha mkono, Mwenyezi Mungu Amemwinua mtu bora

kuiongoza. Mungu Ampatie umri mrefu ili tuendelee kwa muda mrefu kubarikiwa na rehema Zake zinazotushukia kwa sura ya Nuruddin r.a.

Maombi yake daima yapo pamoja nasi. Alimalizia hotuba yake ya Idi kwa haya: 'Mungu Aijalie Jumuiya kuendelea kustawi. Iwe imara na kufungamana kwa upendo. Itiliwe nyoyoni Roho Takatifu na ilindwe isipatwe na misiba ya kidunia na ya kimbinguni na ihifadhiwe na Wewe katika majaribio ya kiroho. Idumu kupata ushindi kwa msaada Wako. Waibuke kutoka ndani ya Wanajumuiya wasemaji wenye busara na wahubiri na wenye kuwaita watu kwa Mungu. Viongozi wao wawe wajuzi sana wa Islam wakidhihirisha mafundisho yake katika mienedo yao na itikadi zao. Wenye madaraka kati yao wawe wanyofu na wenye busara.'

Baada ya sala ya Ijumaa, muda wake mwingi zaidi ulitumika katika kuiombea Jumuiya, mfano wake tumekwisha eleza tayari. Mungu pekee Anajua kwamba vipi, kwa moyo upi na kwa maneno yepi ya kuvutia huruma anaomba mchungaji huyu wa kundi lake kwa Mola wake kwa ajili yao katika saa za usiku zenye giza na unyamavu na upweke, ambapo kila mmoja wao amelala usingizi mzito. Mungu na Ampokelee maombi yake na tujaalie kunufaika nayo. Amin."

Tarehe 26 Desemba 1908, Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. aliuhutubia Mkutano wa Mwaka kwa masaa matatu takriban. Akaeleza jinsi malezi yake yalivyoanza na Hakuna apasaye kuabudiwa isipokuwa Mungu; na jinsi yalivyoendelea mbele. Akasisitiza zaidi umuhimu na baraka za sala, uthabiti wa hali ya juu, Kurani Tukufu na kusaidiana. Kisha akaeleza kirefu hakika ya imani na hali zake nyingi mbalimbali juu ya msingi wa aya hii: Hakika Mwenyezi Mungu Amenunua kwa

waaminio nafsi zao na mali zao (9:111). Na pia akasema ya kwamba gazeti la *'Curzon Gazette'* la Delhi limeandika kuhusu kufariki kwa Masihi Aliyeahidiwa a.s. ya kwamba Waahmadiya wamekatika kichwa chao na wamebakiwa na kiongozi asiyeweza kufanya kitu isipokuwa kuwasomea Kurani msikitini. Juu yake akasema: "Mungu na Anijalie niendelee kuwasomea Kurani Tukufu."

Akahutubia tena Mkutano jioni ya tarehe 28 Desemba. Akachagua 'Upendo wa Mungu' kuwa kichwa cha habari. Kwanza akafafanua 'Upendo', kisha akatoa maelezo ya madaraja yake. Akasisitiza kwamba Yule Anastahiki kupendewa Ambaye uzuri wake na hisani yake inapita uzuri na hisani ya wengine wote. Uzuri Wake ni mkamilifu na hisani Yake inadumu milele.

Sawa na maagizo yake, Maulawii Muhammad Ali alitangaza mwito tarehe 21 Januari 1909, kuhusu kutoa mchango katika mfuko wa kuwasaidia mayatima, maskini na wanafunzi wanaostahiki. Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. mwenyewe aliuchangia mfuko huu asilimia tano ya michango yote kwa jumla.

Akiongea na kundi moja la watoto wadogo wa shule, tarehe 23 Januari 1909, aliwasisitizia umuhimu wa kuepukana na tabia mbaya na kuzoea kusali kama kawaida. Akatamka:

> "Makokwa ya embe yapandwayo katika ardhi, yanaanza kuota katika masika, mwaona watoto wanayang'oa na kutengeneza miluzi. Baada ya miaka mitano au sita kokwa lililopandwa linapoimarika mizizi yake ardhini, mtu mwenye nguvu pia anaona shida kuling'olea mbali. Mazoea na itikadi pia ni kama mimea na miti. Mwaweza kuyang'oa mazoea yenu mabaya kwa urahisi hivi sasa, lakini yakiisha imarika mwaweza kuyakuta hayawezekani kung'olewa. Baadhi ya watoto wanapata kuzoea kusema uwongo. Wasipoiacha tabia hiyo

> mapema, wataikuta shida kuachana nayo. Nimeona kwamba baadhi yao walioshika tabia hiyo utotoni mwao, hawakuweza kuepukana nayo katika utu uzima, ingawaje ni masheikh na wataalamu sasa.
>
> Jambo la pili ambalo ningewasihi ni kuhusu kusali bila kuacha hata sala moja. Msipokuwa waangalifu sasa, mwaweza kujikuta kuwa wasahaulifu mtakapokuwa watu wazima."

Karibu katika zama hizo akapata kujua kwamba mtu fulani amesema kwa uthabiti ya kwamba michango inayoichanga Jumuiya haitumiki kuendeleza mbele miradi iliyokwisha tangazwa, bali hutumika kutimiza shabaha za binafsi. Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akajibu kwa urefu upinzani maalum wa wakinzani na kuwasihi:

> "Uzushi haukuleta wema kwa yeyote. Wapo Wakristo waliowasingizia Manabii wote kutoka Adam a.s. hadi Mtume Mtukufu s.a.w., Mungu Awawie radhi wote hao. Wayahudi toka mwanzo na Waislamu kwa karne kumi na tatu za mwisho wanaendelea kukanusha masingizio hayo. Je, hiyo imeleta tofauti yoyote kwa Wakristo? Kisha Washia wanawasingizia masahaba wa Mtume Mtukufu s.a.w na wale Waislamu waliowafuata na watu wenye imani kubwa. *Bukhari* amesimulia ya kwamba Hadhrat Uthman r.a. alilaumiwa mbele ya Ibne Umar r.a. Kisha 'wajibu' wa kusuta ukashikwa na Ma-Arya. Je Mwislamu yeyote ameweza kuwakomesha? Wafuateni basi Wakristo, Washia na Ma-Arya. Njia hiyo ni ya hatari sana, si sawa, ni ya kuleta madhara. Tunafundisha Islam, tulivyojaaliwa na Mungu, kama alivyofundisha Mtume Mtukufu s.a.w."

Talimul Islam High School, Qadian, ilianzishwa mnamo Januari 1898, na iliendelea kustawi vizuri. Shule na bweni lake, vyote viwili, vilikuwa mjini na vilikuwa majengo ya matofali ya udongo yasiyochomwa na

havikuwa vya fahari. Mwanzoni kabisa mwa *Ukhalifa* haja ilisikika kujenga majengo makubwa ya kufaa kwa shule na bweni pamoja na msikiti nje ya mji. Eneo la eka hamsini lilichukuliwa na ikapangwa ya kwamba kwanza msikiti ujengwe, kisha bweni na tena shule. Msikiti, ulioitwa Masjid Nur, ukajengwa kwa mchango uliopatikana zaidi kwa juhudi alizofanya Mir Nasir Nawab r.a. kwa moyo sana. Mnamo mwaka wa kwanza wa *Ukhalifa* rupia elfu kumi zilikusanywa kwa bweni, na joko moja likaletwa kwa ajili ya kuchoma matofali. Rupia nyingine elfu thelathini zilihitajika kwa kujenga bweni. Mnamo Mei 1909, sawa na maagizo ya Hadhrat Khalifatul Masihi r.a., Maulawii Muhammad Ali akatoa mwito kwa Jumuiya kuchanga kiasi hicho, na kamati moja iliundwa kukusanya fedha hizo, wanakamati wakiwa: Sahibzada Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad r.a., Dkt. Seyyid Muhammad Husain r.a., Dkt. Mirza Yakub Beg r.a. Khwaja Kamaluddin, Mufti Muhammad Sadiq r.a., Sheikh Yakub Ali Irfani na Maulawii Muhammad Ali. Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. binafsi akachanga rupia mia sita. Shule pia ilipata kujengwa katika wakati wake, serikali pia ikatoa rupia elfu ishirini na tano kusaidia ujenzi. Muda fulani baadaye hospitali moja ikaongezwa kwa bidii ya Mir Nasir Nawab. Ikaitwa Nur Hospital. Azimio lake jingine jema lilikuwa kuwajengea makazi wenye hali ndogo. Katika hayo yote yeye alisaidiwa na Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. kwa maombi na michango ya fedha, na akamwona ni mfano kwa wengine.

Maombi ya Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. yalipokelewa kiajabu kwa rehema na huruma ya Mungu. Qadhi Dhuhuruddin Akmal, Mhariri Msaidizi wa *Badr*, alichapisha shairi lake moja mnamo 1909, lililokuwa na kiini cha kisufii ambalo kituo chake kilikuwa: “Nilikuwa sifahamu”. Siku moja baada ya adhuhuri, Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. alipokuwa akipumzika, akamsikia mkewe akisoma shairi hilo kwa sauti iliyomwathiri sana. Akaketi mara moja na kutamka: Alhamdu-

lillahi, mimi nalikuwa nafahamu sikuzote. Akauliza nani mtunzi wa shairi hili? Akaambiwa na pia akajulishwa kwamba mshairi huyo alipata kufiwa na wana wake wawili utotoni mmoja baada ya mwingine katika kitambo kidogo, basi mara moja akampelekea cheti:

> "Nimekuombea kwa moyo wote. Mungu Atakulipa kwa hasara ya wana wako kwa fadhili zake. Sikuwa mwenye bahati mbaya, E Mola wangu, kwa kukuomba."

Wazazi hao waliofiwa wakabarikiwa na mwana mmoja mnamo 1910 ambaye alipewa jina Abdur Rahman na Hadhrat Khalifatul Masihi r.a., na mwingine tena katika 1913 aliyemwita Abdur Rahim. Wote wakahitimu masomo ya chuo kikuu na kupata shahada na wanaendelea vizuri katika maisha.

Kijana mmoja wa Laknao aliyekuwa amezoea kusema yalivyo, huru, si mwangalifu katika mwenedo wake, lakini mwaminifu sana na mwenye huruma na mpole kabisa, alikuwa mwanafunzi wa Lahore Medical College. Yeye alikuwa Ahmadiyya mwenye bidii na mwenye kumsifu sana Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. na akamtembelea mara kwa mara. Sikuzote alizozana na Maprofesa na waalimu wake na akadhani wanamchukia bila sababu yoyote. Akashindwa mara mbili katika mtihani wake wa mwisho. Kwa sababu ya uchungu akamnong'oneza rafiki yake kwa sauti iwezayo kusikika wakati Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. alikuwepo hapo, na pengine kwa nia ya kumchokoza: Ama Mungu hakuna, au Hana madaraka juu ya wakaguaji wangu! Khalifatul Masihi r.a. akamsikia, akamtazama na akasema kwa nguvu, "Ala! Kweli?" na akaendelea na shughuli zake. Mwaka huo mwanafuzi huyo aliyekwisha kata tamaa akafaulu katika mtihani wake. Alipomwarifu Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. katika hali ya kuona haya nyingi kuhusu kufaulu kwake, akatabasamu na kauliza: "Je, umejionea onyesho la uwezo wa Mola wangu Mwenye nguvu?"

Safari moja Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akasema: Wokovu hupatikana kwa fadhili ya Mungu, na fadhili ya Mungu huvutwa na mwenendo mwema. Basi imani pekee haitoshi, haina budi ifuatane na matendo mema. Wakristo hawaifahamu. Hapo mtu mmoja akauliza: Mwenendo gani wahitajika kwa *Ukhalifa*? Akajibu:

> "*Ukhalifa* ni kama naibu wa Unabii, na zote mbili ni neema za Mungu. Nafikiri huduma ya ubinadamu huvutia fadhili hiyo, nami nilitiliwa rohoni maono hayo tangu ujana wangu. Sikuzote nimependa kumhudumia kila mmoja bila kujali tofauti ya kabila, dini, nchi au utaifa, kwa kumwongoza kimawazo au kumsaidia kwa kitendo."

Sheikh Yakub Ali Irfani akandika mnamo Julai 1909:

> "Mgeni yeyote anapowasili Qadian kutoka nje mara ya kwanza, huwa kwa kawaida anamtafuta Hadhrat Khalifatul Masihi. Anapoelekezwa kwake, anashangaa kuona watu wengi wakikaa juu ya mikeka pasipo kujikalifisha bila tofauti ya namna yoyote. Anamkuta baina yao mzee mmoja mhisani, mwenye heba, mwenye uso wa kung'aa; lakini mavazi yake, mwendo wake na jinsi anavyozungumza havidokezi kwamba huyu mtu mwangavu ndiye anayekalia kiti cha *Ukhalifa*. Anawatazama wenye shida na wagonjwa, waliovaa nguo zisizofuliwa zenye kunuka, bila kujikalifisha anakagua maradhi yao na kuwaandikia dawa. Wapo wengine hapo wanaomwuliza maswali ya kila aina kuhusu dini na kusikiliza majibu yatolewayo na midomo yake. Baada ya kitambo mgeni anatambua kwamba huyo ndiye ambaye macho yake yalimtafuta, na anastaajabia upya shani ya *Ukhalifa* katika hali ya shughuli.
>
> *Khalifa* wetu, aliye kiongozi wetu, si mtu wa anasa na si

> mpenda starehe. Anaongea na kila mmoja namna ambavyo mtu huyo anajifikiria kwamba yeye pekee ndiye anayependwa naye na kuangaliwa. Lakini si hayo tu. Yeye ana huruma na upendo kwa kila mmoja. Ndani ya nyumba na nje hadharani, katika hali zote mbili, yu mtu wa kawaida sana; chakula chake ni cha kawaida, mavazi yake nayo ya kwaida. Kile kinachompambanua baina ya wenzake ni uso wake mtukufu ung'aao. Nyakati zake zote hutumika katika kuwatumikia viumbe wenzake na kuihudumia dini."

Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. aliitoa wakfu nyumba yake mjini Bhera kwa kutumika kama msikiti kwa ajili ya Jumuiya ya Ahmadiyya. Baadhi ya jirani wakailaumu hatua yake hiyo kwa kusema amefanya hiyo kwa nia ya kuleta fitina. Hapo yeye akamwandikia Sheikh aliyekuwa kiongozi baina yao ya kwamba:

> "Bwana Sheikh, mimi mnyeyekevu nimechukia daima kwa moyo wangu wote kufitinisha, hata kwamba wazo lolote la kuleta fitina halipati nafasi kuingia mle. Nahakikisha kwa sababu ya ujuzi wangu binafsi ya kwamba fitina ilikuwa inamchukiza baba yangu na babu yangu. Mungu, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu Anajua ukweli; nani mwingine aweza kuujua? Hukukaa pamoja nami wala pamoja na ndugu zangu. Hawakufitinisha. Alhamdu-lillahi, nijuavyo mimi, fitina ilichukiwa sana na mama yangu, nyanya yangu na dada zangu.
>
> Naamini kwa uthabiti kwamba: Hakuna apasaye kuabudiwa isipokuwa Mungu; Muhammad ni Mjumbe wa Mungu. Nasali, nafunga saumu, natoa zaka, nimehiji Kaaba mara mbili, nimewafundisha Kurani Tukufu maelfu ya watu na kuwasihi kufuata maamrisho yake. Sifa zote njema zamhusu

Mungu, Mola wa walimwengu. Idadi ya wanafunzi wangu ni malaki kadha, miongoni mwao wakiwemo *Makureishi*, Mamogholi, Mapatani na Masheikh. Simfundishi yeyote kuleta fitina. Wanajumuiya ya Jumuiya yetu wanajiepusha fitina. Wote si sawa; lakini kwa kulinganisha na wengine, hao wanatekeleza vizuri amri kuhusu sala, zaka na saumu.

Wabhera waliponisumbua msikitini, nikaanza kusali nyumbani kwa kuepukana na fitina msikitini. Daima naweka moyoni: Ni nani mdhalimu mkubwa kuliko yule azuiaye misikiti ya Mungu ya kwamba humo lisitajwe jina lake. Wanajumuiya wetu hawaendi msikitini kwa shabaha yoyote kinyume cha sheria; lakini mfululizo wakapigwa na wakatuhumiwa kwa wizi. Tukaendelea kuwasihi kuwa na subira. Lakini mateso yalipokuwa hayavumiliki tukaamua tuwe na msikiti wetu wenyewe na kutangaza kwamba hakuna yeyote anayekatazwa kusali humo. Unaiita ni kufitinisha. Inna lillahi!

Sisi twawaheshimu binti zenu kama binti zetu. Sisi wenyewe twapenda kabisa kufuata masharti ya kuhifadhi faragha ya kina mama; usisumbuke kuhusu jambo hili. Msikiti huu shabaha yake si kuudhi na kufitinsiha, bali ni kimbilio la mwisho kujihifadhi tusipate madhara na kudumisha amani. Umenunua, bila kutujulisha, nyumba moja iliyomilkiwa nasi pamoja na wengine. Je, hiyo siyo hatua ya kuleta fitina moja kwa moja, isiyo na nia ya kudumisha amani? Tafakari: Hakuna mwabudiwa isipokuwa Mungu; Muhammad ni Mjumbe wa Mungu. Sisi hatukuweka mlango wa msikiti namna ambavyo iwe kinyume cha masharti ya faragha ya wengine.

Huna budi kutuambia tufanyeje? Wewe na shutuma zenu zimetuzuia kuingia msikitini. Sasa tunapopanga kugeuza nyumba yetu wenyewe kufanya msikiti unatushutumu kwamba tunafitinisha. Hii ndiyo Islam? Fikiria na ushauriane na Mwislamu mwaminifu, kisha niarifu. Ama kuhusu udugu, nakuachia wewe utangaze kwa uadilifu jiha hii ya swala hili. Ninachotaka kusema ni kwamba nyinyi mnakubaliwa kuwa *Makureishi*, nasi tu tulivyo.

Bwana Sheikh, je mtu anaweza kutupilia mbali nyumba kubwa yenye ghorofa tatu ya wazazi wake? Tusipoona njia ya kujihifadhi dhidi ya fitina, udhia na ugomvi, tukashika njia hii kwa shabaha ya kudumisha amani. Je wataka kuvunja Jumuiya yetu na kutuzuia tusiweze hata kutaja jina la Mungu katika sehemu hiyo ya mji? Hata hivyo watuita sisi kuwa wafitini! Huna hofu ya Mungu? Twamwomba Yeye tu Akiwa Mlinzi. Twamtegemea Mungu tu pekee, Aliye Mlinzi bora na Mwenye kuhurumia kuliko wote (12:65). Zaidi ya hayo niseme nini? U mzee kuliko mimi. Nduguzo walikuwa wadogo kuliko wewe; hao wote wamekwisha kufa. Nami nitakufa katika zamu yangu. Nyumba yoyote katika hizi na jengo lolote halitakwenda nasi."

Mwanzoni mwa Agosti 1909, Sheikh Yakub Ali Irfani r.a. alimwomba Hadhrat Khalifatul Masihi r.a kumpatia ujumbe kwa tawi la Jumuiya alilopanga kulitembelea; akaandika:

"Nawataka wanajumuiya waitangulize imani juu ya dunia; na hitilafu ikitokea baina ya hizo mbili, msiithamini dunia hata kidogo. Nahitaji watu wenye uthabiti wa hali ya juu kuwa wabashiri watakaohubiri kwa unyofu na ufahamu wa kweli. Nahitaji masheikh wenye busara ambao wanamtegemea

> kabisa Mungu, na wana imani katika maombi na hawajivunii ujuzi wao; wanaoshughulikia saa zote kutafuta njia za kujipatia radhi ya Mungu. Lakini wapo wachache wa aina hii. Namlilia Mungu tu."

Mnamo Januari 19, 1910, akawaandikia wanafunzi wa Kiahmadiyya wa M.A.O. College, Aligarh:

> «Wapenzi, amani iwe kwenu na rehema ya Mungu na baraka Zake. Kule mliko kuna mitihani ya dipolma na digrii, na ulimwengu wa Cambridge na Oxford, lakini sisi tumejitolea kwa ulimwengu wa bonde kame (ambako Ibrahimu a.s. aliwakalisha Bi Hajira r.a. na Ismaili a.s., 14:38). Fungeni nia kwamba mtapita katika majaribio yote mawili mkahesabiwa kati ya wale wanaopata ufaulu mkubwa (33:72)."

Mkutano wa Mwaka wa 1909 uliahirishwa mpaka msimu wa rabiu wa 1910 na ukafanyika katika Machi 25-27, 1910. Mkutano huo ulifana sana, na idadi kubwa ya watu walifanya baiati, lakini Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. hakuridhika kabisa na akaeleza mashaka yake katika hotuba ya Ijumaa iliyofuata ambamo akatamka:

> "Nimefika hapa kwa taabu kubwa. Sisikii vizuri kabisa. Kichwa chaniuma vikali. Katika muda huu wa kuugua nimechunguza sana hali yenu na yangu pia. Wakati mwingine naogopa nitapoteza uwezo wangu wa kuona; na pia nimefikiria kwamba jicho la Mungu halikosi kuona kitu chochote kiwacho. Kwa kifupi, mawazo yangu yamepitia eneo kubwa. Nilikuwa nafikiria kusoma: Nashuhudia kwamba hakuna mwabudiwa isipokuwa Mungu; na kuketi, lakini kuna jambo la muhimu sana linalonilazimisha kusema. Mwaweza kufikiria kwamba hii ndiyo siku yangu ya mwisho, na nitakayonena kuwa maneno yangu ya mwisho.

Mmejumuika hapa, na kuna mikutano pia huko Gurukul, na ya *Anjuman Himayate Islam* mjini Lahore, na ya Educational Conference kule Aligarh, ambako taarifa zitasomwa. Hapa pia mwandikaji wetu wa habari ametuambia habari zote kuhusu mapato na matumizi. Lakini nimeendelea kutafakari kwa nini temekusanyika hapa? Fedha zingeweza kuletwa kwa njia ya posta, na taarifa ingeweza kupigwa chapa na kupostiwa. Mia tatu ndio walihudhuria. Kama viongozi tu miongoni mwao wangalionana nami, ningaliwaombea na kuwatolea mawaidha. Lakini waliofika kuonana nami, wamefika walipokuwa tayari kuondoka nao wakaja kuniaga. Zingatieni ya kwamba sipendi kabisa mikutano ambayo shabaha yake kuu si kuimarisha khulka za kiroho. Kama nilivyosema fedha zingaliweza kutumwa kwa hawala ya posta, na gharama zote za usafiri na matumizi ya wageni yangeweza kuokolewa. Wenye duka hapa wanakusudia faida za kidunia tu, kwani wanapenda Mkutano ufanyike mjini ili mapato yao yapate kuongezeka sana. Wale wanaonisikiliza wanapaswa kukumbuka na kuwaambia wengine kwamba mimi nachukia mikutano yote inayofanywa na fedha zote zinazokusanywa kwa ajili ya shabaha za kidunia. Nimekuwa mgonjwa kwa sababu ya mashaka haya. Ingelikuwa vizuri sana kama makatibu na viongozi wa matawi mbalimbali wangalikaa nami kwa wakati fulani. Nahangaika kwa sababu *wana-Sadr Anjuman* pia walishindwa kuwaambia jambo hili waliowasili kutoka nje. Sijali kiasi gani kilipatikana na kukusanywa. Haja yetu kubwa ni Mungu. Sijui kiasi gani kilikusanywa, wala siijali. Nawasihi tena kumtanguliza Mungu juu ya chochote kingine. Juhudi zetu zote zapaswa kulenga shabaha hiyo. Kama tukiiacha, yafaa nini shule ya sekondari, na kuna faida gani ya majengo yake; yatulazimu tutafute radhi

> ya Bwana wetu. Waandikie marafiki zenu na kuwasihi jambo hili. Niliendelea kuwasubiri marafiki zetu kutoka Lahore na Amritsar, lakini hata mmoja miongoni mwao hakuwahi kurejea kwa shabaha ya kujifunza kwangu. Napenda kwamba nyinyi nyote muwe wema na wanyofu, na mwishughulikie kidogo dunia na mapambo yake."

Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. aliitwa kufika Multan katika Korti ya Rae Kaishu Das tarehe 26 Julai 1910 akiwa shahidi wa mshtakiwa fulani katika kesi ya jinai. Akaondoka Qadian tarehe 24 Julai na kushinda Lahore kwa siku moja akielekea Multan. Alipokuwa Lahore akapokea barua ya Mshia mmoja aliyeshauri kwamba mjadala upatikane baina yake (Hadhrat Khalifatul Masihi r.a.) na Sheikh mmoja wa Kishia aliyewasili kutoka Iran, na akashauri awekwe mwamuzi wa kukubaliwa na pande zote mbili atakayetoa uamuzi wake baada ya kusikiliza mjadala. Akajibu:

> "Niko tayari saa zote kutafuta ukweli. Kwa fadhili ya Mungu mimi nina umri wa miaka sabini, sina nafasi nyingi ya kuishi. Hata hivyo nikipata kujua njia ya ukweli, sitadumu katika kosa, Mungu Akijalia. Lakini mwamuzi atakuwa wa madhehebu au dini gani na kutokupendelea kwake kutawezaje kuhakikishwa?"
>
> Mshia huyo hakufuatia tena jambo hilo.

Yule mshtakiwa katika kesi ya jinai mjini Multan alikuwa askari wa zamani aliyeshtakaiwa kwa hatia ya kuua pasipo kukusudia. Akajitetea kwamba hakuwa na akili timamu. Karibu miezi sita kabla alikuwa amekwenda Qadian kwa kutibiwa na Hakim Nuruddin na kukaa huko wiki moja au siku kumi. Shahidi mtukufu alipofika kortini jaji akamstahi na kumheshimu sana. Akamwomba radhi, kwani kwa kufuata utaratibu wa kanuni ilibidi aitwe akiwa shahidi. Hakuambiwa

kwenda kusimama kizimbani, bali akatoa ushahidi akikaa kitini. Kwa jumla akaeleza akitoa ushahidi:

> "Namtambua mshtakiwa. Alinijia kwa kutibiwa miezi zaidi ya sita iliyopita. Alikuwa amefuatana na mtu mwingine. Uchunguzi wangu ulikuwa kwamba yeye alipatwa na aina fulani ya wazimu. Alama zake ni ulegevu, kusita kumweleza tabibu hali ya kweli, weupe wa macho kutokupenyezeka kwa nuru, kukasirika haraka. Akakaa kwa wiki moja ama siku kumi, lakini hakupata nafuu. Nilimshauri kukaa zaidi, lakini hakukubali. Nikamwangalia mara moja katika siku, kwa dakika chache. Sikumwambia kuendelea kukaa kwangu.
>
> Mimi ni *Khalifa* wa kwanza wa Hadhrat Mirza Sahib a.s., nami ndimi kiongozi wa Jumuiya ya Ahmadiyya. Nimefanya kazi ya utabibu kwa miaka arobaini na mitano. Nilikuwa Tabibu Mkuu wa Maharaja wa Kashmir. Sikusikia kwamba mshtakiwa amewahi kumshambulia mtu. Nikamwandikia dawa. Siweki rejista ya majina ya wagonjwa. Namchunguza kila mgonjwa kwa uangalifu, si kwa juu juu tu ."

Mawakili na mwangalizi wa korti pia wakamtendea vizuri kwa adabu.

Alinuia kuondoka Multan siku hiyo hiyo lakini kwa sababu ya kuombwa na waungwana wa mji akakubali kukawia siku moja. Siku hiyo akawashughulikia wagonjwa kuwachunguza, na jioni akahutubia mkutano wa hadhara katika ukumbi wa *Anjuman Islamiah.* Usiku huo akaondoka kuelekea Lahore na kukaa huko siku tatu. Siku ya Jumapili asubuhi, Julai 31, akahutubia mkutano wa hadhara kuhusu Islamu na Dini nyingine na siku hiyo jioni akarejea Qadian.

Tarehe 22 Oktoba, 1910, akamwandikia rafiki mmoja

akihakikisha imani yake:

> "Si katika uwezo wa mtu kupasua moyo wake na kuonyesha fikira zilizomo ndani. Kama maneno anayosema mtu kwa kuapa yanaaminiwa, basi hakuna uhakikisho mkubwa zaidi wa ukweli kuliko kumfanya Mungu Aliye Mkuu kuwa Shahidi. Baada ya kifo changu, si wewe wala mwingine yeyote awaye atakayekuwa pamoja nami. Nitakuwa tu pamoja na imani yangu na vitendo vyangu. Kila jambo litaamuliwa na Mungu, Aliye Mkuu, Ambaye kwa amri yake mbingu na ardhi zinadumu kuwepo.
>
> Naamini unyofu wa Hadhrat Mirza Sahib a.s. Alikuwa Mjadidi wa karne hii. Naamini kuwa yeye alikuwa mtumishi mwaminifu kabisa wa Muhammad s.a.w., Mjumbe wa Mungu, Nabii Mwarabu wa Makkah, *Khatamun Nabiyyin,* na wa sheria aliyoleta yeye. Hadhrat Mirza Sahib a.s. mwenyewe alijihesabu kuwa mtumishi mwaminifu sana wa Nabii Mwarabu Muhammad s.a.w. bin Abdullahi bin Abdul Muttalib bin Hashim bin Abdi Manaf. Neno Nabii lamaanisha mtu anayetabiri sawa na aliyofunuliwa na Mungu. Hatuamini kwamba Nabii lazima huleta sheria mpya.
>
> Hadhrat Mirza Sahib a.s. na mimi tunashikamana sana na imani ya kwamba yeyote akataaye hata irabu moja ya Kurani Tukufu au ya Sheria ya Muhammad s.a.w., Mjumbe wa Mungu, ni kafiri na anatupiliwa mbali na Mungu. Yeyote anayekataa maneno yangu hayo au kukinza au anayafikiria kuwa si manyofu, yeye mtu huyo ataulizwa na Mungu."

Mhariri wa *Badr* alitoa tangazo lifuatalo katika *Badr* mwanzoni mwa Novemba 1910:

“Hadhrat Khalifatul Masihi ameagiza ya kwamba kwa kuwa afya yake si nzuri, na wakati mwingine anakuwa mgonjwa sana, na maisha ya mtu hayategemewi, hivyo itangazwe kwamba kama mtu yeyote anaona kuwa yeye anamdai fedha aliyokuwa ameweka kwake kama amana au karadha au kwa namna yoyote, au kama kuna mgonjwa anayefikiria hajapata pesa yake kwake anapaswa kujitokeza na kupokea kile anachofikiri kuwa haki yake. Amesema kwamba kwa fadhili za Mungu ni rahisi kwake kutimiza madai yote kama hayo. Mungu Amemjaalia njia za kulipa hayo.”

“Katika siku za Mkutano wa Mwaka uliopita, Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. alipokuwa amesimama upande wa kusini wa nyumba ya Nawab Muhammad Ali Khan r.a., mtu mmoja alimpa fedha. Hakumbuki nani alimpa hiyo fedha na kwa kazi gani. Fedha ziliwekwa kando wala hata hazikuhesabiwa. Wasomaji wa hili tangazo wawaeleze wengine na bidii itiwe kujua nani alitoa fedha hizo na kwa shabaha gani.”

# XV

# UGONJWA

Wakati alipokuwa akitoa hotuba ya Ijumaa, terehe 18 Novemba 1910, Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akaeleza hisia zake kama yafuatavyo:

> "Napenda sana nione kwamba Jumuiya hii inampenda sana Mungu na kumtii Mjumbe wake na kufahamu Kurani. Mola wangu pasipo kunitia katika majaribio na bila mimi kumwomba Amenijaalia fadhili zake nyingi tena kubwa. Yeye amenitimizia haja zangu sikuzote. Yeye Mwenyewe Ananilisha na kunivisha na kunipatia faraja. Amenijaalia nyumba, mke, watoto na marafiki wanyofu na wa kweli. Amenipatia idadi kubwa ajabu ya vitabu, na Amenipa nafasi ya kuvisoma na Amenijaalia afya njema, ujuzi na kila kitu kilichohitajika. Sasa mapenzi yangu ni – nami natumai kabisa kwamba Mola wangu Ananitimizia haja hii yangu pia – kwamba miongoni mwenu wapatikane wanaompenda Mungu na neno la Mungu Alilomteremshia Muhammad s.a.w., Mjumbe wa Mungu, na kumtii Mungu, na kumfuata barabara *Khatamun Nabiyyin* wake. Huenda miongoni mwenu wapo wanaofuata Kurani Tukufu na suna ya Mtume Mtukufu s.a.w. Naomba kwamba nikiaga dunia hii, macho yangu na moyo wangu vitulie kuwahusu nyinyi. Sitaki kwenu ujira, wala sihitaji mnitolee kitu. Sitaki hata mmoja wenu aniamkie. Yote ninayohitaji ni kwamba muwe mnamtii Mungu, na mkiwa wafuasi wa kweli na Muhammad s.a.w., Mjumbe wa Mungu, mzifikishie sehemu zote za dunia, kwa amani na urafiki, ujumbe huu: Hakuna apasaye kuabudiwa isipokuwa Mungu."

Baada ya sala akaamua kumtembelea Nawab Muhammad Ali Khan aliyerejea Qadian siku moja kabla kutoka Malir Kotla. Kwa kuwa ilikuwa safari ya maili moja na nusu takriban, akaamua kumpanda farasi jike, mnyama mwenye nguvu ambaye mtu fulani alimpatia zawadi mwanaye mkubwa, Abdul Hai, kijana mwenye umri wa miaka kumi na mmoja. Alipokwisha msogelea na kumpanda, mtu mmoja aliyekuwa amesimama hapo akaona vikuku viko juu zaidi na akajitolea kuvishusha kidogo chini ili aweze kupanda kwa urahisi, lakini akamkataza akisema kwamba vimewekwa hivyo kuwafaa watoto kwa hiyo visishushwe chini. Akapanda na kuondoka. Wale waliomwona akipita huku akiwa amepanda wakaona kwamba ingawaje farasi alikuwa anakwenda kasi, lakini yeye alikaa vizuri na imara na kufurahia kwenda juu ya farasi. Alipoingia mjini akalazimika kupitia njia nyembamba. Mahali fulani katika njia hiyo nyembamba farasi akaruka upande ghafla, akarushwa kulia, mguu wake wa kushoto ukanasa katika kikuku, na akatupwa upande wa kuume juu ya mwamba mmoja uliobenuka. Akapata vijeraha vidogo vidogo vingi na jeraha moja baya kwenye panja la kuume lililotoka damu nyingi sana. Alipong'amua kilichofanyika akasema kwa sauti ya juu: "Aliyetumwa na Mungu amethibitika kuwa mkweli." Hayo ndiyo marejeo kwenye ruya moja ya Masihi Aliyeahidiwa ambamo alimwona Maulawii Nuruddin ameanguka kutoka kwenye farasi. Alipoota ruya hii, hata Ahmadiyya mmoja katika Qadian hakuwa na farasi wa kupandika. Pengine funuo zake mbili zinataja tukio hilo. Mmoja ni: Uhai wa pili; na mwingine ni: Uhai uliotanguka.

Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. alikuwa mtulivu kabisa, hakuhangaika hata kidogo. Msaada wa kwanza ukapatikana haraka na jeraha la panja likashonwa bila nusukaputi. Waliomtibu hawakuona mshtuko wa msuli mmoja waliposhughulikia kumtibu. Habari ya ajali ilipoenea wanaume kwa wanawake wakaelekea nyumbani kwake wakihangaika

kuhakikisha wenyewe usalama wake. Kwa wanaume akasema atawaombea. Kwa wakina mama akapeleka ujumbe kwamba yeye hajambo, hana wasiwasi wala hofu; wapaswa kurejea nyumbani kwao wakiacha majina yao, naye atawaombea. Kuhusu shauri ya kwamba daktari mkuu wa Delhi anaweza kuitwa, akajibu: "Mtegemeeni Mungu. Tegemeo langu si madaktari wala matabibu. Namtegemea Mungu kikamilifu, nanyi mwapaswa kufanya hivyo."

Jeraha la panja lake likawa donda la kudumu na ugonjwa wake uliendelea kwa miezi mingi. Ilikuwa tarehe 19 Mei 1911, miezi sita kamili baada ya ajali, ambapo akaweza kwenda mskitini na kusalisha sala ya Ijumaa lakini hiyo ilikuwa kwa taabu. Hata hivyo katika kipindi kirefu cha kupata ahueni akajishughulisha kikamilifu na kuweka mfano bora sana wa kujitolea kwa kutimiza wajibu.

Tarehe 29 Novemba 1910, akachapisha na kueneza ujumbe wake ambamo alisema:

> "Jaribio ninamopitia ndiyo nafasi ya onyesho la jiha mbalimbali za huruma, rehema na fadhili za Mungu. Mungu Mtukufu Amenidhihirishia kujitolea kwa nyoyo za wengi ambao napaswa kuwa na upendo kwao. Wapo wengine ambao kuwahusu hao sikuwa na habari kwamba wanipenda mimi na wanajumuiya wenzao. Namna walivyonitumikia mchana na usiku katika siku za mimi kuugua huonyesha kiwango cha upendo wao, na ndiyo kwa njia hiyo Mungu Amedhihirisha sifa zao bora. Hiyo yahakikisha jinsi Mungu Anavyonitunza. Nawashukuru sana wote walioonyesha kwangu moyo mpole katika hali yangu hii ya hivi sasa.
>
> Moyo wangu watulia. Hakuna ninayempenda zaidi kuliko Mungu, wala hakuna aliye msaidizi wangu na tegemeo langu jinsi Alivyo Yeye. Alinijalia fadhili zake na ukarimu wake bila

> hesabu katika hali yangu hii. Akanipatia kutoka huko asikoweza kuwaza yeyote. Ameondolea mbali hata njia dhahiri ya riziki yangu ambayo ndiyo kazi yangu ya utabibu na Ameniruzuku kwa njia za siri. Sidaiwi na yeyote kwa riziki hiyo iliyofika nyumbani kwangu siku hizi: Nawiwa na Mungu tu kwa hiyo yote. Hayo yote ni ajabu sana machoni mwa waonao."

Mnamo Desemba 1910, akatamka siku moja:

> "Ugonjwa ni jaribio kwa njia nyingi. Matumizi yanapanda, na mapato yanapungua, na mtu huwa anawategemea wengine. Njia dhahiri ya kupata riziki yangu ilikuwa utabibu, ambayo imetanguka kwa sababu ya ugonjwa wangu. Wasiojua kweli hasa ya mambo yangu wakafikiri kwamba utabibu wangu ulikuwa ni njia ya kutimiza mahitaji yangu, na Mungu Ameiondoa sasa. Mke wangu akaniambia leo kwamba hana hela iliyobaki, na akasema: Hukufikiria katu kuugua. Katika hali ya ugonjwa mtu anaweza kukosa hata mahitaji la lazima ya maisha. Nikamwambia kwamba njia ya Mungu wangu kunihusu mimi si hivyo. Ningeliweka fedha akiba kama nisingelimtegemea Mungu kikamilifu."

Ikawa hivi kwamba pasipo kujua yeye, hawala mbili za posta zenye thamani ya rupia mia moja ishirini na tano zikawasili ili zilipwe kwake. Alipoarifiwa kuhusu hizo akajawa na maono mazito na akamsifu Mungu kwa moyo wote na akanena: "Ndivyo ilivyo fadhili ya Mungu wangu Mweza. Ameonyesha kwamba ananipatia pasipo kuhesabia ufundi wangu nikiwa tabibu, namna ambavyo haieleweki. Mke wangu hawezi kuitambua kwa sababu ya udhaifu wake. Imani yangu ni imara. Mungu wangu daima Ananitendea hivyo."

Maonyesho hayo ya Mungu kuruzuku yakaendelea sikuzote. Siku moja alimwagiza Sheikh Muhammad Taimur kutengeneza

hesabu ya matumizi yote yaliyofanyika katika siku za maradhi yake kama vile dawa, bendeji na kadhalika, na fedha zote kwa jumla zilipwe kutoka katika fedha zilizokwisha patikana sasa. Akasema: "Mola wangu Aniruzuku. Sipendi kuwiwa na yeyote awaye. Yeye Ameniahidi kwamba Atanitimizia mahitaji yangu yote.»

Tarehe 15 Desemba 1910, taarifa ikatolewa kwamba Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. afya yake inazidi kuwa nzuri. Hana homa, wala hana kikohozi. Alikuwa bado dhaifu sana, ijapokuwa alipata nguvu kidogo. Vijeraha vyake viliendelea kupona pole pole, kimoja cha mdomoni kikapona kabisa na akawa hana shida kula na kuzungumza. Mara moja moja aliona shida ya kupata usingizi. Kila siku akasomewa Kurani Tukufu, asubuhi na jioni. Akaeleza maoni yake kuhusu baadhi ya mambo fulani na akatoa nasaha. Mzungu mmoja akaja kwa kumjulia hali, na Khalifatul Masihi r.a. akaongea naye kiasi fulani kuhusu Islamu.

Mkutano wa Mwaka ulifanyika tarehe 25, 26, na 27 Desemba 1910. Hadhrat Khalifatul Masihi akauhutubia Mkutano jioni ya Desemba 25 juu ya: Hakuna mwabudiwa isipokuwa Mungu; na tena tarehe 27 Desemba, saa za jioni kuhusu: Silaha ya Dua. Akitoa hotuba yake ya pili alisema:

> "Niombeni, nitawajibuni (40:61) ndiyo silaha moja, nayo yafaa sana. Pengine anayeitumia ni dhaifu na anaikataa faida yake. Ndiyo silaha ya dua ambayo imetupiliwa mbali siku hizi na wanadamu. Wanajumuiya wa Jumuiya yetu wanapaswa kuinoa na kuitumia. Wanapaswa kufululiza kuomba pasipo kuchoka kufanya maombi. Mimi naugua sana, wala hakuna awezaye kujua nitaishi muda gani; hivyo, nasaha yangu ya mwisho ni: Pamoja na 'Hakuna apasaye kuabudiwa ila Mungu', inoeni silaha ya dua. Kusiwe na farakano katika Jumuiya, kwani

farakano likipatikana Jumuiya huadhibiwa na Mungu; kama ilivyosemwa ndani ya Kurani Tukufu: Basi waliposahau waliyoyakumbushwa, Tukawaokoa wale waliokuwa wakikataza maovu, na tukawakamata wale waliodhulumu kwa adhabu mbaya kwa sababu walikuwa wakiasi (7:166). Hadi sasa mlihifadhiwa msipatwe na adhabu hiyo. Hata maombi hayasaidii bila ya rehema na huruma ya Mungu. Kwa hiyo, nawasihini: Ombeni mfululizo; nakariri: Ombeni mfululizo ya kwamba Jumuiya ilindwe isipate kufarakana. Fadhili ya Mungu iliyojaaliwa Jumuiya mpaka sasa ni kwa sababu ya maombi. Niombeeni pia kwamba wasaidizi wangu wawe waaminio wanyofu, watiifu kwa Mungu, wema na wakarimu, wasioniasi. Nijaaliwe wabashiri ambao wakiwa na imani inayoeleweka akilini, watambue ukweli, wasiwe na tabia ya kupenda anasa za dunia, na zaidi ya kuwa wanyofu wafahamu suna ya Mtume Mtukufu s.a.w."

Akamalizia:

"Mwawiwa nami wajibu kadhaa:

1. Mmefanya baiati yangu na mnawiwa nami utii. Yule anayevunja ahadi atakuwa mnafiki. Nachelea isije yeyote akawa mnafiki kwa kuniasi.
2. Naomba kwa uchungu kwa niaba yenu.
3. Kwa sababu ya maradhi siwezi kufanya sujuda katika sala, hata hivyo nimewaombeeni kirefu na kwa bidii katika hali ya sujuda.

Basi kwa kukiri wajibu wenu kunihusu mimi, yawapaseni kuepukana na hitilafu na mifarakano."

Mkutano wa Mwaka ulipomalizika, akawaita Maraisi na viongozi wa matawi na akawaambia:

> “Nimewaiteni kwani niliudhika kwa sababu hamkuonana nami mwaka jana, nami nilikusudia ya kwamba nikibaki hai nitawatoleeni nasaha mwaka huu. Mimi hata sikupata kuwaza kwamba nitakuwa Kiongozi wa kirorho wa Jumuiya, lakini Mungu Alipotaka Akanifanya mara moja. Nyinyi ni viongozi katika Jumuiya, na bila shaka mara nyingi mwazikabili shida. Mtu anaweza kufikiri kwa nini yeye hakufanywa kiongozi na akaingiwa na chuki moyoni. Hali yangu mimi binafsi ni kwamba kama baada ya kufariki Masihi Aliyeahidiwa a.s., bintiye Amatul Hafidh aliye mtoto mchanga angelichaguliwa kuwa Khalifa, ningelikuwa wa kwanza kufanya baiati kwake, na kumtii jinsi nilivyokuwa namtii babake, nikiwa na yakini kwamba ahadi za Mungu zitatimia kwa njia yake pia. Kusudio langu kwa kusema hivyo ni kwamba mtu asiingiwe na tamaa kama hizo.
>
> Nasaha yangu ya kwanza ni hii – nami nawaombeni kuiweka sana moyoni – kwamba mkikabili mishikili, zingatieni maagizo ya Mungu! Jiepusheni na mafarakano isije mkakwaa na nguvu yenu ikawatoka. Kaeni imara; bila shaka Mungu Yu pamoja na wakaao imara (8:47). Mungu Akiwa Mwumbaji wa tabia ya sili ya mtu, akatambua kwamba kutakuwa na mafarakano; basi akaagiza: Muwe imara; Mungu Yu pamoja na walio imara. Basi mkihitilafiana na kiongozi mmojawapo, kaeni imara. Mungu Atakuwa pamoja na yule akaaye imara kwa ajili ya radhi Yake.
>
> Ninayo haki ya kuwasihini. Baada ya nyinyi kwisha kufunga ahadi kwamba mtanitii katika mambo yote

mema, nawaambieni kunitii katika jambo hili: Jiepusheni na mafarakano. Wakati wowote mkikabili mafarakano, angukeni katika sujuda mbele ya Mungu ili mjaaliwe uimara. Msiogope mishkili; katika kila hali mtu hulazimika kuikabili. Mimi nalipata kuikabili ile yangu. Baadhi ya wanajumuiya wakaangukia kosa na wakafanya hatia ya ujuvi mkubwa na kukosa adabu; lakini nikavumilia. Hawakutambua walikuwa na wajibu gani kumhusu Kiongozi wa Jumuiya. Kutokutambua huo ni kwa sababu ya kukosa ujuzi. Lakini Mungu Alikuwa mwenye huruma; Yeye Mwenyewe Akanyosha nyoyo zao. Nyoyo zimo mikononi mwa Mungu na Yeye Akazielekeza zote hizo kwangu mimi, kwa hiyo hao na sisi na Jumuiya tutashuhudia huruma yake na ukarimu wake. Basi epukaneni na mafarakano nyinyi wenyewe na waelekezeni wanajumuiya wengine wayaepuke. Mungu Mtukufu Ameamuru kukaa imara katika hali kama hizo.

Jambo jingine ninalotaka mlizingatie ni kwamba katika baadhi ya sehemu ambapo kuna wanajumuiya wengi, maendeleo zaidi yamekuwa kidogo. Naelewa sababu yake, na ninawasihini kujaribia dawa mbili. Ya kwanza ni kwamba viongozi wamwombe Mungu kwa uchungu. Mwajua kwamba jua au mwezi unapopatwa, sala inasaliwa. Mtume Mtukufu s.a.w. alikuwa akihangaika sana wakati wa jua na mwezi kupatwa, ingawaje alielewa hilo huwa sawa na kanuni ya asili inayofanya kazi ulimwenguni, kama ilivyosema Kurani Tukufu: Na mwezi Tumeupimia vituo (36:40). Alijua ya kwamba wakati wa kupatwa mwanga wa jua au mwezi haupungui, bali hukingwa usifikie ardhi. Hata hivyo alikuwa anafadhaika, kwani aliagizwa kufikisha ujumbe na akahofia isije kikwazo fulani kikaja kati kuzuia ufikishaji wa ujumbe

wake. Kwa hiyo wakati wa kupatwa jua au mwezi akafanya maombi, akatoa sadaka, akatoa dhabihu na akawapa uhuru watumwa.

Wataalamu wajinga wa falsafa wakasindwa kutambua siri hii, lakini Nabii anatambua kwamba yeye mwenyewe anang'ara, hata hivyo anachelea isije mng'ao wake ukazuilika jinsi nuru ya jua au mwezi inavyozuilika wakati wa kupatwa. Basi anamwomba Mungu na kutoa sadaka. Kutoa sadaka ni dawa ya pili kwa kuondolea mbali kizingiti cha kati katika maendeleo. Zingatieni sana kwamba popote maendeleo yakipungua, viongozi wa hapo wapaswa kutawadha na kufanya maombi ndani ya sala na kutoa sadaka binafsi ili Mungu Aridhike na kuondoa kizuizi katika njia ya maendeleo. Nawaamuruni kutoa sadaka, kwani sadaka na kutoa mali kwa wanaostahili huzima moto wa ghadhabu ya Mungu.

Mwishoni napenda kuwaonya kudhania viovu kuhusu utumiaji wa fedha za Jumuiya. Wahusikao na jambo hilo waliopo hapa katika makao mkuu ni waaminifu na wenye kutegemewa. Kwa hiyo msiwe na hofu kuhusu habari hii. Mimi nami ni mdhamini wa chochote ninacholetewa. Nataka kuwahakikishieni kwamba Mungu Hakunifanya mwenye tamaa ya mali. Sina tamaa ya mali. Nampa mke wangu fedha kiasi fulani maalum. Wala sina tamaa ya ukuu.

Nasogelea mwisho wangu. Mimi ni mpenda heri kwenu mwaminifu. Nawaombeeni daima dumu. Sikupokea fedha kutoka kwa baba yangu; lakini Mola wangu Amenipa sana na bado Anaendelea kufanya hivyo. Kwa hiyo, tupilieni mbali dhana mbaya kuhusu habari hii. Stawisheni huba baina yenu, epukaneni na fitina, msimdhanie vibaya yeyote; mtu

akiwakasirikieni muwe imara, na dumuni katika maombi.

Hayo yote nilikuwa nayo moyoni tangu mwaka mzima kwamba nitawaambieni. Baadhi yenu pengine walidhani kwamba nilikuwa na madhumuni ya binafsi katika kuwatakeni mnione. Sihitaji chochote kwenu. Jina langu huko mbinguni ni Abdul Basit, maana yake ni mtumishi wa Mpaji sana. Amenipa kila kitu kinachohitajika. Ni kubwa sana hisani yake juu yangu. Kitambo kidogo kimepita nilipoanguka kutoka juu ya farasi jike niliyekuwa nimempanda. Kama angalinipiga teke jichoni, ingelikuwaje hali yangu? Lakini nikalindwa kwa hisani Yake. Makosa mengi yalifanyika katika mwaka unaokaribia kwisha, lakini natumai kwa fadhili Zake kwamba makosa yote hayo hayatarudiwa katika mwaka unaokarubia kuanza."

Taarifa ya daktari ya tarehe 5 Januari 1911 ikaeleza ya kwamba vijeraha vya Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. vilitibiwa kila siku katika siku za Mkutano wa Mwaka na akafungwa bendeji moja, lakini sasa majeraha yamepona na bendeji imeondolewa. Kwa sababu ya shughuli nyingi katika siku za Mkutano wa Mwaka na kupokea wageni na kuongea nao akapatwa na uchovu mwingi. Meno yake mawili yaliyomsumbua yakang'olewa. Akapatwa na homa kwa siku mbili. Sasa hajambo, lakini anapata maumivu ya neva mara kwa mara. Yu mchangamfu saa zote, hana shida au wasiwasi. Baada ya meno yake kuong'olewa akasema: "Kila maumivu yana malipo yake. Sasa naweza kunywa na kuyafurahia maji baridi."

Baada ya wiki moja ikaripotiwa ya kwamba bado anasumbuka kwa maumivu ya neva mara kwa mara na ana uvimbe shavuni unaouma ambao umesababishwa na meno yake kung'olewa.

Taarifa ya tarehe 19 January ikaonyesha kwamba maumivu

ya neva yanaendelea mara moja moja, hana utulivu, usiku mmoja hakupata usingizi.

Dkt. Mirza Yakub Beig alitoa taarifa tarehe 22 Januari kuhusu maendeleo mazuri kwa kila jinsi. Mgonjwa mtukufu alilala vizuri usiku, hana homa. Anaendelea kupata nguvu kidogo kidogo. Daktari alipokuwa anatoka baada ya kumchunguza akamwuliza mgonjwa kuhusu chochote apendacho. Akajibu:

> "Yote unayopenda moyo wangu ni kwamba Mungu Aniwie radhi. (Akarudia haya mara tatu) Napenda mwendelee kuwa watii wala msifarakane. Msilete ukinzani. Nimekwisha pata shibe ya dunia. Sina hamu ya kidunia. Kila nipendacho ni kwamba nitakapokufa Mungu Awe Amekwisha niridhia. Mwambie hayo kila mmoja. Siijali dunia hii. Nilijaaliwa nyingi na nilipewa nyingi, nilitumia nyingi na nilitoa nyingi. Sina tamanio tena. Wakati mwingine natamani nipate afya isije ugonjwa unaofululiza ukaharibu imani yangu. Mungu, nakuomba, niwie radhi.
>
> Napenda sana kwamba kusizuke fitina katika Jumuiya yangu. Dunia haina maana kwangu. Nitaridhika sana kama mtaendelea na umoja. Siwezi kufanya sujuda kwa sababu ya ugonjwa wangu; hata hivyo nawaombeeni nikisujudu. Nimewaombeeni mara kwa mara kwa wema wenu. Sihitaji kwenu chochote, wala sina tamaa yoyote ya kidunia. Mola wangu Ananipatia kwa wingi kwa njia za siri, kwa wingi zaidi kuliko mahitaji yangu. Jihadharini na hitilafu na ukinzani. Mkiepukana na hayo mtabarikiwa sana na Mungu, na heshima yenu na nguvu yengu itadumu; la sivyo matapoteza kila kitu.
>
> Mimi sikutoa agizo lotole kwa matilaba ya ubinafsi; maagizo yangu yote ni kwa kutafuta radhi ya Mungu. Tieni

bidii katika kusali na kuomba kwa kudumu. Sala ndiyo dua. Msizidishe hitilafu na ukinzani; hivyo vimeleta uharibifu sana. Hitilafu zikizuka, kaeni kimya. Jiombeeni nyinyi na wapinzani wenu. Tubuni sana: Hamna mwabudiwa isipokuwa Mungu; Muhammad ni Mjumbe wa Mungu. Shikamaneni na Kurani. Isomeni sana na tendeni sawa nayo. Ama kunihusu mimi, namridhia Mungu kuwa Mola, Islam kuwa dini na Muhammad s.a.w. kuwa Mjumbe. Kwa hayo nawawekeni chini ya himaya ya Mungu."

Taarifa za baadaye za kidaktari zaonyesha ya kwamba Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. aliendelea kupata nafuu pole pole akielekea kupona kikamilifu. Majeraha yake yote yakapona isipokuwa jeraha la panja la kuume likawa kidonda kisicho kauka. Alijilazimisha kupitisha mchana katika sebule yake kushughulikia kazi yake na kutimiza wajibu wake kadiri alivyoweza. Alitoa darasa na mara moja moja aliwatazama wagonjwa na kuwaandikia dawa. Tarehe 30 Januari, alimwita Makhdum Mian Muhammad Siddik aje na karatasi na vifaa vya kuandikia; akamwambia kusoma mara tatu aya hii ya Kurani Tukufu: "Je, hayakuwatosha ya kwamba Tumekuteremshia Kitabu wanachosomewa? Bila shaka katika haya mna rehema na mauidha kwa watu wanaoamini (29:52);" na, akiisha fanya hivyo, akamwambia:

''Katika aya hiyo Mungu Ameeleza hatua zote za kusonga mbele kwa mtafuta ukweli. Anauliza: Je, Kitabu Tulichomteremshia Muhamamd s.a.w. hakitoshi kwa mahitaji yote ya waaminio? Ndani yake mna rehema na mauidha ya kila namna.

Natambua vizuri maonyesho ya kudra na kila namna ya kashfi, lakini baada ya ushahidi wa Mungu naona itakuwa utovu wa hali ya juu sana wa shukurani kukimbilia njia

nyingine yoyote ya maendeleo ya roho. Naihesabu kuwa mchezo tu. Kumbukeni hiyo, nyinyi nyote. Kama wazo lolote kinyume chake likizuka nyoyoni mwenu baada ya mimi kuaga dinia, tafuteni mwongozo kutokana na hii: Hakuna nguvu ya kuondoa ubaya wala hakuna nguvu ya kuleta wema isipokuwa kwa Mungu Mtukufu Mkuu.

Tena, zingatieni ushahidi mwingine wa Mungu uliopo mwanzoni kabisa mwa Kurani Tukufu, yaani: Mimi, Mungu, Najua sana, Nahakikisha kwamba hiki ni Kitabu Kikamilifu, hamna shaka ndani yake. Ndio mwongozo kwa wamchao Mungu (2:2-3). Ndiyo kusema kwamba Kurani yatoa njia ya pekee ya kupata wema. Nawaambieni hayo nikielekezwa na Mungu. Imesimuliwa katika Hadithi ya kwamba Mtume Mtukufu s.a.w. alikuwa anatumia njia mbali mbali za kupata ulinzi wa Mungu, lakini baada ya sura mbili za mwisho za Kurani Tukufu kuteremka akaacha kila kitu na akafungamana na hizo tu.

Ushahidi wa tatu ni: Sema: Hakika nayafuata yaliyofunuliwa kwangu kutoka kwa Mola wangu. Hizi ni dalili zitokazo kwa Mola wenu na ni mwongozo na rehema kwa watu wanaoamini. Na Kurani isomwapo, basi isikilizeni na nayamazeni ili mpate kurehemiwa (7:204-205).

Tarehe 10 Februari 1911, Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. aliwaambia wale aliokuwa nao maneno yafuatayo:

"Ni kubwa sana rehema ya Mungu iliyo juu yangu. Ameonyesha nguvu Yake na himaya Yake kwa mtumishi Wake mnyenyekevu kwa njia za ajabu katika siku za maradhi yangu. Nimepata uhakikisho upya kuhusu maombi kupokelewa. Maombi ndiyo njia kubwa sana kwangu kupata

hisani Yake. Mola wangu Amenijaalia hisani zake kubwa. Laiti ningekuwa na uwezo wa kuwaambieni kirefu. Leo tu nilifunuliwa: 'Nijaalie kwa fadhili yako nisimhitaji yeyote minghairi yako.' Nilikuwa na shida ya kutopata usingizi. Madaktari wakaninywesha dawa, lakini bure. Usiku uliopita sikutumia dawa, nikalala masaa matano. Mungu Yu Mfalme Mwenye nguvu; Hufanya Apendavyo. Kumbukeni nasaha hii yangu. Muwe na imani katika Mungu, na mtarajie kujipatia fadhili yake. Msivunjike moyo kwa sababu ya kuzikabili shida; hizo zinaletwa kuwanyanyueni. Mwombeni Mungu msaada. Jambo hilo ni dogo tena rahisi lakini ni la muhimu sana. Lizingatieni, msiliachilie mbali. Mungu Awe pamoja nanyi, Awalindeni na kuwahifadhi. Amin."

Mtu fulani alimwuliza Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. tarehe 27 Februari 1911, ya kwamba hitilafu za kiitikadi baina ya Waahmadiyya na wasiokuwa Waahmadiyya ni katika mambo makubwa ya kimsingi au katika maelezo? Akajibu kwamba si sawa kusema kwamba hitilafu hizo zinahusu mambo ya maelezo. Sala yetu ni kama sala yao, pia hamna hitilafu kuhusu zaka, haji na saumu. Naona tuwahitilafiana kuhusu jambo la msingi. Twaweza kueleza habari hiyo kwa njia hii. Imani huhitaji kumwamini Mungu, Malaika Zake, Vitabu Vyake, Mitume Wake, Kadri Yake njema na mbaya na Ufufuo. Wapinzani wetu pia wanatangaza kuamini hivyo vyote, lakini hapo ndipo hitilafu ianzapo. Mtu hawezi kuwa mwaminio isipokuwa awe anawaamini Mitume wote wa Mungu pasipo kutofautisha baina yao kwa sababu ya zama zao au mahali pao. Kumkataa Mtume yeyote wa Mungu kwamfanya mtu kafiri. Wapinzani wetu wanakataa madai ya Hadhrat Mirza Sahib a.s. kuwa ametumwa na Mungu. Hili halihusiani na habari ya maelezo. Kurani Tukufu yausia: 'Hatutofautishi baina ya mmoja wa Mitume Wake' (2:286). Kumkataa Masihi Aliyeahidiwa

kwamaanisha kutofautisha. Twamwamini Mtume Mtukufu s.a.w. kuwa *Khatamun Nabiyyin* kama alivyoitwa ndani ya kurani Tukufu (33:41). Twaamini ya kuwa asiyemkubali kuwa *Khatamun Nabiyyin* ni kafiri. Twahitilafiana na wapinzani wetu kuhusu maelezo ya neno hili; lakini hitilafu hii haihusikani na: Hatutofautishi baina ya mmoja wa Mitume wake. Hivyo, naona kwamba kuna hitilafu ya kimsingi baina ya wasiokuwa Waahmadiyya na sisi.

Siku hiyo akamwandikia Nawab Fateh Ali Khan wa Lahore akiahidi kutoa rupia elfu moja katika mfuko wa Chuo Kikuu cha Waislamu, na akatoa maagizo yafuatayo kwa wanajumuiya wa Kiahmadiyya:

> "Upo mpango wa kuanzisha Chuo Kikuu cha Waislamu katika India, na baadhi ya marafiki zetu wameuliza kwamba je, wanaweza kukichangia. Ili kuwajulisha wanajumuiya inatangazwa kwamba ingawaje Jumuiya yetu ina mahitaji maalum na wanajumuiya wanapaswa kuyachangia vya kutosha, hata hivyo, kwa kuwa mpango wa Chuo Kikuu cha Waislamu unafaa, hivyo nafikiri yawalazimu marafiki zetu kukichangia kwa kila njia ili kukisaidia."

Mwanzoni mwa Aprili 1911, gazeti moja la Waislamu la Lahore lilipendekeza kwamba siku ya kuzaliwa Mtume Mtukufu s.a.w. iwe inasherehekewa kama sikukuu, na tawi letu la Simla likamwomba Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. mwongozo kuhusu pendekezo hilo. Akajibu:

> "Mtume Mtukufu s.a.w. aliweka sikukuu mbili tu kwa Waislamu, na siku ya Ijumaa pia kama Idi. Sikukuu yoyote nyingine itakuwa bidaa isiyotakikana. Kwa njia hiyo watu wataendelea kuongeza sikukuu nyinginezo. Waahmadiyya pengine watapenda kusherehekea kila mwaka siku alipopokea

> Masihi Aliyeahidiwa a.s. ufunuo wake wa kwanza na pia siku ya kufariki kwake. Masahaba wa Mtume Mtukufu s.a.w. walikuwa wamejitolea sana kwake, lakini katu hawakusherehekea sikukuu ya tatu. Masihi aliyeahidiwa a.s. alikuwa anampenda sana Mtume Mtukufu s.a.w., kama sikukuu kama hiyo ingeliruhusiwa angelisherehekea. Mapendekezo kama hayo ni ya kijinga, wanaoyaleta hutafuta kupendwa na watu; hawaongozwi na sababu ya kiroho."

Hadhrat Khalifatul Masih r.a. alisalisha sala ya kwanza ya Ijumaa baada ya kupata ajali, baada ya kitambo cha miezi sita. Huo ulikuwa wakati wa furaha kubwa katika Jumuiya nzima. Tangu hapo akaendelea kwa muda mrefu sana kuhudhuria sala ya Ijumaa msikitini, lakini sala zote pamwe na sala za Ijumaa ziliendelea kusalishwa na Sahibzada Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad r.a. Wakati fulani Maulawii Muhammad Ali alimshauri Hafidh Raoshan Ali r.a. kwamba amwulize Hadhrat Khalifatul Masihi kwa nini yeye anamwagiza kijana Sahibzada kuongoza katika sala ilhali wapo masheikh walio wazee na wataalamu zaidi. Hafidh Raoshan Ali r.a. aliuliza hilo bila kueleza nani alimwambia kuuliza hivyo, naye akajibiwa:

> "Kurani Tukufu yasema: Hakika aheshimiwaye sana miongoni mwenu mbele ya Mungu ni yule amchaye zaidi katika nyinyi" (49:14). Mtaje hata mmoja miongoni mwa Jumuiya nzima aliye mcha-Mungu zaidi kuliko Mian Mahmud Ahmad. Ndipo nitamfanya Maulawii Muhammad Ali awe anaongoza katika sala na kutoa hotuba."

Serikali ya Kiingereza ilitangaza kwamba Baraza la kumvika Mfalme taji litafanywa mjini Delhi tarehe 12 Desemba 1911, kwa kutangaza kutawazwa kwa Mtukufu Geroge V Mfalme wa India. Hadhrat

Khalifatul Masihi r.a. akaona itakuwa nafasi nzuri ya kumwomba Mfalme Mtawala, kwa kumpitia Mheshimiwa Gavana Jenerali wa India, kwamba Waislamu walio wafanyakazi wa Serikali wapatiwe ruhusa ya masaa mawili kila siku ya Ijumaa ili kuwawezesha kushiriki katika sala ya Ijumaa. Kwa shabaha hii akaandika hati ya maombi kuhusu hayo akatangaza tarehe 1 Julai 1911:

> "Ijumaa huhesabiwa katika Islam kuwa ni siku iliyobarikiwa sana, na Waislamu wanaiheshimu kama sikukuu. Kuhudhuria katika sala ya Ijumaa ni jambo la lazima na inasisitizwa sana kuliko kuhudhuria katika sala za idi mbili, ilivyosemwa na Kurani Tukufu: Enyi mlioamini, inaponadiwa kwa ajili ya sala siku ya Ijumaa, basi nendeni upesi kumkumbuka Mwenyezi Mungu na acheni biashara (62:10). Ndiyo sababu tangu mwanzo wa Islam, siku ya Ijumaa ni ya ruhusa katika nchi zote za Kiislamu. Katika India pia Ijumaa iliendelea kuwa siku ya ruhusa kwa karne nyingi. Aya iliyotajwa sasa hivi haimruhusu mtu kusali sala ya Ijumaa peke yake; yamlazimu kuhudhuria msikitini, kusikiliza hotuba na kisha kusali nyuma ya Imam pamoja na waaminio wengine.
>
> Jumapili ni siku ya ruhusa sawa na dini ya Mfalme, na shughuli za serikali hazina nafasi ya kutoa ruhusa mbili katika wiki. Kwa hiyo imebidi kutoa shauri itakayotimiza matakwa ya Waislamu pasipo kuzusha matatizo kwa kuendesha mambo ya serikali. Njia moja rahisi itakuwa kufunga ofisi, mahakama na shule zote na vyuo vyote kwa masaa mawili wakati wa sala ya Ijumaa, au kuwaruhusu wafanyakazi na wanafunzi walio Waislamu, kwa muda huo ili waweze kushiriki katika ibada ya Ijumaa. Idara na ofisi zote zaweza kupelekewa barua kuhusu habari hii.

> Tumetayarisha hati ya maombi kwa shabaha hii ili kumpelekea Gavana-Jenerali. Lakini kwa kuwa habari hii inawahusu Waislamu wote kwa jumla, hivyo kabla ya kupeleka hati hii, inabidi Waislamu wote, magazeti na vyama viarifiwe ili viiunge mikono kwa njia ya maazimio, matangazo, makala na kadhalika, na serikali ikipata uhakikisho wa haja hii ya Waislamu, iweze kutoa nafasi hiyo. Tunahusika na habari hii kwa njia hii tu ya kwamba kwa kuwa hiyo ni haja ya Waislamu wote, basi ombi lipelekwe ili liungwe mkono na Waislamu wote. Sio utashi wetu kwamba ombi lepelekwe na sisi tu pekee. Jinsi Mungu Alivyotuongoza ndivyo tuliyopendekeza shauri hii. Kama chama chochote cha Waislamu kikikataa pendekezo letu hili kwa sababu tu tumelitoa sisi, hatutalipeleka bali njia nyingine yoyote inayofaa itumiwe kulipeleka hilo serikalini."

Kutoka Aligarh ikashauriwa ya kwamba kumbukumbu iliyopendekezwa itumwe serikalini kwa niaba ya chama cha All India Muslim League. Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akatoa kibali chake. Matokeo ya kumbukumbu yakawa kwamba serikali ikawapa Waislamu nafasi iliyoombwa.

# XVI

## MAWAIDHA YA MWISHO

Mkutano wa Mwaka wa 1911 ulifanyika tarehe 26-29 Desemba. Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. aliuhutubia Mkutano kwa masaa mawili na nusu jioni ya Disemba 27. Matini yake ndiyo hii:

> “Enyi mlioamini, Mcheni Mwenyezi Mungu ipasavyo kumcha; wala msife isipokuwa mmekwisha kuwa watiifu. Na shikeni kamba ya Mwenyezi Mungu nyote, wala msiachane; na kumbukeni neema ya Mwenyezi Mungu iliyo juu yenu mlipokuwa maadui naye Akaziunganisha nyoyo zenu, hivyo kwa neema Yake mkawa ndugu; na mlikuwa ukingoni mwa shimo la moto naye Akawaokoeni nalo. Hivyo ndivyo Mwenyezi Mungu Anavyokubainishieni aya Zake ili mpate kuongoka. Na liwepo miongoni mwenu kundi linaloita kwenye heri na kuamuru kutenda mema na kukataza maovu, na hao ndio watakaostawi. Wala msiwe kama wale waliofarikiana na kuhitilafiana baada ya kufikia dalili zilizo wazi; na hao ndio watakaokuwa na adhabu kubwa (3:103-106).”

Katika hotuba yake alisisitiza baadhi ya mambo ambayo kwa kirefu ni haya:

> ‘’Mna wajibu gani kumhusu Mungu? Ni kwamba mshike vizuri itikadi za kweli, vitendo vyenu viafikiane nazo, na muwe wacha-Mungu. Ucha-Mungu unamhifadhi mtu katika shida na kumpatia raha. Mcha Mungu huondolewa hali zote za kulemewa. Anapendwa na Mungu na anaruzukiwa namna asivyotambua. Maombi yake hupokelewa na anajaaliwa ushindi juu ya maadui zake wanaoangamia. Milango ya elimu

ya haki hufunguliwa kwa mcha-Mungu. Kwa hiyo, nasaha yangu ya kwanza ni: Muwe wacha Mungu, muwe wacha Mungu, muwe wacha Mungu kwa ajili ya Mungu. Muwe watii kwa Mungu sawasawa, mwisho wenu uwe katika hali ya kuwa watii kwa Mungu. Ibrahimu a.s., Mzee mtukufu, alihesabiwa kustahiki kupata baraka zote kwa sababu ya utii wa aina hiyo, kama ilivyosemwa: 'Mola wake Alipomwambia: Uwe mtiifu, akanena: Nimekwisha kuwa mtii kwa Mola wa walimwengu' (2:132). Kwa hiyo, kama nyinyi nanyi mwataka kujaaliwa baraka za kimbinguni, muwe wacha-Mungu. Ucha Mungu wa kweli huchipua katika Mwislamu wa kweli; kwa hiyo, kuweni Waislamu, na kifo kiwakuteni Waislamu.

Tena jumuikeni pamoja, na kwa nguvu ya pamoja shikeni kwa imara kamba ya Mungu, wala msifarakane. Nawasomeeni ile aya mara nyingine: 'Shikeni kamba ya Mwenyezi Mungu nyote, wala msiachane.' Basi shikamaneni na kamba ya Mungu nyote pamoja, wala msiiache kabisa. Katika Islam kamba ya Mungu ni Kurani Tukufu. Ma-Aria, Ma-Barahman, Ma-Sanatan, Wakristo, wasiomwamini Mungu na wapagani, wote hao wanaendelea kuivuta kamba hii upande wao kwa nguvu zao zote na wanataka kuivutia kwao kutia nguvu upande wao. Upande mwingine mwadai kuishika kwa nguvu hii kamba ya Mungu. Msiyaache madai hayo bila kuhakikisha ukweli wake. Tumieni nguvu zenu zote kwa pamoja kwa imara na ishikeni kwa nguvu, isije wapinzani wa Islam wakakawashindeni katika kuvutana huku. Kuishika kwa imara inamaanisha kwamba muifanye Kurani Tukufu kuwa kanuni yenu na mwongozi wenu. Shughuli zote za maisha yenu ziwe sawa na mafunzo yake. Mambo yenu yote, kila mwendo wenu na kimya chenu

kirekebishwe na Kitabu hiki Kitakatifu cha Mungu ambacho ni ponyo na mwanga. Nawafikishieni mara nyingine agizo la Mungu, lisikieni, na tegeni masikio barabara. Shikeni nyote kamba ya Mungu, wala msifarakane. Je, mwajua mkifarakana matokeo yatakuwa nini? Kamba itaponyoka mikononi mwenu, nanyi mtaondokewa nguvu yote, kama Mungu Mtukufu Alivyosema: 'Msigombane, msije mkatenguka mioyo na kupoteza nguvu zenu' (8:47). Mtavunjika na nguvu zenu zitatapanyika na maadui zenu watawashindeni.

Sikilizeni! Mimi ni Khalifatul Masihi, na Mungu Amenifanya *Khalifa*. Nilikuwa sitamani niwe *Khalifa*, lakini sasa kwa kuwa Mungu Amenivika joho hili, sipendi kabisa mafarakano. Sipendi asilani mwingiwe na mafarakano. Napenda kuodolea mbali sababu zote zile za mafarakano. Hamwezi kutambua jinsi wazo lenyewe la mafarakano linisumbuavyo mimi. Hamjui kipeo cha maumivu hayo; hamwezi kuyawaza. Napenda, na hii yategemea fadhili ya Mungu, ya kwamba nisisikie habari ya mafarakano yoyote kati yenu wala utengano, na kwamba niweze kushuhudia kwa macho yangu kwamba nyinyi ni mfano kwa kitendo wa agizo hili la Mungu: Shikeni kamba ya Mungu nyote, wala msitengane.

Nakariri, yule aliyekuwepo na asikilize na kuwafikishia wengine, epukaneni na ugomvi. Baada ya kufa kwangu mtakuwa na nafasi kubwa ya kugombana. Pengine mwafikiri nimekuwa *Khalifa* kwa urahisi kama Abu Bakr r.a. Hamtambui uhakika ulivyo, wala hamwezi kuelewa uzito wa wajibu niliobebeshwa, na mashaka yaliyosababishwa nao. Ni fadhili hasa ya Mungu kwamba nimewezeshwa kubeba mzigo huu mzito. Hakuna yeyote kati yenu anayeweza kuukisia barabara

licha ya kuubeba. Je, anayepaswa kuwasimamia malaki ya watu aweza kulala usingizi kwa raha?

Nikisimama msikitini humu, Kurani mkononi, ninaapa ya kwamba sikutamani hata kidogo wakati wowote niwe mwalimu wa kiroho. Lakini hakuna ajuaye mpango wa Mungu. Amefanya Alivyopenda. Amewaunganisha nyote kwa mikono yangu, na Yeye Mwenyewe, si mmoja wenu, Akanivika joho la *Ukhalifa*. Ni faradhi yangu kulitukuza na kuliheshimu. Sitaki kwenu fedha au chochote kiwacho. Sijali mmoja wenu ananisalimia au hapana. Mpaka Aprili iliyopita nilikuwa nampelekea Maulawii Muhammad Ali michango yote mliyokuwa mnaniletea, lakini mtu fulani akamwongoza vibaya naye akasema fedha hizo ni mali ya *Anjuman*, naye akiwa katibu wa *Anjuman* ndiye mwangalizi wake. Ndipo nikaacha kumpelekea fedha hizo kwa kuthamini radhi ya Mungu, ili nione watafanya nini kuhusu habari hii. Wale wanaofikiri hivyo wamo katika kosa nao wamefanya hatia ya utovu wa adabu. Wapaswa kutubu; nakariri kwamba wapaswa kutubu. Wasipotubu watakuwa katika hali mbaya.

Sasa naweka kando fedha mnazoleta kwangu mimi binafsi na kuzigawanya ili kupata radhi ya Mungu. Siwategemei kwa mahitaji yangu wala kwa mahitaji ya familia yangu. Mungu Hakunifanya katu nimtegemee yeyote yule; Yeye Anipatia vya kutosha sana kutoka katika hazina Zake zilizofichikana. Isitoshe, bado nina uwezo wa kufanya kazi ya utabibu Aliyonijaalia Yeye. Zingatieni, nami narudia, sihitaji fedha zenu, wala siwaambieni mnipe. Mkiniletea chochote nakitumia katika njia ya radhi ya Mungu, jinsi nifikirivyo. Kitu gani, basi, kingeweza kuchochea utashi nafsini mwangu kwamba

niwe mwalimu wa kiroho? Mungu Ametenda Alivyopenda; nyinyi wala yeyote mwingine hawezi kufanya chochote kuhusu jambo hili. Kwa hiyo jifunzeni kuheshimu mpango wa Mungu; ndiyo njia ya kujinyakulia baraka za Mungu. Hii pia ndiyo kamba ya Mungu iliyofungia pamoja mambo yenu yaliyokuwa yametawanyika. Ishikeni kwa imara.

Zingatieni vizuri kwamba nyinyi hamna madaraka ya kumwondoa *Khalifa*. Kama mkiona ndani yangu jambo fulani mnalofikiria ni kosa, niambieni kwa adabu. Ni Mungu Anayeweka *Khalifa*; hiyo siyo kazi ya binadamu. Mungu Alimfanya Adamu kuwa *Khalifa*, na pia Daudi. Tena Anaweka *Makhalifa* sawa na aya 24:56; nyinyi nanyi Akawafanyeni pia *Makhalifa*. Kama nimefanywa *Khalifa*, ndiyo kazi ya Mungu sawa na hekima yake na kwa faida yenu. Hakuna yeyote awezaye kumwondoa *Khalifa* aliyewekwa na Mungu. Hivyo yeyote kati yenu hana madaraka kuniondoa mimi. Kama Mungu Akitaka kuniondoa, Atanifisha. Afadhali mliache jambo hili mkononi mwa Mungu; nyiye hamna uwezo wa kuniondoa. Sidaiwi na yeyote kati yenu. Anaongopa yule asemaye amenifanya *Khalifa*. Naudhika nikisikia kauli hii kwamba hizi ni zama za Sheria na Bunge; Iran na Ureno na Uturuki zote zimeunda Mabunge. Nasisitiza kwamba yule anayeifikiria Jumuiya hii kuwa kama Bunge atubie kosa lake. Ni raha gani mnayofikiria ambayo Iran na nchi nyinginezo zimeletewa na Bunge? Wengi waliangamizwa chini ya enzi ya Muhammad Ali Shah, na wamfuatao nyuma wanaonywa-onywa. Je, Waturuki walilala kwa amani baada ya kuunda Bunge?

Nawakumbusheni mara nyingine kwamba ndani ya

Kurani Tukufu imefafanuliwa bayana ya kuwa Mungu ndiye Anayeweka *Makhalifa*. Alipomweka Adamu a.s., Akasema: Hakika Mimi Nitamweka *Khalifa* katika ardhi (2:31). Malaika wakaleta ukinzani, lakini huo ukawafaa nini? Someni Kurani mjue. Kama hiyo ilikuwa hali ya malaika na wakalazimika kuungama: Utakatifu ni wako! Hatuna elimu isipokuwa Uliyotufundisha (2:33); basi nyiye m nani kunikinza? Afadhali mjiangalie ndani ya vioo vyenu. Nakumbuka vizuri kauli ya mtu fulani: Bunge limeundwa katika Irani; hizi ni zama za kuunda kanuni. Mawazo kama hayo ni uasi na utovu wa heshima. Wanaofikiria hivyo walikwisha onyeshwa matokeo yake na ghera Ya Mungu katika Iran yenyewe. Narudia, wanapaswa kutubu hata sasa.

Naletewa fedha na nguo kwa ajili ya mayatima na mafukara. Fedha kama hizo namkabidhi Maulawii Muhammad Ali sawa na agizo: Wala msikaribie mali ya yatima (6:153). Pamoja na nguo wakati mwingine vitu vyenye thamani kubwa vinapokelewa. Nikamwambia mke wangu kuuza vitu hivyo na kutoka katika fedha hizo kutengeneza mavazi ya kawaida ili watu wengi zaidi wanaostahili wapate kusaidiwa. Mke wangu akauliza kwamba, je, anaweza kujinunulia baadhi ya vitu katika hivyo. Nikamwambia katu hapana, lakini wanawake wasio jamaa zetu wanaweza kuvinunua. Mara kwa mara watu wenye hali ndogo wanaoa, na mabibi arusi hupatiwa nguo na mapambo. Kisha kuna fedha ambazo naombwa zitumiwe sawa na maagizo yangu, ama kwa namna ambavyo marehemu fulani apatiwe thawabu yake. Fedha nyingine zinapokelewa kwa sadaka ya kawaida. Fedha nyingine zinatumwa kwa ajili yangu binafsi, nami najua hiyo hufanywa na mpango maalum wa Mungu.

> Sikueleza hayo yote kujitetea. Mungu Anajua sana kwamba sithamini kibali chenu au kutokubali kwenu au kunichukia. Nimewaambieni isije mkafanya dhambi ya kudhania vibaya. Mimi sihitaji fedha zenu. Hata katika zama za uhai wa Masihi Aliyeahidiwa nilikuwa naletewa fedha kama hizi nami nikakubali. Nawaambia hayo, kwani nawatakia heri. Sina hofu hata kidogo ya yeyote kati yenu; namhofia Mungu pekee. Msifikirie vibaya. Kama nimo kosani, niacheni kosani. Katika umri huu kama sijajifunza kutoka katika Kurani Tukufu, mtanifundishaje? Hali yangu ni kwamba nikiendelea kuketi miguu yangu yaniuma; nasimama kuwahutubia, kwani Mtume Mtukufu alitoa hotuba akisimama. Basi nisikilizeni kwa ajili ya Mungu, kwani nawafikishieni agizo Lake: Ishikeni nyote pamoja kamba ya Mungu, wala msifarakane.

Akiongea na mgonjwa mmoja, tarehe 11 Juni 1912, Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. alinena:

> "Katika kila kazi utaratibu huweza kuwekwa, isipokuwa katika kazi ya utabibu. Mjenzi anaweza kuchukua jukumu la kumaliza ujenzi wa jengo katika muda maalum; karani anaweza kuahidi kutayarisha taarifa katika siku kadha, mshonaji aweza kusema atatoa suti siku fulani; lakini tabibu hawezi kusema atamponya mgonjwa katika muda fulani, ingawaje baadhi ya matabibu wajinga wakati mwingine wanadai hivyo. Tabibu hodari hadiriki kutoa madai kama hayo. Mimi wakati mwingine napata dawa kutoka China, lakini ni mwangalifu sana hata kwamba hadi sasa sijaijaribu dawa yoyote katika hizo zilizo nyingi nilizopata kwa bidii kubwa na kwa bei ghali, kwa mgonjwa yeyote, kwani tabibu yeyote hajaniambia matokeo ya majaribio yake mwenyewe ya hizo wala njia ya

> kuzitumia. Siandiki mimea au dawa ambazo hazipatikani kwa urahisi."

Sheikh Rahmatullah r.a. wa Lahore aliahidiwa na Masihi Aliyeahidiwa a.s. kwamba yeye ataweka msingi wa jengo lake alilonuia kulijenga mjini Lahore, lakini Masihi Aliyeahidiwa a.s. akafariki mapema. Mnamo juni 1912, Sheikh Rahmatullah r.a. akamwomba Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. kutimiza ahadi ya Masihi Aliyeahidiwa a.s., naye akakubali mara moja. Akaenda Lahore tarehe 15 Juni na jioni hiyo akaweka msingi baada ya kutoa hotuba fupi ambamo alisema:

> "Mpendwa wangu na mfadhili wangu alimwahidi Sheikh Sahib kwamba ataweka msingi wa jengo lake kwa mkono wake mwenyewe, lakini mpango wa Mungu ulikuwa ya kwamba ahadi hiyo itimizwe na mtumishi wake mmoja. Bwana Sheikh akaniandikia nifike kwa shughuli hii. Sina afya nzuri, naumwa sehemu kadha za mwili, lakini nina shauku ya kutimiza ahadi ya bwana wangu mpendwa.
>
> Majengo mengi yamejengwa na yanajengwa pembeni mwa kiwanja hiki, lakini sisi twalipenda hili jengo litakalojengwa kwa sababu ya kibinafsi na ya Kijumuiya. Upendo wa kibinafsi ni kwamba marehemu Hadhrat Mirza Sahib a.s. aliahidi kuweka msingi wake, na kwamba ahadi hii itatimizwa na mtumishi wake. Upendo wa Kijumuiya ni kwamba Jumuiya yetu pia ina sehemu yake katika jengo hili. Wanajumuiya wapaswa kuomba kwa bidii kwamba matokeo yake yawe mema na wakazi wa jengo hili na waliosimamia wawe wema na wapende mema.
>
> Nimesema ya kwamba Jumuiya nzima inahusiana na jengo hili: Natumai nyinyi nyote mtaomba kwa bidii kwamba Mungu Alibariki na kwamba wazao wa Bwana Sheikh anayetupenda

> nao watupende kama apendavyo yeye. Sasa nitaliweka tofali moja la msingi kwa maombi, na kisha Sahibzada Mirza Mahmud Ahmad, Bashir Ahmad, Sharif Ahmad na Nawab Muhammad Ali Khan, kila mmoja wao aweke tofali moja moja kwa maombi."

Tangu safari yake ya kwenda kutembelea Lahore hapo kabla, msikiti ulikwisha jengwa tayari katika "Ahmadiyya Buildings." Hivyo tarehe 15 Juni alipowasili tu Lahore akaelekea msikitini, akasali rakaa mbili na akaomba kwa bidii sana kwa wale waliochukua jukumu la kuujenga msikiti na kwa wazao wao. Kesho yake akauhutubia mkusanyiko mkubwa wa wanajumuiya. Katika hotuba yake alisema:

> "Mungu Mtukufu amewakusanyeni baada ya Mtume Mtukufu s.a.w. kwa njia ya mfalme wetu, Masihi Aliyeahidiwa a.s., na baada ya kufariki kwake Akawahifadhini kwa mikono yangu msifarakane. Thaminini ukarimu huu wa Mungu ipasavyo, wala msijiingize katika mabishano na dhana mbaya. Siwezi kuwaza faida ipi ya kikhulka au ya kiroho mnapata kutokana na mabishano hayo. Mungu Mwenyezi Amemfanya *Khalifa* yule Aliyempenda na Akawafanyeni kumtii yeye. Ni ujinga wao tu wanaolaumu kazi ya Mungu. Nimewaambieni mara kwa mara na kuwaonyesheni kutoka katika Kurani Tukufu ya kwamba si kazi ya binadamu kumfanya mtu yeyote kuwa *Khalifa*. Ni Mungu tu Anayefanya *Makhalifa*. Nani alimfanya Adamu kuwa *Khalifa*? Mungu Akasema: Mimi Nitamweka *Khalifa* katika ardhi (2:31). Malaika wakapinga: Ataleta uharibifu ardhini na kumwaga damu. Lakini ukinzani huu ukawafaa nini? Mwaweza kusoma ndani ya Kurani Tukufu kwamba mwishowe wakalazimika kutii. Kama mmoja wenu ananitoa kosa, na hata kama yu malaika, nitamwambia: Yafaa uutii *Ukhalifa* wa Adam. Na akikataa kwa kiburi na kushika

kazi ya *Iblisi*, hapo akumbuke kumpinga Adamu kulimfaa nini *Iblisi*. Nakariri ya kwamba mtu hata kama ana tabia ya kimalaika akipinga *Ukhalifa* wangu, tabia yake njema itamwongoza kumtii Adam; lakini kama yu *Iblisi*, ataiondoka jamii hii tukufu.

Daudi a.s. alikuwa *Khalifa* mwingine, kama ilivyonenwa: Ewe Daudi, hakika Tumekujaalia kuwa *Khalifa* ardhini (38:27). Yeye naye alifanywa *Khalifa* na Mungu. Wapinzani wake walikuwa wachochezi wa fitina dhidi ya utawala wake, ambao baadhi yao walipata kuingia katika ngome yake; lakini nani awezaye kufaulu katika kumpinga yule aliyefanywa *Khalifa* na Mungu?

Kisha Mungu Mwenye Enzi Akawafanya Abu Bakr r.a. na Umar r.a. kuwa *Makhalifa*, Mungu Awaridhie wote hao wawili. *Marafidhii* (Washia) hadi sasa wanapiga kelele na kulia kwa nini walipata *Ukhalifa*. Lakini hamwoni kwamba mamilioni ya Waislamu wanawaombea baraka Abu Bakr r.a. na Umar r.a. Wallahi mimi nami nimefanywa *Khalifa* na Mungu. Msikiti huu umenipendeza moyo wangu. Nimewaombea kwa bidii wale wote ambao waliuchangia ujenzi wake kwa njia yoyote, nami nina yakini kwamba maombi yangu yamefikia Arshi. Nikiisha wasili mjini humu na nikisimama katika msikiti huu ulionipendeza, natangaza kwamba jinsi Mungu Alivyowafanya Adamu, Daudi, Abu Bakr na Umar kuwa *Makhalifa*, ndivyo Alivyonifanya mimi kuwa *Khalifa*.

Kama mtu akisema *Anjuman* imenifanya *Khalifa*, ataongopa. Fikira kama hizi zaleta maangamio; jihadharini nazo. Sikilizeni sana mara nyingine, hakuna mtu wala *Anjuman* iliyonifanya *Khalifa*; sioni *Anjuman* yoyote ina uwezo wa

kumfanya mtu yeyote kuwa *Khalifa*. Hakuna *Anjuman* yoyote iliyonifanya *Khalifa*, wala sithamini kabisa *Anjuman* kufanya hivyo. Sijali katu *Anjuman* yoyote kutengana nami. Hamna mtu awezaye kuninyang'anya joho hili.

Katika fikara yao, nani alistahili kuwa *Khalifa*? Kuna Mahmud nimpendaye ambaye ndiye mwanaye mpenzi wangu na mfadhili wangu. Tena kuna Nawab Muhammad Ali Khan r.a. aliyemwoa bintiye, na mkwewe Mir Nasir Nawab r.a., na mkewe Ummul Muminina r.a. Hao tu ndio pekee wanaoweza kufikiriwa kwamba wanadai *Ukhalifa*. Ni la ajabu ya kwamba wale wanaodhani kuwa haki ya hao imenyang'anywa hawazingatii kwamba hao wote ni watii waaminifu kwangu. Hawakupeleka madai yao mbele ya wakinzani. Warithi wa Hadhrat Mirza Sahib a.s. na jamaa zake wa karibu, wote hao ni waaminifu kwangu. Nawaambieni kweli kwamba kati yenu hakuna hata mmoja anitiiye kama watiivyo wapenzi wangu Mahmud, Bashir, na Sharif, tena Mir Nasir Nawab na Nawab Muhammad Ali Khan. Sisemi hivyo ili kuwafurahisha, bali naieleza kweli ilivyo kwamba wananipenda kwa kutaka wapate radhi ya Mungu. Nimepata kusikia Ummul Muminina akihakikisha mara ma-ishirini kwamba yeye anajifikiria kuwa mtumishi wangu. Mian Mahmud yu mtu mzima; atawaambieni kwamba ananitii kwa uaminifu. Mkinzani aweza kusema kwamba huyo si mwaminifu kwangu katika kunitii; lakini nina hakika kabisa kwamba yu mtii kwangu kwa uaminifu zaidi sana kuliko yeyote kati yenu. Ahali zake Hadhrat Mirza Sahib a.s., wananitii wote kama vile Ali r.a., Fatima r.a. na Abbas r.a. walivyomtii Abu Bakr r.a., bali zaidi. Kila mmoja wao ni mwaminifu sana hata kwamba siwezi kuwaza ya kuwa yeyote kati yao aweza kunidhania vibaya.

Sikilizeni, abadan sikuwa na uchu wa kuwa *Khalifa*. Nilivyyovaa kabla sijawa mfuasi wa Hadhrat Mirza Sahib a.s., ndivyo ninavyovaa hivi leo. Nimewahi kuishi kati ya waheshimiwa na watawala kwa heshima nami nikavaa hivyo hivyo. Baada ya kuwa mwanafunzi wa Hadhrat Mirza Sahib a.s. sikugeuza mtindo wangu wa maisha. Baada ya yeye kutuacha mkono, Mungu Akafanya Alivyopenda. Hata sikupata kuwaza kwamba nitakuwa *Khalifa*, lakini Mungu kwa hekima Yake Akapenda na kunifanya Imam na *Khalifa* wenu, na wale mnaowafikiria wanastahiki kupata *Ukhalifa* Akawafanya wanitii. Sasa m nani kubisha? Kama hamna budi kutafuta kosa, basi nendeni mkamtafutie Mungu kosa, lakini jihadharini na adhabu kwa kufanya ufidhuli huu na utovu wa adabu. Simsifu yeyote isivyostahili, sipendi hata nisalimiwe na mtu yeyote. Sihitaji sadaka zenu na riziki yenu. Mungu Anilinde nisiwaze hata kuipata. Mungu Mweza Amenijaalia hazina zilizofichikana ambazo hakuna mtu wala kiumbe anayezijua. Mke wangu na watoto wangu hawamtegemei yeyote kati yenu. Mungu Anawapatia. Mwaweza kumpa nini mtu yeyote. Mungu yu Mkwasi; nyinyi ni mafakiri (47:39)

Aliyepo hapa asikilize vizuri na kuwafikishia wasiokuwapo ya kuwa wazo hili kwamba waliostahiki *Ukhalifa* wamenyimwa ni wazo la *Marafidhii* (Mashia), na lazima liepukwe. Mungu Mweza Amemfanya kwa mkono wake *Khalifa* Aliyemwona anastahiki kupata *Ukhaifa*. Ampingaye yu mkosefu na mwasi. Muwe malaika na kujitoa na kutii; msiwe kama *Iblisi*. Kuzusha kwenu swala la *Ukhalifa* ni *Urafidhii* (Ushia). Basi pelekeni malalamiko yenu mbele ya Mungu kwamba mkazi wa Bhera amekuwa *Khalifa*. Tena kuna wengine wasemao: *Khalifa* anafanya nini? Baadhi yao wasema: Yeye

anawasomesha tu vijana. Wengine wanasema: Yu msomi, na saa zote anashughulikia vitabu tu. Mwaweza kunitoa mokosa elfu; kunitoa kwenu makosa kutakuwa kumpinga Mungu Aliyenifanya *Khalifa*. Hao watafuta makosa ni kama *Marafidhii* (Mashia) wanaoendelea kuwatafutia makosa Abu Bakr r.a. Umar r.a.

Swala jingine mnalohitilafiana juu yake ni: Tuwafikirije wapinzani wetu? Sikilizeni sasa vyema. Neno la Mungu limekwisha fafanua kawaida kuhusu kumkubali Nabii na kumkataa. Wakati wowote nabii adhihiripo kunakuwa hakuna mushkili katika kupambanua wanaomwamini na wamkataao. Achilia mbali elimu ya kupambanua mema na mabaya, Mwenyezi Mungu Amekwisha weka kanuni kuhusu kutoamini, kuamini na kufanya ushirikina. Manabii wamepita zamani. Kila mara walipatikana walioamini na waliokataa. Je, mna shaka kuhusu habari hii; na je, mliona mushkili muwapange katika kundi gani wale wasiowaamini hao manabii?

Mwaambiwa kanuni za imani na ukosefu wa imani. Hadhrat Mirza Sahib a.s. alikuwa Mjumbe wa Mungu. Kama asingelijiita Nabii, angelifanya kosa la kuikataa Hadithi ya Mtume s.a.w. iliyomo katika kitabu cha *Muslim* ambamo ameitwa yule ajaye kuwa Nabii. Swala la kumwamini au kumkataa lipo wazi. Kama yule amkanaye ajiita Mwislamu, yeye mtu huyo yupo karibu nanyi jinsi Wakristo walivyo karibu nanyi kuliko Wayahudi. Kadhalika Waislamu wanaomkataa Hadhrat Mirza Sahib a.s. waweza kuwa karibu nasi kuliko watu wengine. Yule amwaminiye Hadhrat Mirza Sahib r.a. lakini anikataa mimi ni kama *Warafidhii* (Washia) wanowakataa masahaba wa Mtume Mtukufu s.a.w. Jambo liko wazi sana,

lakini wasio na shughuli nyingine wanajishughulisha katika ukinzani usiofaa.

Tena baadhi ya marafiki zangu wanasema kwamba wanajumuiya wa Lahore wanapinga *Ukhalifa*. Nimewahi kutaali Kurani Tukufu na Hadithi kwa waalimu, nami naziamini kwa uaminifu. Moyo wangu umejaa mapenzi ya Kurani na Hadithi. Nimetumia maelfu ya rupia kwa kujinunulia vitabu vya maisha ya Mtume s.a.w. na historia ya Islam. Mtaala wote huo umehakikisha imani yangu ya kwamba hakuna awezaye kuzuia kitu Anachonuia Mungu kukifanya. Nimetaja kwamba Adam a.s. na Daudi a.s. walikuwa *Makhalifa* na nimeeleza Abu Bakr r.a. na Umar r.a. walikuwa *Makahalifa*. Aidha, nimewaambieni kwamba jinsi Abu Bakr r.a. na Umar r.a. walivyo *Makhalifa*, ndivyo Mungu Alivyonifanya kuwa *Khalifa* baada ya Hadhrat Mirza Sahib a.s. Lakini hapa kuna habari zaidi kidogo. Mungu Amesema: Kisha Tukawafanyeni *Makhalifa* ardhini (10:15). Nyinyi nanyi mlifanywa *Makhalifa* katika ardhi, japo huo ni *Ukhalifa* wa aina nyingine. Basi, ni Mungu pekee Anayefanya *Makhalifa* wala hakuna awezaya kumzuia Yeye.

Lahore si kwetu. Kwetu ni Bhera, na sasa ni Qadian. Nawaambieni, mtu yeyote mjni Lahore hakupinga *Ukhalifa* wangu wala hawezi. Msimfikirie vibaya yeyote. Kama mmeamini, mshukuruni Mungu; waila jitahidini kupata uthabiti. Ijapokuwa naugua na kusimama kwangu ni shida, hata hivyo nachukua nafasi hii ili kusisitiza kuwahakikishieni kwamba *Ukhalifa* si jambo hafifu la kuchezea. Hamwezi kunufaika na ubishi huu. Hakuna atakayewafanyeni *Khalifa*, wala yeyote hawezi kuwa *Khalifa* katika uhai wangu.

Nikifa, yule tu atakuwa *Khalifa* ambaye Mungu Mwenyewe Atamfanya. Mmefanya baiati kwangu, msiwaze kujichukulia daraka la *Khalifa*. Mungu Amenifanya *Khalifa* nami siwezi kuondolewa kwa amri yenu, wala hamna yeyote mwenye uwezo wa kuniondoa. Kama mkijidai sana, basi tambueni kwamba ninao Ma-Khalid bin Walid watakaowaadhibuni kama waasi waadhibiwavyo.

Sikilizeni! Maombi yangu hufikia Arshi, na Mola wangu Hutimiza mipango yangu hata kabla sijamwomba. Kunikaidi ni kumkaidi Mungu. Basi komeni na tubuni. Subirini kwa kitambo; kisha yule atakayenifuata atawatendeeni kama Apendavyo Mungu.

Baadhi ya mambo ambayo mnahitilafiana yamekwisha fafanuliwa tayari na Hadhrat Mirza Sahib a.s. Yule aendaye kinyume cha kauli yake si Ahmadiyya. Juu ya mambo asiyoyaeleza maoni yake, nyinyi hamna ruhusa ya kuyafikiria-fikiria pasipo idhini yangu. Basi zuieni kalamu zenu na ndimi zenu kuhusu hayo mpaka *Khalifa* ayataje, ama *Khalifa* wake adhihiri. Msidiriki, basi, kupiga domo juu ya mambo ambayo Imam na Kiongozi wetu amenyamaa kuhusu hayo, la sivyo maandiko yenu yatakuwa bure. Hamwezi kutoa udhuru kwamba mnalazimika kushika kalamu zenu kwani mimi situmii kalamu yangu. Someni vitabu vyangu *Nuruddin*, *Tasdiq Barahine Ahmadiyya, Faslul Khitab*, *Ibtal Uluhiyyate Masihi,* mjue kwamba naelewa sana kuandika. Nimezuiwa na hekima ya Mungu tu; naam, kwa hakika ni Mungu Aliyenizuia.

Nawasihini mara nyingine. Angalieni umri wangu na maradhi yangu. Kisha fikirini kwamba je, mabishano yenu yatawasogezeni karibu na Mungu? Kama hapana, basi tegeni

> masikio kwa ninayowaambieni na kuzeni mapenzi baina yenu. Basi onyesheni adabu nzuri ili niridhike jinsi nilivyopendezwa na kuona msikiti huu katika ziara yangu ya mji huu. Mungu na Ajaalie kwamba nikiondoka nisikie mmekuwa kitu kimoja na mnapendana. Daima yakimbilieni maombi. Mimi nami nitawaombeeni."

Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. mara nyingi alieleza tukio moja lifuatalo lililokuwa mfano maalum wa njia yake ya kuhojiana: "Sheikh mmoja asiyekuwa Ahmadiyya alinialika kwenye chakula cha mchana. Nilipowasili nikakuta amemwalika pia Sheikh mwingine asiyekuwa Ahmadiyya aliyekaa pamoja nami. Akaongea nami kwa upole juu ya mambo ya dini. Alieleza kwamba anaamini Nabii Isa alikufa kifo cha ajali, alimheshimu Hadhrat Mirza Sahib a.s. kuwa mtu mkweli, na alikubaliana naye katika mambo yote, na alikuwa kama mwanafunzi wake, lakini akataka kuniuliza jambo moja dogo. Namfikiriaje yule asiyekubali madai yake? Nikamwambia: Kuna njia rahisi ya kujibu swali hili. Tunaye Musa a.s., na tunaye Muhammad s.a.w., Mjumbe wa Mungu na tena tuna Masihi wa silsila ya Musa a.s. na Masihi wa silsila ya Kiislamu. Unatambua utamfikiria nini anayemkataa Musa a.s., na pia wajua utamfikiria nini anayemkana Muhammad s.a.w, Mjumbe wa Mungu. Sasa, jinsi utakavyomfikiria anayemkataa Masihi wa silsila ya Musa a.s. ndivyo utakavyomfikiria anayemkataa Masihi wa Kiislamu. Aliposikia hayo, mwenyeji wetu akamwita mwanaye na kumwambia: Lete chakula haraka; si jambo rahisi kuhojiana naye."

Mnamo Julai 25, 1912, Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. aliweka jiwe la msigi wa Talimul Islam High School akinena:

> "Nimewahi kusoma mahali fulani ya kwamba kama waaminio arobaini wakiomba pamoja, dua yao hupokelewa na Mungu kwa fadhili yake. Wakati huu tumejumuika hapa zaidi ya

arobaini. Baadhi yetu pengine wamekwisha fanya kosa fulani. Hao wapaswa kutubu na kuomba msamaha. Kisha tutaomba pamoja ya kwamba Mungu Mtukufu Apendezwe kwa kutayarisha katika shule hii watumishi waongofu wa dini na kwamba Awaweke mbali na shule hii wenye moyo mwovu wawezao kuwapotosha wengine; na kama mmoja wao apate kuingia humu, Yeye Amwezeshe kutubu kweli kweli. Shabaha ya shule hii ni kwamba wataalamu watawa na wema watokee katika shule hii."

Kisha wote waliokuwapo wakaungana naye katika maombi ya kimya. Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akaulizwa na Sheikh mmoja asiyekuwa Ahmadiyya: Je, Hadhrat Mirza Sahib alikuwa mtaalamu mkubwa wa elimu ya dini? Kajibu:

"Yeye hakuwa mtaalamu katika maana hii kwamba alijisomea katika Chuo Kikuu cha dini. Baba yake alimwajiri Sheikh mmoja wa kishia wa Batala aitwaye jina Gul Ali Shah kama mwalimu wake alipokuwa kijana. Lakini Mwenyezi Mungu Akamjaalia utaalamu wa hali ya juu hata kwamba masheikh wa India na Uarabu hawakuweza kuleta mfano wa vitabu vyake kwa lugha ya Kiarabu. Aliamini sana katika dua, na Mungu Akimpokelea maombi yake Akamjaalia ujuzi wote uliotakikana."

Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. aliamini ya kwamba hali hiyo ya utaalamu itakuwa ya Mwana Aliyeahidiwa wa Hadhrat Mirza Sahib a.s., Sahibzada Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad ambaye alieleza habari za kujifunza kutoka kwake:

"Nilijifunza Kurani Tukufu kutoka kwa Hadhrat Khalifatul Masihi I r.a. katika muda wa miezi sita. Kwa kuwa koo langu lilikuwa dhaifu, hakuniruhusu kusoma matini yake. Yeye

mwenyewe aliisoma na kuitafsiri, nami nikasikiliza tu. Kisha akatoa maelezo ya baadhi ya sehemu za muhimu kwa midomo na akamaliza katika mwezi mmoja. Nilihudhuria katika darasa lake la Kurani Tukufu lililokuwa kwa watu wote, lakini hayo tu ndiyo aliyonifunza. Kisha akanisomesha kitabu cha Hadithi za Mtume s.a.w. zilizokusanywa na *Bukhari*, katika miezi mitatu. Hafidh Raoshan Ali r.a. akaungana nami katika masomo hayo. Yeye alikuwa mfahamivu na mara nyingi aliuliza maelezo kadha wa kadha. Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akatoa maelezo. Mara moja au mara mbili mimi pia niliuliza swali. Nikajibiwa. Mara ya tatu nilipouliza swali, akasema: Mian, Bwana Hafidh ni Sheikh, anauliza nami najibu. Lakini sitajibu maswali yako. Yote niyajuayo nakueleza; siwezi kukuambia nisiyojua. U mtumishi wa Mungu, na mimi kadhalika. U mfuasi wa Muhamad s.a.w., nami kadhalika. Kuitetea Islam si kazi yangu mimi pekee, ni yako pia. Wapaswa kutafakari na kutafuta majibu. Usiniulize. Hapo baadaye sikumwuliza tena maswali. Nafikiri hilo lilikuwa somo lenye thamani ya juu sana alilonifundisha."

Vipi mtu aweza kuepukana na dhambi, ni swali ambalo jibu lake Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. aliwauliza watu wengi mashuhuri. Jawabu la Maulana Muhammad Qasim Nanautwi lilikuwa:

"Kukikumbuka kifo kwamkinga mtu na dhambi."

Tiba iliyopendekezwa na Shah Abdul Ghafur Mujaddidi ilikuwa:

"Mtu anayemtanguliza Mungu moyoni mwake hulindwa na dhambi."

Masihi Aliyeahidiwa a.s. alisema:

"Kufululiza kuomba kuzuia maelekeo kwenye dhambi

(*Istighfar*) ni kinga kwa kujilinda na dhambi."

Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. alifikiri kwamba kukaa na watu wema na kuomba daima pia ni tiba za kufaa. Kwa ajili yake mwenyewe, safari moja akajaribu nji hii ya kwamba aliweka Kurani Tukufu mahali alipoweza kuiona saa zote, ili aweze kujisihi mwenyewe: 'Unakiamini Kitabu hiki, hata hivyo waelekea kukiasi.' Hiyo ikamzuia hata kwamba wazo hilo likamtoka moyoni mwake. Aliona njia hizo zote zinasaidia. Baadhi yao wanaathirika na njia hii na wengine wanaathirika na nyingine. Jambo kubwa zaidi ni kwamba mtu adumu kutia bidii hadi ufaulu upatikane.

Mkutano wa Mwaka wa 1912 ulifanyika tarehe 25-27 Disemba. Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akiuhutubia Mkutano alinena:

> "Uhusiano wa mtu unapoendelea kusonga mbele, Mungu Anamwagiza Jibrili a.s. kuimarisha uhusiano naye, basi mtu huyo anaanza kujifaidisha kutokana na malaika. Tajiriba kama hizo zinaanza kuwa kwa nadra. Nasema kwa uthabiti si kwa kujikweza, majivuno au kiburi, bali kwa kutoa mfano tu wa fadhili ya Mungu, ya kwamba nimewaona malaika hao, nao wamenisaidia namna ambavyo haiwezi kufahamika. Wakaniambia nizingatie namna wanisaidiavyo."

Akataja mifano ya ufaulu usio wa kawaida waliopata masahaba wa Mtume Mtukufu s.a.w., kwa kueleza manufaa ya kukaa na watu wema, na akakazania kufafanua baraka za utii na kujitupa kwa Mungu. Mzingatie wajibu wenu kumhusu Mungu kwa kila jiha, saa zote maishani mwenu, ili kifo, wakati wowote kikiwafikieni, kiwakuteni katika hali ya utii mkamilifu kwa Mungu. Ishikeni kwa imara, nyote pamoja, kamba ya Mungu wala msifarakane (3:103,104). Akasihi kukuza kupendana, kupatana na kuungana pamoja, na akasisitiza kubeua uadui, ukinzani na mafarakano.

Akamalizia kwa kusema:

> "Watu wa dunia waliponiambia: Tumekufanya mkuu wetu, posho yako kila mwezi iwe kiasi gani? Nikaelekea kwa Mungu na kumwomba: Mola wangu, Hujanifanya abadan nimtegemee yeyote. Je, sasa ninapoelekea mwisho wangu Utanifanya niwategemee viumbe vyako? Yu Mkarimu sana kwangu, Akanipatia kutoka pale nisipoweza kufikiria. Nawaambieni tu: Itangulizeni imani yenu juu ya dunia; epukaneni na pupa, ulaghai na fitina."

Disemba 27 ilikuwa siku ya Ijumaa. Katika hotuba yake ya Ijumaa akasema:

> "Msikiti huu (Masjid Nur) unachukua jina langu, likini ni mdogo. Yafaa upanuliwe, lakini kwa kuzagaza wema. Anzeni shule humu ndani yake kwa kufundisha Kurani Tukufu. Talimul Islam School ina jengo zuri, inapata fedha kutoka serikali na inaangaliwa vizuri; lakini hakuna anayetunza Madrasa Ahmadiyya ambayo haiangaliwi. Niliwaelekeza kwenye hiyo, na kamati moja iliundwa, lakini kwa vitendo hakuna kilichotendeka."

Hafidh Raoshan Ali r.a., mwanafunzi mkuu wa Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. alieleza ya kwamba Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. alikuwa ameandika katika daftari ya ukumbusho baadhi ya faida alizopata kwa sababu ya kukaa Qadian. Mojawapo ilikuwa:

> "Kabla sijahamia Qadian nilitia bidii yote kufaulu kupata kwa uchache rafiki mmoja atakayenipenda kwa ajili ya Mungu tu pekee, nami nikatumia maelfu ya rupia katika utafutaji huo lakini sikufaulu. Nilipofika Qadian, Mwenyezi Mungu Akanijaalia jamii nzima ya marafiki ambao roho yangu

ilikuwa na kiu yao, tena sikutoa hata peni moja.

Faida nyingine niliyopata kwa kukaa na Hadhrat Mirza Sahib a.s. ilikuwa kwamba mapenzi ya dunia yalijifia kabisa moyoni mwangu. Chunguzeni kila jiha ya maisha yangu. Je imo hata chembe ya mapenzi ya dunia ndani yangu? Hiyo yote ni neema ya usahibu mtukufu wa Hadhrat Mirza Sahib a.s. Kuna methali inayojulikana sana: Mapenzi ya dunia ni chanzo cha kila hatia. Nimejipatia manufaa kutoka kwa usahibu wa Hadhrat Mirza Sahib a.s. ambayo ndiyo shabaha ya mafundisho ya Mungu, ni chanzo cha wokovu na yaleta maisha ya kimbinguni katika dunia hii hii."

Dkt. Bhagwan Das Kushta, Mwalimu Mkuu wa shule moja katika Saharanpur, alihudhuria mbele ya Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. tarehe 22 Machi 1913, na akatangaza kukubali Islam. Akamsihi Mwislamu mpya huyo akisema:

"Hakuna apasaye kuabudiwa isipokuwa Mungu pekee Aumbaye na kumjaalia mtu mahitaji yake yote. Hakuna yeyote mwingine anayestahiki kuabudiwa wala kuchukuliwa kuwa Mungu. Kumwabudu yeyote minghairi yake ama kumsujudia ni ushirikina. Pamoja na kuagiza kuamini Umoja wa Mungu, Islam inataka pia kumwamini Muhammad s.a.w. kuwa mtumishi Wake na Mjumbe Wake. Kwani, katika zama zilizopita alipodhihiri duniani wakati wowote mtu mwema, wafuasi wake, baada ya muda fulani, wakamfanya mungu. Hiyo ndiyo ilitendeka kumhusu Ram Chandra a.s. na Krishan a.s. Yesu a.s. pia akafanywa Mungu, akaitwa Mwana wa Mungu, ingawaje alisema: Mbona waniita mwema? Hakuna mwema isipokuwa Mungu. Kwa hiyo, Mtume Mtukufu s.a.w. akaogopa isije yeye naye akafanywa mungu akaongeza katika

shahada: 'Hakuna mwabudiwa ila Mungu,' na kwamba yeye yu mtumishi na Mjumbe wa Mungu.

Jiha ya pili ya Islam ni huruma kwa viumbe wa Mungu. Zaka na Hija hutilia moyoni huruma ya watu, na sala na saumu humfanya mtu kujihurumia, kuna baraka kubwa katika saumu. Hiyo humzoesha mtu kuepukana na matumizi yasiyo halali ya kitu chochote; kwani yule anayejitenga mbali na kile kilicho halali katika saumu, lazima atatengana na kilichoharamishwa na Muhammad s.a.w. kama akimwamini yeye. Basi maana ya kanuni ya imani ndiyo kusisitiza Umoja wa Mungu na kwamba Muhammad s.a.w. ni mtumishi Wake na Mjumbe Wake, na kwamba sala, saumu, Haji na zaka vimewekwa kwa faida ya mtu binafsi na pia kwa jamii nzima. Kuna faida gani kumnyunyuzia mtu maji kama alama ya kukubali imani? Yesu alisema, ni rahisi ngamia kupita ndani ya kitundu cha sindano kuliko tajiri kuingia katika ufalme wa Mungu."

Katika kharifu (msimu baina ya kiangazi na kipupwe) na kipupwe cha mwaka 1912-1913, Sahibzada Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad r.a. alikwenda kutembelea Misri na Hijaz na katika safari hiyo akahiji pia. Akarejea Qadian Februari 3, 1913. Mnamo kiangazi cha mwaka huo akaamua, kwa kupata kibali cha Hadhrat Khalifatul Masihi r.a., kuanzisha kutoa gazeti la kila wiki ambalo Hadhrat Khalifatul Masihi akaliita *Al-Fadhl*. Tolea la kwanza lilitolewa Juni 19, 1913. Baadaye likawa gazeti la kila siku na sasa tangu zaidi ya nusu karne ni gazeti la Jumuiya ya Ahmadiyya.

Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akashikwa na homa kali sana mnamo Juni 25. Keshoye, ijapokuwa alikuwa bado dhaifu, akatoa darasa la Kurani Tukufu, na mwishowe akanena:

"Niuguapo, nachelea kwamba pengine ndio mwisho, safari

hii pia nikafikiri hivyo. Nikasali *Rakaa* mbili. Katika *Rakaa* ya kwanza baada ya sura *Fatiha* nikasoma sura *Dhuha* (93) na katika *Rakaa* ya pili Sura *Inshirah* (94). Kisha nikashughulikia kumsifu Mungu na kuomba ghofira. Ndipo nikaomba dua ambayo nina yakini imepokelewa. Narudia ili nyote mshirikiane katika hii. Nayo ndiyo hii: Hakuna apasaye kuabudiwa isipokuwa Mungu, Mjuzi wa kila kitu, Mpaji. Hamna mwabudiwa minghairi ya Mungu, Mola wa Arshi kuu. Hamna mwabudiwa ila Mungu, Mola wa mbingu na ardhi, Mola wa Arshi Tukufu. Nakuomba njia za kuvutia rehema Yako, na njia imara za kupata msamaha Wako, na hadhi kubwa ya kila wema, na usalama katika kila dhambi. Usiache kosa langu lolote bila kulisamehe, wala ghamu yangu yoyote bila kuiondoa, wala mahitaji yangu yoyote ya kweli bila kuyatimiza, Ewe Uliye Mrehemevu sana. Mola, tumeelemewa sana kutoka kila upande, Islam imeshambuliwa vikali. Waislamu ni walegevu, wana elimu haba ya dini, au ya Kurani Tukufu, au ya mfano wa Mtume Mtukufu s.a.w. Maadui wanasonga mbele. Mola, mwinue mtu mwenye kuvutia, asiye mzembe, shujaa sana, mvumilivu, mwenye kukimbilia daima kuomba dua, mwenye kutimiza matakwa yako, mtaalamu wa ujuzi wa Kurani Tukufu na Hadithi za kweli. Tena Umjaalie Jumuiya ambayo wanajumuiya wake wawe na sifa hizo zote. Mola, kama kuna majaribio, basi wajaalie imara, na Usiwatwishe mizigo wasiyoweza kuibeba (2:287); na Uwakuze jinsi nilivyoomba.

Nahisi Mungu Atatimiza utashi wangu. Nyinyi nanyi mwombe kwa moyo huo, na muwe wasaidizi katika njia ya Mungu."

Keshoye ilikuwa Ijumaa, akawasihi jamii ya waabuduo katika hotuba ya pili kama ifuatavyo:

> "Sina la kukazania isipokuwa maombi. Dumuni kufanya maombi. Nawasisitizieni hiyo kwa manufaa yenu. Sitaki kutoka kwenu chochote, hata kwamba mwinuke kwa kuniheshimu. Kama ningalitazamia chochote kwenu, ningalifanya kosa kubwa kabisa la utovu wa shukurani kwa Mungu. Je, Yule Mungu Aliyenijaalia fadhili zake sikuzote, zaidi kuliko nilivyotazamia, Atanifanya sasa niwategemeeni katika uzee wangu kwa siku zangu chache zilizobakia?
>
> …. Fadhili zake zifululizazo zanilazimisha niwe Wake kikamilifu. Nguvu zangu zote ni fadhili Zake, heshima zote na taadhima nilizo nazo ni zawadi Zake."

Ni la kushangaza kwamba mawaidha yote ya Hadhrat Khalifatul Masihi r.a ya kusisitiza mwafaka na umoja baina ya wanajumuiya, maonyo yake yote kuhusu matokeo ya kuogofya ya mafarakano na fitina, yakawaathiri wafitini wagumu kwa kitambo kidogo tu, kama yaliathiri kwa vyoyote. Kwa hakika wakaonekana kukaza ukaidi wao. Ni kweli ya kwamba jumuiya kwa jumla kwa kutahadharishwa ipasavyo na kuonywa ikasalimika katika ujanja mbaya wa watu wachache wenye mikono mirefu wasiotaka kupatana; na huo kweli ulikuwa ufaulu mkubwa. Hata hivyo ni jambo la kujutia kwamba mtengano haukuweza kuepukika.

Uongozi wa wafitini ulikuwa na nguvu katika Lahore. Afya ya Khalifatul Masihi r.a. ilipoendelea kwa vyovyote kuwa hafifu na ikaanza kuharibika, kundi la wafitini likaanza kufanya propaganda kwa ushupavu kukabili hatari isiyoepukika. Hatua ya kwanza waliyochukua ni kwamba wakaanza kutoa gazeti kutoka Lahore waliloita *Paighame Sulh* (Ujumbe wa Amani). Toleo la kwanza lilitolewa Julai 10, 1913.

Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akawa mnunuzi wake, lakini baadaye akakataa kulipokea, kwa kuona madhara ya sera zake na kazi yake hata kwamba akaliita *Paighame Jang* (Ujumbe wa Vita). Mara kwa mara ahadi za uaminifu kwa Khalifatul Masihi r.a. zilichapishwa, lakini walipungukiwa nia. Ilipigwa kampeni mfululizo kumvunjia heshima Shaibzada Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad r.a. Walichelea isije Sahibzada Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad, japo alikuwa kijana tu, akachaguliwa kuwa *Khalifa* baada ya Khalifatul Masihi r.a. ambaye hakuficha kwamba alimheshimu sana Sahibzada. Itikadi na mafundisho ya Jumuiya ya kupambanua yaliyotolewa na Masihi Aliyeahidiwa a.s. yalielezwa mara kwa mara na Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. na hadi wakati huo yalikuwa yanakubaliwa na viongozi wa wafitini wenyewe, yakaanza kubomolewa taratibu na kuzimuliwa na wafitini kwa nia ya kupendwa na Waislamu wengi wasiokuwa Waahmadiyya.

Ijapokuwa afya yake iliendelea kuharibika Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. alitoa darasa la Kurani Tukufu nzima katika mwezi wa Ramadhani mnamo Agosti – Septeba 1913.

Shambulio kubwa zaidi lilifanywa kwa niaba ya wafitini kutoka nyuma ya pazia nyembamba na ya woga katika Oktoba 1913, kwa sura ya vijitabu vidogo viwili bila ya jina la mwandishi, kimoja baada ya kingine katika kitambo kifupi, vilivyoitwa *Idh-harul Haq I* na *Idh-harul Haq II* (kudhihirisha haki). Vilikuwa vichafu na vya aibu, vilivyojaa madai ya uwongo ya uchongelezi dhidi ya Hadhrat Khalifatul Masihi na watu wa familia ya Hadhrat Masihi Aliyeahidiwa a.s., akiwemo Hadhrat Ummul Muminin r.a. pia. Kweli hii kwamba vilitolewa hivyo kwa kushauriwa na viongozi wa wafitini – ingawa walikana – inahakikishwa na maneno ya Mahriri wa *Paighame Sulha* la 16 Novemba 1913, ambayo ni haya:

“Tumeona katika vijitabu hivyo kwamba maneno mengi

> yaliyoandikwa humo hayana shaka hata kidogo kwamba ni ya kweli.... Kama *Ansarullah* ya Lahore ikiona inafaa kujiingiza katika habari hii na kukusudia kuandika chochote dhidi yetu ili kuzalisha kuelewana kubaya kwa sababu tumeyaunga mkono maneno yaliyomo ndani ya vijitabu hivyo, hapo lawama itakuwa juu yao kama tukichapisha lolote kwa kujibu."

Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akaiagiza *Anjuman Ansarullah* kutayarisha na kuchapisha majibu ya vijitabu hivyo. Muswada wa majibu ulipopelekwa kwake, akaukagua na akandika juu yake: *Paigham (Sulha)* linastahili kupata lawama elfu kwa kutuletea ujumbe wa vita kwa kuchapisha barua yake wazi, na kwa njia hiyo limetangaza unafiki wake. Amelaaniwa yule anayezindua msiba ulalao.

Majibu yalitolewa katika vijitabu viwili: *Khilafat Ahmadiyya* kikachapishwa Novemba 23, na *Idh-ahare Hakikat* tarehe 28 Novemba 1913. Majibu hayo yakathibitika kuwa yenye kuathiri mno kama kanusho kamili la masingizio na uchochezi ya kuadhiri na ya uwongo yaliyoandikwa katika vijitabu vya kuchukiza, na yakailinda Jumuiya kikamilifu dhidi ya fitina ambayo vijitabu vyao vilikusudia kuchochea.

Khalifatul Masihi r.a. alipougua sana baada ya kuanguka kutoka juu ya farasi jike, akaona katika ruya kwamba mtu fulani ametia rupia moja mfukoni mwake. Akaagua kwamba atapata mwana. Ruya hiyo ikatimia tarehe 18 Novemba 1913 ambapo alijaaliwa mwana wa tano aliyemwita Abdullah.

Mkutano wa Mwaka wa 1913 ulifanyika Desemba 25-27. Wahudhuriao walikuwa wengi zaidi kuliko mwaka uliopita. Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akiendelea kuhutubia alinena:

> "Kutimiza mapatano ni jambo la faradhi. Nawaelekezeni

kwenye ahadi mojawapo ili muweze kutafakari kwamba mnaitekeleza. Ndiyo ahadi ya utii mliyofanya nami. Tena kati yenu kuna wenye hali mbaya wasemao: *Khalifa*, ati, ni nini? Yu mkongwe. Angalieni, sikilizeni na kumbukeni ya kwamba Mungu Mtukufu Amenifanya *Khalifa*, nami simtegemei yeyote kati yenu kwa chochote. Nimekwisha omba dua kulindwa na matokeo ya uzee, na Yeye Amenihifadhi. Amenijaalia ujuzi wa Neno lake. Kunilaumu kwenu hakukubaliwi na Mungu. Yeye Ana ghera kwangu. Tubuni kwa fikira yenu mbovu. Yeye Amehifadhi kikamilifu nguvu zangu. Sifa zote njema ni Zake kwa fadhili Zake zote.

Nyinyi hamna uhuru wa kueneza habari zinazohusikana na ulinzi au hatari. Mwapaswa kumfikishia chochote cha aina hiyo Amiri au Mwenyekiti wenu ili aweze kuchukua hatua yoyote ifaayo. Waliochapisha vijitabu viwili, *Idh-harul Haq,* na barua moja ya wazi kwa *Ansarullahi*, na kuendeleza majadiliano juu ya *Ukhalifa*, hawakuwa na madaraka kufanya hivyo. Barua ya wazi iliniudhi sana moyo wangu. Tena mtu fulani akaniletea kadi iliyochapishwa na akaniomba ruhusa kuichapisha. Nikamwambia hiyo ni kinyume cha Kurani. Akaomba ruhusa ya kufanya jambo alilokwisha fanya tayari. Watu kama hao wanavunja maagizo ya Kurani, na wanatafuta kufarakisha watu ambao Mungu kwa rehema yake Ameunganisha kwa mkono wa mtu mmoja. Mjihadhari kwao. Tena mtu fulani alisema kwamba nilipoanguka kutoka juu ya farasi jike, hiyo ikamaanisha kuwa nimeanguka kutoka *Ukhalifa*, na kwamba hiyo ilikuwa kwa sababu ya ukosefu wa uimara. Huku ni kuelewa vibaya sana kashfi moja ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. Mungu Ameniagiza kuhusu majibu ya hayo yote. Tenganeni na watu kama hao na epukaneni na fikara mbovu”

Baada ya Mkutano akaandika kumbukumbu ifuatayo:

> “Mungu Mtukufu Amesema katika Kurani Tukufu: kama mkishukuru kwa neema zangu, Nitawazidishieni (14:8). Shukurani kwa neema za Mungu zinakuwa chanzo cha neema nyingine zaidi. Kwa hiyo, kwa kuthamini fadhili za Mungu naeleza shukurani yangu kwa Mungu kwamba Yeye ndiye Mkarimu kwetu sisi.
>
> Mnamno mwaka huu baadhi ya wajinga walijaribu kuleta msukosuko katika Jumuiya, na kwa shabaha hiyo wakaeneza vijitabu vilivyoitwa *Idh-harul Haq,* ambamo mimi pia nikafanywa lengo la lawama. Shabaha ya mtungaji wa vijitabu hivyo ilikuwa kueneza mfarakano katika Jumuiya. Lakini Mungu kwa fadhili yake Akailinda Jumuiya na mimi pia katika fitina yake. Msaada Wake na nusura Yake ikadhihirishwa kwa namna ambavyo mipango yote ya wafitini ikavunjika kabisa na Jumuiya ikakingwa isipate madhara. Hiyo ikathibitishwa hadharani katika siku za Mkutano wa Mwaka. Hili lilikuwa dhihirisho maalum la msaada na nusura ya Mungu Mweza ya kwamba ijapokuwa zilikuwapo sababu kadha zenye kisirani na uenezaji wa vijitabu vyenye kusumbua vilivyoitwa *Idh-harul Haq,* mahudhurio katika Mkutano yalikuwa makubwa zaidi kuliko miaka iliyopita. Nyuso za washiriki zilidhihirisha mapenzi na uaminifu ulioshuhudia bayana kwamba Jumuiya ya Ahmadiyya inakingwa kikamilifu dhidi ya kila athari mbaya. Aidha, matawi mbalimbali ya Jumuiya yaliweka mfano mwema wa kujitolea ambao ndio ushuhuda wa fadhili ya Mungu isiyo na kifani. Mnamo mwaka huu Jumuiya ilitimiza wajibu mzito wa kutoa michango, hata hivyo *Sadr Anjuman* ilikuwa na hasara. Matawi yalichukua, kwa uchangamfu na

furaha, jukumu la kuondoa hasara, na fedha nyingi taslimu zilichangwa. Kwa jumla fedha zilizoahidiwa na kutolewa zilikuwa mara tatu kuliko zilizochangwa mwaka jana, jambo linaloonekana ni fadhili kubwa za Mungu, tukiona kwamba idadi ya wanajumuiya ni kidogo tu.

Mkutano pia ulikanusha vizuri sana masingizio ya wale walioeleza kwamba kuanguka kwangu kutoka juu ya farasi jike kunamaanisha kuondolewa kwangu katika cheo na heshima ya kuwa *Khalifa*. Msukosuko ulipoanza dhidi ya *Ukhalifa*, Mungu Akanionyesha katika ruya kwamba nikiwa juu ya farasi napitia nchi iliyo kavu na kame. Nikamwendesha farasi mbele naye akaanza kukimbia mbio sana hata ikawa vigumu kwangu kumuweza, lakini kwa fadhili ya Mungu nikaendelea kukaa juu yake kwa imara. Baada ya mwendo mrefu, farasi akaingia katika bonde lenye rutuba ambako kila mahali ilionekana migunda futi mbili juu. Farasi akaendelea kukimbia mbio, na alipofika katikati ya bonde nikazinduka. Kutokana na ruya hiyo nikafahamu kwamba wale wanaodai nitaondolewa katika cheo cha *Ukhalifa* watathibitika kuwa waongo, na kwamba si tu Mungu Atanitetea, bali Atanijaalia ufaulu. Ni fadhili ya Mungu kwamba Ametimiza ruya yangu hii pia. Mkutano wa Mwaka, wa mwaka huu, umehakikisha kwamba ruya hiyo ilikuwa ya kweli. Juu ya upinzani na uenezi wa vijitabu bila jina la mtungaji, Amedhihirisha msaada baada ya msaada, Ameongeza mapenzi na uaminifu nyonyoni mwa wanajumuiya, Amevuta nyoyo zao kwangu, kawatilia roho ya utii mioyoni mwao na Amewakinga dhidi ya hila za wafitini"

Mnamo Februari 2, 1914, Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. alitoa agizo:

"Kumbukeni, watoto wangu wasipewe chochote katika mali ya

sadaka au zaka, au katika mali yoyote iliyowekwa kwa ustawi wa mayatima au maskini. Mungu Atawajaalia riziki. Yeyote atakayeandika habari za maisha yangu apaswa kutaja agizo langu hili na ajizuie kulivunja. Sina fedha. Madeni yangu yote yamelipwa. Sidaiwi na yeyote. Mtu yeyote asiwadai chochote watoto wangu."

# XVII

# KUMBUKUMBU YANGU

Baba yangu Chaudhri Nasrullah Khan, alikuwa mwanasheria (wakili) aliyekuwa anafanya kazi katika Sialkot, Panjab. Mwanzoni mwa karne hii, yeye aliajiriwa kutetea daawa ambamo maswali ya kuvutia na kukanganya yalizuka yaliyotakiwa kuamuliwa na mahakama. Miaka kadha hapo kabla, Maulawii Mubarak Ali, Imam na Msimamizi wa Jamia Masjid wa Sialkot Contonment, alijiunga katika Jumuiya ya Ahmadiyya; msikiti huo ulikuwa mkubwa sana na uliwekewa wakfu mali nyingi. Itikadi zake zilizolaumiwa vikali na Masheikh wa kisuni, zikawa chanzo cha uchungu na mahangaiko kwa wale waliokuwa wanasali humo msikitini, ambazo pole pole zikawa sababu ya kutokuvumilia na uadui. Hatimaye watu kadha miongoni mwao wakapeleka mashtaka mahakamani kutaka kwamba itangazwe ya kuwa kwa sababu ya kujiunga katika Jumuiya ya Ahmadiyya mshtakiwa, Maulawii Mubarak Ali, ametoka katika Islam, kwa hiyo hafai kufanya kazi kama Imam au Msimamizi wa Jamia Masjid. Kulikuwa hakuna wakili Ahmadiyya mjini Sialkot katika zama hizo; baba yangu akaajiriwa kuwa wakili wa mshtakiwa. Yeye akataali kwa makini sana na kwa ukamilifu maswali ya kidini yaliyoulizwa na wenye kushtaki kuimarisha madai yao ya kwamba Ahmadiyya hawezi kufikiriwa kuwa Mwislamu; akawa na moyo wa huruma kwa maoni ya Waahmadiyya. Jambo jingine lililomwathiri sana lilikuwa kwamba wadai na mashahidi wao wakitoa ushuhuda kwa kuapa hawakusita kusema uwongo au kugeuza habari kama wakiona majibu yaliyo sawa yaweza kudhuru kesi yao; lakini mshtakiwa na mashahidi Waahmadiyya wakashikamana na ukweli bila kujali maneno yao yataiathiri vipi kesi yao. Akafikiria kwamba kiwango cha

juu cha khulka njema za Waahmadiyya zilizodhihirika kwa namna ya kustaajabisha ni dalili kwamba msingi wao ni katika ukweli. Uchunguzi wa hakimu ukathibitisha mshtakiwa ndiye mwenye haki, kwa hiyo kesi ikafutwa. Wadai wakakata rufaa dhidi ya hukumu ya hakimu, lakini rufaa nayo ikafutwa. Jambo hilo likamwelekeza baba yangu kwenye Ahmadiyya.

Baada ya muda kidogo akaitwa kuhudhuria kama shahidi wa mshtakiwa katika Korti ya Hakimu mjini Gurdaspur katika kesi ya jinai ambamo Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s., Mwanzilishi wa Jumuiya ya Ahmadiyya, alishtakiwa kumwumbua Maulawii Karam Din, adui mmojawapo mkali mno. Hiyo ikampatia nafasi ya kuonana na mtu mtukufu, naye akaathirika sana na utakatifu wake.

Katika kipindi hicho, mnamo kiangazi cha 1904, mama yangu asiyekuwa na uhusiano na Ahmadiyya wala hakuwa na habari ya Jumuiya hiyo, ingawa muda kidogo hapo kabla baba yake na ndugu yake wa pekee walijiunga katika Ahmadiyya, akajaaliwa kuona ruya zenye maana sana za kiroho ambamo aliwahi kumwona mtu mmoja mkubwa mtukufu ambaye, mama alifikiri, alitaka kumwongoza katika njia ya wema. Ruya hizo zikamchangamsha na kumwathiri mno moyoni. Hakujua asilani yule mtukufu alikuwa nani, na katika ruya ya tatu akamwomba amweleze yu nani. Akamwambia, yu Ahmad. Alipomweleza baba yangu, yeye akasema kwamba kwa kuwa Ahmad ni jina moja la Mtume Mtukufu s.a.w. wa Islam, pengine mama amebahatika sana kujaaliwa kumwona yeye kiroho. Lakini mama akamweleza kwamba yeye anahisi kwamba mtukufu ambaye yeye alimwona katika ruya zake anaishi katika zama hizi ambaye anaongozwa naye katika ukweli na wema. Baada ya siku chache nduguye akaja kumtembelea na aliposikia ruya yake ya mwisho akasema Ahmad ni jina la Masihi Aliyeahidiwa na kwamba wewe

umemwona yeye tu ndani ya ruya zako. Mama akasema ana yakini kwamba Mungu Aliyechagua njia hii ya kumwongoza, Atamweleza katika muda ufaao shabaha Yake kwa uwazi zaidi.

Ilitangazwa ya kwamba Masihi Aliyeahidiwa a.s. yuko Lahore matembezini na kwamba hotuba yake itasomwa huko Lahore tarehe 3 Septemba 1904, naye atakuwapo hapo mwenyewe. Baba yangu akaenda Lahore kwa shabaha hiyo, na kwa bahati njema sana akanichukua pia pamoja naye. Pindi nilipotazama uso uliobarikiwa wa mtukufu huyo, nikafurahishwa mno, na muda wote alioendelea Maulawii Abdul Karim kusoma hotuba, nikaangazia macho uso wake ung'aao. Ukweli wake ukapenya moyo wangu na roho yangu nami nikahisi kwamba nimejitolea kwake kabisa. Nilikuwa mwanafunzi tu wa shule, mwenye umri wa miaka kumi na miwili, lakini nilikuwa na yakini kwamba Mungu Amenibariki sana mno kwa fadhili zake kwa kunijaalia nafasi hiyo njema.

Masihi Aliyeahidiwa a.s. akawasili Sialkot matembezini tarehe 27 Oktoba 1904, pamoja na watu wa familia yake na baadhi ya wafuasi wake akiwemo Maulawii Nuruddin r.a. Keshoye asubuhi, baba yangu alipokuwa akijitayarisha kwenda kortini, mama yangu akamwuliza, je, naweza kwenda kumtazama mgeni mheshimiwa na kumwona kama ni yule yule mtukufu nimwonaye katika ruya.

"Nenda kwa vyovyote," akasema, "Ukachunguze, lakini usifanye uamuzi wa mwisho."

"Kama ndiye huyo huyo, nitakosea machoni mwa Mungu, nikibaki nyuma baada ya mwongozo wa wazi Alionijaalia."

"Hili ni jambo la muhimu sana, nami sipendi tufarakane juu ya hilo. Ujuavyo, ninaendelea kuisoma habari hii. Tutazungumzia habari hii pamoja, na ninafikiri tutafikia

uamuzi huo huo."

"Wewe umesoma sana, nami sikuwahi kusoma vitabu. Lakini nafikiri Mungu kwa fadhili Yake Amechagua njia Yake kuniongoza. Nikiona mwongozo Wake unaashiria upande huu, lazima nisogelee ipasavyo. Kama ni vingine, nitafurahi kuzungumza habari hii nawe na twaweza kuamua pamoja."

"Kukawia kidogo hakudhuru. Nahofia kufarakana juu ya swali hili la muhimu kabisa."

"Nimekwisha kuambia nifikirivyo."

Nikafuatana na mama yangu alipoondoka kutafuta alichothamini sana ambacho alisukumwa kwacho na roho yake. Alipofika nyumbani alimokaa Masihi Aliyeahidiwa a.s. pamwe na ahali zake akahudhuria mbele ya Hadhrat Ummul Muminin na kumwomba amfanyie mpango ili aweze kumtazama mara moja mumewe mtukufu. Akapelekewa ombi, naye akarudisha jibu kwamba baada ya muda kidogo atapitia hapo na atakawia kwa dakika chache akielekea msikiti wa jirani ili kushiriki kusali. Halafu akawasili na kuketi karibu na Hadhrat Ummul Muminin, futi chache kutoka alipokaa mama yangu pamoja nami. Alipomwona tu, uso wake ukang'ara na kwa tabasamu yenye jazba akasema: Bwana wangu, ningependa kufanya baiati. Akakubali kwa ukarimu: "Kariri nyuma yangu nitakayosema." Kisha akatamka fungu kwa fungu maneno ya ahadi ya baiati na mama akakariri nyuma yake. Mwishowe akafanya maombi ya kimya ambamo ahali zake, mama yangu na mimi tukaungana naye, na yeye akaondoka. Nikapata kujua baadaye kwa sababu ya kuchunguza mwenyewe kwamba hiyo ilikuwa si kawaida ya Masihi Aliyeahidiwa, hususan aliyekuja kufanya baiati akiwa mwanamke ambaye mumewe hakuwa mwanajumuiya wa Kiahmadiyya, Swali lolote halikuulizwa na pande zote mbili, halikutamkwa hata neno moja zaidi ya maneno maalumu

ya ahadi ya baiati. Ilionekana kuna mwafaka mtimilifu baina ya atafutaye na atafutwaye. Roho ya mama yangu ikapata utulivu, utafiti wake ukamwongoza kwenye pepo zake za kiroho. Hakumwona tena isipokuwa katika ruya, lakini kujitolea kwake kulidumu kikamilifu na kwa uhalisi katika majaribio na mateso yote mpaka pumzi yake ya mwisho aliyopumua katika hali ya kufahamu, zaidi ya theluthi ya karne baadaye. Chochote hakikuvuruga utulivu wake, imani yake ilikuwa imara kukikabili chochote, na ikamtetea katika hali zote.

Akakaa pamoja na Hadhrat Ummul Muminin kwa nusu saa ambamo msingi wa urafiki baina yao uliwekwa ambao ulidumu maisha yake yote. Tuliporejea nyumbani, alikuwa hana budi kufikiri kwamba katika kitambo cha masaa mawili hivi ataagizwa kuhudhuria kukabili jaribio gumu mno la maisha yake. Lakini alikuwa na yakini kwamba hatua aliyochukua aliagizwa na Mungu kuichukua hata kwamba hakuwa na shaka kwamba Yule Aliyemwongoza mpaka sasa Atamsaidia daima dawamu. Hakuhitilafiana na mumewe hapo kabla katika jambo lolote kubwa, lakini sasa wakakabili jambo zito lihusulo wokovu wa roho zao. Akisubiri kurudi kwake nyumbani haikosi akaomba sana mwongozo na nguvu.

Akawasili, na tena nikabahatika kupata nafasi ya kusuhudia yaliyotokea. “Je, ulikwenda?” Akauliza kwa hamu na shauku, akiongeza sawa na kawaida yake maneno ya kuonyesha upendo.

“Ndiyo, nilikwenda.”

“Tena?”

“Mtu huyo ndiye”; akitetema kidogo.

“Natumaini hujafanya uamuzi wa mwisho.”

Akaweka mkono wake wa kuume juu ya moyo wake na akahakikisha:

“Nimefanya baiati.”

Uso wake ukafifia rangi, na midomo yake ikamtetemeka, lakini akajaribu sana kujizuia na akanung’unika: «Haikutendeka vizuri.”

Kisha akamwita mtumishi na kumwamuru:

“Ondoa kitanda changu ukipeleke katika chumba cha pili.”

Hapo mama akapaza sauti kidogo na kumwambia mtumishi: “Peleka kitanda chake katika makazi ya wanaume!”

Hiyo haina budi ikamshangaza, kwani akasema kwa uchungu: “Kwa nini?”

“Kwa sababu Mungu kwa hisani Yake Amenijaalia kuona mwanga, nawe bado umo gizani!”

Akatambua kwamba mama kashinda. Akamgeukia mtumishi na kumwambia aondoke hapo akisema kwa masikitiko: “Mama hana budi kushinda.”

Kipeo cha hatari kikapita, kila mmoja akatulia; lakini baba yangu bado akatakiwa kuamua; mama yangu akafululiza kufanya maombi kwa mwungano wao kiroho.

Mwanasheria mmoja mwenzake kule mahakamani pia alikuwa na moyo wa kuipenda Jumuiya; baba yangu aliyeelekea mwenyewe kusonga mbele akamwuliza kama atashirikiana naye. Mwenzake akapenda kupata maelezo bayana kuhusu baadhi ya mambo fulani makubwa, na ikakubaliwa wapate mwongozo kutoka kwa Maulawii Nuruddin r.a. ambaye kwa ukarimu akawaarifu kwamba atafurahi kuonana nao kila jioni kwa muda wa saa moja hivi. Katika vikao vinne mimi pia nilipata bahati njema kuhudhuria. Hiyo ikanipa nafasi ya kumwangalia Maulawii Nuruddin r.a. kwa karibu sana; yeye naye pengine akaniangalia kama mwana wa rafikiye Nasrullah

Khan. Akirudi kutoka kikao cha mwisho, baba yangu akamwuliza mwenzake kama yeye anaweza sasa kufanya uamuzi. Akasema, maswala aliyouliza yametatuliwa yote. Baba yangu akauliza: Je, basi, tutafanya baiati?"

"Wafikirije?" Akauliza.

"Niko tayari, kama uko"

"Vizuri sana, basi. Kesho asubuhi ukija kwenye sala ya Alfajiri, nichukue pia pamoja nawe, nasi tutafanya baiati."

Kesho asubuhi nikafuatana na baba yangu kwenda kusali sala ya Alfajiri pamoja na jamaa; njiani kwenda msikitini tukamtaka mwenzake kufuatana nasi, lakini akaona bado hayuko tayari kubeba jukumu lilazimishwalo na ahadi ya baiati. Basi babangu akafanya baiati faraghani akikaa na Masihi Aliyeahidiwa baada ya sala ya Alfajiri. Nilikuwapo pia. Kufanya baiati kwa babangu muda kidogo baada ya baiati ya mamangu ilikuwa pia sawa na ruya mojawapo ya mama. Mapatano yakarudishwa kwa furaha katika familia. Miaka kumi baadaye ukatokea msukosuko, lakini mambo yakarekebishwa kwa njia hiyo hiyo.

Baada ya kujiunga katika Jumuiya, baba yangu akakaa Qadian siku nyingi zaidi za Septemba, mwezi wa likizo ya korti za wilaya. Akahudhuria pia katika kila Mkutano wa Mwaka uliofanywa katika wiki ya mwisho ya Disemba. Nikafuatana naye kila mara. Huko kulikuwa na fursa ya kuwa pamoja na Masihi Aliyeahidwa alipokwenda kupunga hewa asubuhi na alipokaa katika msikiti (Masjid Mubarak) baada ya sala ya Adhuhuri, na baada ya sala ya Alasiri. Muda uliobakia nikafaidika na kila nafasi niliyopata kukaa na Hadhrat Maulawii Nuruddin r.a. Nakumbuka kwamba kwa muda fulani alikuwa akisomesha kabla ya saa sita za mchana *Mathnawi* ya

Maulana Jalaluddin Rumi.

Baada ya kumaliza darasa la kumi mnamo Aprili 1907, nikaingia Government College Lahore kwa kozi ya Shahada ya Chuo cha Panjab mnamo Mei. Katika likizo za kiangazi za mwaka huo nilipokuwa nyumbani baba yangu akapokea kadi ya posta (barua) kutoka kwa Hadhrat Maulawii Nuruddin r.a. iliyomaanisha nifanye baiati ya Masihi Aliyeahidiwa a.s. Nilivyoona mimi, nilikuwa mwanajuwuyia wa Kiahmadiyya tangu Septemba 3, 1904, nilipopata bahati kuuona uso uliobarikiwa wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. mjini Lahore, na nikajihesabu nimo katika baiati za wazazi wangu walizofanya wiki chache baadaye mjini Sialkot nami nilikuwapo hapo. Hata hivyo kwa kufuata agizo la Hadhrat Maulawii Nuruddin r.a. lililotolewa kwa baba yangu, nikafanya baiati kwa mkono wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. katika Qadian tarehe 16 Septemba 1907. Namshukuru sana mno Hadhrat Maulawii Sahib r.a. kwa kutoa agizo lake hilo, kwani alipofariki Masihi Aliyeahidiwa tarehe 26 Mei 1908, orodha tukufu ya heshima ya masahaba zake ilikamilika na kufungwa. Siku hiyo ya msiba mkubwa kabisa na huzuni ya kushinda nilikuwa Lahore na nikafuatana na mwili wa kiongozi aliyeaga dunia, hadi Qadian ambako keshoye jioni Hadhrat Maulawii Nuruddin alitangazwa kuwa Khalifatul Masihi, na wanajumuiya wote wa Kiahmadiyya waliokuwako Qadian, nikiwa mmojawapo, wakafanya baiati kwake.

Katika muda niliokuwa katika College (chuo) niliendelea kutembelea Qadian mara kwa mara, nikakaa huko sehemu ya likizo za kiangazi na kuhudhuria Mkutano wa Mwaka kama kawaida kila mara. Hivyo nikajulikana kwa Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. na nikapokea hisani zake nyingi kwa ukarimu wake na misaada kutoka kwake.

Baada ya mtihani wangu wa mwisho wa kupata shahada mnamo Arpili 1911, nilikwenda kwetu Sialkot na baada ya kukaa huko kwa wiki

kadhaa nikaenda Qadian mnamo mwezi wa Juni. Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. alikuwa bado mgonjwa, akipitisha mchana katika sebule akitoa darasa, kushughulikia kazi za Jumuiya, kuwaangalia wagonjwa na kupokea wageni. Jeraha la panja la kuume likawa donda la kudumu na likafungwa dawa kila siku. Baada ya kutembelewa na daktari akaendelea kulala kwa kitambo, na mwanafunzi wake mmojawapo akamkanda mikono na miguu taratibu. Alikuwa bado hajapata nguvu ya kwenda msikitini kwa sala za kila siku hivyo zilisaliwa katika sebule yake kwa ajili yake. Mwanafunzi wake aliyempenda na aliyekuwa anamsimamia, Sheikh Muhammad Taimur, aliongoza sala; Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akasali akikaa. Maamuma walikuwa wanafunzi wanne au watano. Iliposikika adhana kutoka msikiti wa karibu zaidi Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akamwagiza kila mmoja aondoke akaungane na sala ya jamaa msikitini. Siku ya kwanza ya ziara yangu, adhana ya sala ya adhuhuri iliposikika na wote waliambiwa kwenda nikainuka kuondoka. Ndipo Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. kwa ukarimu na upendo akaniagiza: Mian, utasali hapa pamoja nasi. Hivyo, nikasali sala ya adhuhuri pamoja na jamaa katika sebule.

Kulikuwa na mstari mmoja tu wa waabuduo nyuma ya Imam. Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akakaa upande wa kushoto kabisa baada ya kitanda chake. Nikasimama upande wake wa kuume na maamuma wengine wakajipanga kulia kwangu. Kwa sababu ya kupenda nisimsumbue na pia kwa kumheshimu sikusimama karibu sana naye, lakini akaweka mkono wake kuzunguka miundi yangu na akanisogeza karibu yake. Safari moja ambapo Sheikh Muhammad Taimur hukuwepo hapo kuongoza katika sala ya alasiri, Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akaangalia huko na huko, akaniambia: Mian, umekwisha soma Kurani Tukufu, tafadhali uongoze katika sala. Nikalazimika kutii.

Siku moja ikawa hivi kwamba daktari alipoondoka baada ya kumfunga dawa jeraha lake, nilikuwa peke yangu ndani ya chumba. Sikujua kukanda sawasawa. Je, niondoke chumbani taratibu, ama nijaribu kumkanda mikono na miguu mgonjwa mheshimiwa – jambo litakalomsumbua pengine kuliko kumpa raha? Ilivyokuwa desturi yake, akalala kwa ubavu wake wa kushoto. Nikaenda taratibu kukaa juu ya kitanda chake nyuma yake, nikaanza kutoa utumishi wangu kwa hadhari na kushikashika kwa vidole vizito. Baada ya dakika tano hivi nikaacha, kwa nia ya kuondoka na kumwacha apumzike. Alipotambua hiyo, akainua mkono wake wa kuume na akauweka pembezoni mwa shingo yangu, akauelekeza uso wangu kwa upole karibu na uso wake, akaniweka katika hali hiyo kwa dakika mbili hivi akiwa kimya. Aliponiacha, akanena: "Mian, nimekuombea maombi mengi sana!" Kweli, ilikuwa dua ya heri ambayo harufu yake njema imedumu nami miaka sabini.

Nilipokuwa bado Qadian babangu akaniandikia nimpelekee Hadhrat Khalifatul Masihi maombi kadha wa kadha, mojawapo katika hayo lilikuwa kumwomba ruhusa kwamba niende Uingereza kwa masomo ya juu. Nikampelekea maombi hayo katika maandishi. Kunihusu mimi nikaandika kwamba, kwa fadhili ya Mungu, nimefanya vizuri katika mtihani wangu wa Shahada ya B.A. na kwamba natumai nitapita, na kama akitoa kibali na kuniruhusu, baba yangu anapenda niende Uingereza kwa masomo ya juu. Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akaagiza ya kwamba baba yangu na mimi twapaswa kutafuta mwongozo wa Mungu kwa sala ya *Istikhara* kwa njia iliyofundishwa. Na kama sote wawili tukiridhika baada ya sala hiyo, nitaweza kwenda kama alivyotaka baba yangu. Nikamwarifu baba yangu agizo lake na nikaomba mwongozo wa Mungu kwa wiki moja, hatimaye nikahisi dalili dhahiri kuafikiana na upendo wa baba yangu, ingawaje binafsi sikupenda kwenda ng'ambo.

Matokeo ya mtihani yalitangazwa, na rafiki mmoja kutoka Lahore akaniandikia kwamba nimepita katika Divisheni ya Kwanza. Nikampelekea barua hiyo Khalifatul Masihi r.a. ambaye alifurahi sana hata kwamba kila mmoja aliyemjia kumwona jioni hiyo akamwambia: "Nina furaha kubwa leo, huyu, akiashiria kwangu, amefaulu katika mtihani wake wa B.A., tena ni la ajabu kwamba alijua atafaulu."

Ikajulikana baadaye kwamba nilikuwa wa kwanza katika Arabic Honours (Daraja la juu la Kiarabu). Na kama ningelikuwa na nia ya kufanya M.A. kwa Kiarabu, ningelipatiwa malipo ya kutosha kwa kuendelea na masomo hayo. Hilo likanivutia, lakini upendo wa babangu ulikuwa bora zaidi.

Baada ya alasiri, Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. alikuwa anapenda kukaa katika behewa la nyumba yake ndogo ambalo wakati huo katika saa za mchana lilikuwa na baridi kidogo ya kufaa. Huko pia nikakaa naye. Siku moja akasema: "Hizi ni saa za kucheza.» Hutaki kushiriki katika mchezo wowote?"

Nikasema kwa heshima: "Mpenzi, nina furaha sana hapa nilipo."

Halafu nikatakiwa kumwomba ruhusa niende kwetu nikajitayarishe kwa safari yangu ya kwenda Uingereza. Mama yangu akahofia mtengano mrefu ujao, nami nikajikunyata kwa kujitupa pasipojulikana na kwenda kushinda kule nilikojua kidogo, na hicho kidogo pia cha uvumi tu, kukaa na watu ambao imani yao, utamaduni wao na namna walivyoishi ni tofauti kabisa na ile yangu. Kwa hiyo kujitayarisha hakukuwa na msisimko, na nikashikwa na fadhaa nyingi na wahaka.

Safari yangu iliandikishwa toka Bombay hadi Trieste na meli ya Austrian Lloyd iliyopangwa kung'oa nanga Septemba 1, 1911.

Wazazi wangu, babangu mdogo na hadimu wa familia wakaondoka Sialkot asubuhi na mapema tarehe 28 Agosti kwa garimoshi kwenda mpaka Batala na wakawasili Qadian jioni. Nikamwomba ruhusa Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. keshoye. Akaagana nami kwa upendo na maombi. Akaniandikishia maagizo kadha na maombi ambayo nikaandika; pia akanipa nasaha kwa mdomo. Akaniagiza nimwandikie mara kwa mara. Mama yangu akafurahi sana kuonana na Hadhrat Ummul Muminin. Tukaondoka Qadian jioni hiyo kuelekea Batala na kupanda garimoshi kwenda Amritsar ambako mamangu, baba mdogo na hadimu walifunga safari ya garimoshi kuelekea Sialkot; babangu na mimi tukachukua treni ya posta (garimoshi linalochukua barua pia, na linakwenda kwa kasi) kwenda Bombay, umbali wa maili elfu moja. Nilikuwa sijasafiri kupitia Amritsar hapo kabla, kwa hiyo kutoka hapo kila kitu kilikuwa kipya kwangu. Tukawasili Bombay Agosti 31, na keshoye saa sita za mchana nikaingia meli ya S.S. Koerber, yenye kuhamisha maji tani 4,000. Babangu akapeana mikono nami kama alama ya kuagana, chini ya ubao wa kuingilia melini; na zaidi ya kupeana mikono hata neno moja halikusemwa na sote wawili.

Haikupita saa baada ya meli kuondoka nikapatwa na ugonjwa wa taabu ya bahari (kuchafuka tumbo na kutapika chomboni), hali ambayo sikuhadharishwa nayo kabla wala sikuijua. Upepo wa kusi ulikuwa ukivuma kwa nguvu zote na siku nne zijazo zilikuwa za taabu kubwa kabisa isiyofifia ya kufadhaisha. Tulipotoka tu eneo la upepo wa kusi, kila kitambo cha safari kikathibitika cha kufurahisha. Baada ya kutokula kwa siku nne nikasikia njaa kali sana, nikafurahia kila mmego wa chakula kizuri sana kilichotolewa melini. Tukawasili Trieste jioni ya Septemba 14, tukasafiri upande wa kaskazini kwa garimoshi liendalo mbio sana kuelekea Ostende, tukavuka hadi Dover na kuwasili London asubuhi ya Septemba 16.

London ilikuwa mji mkuu wa dunia nzima siku hizo. Kwa kuacha waliofilisika wenye hali ya chini sana, maisha yalikuwa mazuri na ya kuburudisha na yaliendelea bila shida. Nilikuwa na bahati sana kupatiwa makazi kama mgeni wa kulipa na watu fulani waliothibitika kuwa wapole sana walionitendea kwa ukarimu na huba sikuzote. Niliazimu kusoma sheria, na muda si muda nikajiona niko kwetu isipokuwa nilikuwa mbali na wazazi. Nikawaandikia kila wiki na kujibiwa nao kila wiki. Pia nikamwandikia Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. kama kawaida naye akanipa heshima kwa kunirudishia majibu kwa upendo akiandika kwa mkono wake. Nikamwandikia chochote nilichokuta cha kuvutia bila kusita, naye akinijibu akadhihirisha moyo wa kupenda sana kile nilichomwandikia. Haikupita kitambo kirefu nikawa napenda kusafiri; nikapitisha likizo nje ya London, lakini kila nilipotaka kwenda nje nikapata ruhusa kwake. Katika barua zake akanisalimia kwa upendo. Wakati mwingine aliniandikia kwa kuniombea:

> “Mungu Akufanye uwe Zafarullah Kweli (yaani ufaulu kwa fadhili ya Mungu), au uongozwe na Mungu na uwe mwenye bahati njema.”

Barua yake ya Septemba 16, 1913 niliyoandikiwa imekwisha chapishwa. Naandika hapa tafsiri yake kama mfano:

> “Kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.
>
> Twamhimidia Yeye, na kumsalia Mjumbe Wake Mtukufu.
>
> *Assalamu alaikum wa rahmatullahi wa barakatuh.*
>
> Mfikishie maamkizi yangu ya upendo sana Muhammad Akbar Sahib: *Assalamu alaikum.* Haya ni maamkizi yenye baraka. Ni masikitiko kwamba Waislamu wa India hawayajali.

Kila safari yapaswa kuwa na shabaha, iwe ya kidunia au ya kidini. La sivyo, ni bure.

Mungu Aujalie msikiti katika Petersburg kuwa chanzo cha baraka.

Huko Finland nyakati za sala na saa za saumu zitapangwa kwa masaa. Mungu Amesema: Na mwezi Tumeupimia vituo (36:40). Hiyo ni kwa kuwaongoza waishio katika nchi za aina hiyo.

Fikiria sana, E Mpenzi, ya kwamba bajeti ya Kanisa la Uingereza yafikia pauni milioni ishirini na nne za Kiingereza. Kama wao hawauamini Ukristo, mbona wanatumia fedha nyingi sana hivyo kama maji?

Kwa nini nchi za Balkan, Italia na Ufaransa zilimwaga sana damu katika Uturuki, Tripoli na Moroko, kwa kupinga Islam, katika miaka miwili iliyopita?

Hoja haiisaidii itikadi ya Utatu, ambayo yaweza kumtuliza mtu mwenye akili. Kurudi nyuma kwa dini hiyo kunafungamana na Masihi Aliyeahidiwa a.s. Wafuasi wake ni watupu kwa undani wao, lakini wanasita kukubali Islam hadharani.

Unapaswa kukazania kueneza Umoja wa Mungu. Itatosha kuwafikishia wanafunzi wa Kipanjabi na wa Kihindi jina la Allah na la Mjumbe Wake.

Usilegee kusali, soma Kurani Tukufu kwa kawaida, na daima ufanye maombi.

Amekuwaje rafiki yako Mjerumani? Hukuandika yu hali gani. Nashangaa.

*Waslamu*

Nuruddin."

Khwaja Kamaluddin alikuwa mwanajumuiya maarufu wa Kiahmadiyya. Alikuwa mwanasheria. Alifanya kazi ya kuwa wakili kwa muda fulani mjini Peshawar na akahamia Lahore. Yeye mara nyingi alisema kwamba wakati fulani alipata kuvutika sana na Ukristo, lakini bahati yake njema ikamkutanisha na Masihi Aliyeahidiwa a.s., ambaye chini ya uongozi wake akaimarika imani yake katika Islam naye akawa Mwislamu mwaminifu. Masihi Aliyeahidiwa a.s. alipokuwa Lahore katika matembezi yake ya mwisho na alikuwa akikaa katika Ahmadiyya Buildings, Khwaja Kamaluddin akaona katika ndoto kwamba amekamatwa na polisi pamoja na Maulawii Muhammad Ali na Waahmadiyya wengine watatu au wanne. Wakaambiwa kwamba wana hatia ya uhalifu na watapelekwa mbele ya mfalme. Wakaongozwa kwenye ukumbi mmoja mkubwa ambamo katika sehemu yake ya mwisho Maulawii Nuruddin r.a. akakaa juu ya kiti cha kifalme kilichowekwa juu ya jukwaa chini ya kipaa. Yeye akawaambia: "Nyinyi mmefanya maasi dhidi yangu. Niwatendeje?" Khwaja Kamaluddin akajibu: "U mfalme sasa, waweza kututenda upendavyo." Hapo Maulawii Nuruddin r.a. akasema: "Mnahukumiwa kufukuzwa nchini"

Khwaja Kamaluddin akamweleza Masihi Aliyeahidiwa a.s. ndoto yake, ambaye akamsitisha akisema kwamba ndoto hiyo haitabiri msiba kwake. Halafu bwana huyo akamweleza Maulawii Nuruddin r.a. ndoto yake, ambaye akazama katika fikira kwa kitambo kidogo, kisha akamwonya asimweleze yeyote ndoto yake. Baada ya siku chache Masihi Aliyeahidiwa a.s. akafariki na Khwaja Kamaluddin akamwendea Maulawii Nuruddin r.a. na kasema: Wakati wa ndoto yangu kutimia umewadia. Niko tayari kufanya baiati kwako. Akaambiwa asubiri mpaka wajumbe wa Jumuiya wapate nafasi ya kukusanyika Qadian na kuweza kushauriana.

Halafu baada ya Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. kutangazwa kuwa *Khalifa* na kuchukua majukumu ya kazi yake tukufu, Khwaja Kamaluddin akaota tena ndoto hiyo, kwa tafauti hii kwamba safari hii Hadhrat Khalifatul Masihi, alivyokuwa sasa, akamhukumu akisema: "Umeasi mara ya pili. Naamuru ukatwe kichwa." Katika ndoto Bwana Khwaja akapelekwa pale penye kuuawa. Na shoka lililopigwa na mwenye kumkata kichwa lilipoanguka juu ya shingo yake akazinduka kwa hofu.

Mnamo mwaka 1912 mkewe Khwaja Kamaluddin alifariki; yeye akapatwa na huzuni ya kupita kiasi. Fikara zake zikaelekea zaidi kwenye dini na akafunga safari ndefu kwa shabaha ya kuhutubia juu ya Islam. Alipowasili Bombay, tajiri mmoja mwungwana wa Hyderabad Dakkan, aliyeelekezwa vyema kwenye Uahmadiyya, akamwomba kutekeleza kazi yake fulani ya siri iliyohusikana na mambo ya nyumbani na aende Uingereza kwa kuitimiza. Akaahidiwa ada kubwa. Kazi yenyewe ilihusikana kidogo na sheria, wala haikuwa na matata, basi hakuwa na haja abembelezwe kuikubali. Akawasili Uingereza karibu ya mwisho wa mwaka 1912. Baada ya kutimiza kazi yake hiyo akanuia kukaa Uingereza na kujitolea kwa kazi ya kuzagaza na kuhudumia Islam. Huko Uingereza wakati huo kulikuwa na Waahmadiyya watatu tu. Mmoja alikuwa anajifunza udaktari kule Newcastle, Dkt. Ibadullah alikuwa anashughulikia kozi ya masomo ya juu katika udaktari wa meno, na mimi nilikuwa nasoma sheria. Baada ya Khwaja Sahib kuwasili, Dkt, Ibadullah akajikalifu kumpatia makazi kwa kusumbuka na kutaabika sana katika nyumba alimoishi. Upande wake, Khwaja Sahib akaazimu kuishi kikawaida, hakujali kupata chakula kizuri, nguo nzuri na kadhalika. Lakini haukupita muda mrefu, chumba chenye kufaa kikapatikana katika nyumba nilimoishi, naye akahamia humo. Hivyo, tukashirikiana sana kwa muda wote aliokaa nasi, nami nikapata kumjua vizuri sana. Siku hizo

akafikiria kuanzisha jarida la kila mwezi aliloliita *"Muslim India and Islamic Review".* Baadaye "Muslim India" ikaachwa katika jina lake na likaendelea kutolewa kwa miaka mingi kwa jina *"Islamic Review."* Maongezi yetu kwa kawaida yakawa kuhusu Islam na Uahmadiyya ambamo Khwaja Sahib akatangulia. Hivyo nikapata ujuzi wa mambo fulani ambao nisingeupata bila kuongea naye.

Safari moja, kwa mfano, akasema: "Maulawii akifa, (mara nyingi akasema Maulawii kwa ukunjufu na huba akimaanisha Hadhrat Khalifatul Masihi r.a.) hakuna budi matatizo kutokea kuhusu kumteua atakayekuwa *Khalifa* mahali pake. Hebu tuone sasa. Yupo Mahmud, (akimaanisha Sahibzada Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad r.a.) lakini yu kijana tu mdogo; na yupo Muhammad Ali, yeye si mvumilivu hata kidogo, huanza kupiga kelele juu ya kila jambo dogo. Ama mimi, nashindwa kujizuia kufoka kweli, ikifaa, isipofaa."

Kwa bahati mbaya, nilivyojua habari zake, wakati mwingine nikapenda anihakikishie kweli anaudhika sana. Lakini nikafikiri kwamba pengine anachukua maana fulani ya ukweli iliyo tofauti na ile yangu. Kuhusu swala la *Khalifa* baada ya kufariki Khalifatul Masihi wa kwanza, nikamkumbusha kwamba ni jambo ambalo haujafikia wakati wake, tena halina haja ya kujadiliwa. Hadhrat Khalifatul Masihi amekariri kuhakikisha kwamba wakati ukiwadia Mungu Mwenyewe Ataamua na kumfanya *Khalifa*.

Safari moja Khwaja Sahib alisumbuka sana mno kwa kushuhudia mandhari fulani iliyomkumbusha ndoto yake ambamo akaota yuko tayari kukatwa kichwa. Alikuwa na uchungu mkubwa wa kutisha hata kwamba bila kujua sababu yake nikahuzunika. Baada ya kitambo alipopata kutulia, akanieleza ndoto zake.

Dkt. Henry Leitner, mtaalamu wa elumu ya nchi za mashariki, alikuwa Mwalimu Mkuu wa Oriental College, Lahore, mnamo miaka

ya mwisho ya karne ya kumi na tisa. Kwa kutumaini kustaafu akapanga mpango wa kuanzisha Idara ya Elimu ya Nchi za Mashariki katika au karibu ya London, na akawaendea watawala Waislamu wa maeneo mbalimbali ya India ili waichangie hiyo idara. Miongoni mwa waliotoa michango mikubwa walikuwepo Mtukufu Begum wa Bhopal, mtu mwenye cheo cha kwanza na Waziri Mkuu wa Hyderabad, Nawab Sir Salar Jang. Akirejea Uingereza, Dkt. Leitner akachagua na kununua eneo kubwa la ardhi karibu ya Woking, katika Surrey, kwa mpango wake na akaanzisha ile Idara ya Elimu ya Nchi za Mashariki katika eneo hilo, na pia akajenga msikiti mdogo na nyumba katika sehemu ya eneo hilo. Msikiti ukaitwa Shah Jahan Mosque kwa jina la Begum wa Bhopal, na nyumba ikaitwa Sir Slaar Jang Memorial House. Woking iko umbali wa maili ishirini na nne kutoka London. Kwa kuwa huko Woking wala karibu yake hawakuwepo Waislamu, sala hazikusaliwa katika msikiti huo na ukawa kama nyumba ya makumbusho, au kitu cha sanaa ya ujenzi kwa wanye kuzuru.

Dkt. Leitner alipofariki, mali hiyo yote ikamilikiwa na watu wa familia yake na ikaja chini ya usimamizi wao. Karibu wakati huo, Seyyid Amir Ali, Jaji wa Korti Kuu ya Calcutta, Mwislamu mwenye moyo wa kufadhili watu kuliko nafasi yake na mtaalamu mashuhuri, aliyejulikana kwa vitabu vizuri alivyotunga, *The Spirit of Islam and History of Saracens,* akafanywa kuwa mwanakamati wa kamati ya wanasheria ya Baraza la Mtukufu Mfalme, na akaanza kukaa London. Mwislamu mwingine mashuhuri katika London wakati huo alikuwa Mirza Abbas Ali Beig aliyekuwa mshauri mmojawapo wa Baraza la washauri la Katibu wa Utawala kwa India. Hao wawili baada ya kushauriana wakapendekeza kwa watu wa familia ya marehemu Dkt. Leitner ya kwamba kwa kuwa Idara hiyo na majengo yaliyoihusu pamwe na Shah Jahan Mosque na Sir Salar Jang Memorial House, vilijengwa na kuanzishwa kwa fedha za Waislamu, basi hivyo kwa

kweli ni mali ya ushirika ambayo yapaswa kusimamiwa na kutawaliwa kama mali ya watu, na Waislamu au kwa niaba ya Waislamu.

Hilo halikukubaliwa na familia ya Leitner, waliodai mali yote kuwa yao binafsi. Jambo hilo likakabidhiwa kwa wanasheria, na baada ya kushauriana kirefu ikakubuliwa kwamba msikiti na Memorial House na eneo la kuzunguka wakabidhiwe Waislamu, na wakina Leitner wanaweza kubakiwa na Idara pamoja na eneo kubwa linalohusikana nayo. Hapo ndipo Khwaja Kamaludddin akaonana na Mheshimiwa Seyyid Amir Ali na kupendekeza kwamba Shah Jahan Mosque na Memorial House aweza kukabidhiwa yeye; hapo atakaa katika Memorial House na atasimamia sala tano za kila siku zisaliwe kama kawaida. Seyyid Amir Ali akashauriana na Mirza Abbas Ali Beig na Waislamu wengine katika London, na pendekezo la Khwaja Sahib likakubaliwa. Ushirika wa Msikiti wa Woking ukafanywa na Bwana Khwaja akaenda kukaa katika Memorial House na kushika usimamizi wa msikiti, lakini sala ya Ijumaa ikasaliwa katika ukumbi fulani uliopangwa kwa shabaha hiyo huko Notting Hill Gate, London, na sala ya Ijumaa ikaongozwa na Khwaja Kamaluddin, aliyewasili kutoka Woking kwa shughuli hiyo.

Wajibu wake kuhusu usimamizi wa msikiti na kutoa jarida la *Islamic Review* ikawa kazi ambayo Bwana Khwaja akaona shida kutekeleza ipasavyo akiwa peke yake. Akamwomba Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. msaada, ambaye akamtuma Chauhdri Fateh Muhammad Sial r.a., M.A., kijana Mwahmadiyya mwaminifu aliyejitolea mhanga, mnamo kiangazi cha mwaka 1913, ili kumsaidia. Bwana Khwaja akafanya mpango kwamba Sheikh Nur Ahmad, mtu mwema sana lakini mzee kidogo, aliyekuwa karani wake kwa kazi ya uwakili katika Lahore, aweze kusafiri pamoja na Bwana Sial r.a., ili kuangalia mambo ya Bwana Khwaja ya binafsi.

Maisha yangu huko Uingereza yaliendelea vizuri. Ombi moja aliloniagiza Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. kuomba lilikuwa: Mola, nijalie rafiki mwema. Hilo likaleta tunda katika muda wa wiki nane baada ya mimi kuwasili London. Kwa bahati njema nikapata kuonana na mwanafunzi mmoja Mjerumani mwenye umri kama mimi aliyewasili London kwa masomo ya uhandisi na akaingia katika King's College, ambako mimi niliingia kwa ajili ya masomo ya Sheria. Huyo bwana alitokana na familia ya ukoo wa waungwana wa Pomerania. Babake alikuwa mjumbe wa serikali lakini sasa alikuwa amestaafu na akawa anaishi Brussels ambako alikuwa na shughuli kubwa za viwanda. Mamake alikuwa Mfaransa. Upesi tukawa marafiki sana; akathibitika kuwa ndugu kweli kwangu. Ndiye yule rafiki Mjerumani aliyetajwa mwishoni mwa barua ya Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. ya Septemba 16, 1913. Urafiki wetu ukadumu maisha yake mazima. Alipigana upande wa Ujerumani katika Vita Vikuu Vya Kwanza, alijeruhiwa mara mbili, alipata nishani ya Iron Cross na akafanywa Knight of Hohenzollern. Baada ya vita tukaanza tena kuandikiana. Alipoteza kila kitu lakini akaendelea kishujaa. Akaenda Uingereza mnamo 1924 na akakaa London. Mara nyingi tulipata kuonana London, naye akatutembelea mara nyingi huko India.

Pindi nilipokuwa Uingereza kama mwanafunzi, barua za Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. zilikuwa chanzo cha kunifariji sana na kunichangamsha mno. Mara nyingi nilihisi kusaidiwa kidhahiri kwa sababu ya yeye kuniombea. Mwanzoni mwa Machi 1914 nikapata idhini yake ya kwenda bara katika likizo za Pasaka. Kabla sijaondoka habari ya kuhuzunisha sana ya kifo chake ikapokelewa kwa njia ya Khwaja Kamaluddin. Nilipomwendea kwa maelezo akaniambia:

> "Hali yenyewe ni ya kutia wasiwasi. Sijui sana. Nimepokea simu tatu fupi sana za maandishi. Ya kwanza iliarifu kufariki

> kwa Maulawii Sahib. Ya pili ikasema kwamba Mian Mahmud ametangazwa kuwa *Khalifa*. Ya tatu ikasema kwamba kulitokea mafarakano na waliotengana wakaitwa waasi. Sielewi nisemeje kwa hayo yote!"

Siku hizo barua kutoka Panjab zilikuwa zinawasili London baada ya siku kumi na tano. Nikafadhaika sana, na nikafahamu kikamilifu lakini ikashindikana kufanya chochote. Nikaenda likizo zangu kwa moyo wa kusumbuka na mashaka, lakini kwa kufanya maombi. Niliporudi baada ya wiki tatu nikakuta barua chunguchungu zaningojea. Barua ya mama yangu ikasema ya kwamba Jumuiya imepatwa na msiba mkubwa sana. Kulitokea mafarakano ya kusikitisha. Hadhrat Sahibzada Mirza Bashiruddin ndiye *Khalifa* wa haki. Mimi nimekwisha fanya baiati yake, nawe ufanye hivyo mara moja. Babangu akaandika kwamba hili ni swala linalohusu dhamiri, na kwamba yeye hataniagiza lolote. Napaswa kujiamulia mwenyewe baada ya kutafakari sana na kuomba dua kwa bidii kwa kupata mwongozo. Usomaji wa haraka wa barua zangu nyinginezo ukanihakikishia kwamba kiini cha hitilafu ni kuwepo au kutokuwepo kwa Imam wa kiroho wa Jumuiya mwenye madaraka ya juu kabisa. Kuhusu swala hilo moyo wangu ulikuwa mweupe; sikuwa na wasiwasi hata kidogo. Barua zilikuwa ziende jioni hiyo hiyo. Nikashika kalamu na kumwandikia Hadhrat Khalifatul Masihi wa pili barua ya kufanya baiati. Pia nikaandika nyumbani kuwaarifu wazazi wangu habari hiyo.

# XVIII

# MANDHARI YA MWISHO

Afya ya Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. ilianza kuharibika mwanzoni mwa Januari 1914. Alihisi maumivu katika mbavu, mara kwa mara alipata homa na kichefuchefu. Akaanza kudhoofika, lakini alikuwa mchangamfu na akaendelea kutoa darasa la Kurani Tukufu kila siku. Alipoona shida kupanda ngazi za Masjid Aqsa, akatoa darasa katika uwanja wa Madrasa Ahmadiyya, lakini alitakiwa kusaidiwa kutembea umbali kidogo hadi Madrasa, kwenda na kurudi. Udhaifu wake ukazidi na darasa likahamishwa katika chumba kimoja katika nyumba ya mwanaye mkubwa, iliyo jirani na nyumba yake mwenyewe, na akatoa darasa akiketi. Madaktari wake wakamshauri kuacha kutoa darasa, lakini akakazania kwamba maadamu anaweza kusema, hana budi kuendelea kufafanua Neno la Mungu.

Mwanzoni mwa Februari ikafikiriwa ya kwamba yeye anaugua kifua kikuu. Dkt. Mirza Yakub Beig akawasili kutoka Lahore na pamoja na Dkt. Khalifa Rashiduddin akajitolea kumwangalia mgonjwa mtukufu ambaye kidogo kidogo akawa dhaifu, sauti yake ikawa ndogo, akala chakula kidogo sana. Tarehe 14 Februari, Col. Melville akatumwa kutoka Lahore. Akawasili pamoja na Dkt. Seyyid Muhammad Husain na akamchunguza kikamilifu, matokeo yake akahakikisha usawa wa uchunguzi wa madaktari waliokuwa wakimtibu, akakubali dawa waliyotoa na akapendekeza chakula kiongezwe. Baada ya yeye kuondoka, Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akanena:

> "Daktari kutoka Lahore alichukua muda mwingi kunichunguza. Ugonjwa ninaougua ni rahisi sana kuchunguzwa kiasi hiki

> kwamba ninaposhughulika katika zahanati yangu na mtu anapoingia mlangoni na kuniamkia, mimi natambua kwa sauti yake pasipo kumtazama kwamba anaugua maradhi haya."

Kwa kuona udhaifu wake unaendelea kuzidi, madaktari wake wakaamua kwamba ahamishiwe kwenye nyumba ya Nawab Muhammad Ali Khan r.a., iliyokuwa katika bustani kubwa nje ya mji na ambako atakuwa na raha zaidi. Nawab Sahib alipenda sana kumkaribisha na mara mbili akamwomba pia. Hatimaye akatoa kibali chake na akahamia huko mnamo Februari 26.

Mwanzoni mwa Machi, Dkt. Seyyid Muhammad Husain alimtembelea Hadhrat Khalifatul Masihi r.a., na katika maongezi akasisitiza uzuri wa kushirikiana na madhehabu mbalimbali ya Waislamu kutafuta shabaha zilizo sawa baina yetu; hapo Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akasema:

> "Tumeweka mfano wa ushirikiano wa aina hii kuhusu habari ya kuanzisha Chuo Kikuu cha Waislamu. Ushirikiano wa aina hii unafaa, lakini ni muhimu kabisa kudumisha umoja wetu wazi wazi. Maendeleo huongezeka kwa sababu ya kupambanuka. Kuchangamana kwa jumla huharibu nguvu ya kuchukua hatua na kuzuia maendeleo. Tena hatuwezi kujiweka chini ya waliokataa Mwanzilishi wetu aliyetumwa na Mungu. Na kipambanuzi kisipodumishwa, kuamrisha mema na kukataza maovu hakuwezi kutunzwa. Kundi moja linapopambanuka, upinzani hupatikana; na jinsi upinzani unavyozidi, wale waliopambanuka hukimbilia kuomba dua na kutia bidii nyingi zaidi. Shida huhimiza kutia bidii, kujitahidi na kufanya maombi. Mtu anayeafikiana na kila kitu hafaulu kupata kitu."

Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akaandika wasia wake kwa mkono

wake mwenyewe mnamo Machi 4, ambao ni huu ufuatao:

> "Kwa jina la Mungu, Mwingi wa rehema, Mwingi wa ukarimu.
>
> Twamhimidia Yeye na kumsalia Mjumbe Wake Mtukufu.
>
> Mnyenyekevu huyu, akiwa mwenye akili timamu, anahakikisha: Hakuna mwabudiwa isipokuwa Mungu; Muhammad s.a.w. ni Mjumbe wa Mungu. Watoto wangu bado ni wadogo, nami sina mali. Mungu Atawahami. Wasipewe kutoka katika mfuko wa mayatima ama maskini. Waweza kupatiwa karadha njema itakayolipwa na baadhi ya wanangu wenye uwezo. Vitabu vyangu na milki yangu ifanywe Trust (Amana) kuwanufaisha watoto wangu. *Khalifa* baada yangu awe yule aliye mwema, apendwaye na watu, mtaalamu na mwenye mienendo mizuri. Asamehe makosa na awavumilie marafiki wa zamani na wapya wa Hadhrat Sahib a.s. Jinsi nilivyokuwa mwenye kuwatakia heri wote, ndivyo anavyotakiwa kuwa yeye. Darasa la Kurani Tukufu na la Hadithi liendelee.
>
> *Wassalamu*.
> Nuruddin. Machi 4, 1914."

Akampa Maulawii Muhammad Ali wasia huo na kumwambia awasomee waliopo. Akaagiza kusomwa mara ya pili na mara ya tatu, kisha akauliza kama jambo lolote limebakia; akajibu Maulawii Muhammad Ali kwamba huo ni sawasawa. Halafu akaukabidhi kwa Nawab Muhammad Ali Khan r.a. kuuhifadhi.

Udhaifu ulivyoendelea kuzidi wa Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. ukazusha fikira kwamba itakuwaje akifariki. Fikira hiyo ikafichua

hitilafu kubwa zilizotoa ishara ya fitina na mafarakano. Katika hali hiyo Sahibzada Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad akaandika tangazo kwamba kueleza hitilafu ambapo Hadhrat Khalifatul Masihi angekuwa na afya njema isingeleta uharibifu mkubwa, kwani yeye angeweza kuizuia na kuiweza. Lakini sasa kwa kuwa yu mgonjwa sana, mabishano hayo yanaweza kusababisha taabu, kwa hiyo mabishano ya aina hii yaachwe kwa muda mpaka Mungu Amjaalie afya kamilifu. Mwandiko huo wa tangazo akampelekea Maulawii Muhammad Ali na akapendekeza kwamba hilo laweza kuchapishwa kwa sahihi zao za pamoja. Lakini Bwana huyo akakinza na kusema kwamba njia nzuri itakuwa kuitisha kikao na sisi wawili tukihutubie namna tupendavyo. Basi kikao kikaitishwa katika Masjid Nur na Maulawii Muhammad Ali akamwomba Sahibzada Sahib kusema kwanza. Hapo yeye akaeleza aliyokuwa ameandika katika tangazo. Halafu Maulawii Muhammad Ali akazungumza, na akawakaripia vikali wale waliomlaumu Khwaja Kamaluddin na wenzake waliofikiria kama yeye. Akasikilizwa kwa kimya chenye uchungu. Mwishowe akaongeza maneno machache kwa sauti kali kuhusu haja ya kuwa na upatano. Hotuba yake ikazidisha udhia uliokuwapo mapema.

Sahibzada Sahib akaendelea kushughulikia maombi na dua, na akawahimiza marafiki zake kufanya hivyo. Yeye hakujali sana hitiliafu za rai kuliko kulinda umoja wa Jumuiya ambao aliuthamini zaidi sana. Akaongea na wanajumuiya wengi wenye kuathiri na akagundua kwamba waliokuwa na maoni ya kuwepo kwa *Ukhalifa* na wakauamini unabii wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. hawawezi kufanya baiati ya yule azipingaye itikadi hizo, kwani hiyo itamaanisha Uahmadiyya kukoma. Lakini akaamini kwamba umoja una thamani zaidi wala usitupiliwe mbali kwa ajili ya watu fulani. Akaanza kuwasisitizia marafiki zake ya kwamba kama baada ya kufariki Hadhrat Khalifatul Masihi ikitokea hatari ya mafarakano, wapaswa kujiweka tayari kufanya baiati ya

mmojawapo wa kundi la watu wachache, kwani wao hawatamkubali asilani yule anayehitilafiana naye na Jumuiya itafarakana. Lakini yeye akifanya baiati ya mmojawapo kati ya hao, marafiki zake watafuata mfano wake na umoja wa Jumuiya utahifadhiwa. Jioni moja akatumia masaa mawili kumsisitizia Maulawii Seyyid Muhammad Sarwar Shah r.a., Sheikh mmojawapo wa mstari wa mbele wa Jumuiya, kukubali maoni yake kwamba hitilafu ikitokea kuhusu nani awe *Khalifa*, watakuwa tayari kufanya baiati ya mmojawapo wa kundi la watu wachache. Ama kuhusu mambo ya hitilafu, ni hivi kwamba maadamu *Khalifa* hatoi maagizo kuhusu hayo, watakuwa na uhuru wa kufuata na kuendelea kuamini wanayofikiria ni sawa na kweli. Na kama *Khalifa* akitoa agizo kuyahusu hayo, watalazimika kumtii na kukaa kimya, wakimwachia Mungu swala hilo mkononi Mwake, Ambaye ndiye Mlinzi wa kweli wa Jumuiya.

Katika siku za mwisho za ugonjwa wa Hadhrat Khalifatul Masihi r.a., Pir Iftikhar Ahmad r.a. akamwambia ya kwamba *Masufii* wanaamini kwamba maisha ya *Sufii* ni baraka kwa ajili yake mwenyewe na pia kwa wengineo, na akamsisitizia ajiombee kwa kupata afya. Akajibu: Nasikia daima: "Sivyo! Bali nyinyi mnapenda maisha ya sasa, na mnaacha maisha ya Akhera (75:21-22)." Hayo yalikumbusha majibu aliyotoa Hadhrat Abu Bakr r.a. kwa pendekezo la aina hiyo alipokuwa katika hali kama hiyo. Alisema: "Nimeomba na nimepokea jawabu: Najua vizuri zaidi. Nitafanya nitakavyopenda."

Kabla ya saa sita za mchana, siku ya ijumaa, Machi 13, Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akamwita mwanaye mkubwa, Mian Abdul Hai na kumwambia:

> "Siku zote nimeamini: Hakuna mwabudiwa isipokuwa Mungu, nami nafa nikiamini hiyo. Nawaheshimu masahaba wote wa Mtume Mtukufu s.a.w. Baada ya Kurani Tukufu naona kitabu

cha *Bukhari* cha Hadithi za Mtume s.a.w. chakubalika zaidi kwa Mungu. Namwamini Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s. kuwa Masihi Aliyeahidiwa na Mteule wa Mungu. Nilimpenda sana hata kwamba niliwapenda watoto wake zaidi kuliko wewe. Nakutupa kwa Mungu Mtukufu, nami nina yakini ya kwamba hatakuacha uangamie. Nakusihi kusoma Kitabu cha Mungu, kukifundisha na kutenda sawa nacho. Nimejionea vitu vingi sana, lakini sijaona kitu kama Kurani. Pasipo shaka yoyote, hicho ni Kitabu Chake Mungu Mwenyewe. Kwa mengine nakuacha mkononi mwa Mungu."

Saa za sala ya Ijumaa zikawadia, na kwa kuacha wahudumu wawili au watatu, wengine wote wakaenda Masjid Aqsa kusali. Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akafanya *Tayammamu* na kusali. Alipomaliza tu kusali, kupumua kukawa taabu na katika dakika chache roho yake ikaaga mwili wake dhaifu kwenda kupumzika milele. Sisi ni wa Mwenyezi Mungu na Kwake tutarejea.

Habari hii ya msiba mkubwa ilipofika msikitini, Masjid Aqsa, ambapo sala ya Ijumaa iliyokuwa inaongozwa na Sahibzada Mirza Bashiruddin Mahmud Ahmad ilikwisha tu, kila mmoja akakimbilia nyumba ya Nawab Muhammad Ali Khan r.a. ili kuona uso uliopendwa wa yule ambaye kila dakika yake ilikuwa imetolewa wakfu kusogeza mbele miradi ya ustawi wa kiroho na wa kimwili. Kwa hiyo watu wengi sana wakashiriki katika sala ya alasiri katika Masjid Nur, msikiti uliokuwa karibu zaidi na nyumba ya Nawab Muhammad Ali Khan r.a. Baada ya sala, Sahibzada Mriza Mahmud Ahmad r.a. akawahutubia kama ifuatavyo:

"Sawa na matakwa ya Mungu, Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. amefariki. Mungu Amrehemu na kumbariki sana, na kumnyanyuakwenyemadarajayajuukabisanakumwunganisha

na Mtume Mtukufu s.a.w. na Masihi Aliyeahidiwa a.s. ambao alijitolea kwao na kujaa mapenzi yao.

Sasa wanajumuiya wa Jumuiya Ahmadiyya wana wajibu mzito sana. Jumuiya nzima inakabili jaribio. Yule atakayefaulu katika mtihani huu atajinyakulia kibali na huba ya Mungu; na atakayefeli katika mtihani huu hatahesabiwa mwema mbele yake. Hatuna budi kujitayarisha kikamilifu kupita katika mtihani huu. Zingatieni vizuri kwamba mpango mzuri kabisa hugeuka kuwa chanzo cha hatari ikiwa nia inayouongoza si safi. Sala ndiyo njia njema mno ya kupata usafi, hata hivyo ikanenwa: 'Basi ole kwa wanaosali, ambao wanapuuza sala zao, ambao hufanya ili waonwe" (107:5-7). Hivyo, sala iliyoongozwa na nia mbovu haiwi njia ya kupata usafi na ukaribu wa Mungu, bali huwa laana.

Twasihiwa kutafuta kinga ya Mungu dhidi ya Shetani kabla ya kusoma Kurani Tukufu, na kila sura inaanza kwa Jina la Mungu, na hii ndiyo njia ya kupata msaada wa Mungu. Hili ni dokezo ya kwamba kabla ya kuanza jambo zuri kabisa kama usomaji wa Kurani Tukufu, mtu hana budi kujikinga kwa Mungu katika shaka na wasiwasi wa Shetani, na kutafuta msaada wa Mungu ili kujaaliwa uwezo na nguvu ya kutekeleza kazi kubwa ya usomaji wa Kurani. Watu wengi hupata rehema ya Mungu na baraka Zake kutokana na aya moja pekee ya Kurani Tukufu, na aya hiyo hiyo yawa chanzo cha maangamio kwa wengi. Ndiyo sababu imeamriwa kujikinga kwa Mungu. Kwa kifupi, mpango hata ukiwa mzuri namna gani, lakini kama haukupendekezwa kwa uaminifu na nia safi, kuna hatari ya kwamba mpango huu utapeleka mbali na Mungu.

Hatuwezi kutekeleza wajibu mzito tuliotwishwa saa hizi

pasipo rehema ya Mungu na kujaaliwa uwezo naye. Hivyo, nawasihi kutumia wakati wote mlio nao katika kuomba: E Mola, Tuongoze njia ya haki ili tulindwe katika maangamio na tukusogelee karibu zaidi. Huu ni wajibu mkubwa usioweza kutekelezwa bila msaada wa Mungu. Kazanieni dua hii: Utuongoze njia iliyonyoka (1:6). Hatuelewi itabainika nini kesho au kesho kutwa. Yote hiyo imefichikana tumboni mwa wakati ujao, nasi tusipoongozwa na kusaidiwa na Mjuzi wa mambo ya ghaibu tutajitia katika hatari ya kuangamia. Kwa hiyo, ombeni dua, ombeni kusamehewa na kukingwa dhidi ya kufanya kosa, ombeni kuongozwa na kumsalia Mtume Mtukufu s.a.w. Ombeni kwa uchungu: Mola, tusaidie kupita katika mtihani huu kwa huruma Yako. Masihi Wako alitokea, na wengi wakamkana na wakajikwaa na kuanguka juu ya mwamba huo na kujiangamiza; lakini wewe Ukatuongoza kwa huruma Yako. Alipofariki tukakabili jaribio, nawe Ukatuongoza tena. Sasa twakabili jaribio mara nyingine. Utujaalie tena rehema Yako na Utuongoze, na Ututilie baraka katika mambo yetu, wala Usiwafanye maadui zetu kufurahia kushindwa kwetu, na Umchague mtukufu kati yetu kwa huduma Yako. Amin.

Kila mmoja ashughulikie maombi wakati wote. Amkeni usiku kumuomba Mungu. Mungu Hutatua matatizo yote kwa rehema Yake. Mtegemeeni Mungu. Ahadi Zake zote ni za kweli. Ahadi Alizomwahidi Masihi Aliyeahidiwa zimetimia na zinaendelea kutimia. Binadamu aweza kufanya ahadi ya uwongo, lakini ahadi za Mungu ni za haki, naye Yu Mwaminifu kwa ahadi Zake. Mwalazimika kumtawakali na kumtegemea Yeye. Sasa nitaomba, nanyi mwungane nami katika maombi yangu, na halafu mwendelee na maombi yenu.”

Akainua mikono yake kwa maombi ya kimya, na wote waliokuwapo msikitini nao wakafanya hivyo. Kila mmoja akajawa na maono na mara moja msikiti ukawa nyumba ya vilio. Maombi yakaendelea kwa muda na yalipomalizika nyoyo zikawa zimetulia. Sahibzada Sahib akasisitiza kwamba awezaye afunge saumu kesho. Kisha akaondoka kwenda nyumbani kwa Nawab Muhammad Ali Khan r.a. Lakini hakuwa na utulivu na akapenda kuomba dua katika upweke. Akaenda huku akimwomba Maulawii Seyyid Muhammad Sarwar Shah r.a. awe macho ili mtu yeyote asimfuate kwani ataka kuwa katika upweke. Alikuwa akipita bustanini haraka haraka ambapo Maulawii Muhammad Ali akapata kumwona kutoka mbali na kumjia upesi pamwe na marafiki zake na kumshughulisha katika maongezi. Wakaendelea kutembea juu chini wakiongea kwa bidii hadi adhana ya sala ya magharibi ikatolewa.

Baadaye Sahibzada Sahib r.a. akaeleza kwa kifupi maongezi hayo kama ifuatavyo:

Maulawii Muhammad Ali:

> "Mambo yote huamuliwa vizuri katika kushauriana. Baada ya Hadhrat Khalifatul Masih r.a. kwisha kufariki lolote lisiamuliwe kwa haraka. Kupatikane kushauriana kikamilifu."

Sahibzada Sahib r.a.:

> "Haraka haifai, na hakuna budi kushauriana. Watu wengi wanaendelea kuwasili na mpaka kesho idadi kubwa itakuwa imefika. Wanajumuiya waongozi wanaishi karibu sana, watawasili hadi kesho. Kushauriana kwawezekana baada ya hao kufika."

Maulawii Muhammad Ali:

"Haraka hiyo haipendezi. Kwa kuwa zipo hitilafu, uamuzi ufanywe kwa umoja baada ya kujadiliana kikamilifu. Yafaa Jumuiya nzima ifikirie jambo hili kwa miezi minne au mitano. Kisha kupatikane kubadilishana maoni ndipo uamuzi wowote utakaofanywa utekelezwe."

Sahibzada Sahib r.a.:

"Swali la kwanza ni: Kuna hitilafu zipi? Swali la pili ni: Kama katika muda huo kutokee uchafuzi katika Jumuiya, nani atakuwa mwenye madaraka pasipokuwa Kiongozi? Watu waliojumuika alipofariki Masihi Aliyealhidiwa a.s. walishauriana mara moja na kuamua. Njia hii ilifuatwa hata katika nyakati zilizopita. Kulikuwa hamna muda wa miezi sita kungoja kabla ya ujaji wa Masihi Aliyeahidiwa a.s. au baadaye."

Maulawii Muhammad Ali:

"Zamani hitilafu hazikuwepo, sasa hitilafu zipo. Tena, kuna shida gani katika kungoja kwa muda fulani? Kuna nini *Khalifa* anayolazimika kufanya kesho?"

Sahibzada Sahib:

"Alipofariki Masihi Aliyeahidiwa a.s., Jumuiya iliamua kwamba *Ukhalifa* uwepo katika Jumuiya. Haina haja ya kushauriana juu ya swala hili tena, wala haliwezi kuletwa sasa. Kushauriana kwaweza tu kuhusu nani apaswa kuwa *Khalifa*? Ama swali lako kwamba: Ni nini anayolazimika *Khalifa* kufanya kesho? Jibu lake ni kwamba zaidi ya kuangalia hali ya kiroho, ni kazi ya *Khalifa*, kuweka Jumuiya katika hali ya umoja na kuilinda dhidi ya machafuko, na utekelezaji wa kazi hiyo si kitu cha kuonekana ili nikutolee

mifano. *Khalifa* hana budi kuipatia Jumuiya malezi ya kiroho na kudumisha nidhamu. Malezi ya kiroho si kitendo cha kiwiliwili kinachoweza kuonyeshwa, wala machafuko hayana wakati maalum hata isemwe hayawezi kutokea kabla ya tarehe fulani. Yawezekana kesho litokee jambo fulani linalohitaji mwenye kuongoza. Hivyo, achilia mbali swali hili kwamba *Khalifa* awepo ama hapana. Kushauriana kwaweza kufanyika kwamba nani atakuwa *Khalifa*."

Maulawii Muhammad Ali:

"Sasa hili lazusha tatizo. Kwa sababu kuna hitilfafu katika itikadi, basi kutakuwa hitilafu katika uchaguzi wa mtu. Hatuwezi kufanya baiati ya mtu tunayehitilafiana naye katika itikadi."

Sahibzada Sahib r.a.:

"Nielewavyo mimi, hitilafu haiendi mbali sana mpaka iwe kizuizi kufanya baiati ya mtu wa upande mmoja au wa pili. Kwa vyoyote tuko tayari kufanya baiati ya mmojawapo miongoni mwa kundi lako."

Maulawii Muhammad Ali:

"Hii ni ngumu. Wapaswa kutafakari zaidi na kushauriana nyinyi kwa nyinyi, na kesho tukutane tena."

Kwa kufuata pendekezo hilo la Maulawii Muhammad Ali, Sahibzada Sahib akaorodhesha majina sitini na akamwomba Maulawii Seyyid Muhammad Sarwar Shah r.a. awaite hao ndugu ili kuhudhuria katika mkutano usiku huo kwa kushauriana. Baada ya kushauriana, wote wakakubali kwamba kabla hajazikwa Hadhrat Khalifatul Masihi r.a., *Khalifa* mwenye madaraka kamili achaguliwe ambaye atapanga

mazishi. Pia ikakubaliwa ya kwamba usiku huo maombi yafanywe ili Mungu kwa fadhili Zake Aridhie kuidumisha Jumuiya katika njia iliyonyoka na kuijaalia kukanyaga njia za radhi Yake, na kwamba kesho wote wafunge saumu na maombi maalumu yaendelee.

Keshoye, saa za adhuhuri Wanajumuiya zaidi ya elfu moja walikuwa wamewasili Qadian kutoka nje. Sahibzada Sahib r.a. akashauriana na watu wa familia yake kuhusu hali iliyozuka. Baadhi yao walikuwa na maoni ya kuendelea kueneza itikazi walizoamini kuwa sawa, na kwa shabaha hii wakahisi kwamba hakuna budi *Khalifa* kuwa yule anayeafikiana nao katika itikadi hizo. Lakini Sahibzada Sahib akasisitiza kwamba kuhifadhi umoja wa Jumuiya ni muhimu kabisa. Katika rai yake, uchaguzi wa *Khalifa* ni wajibu wa kidini. Kama hii ikubaliwe, basi njia ifaayo sana ni kumchagua *Khalifa* kwa kupigwa kura na wale waliopo. Kama hiyo haikubaliki, wote waafikiane kumteua mtu baki. Kama hiyo nayo ikishindikana baiati yaweza kufanywa kwa yule anayekubaliwa na kundi la pili au mmojawapo miongoni mwao. Hatimaye watu wote wa familia yake wakakubaliana na pendekezo lake.

Hapo ndipo ujumbe ukapokelewa kutoka kwa Maulawii Muhammad Ali ya kwamba anataka kuendelea na maongezi ya jana. Akaombwa afike hapo. Akawasili pamwe na baadhi ya marafiki zake. Wakati huo, Sahibzda Sahib r.a. alikuwa na Maulawii Muhammad Ahsan r.a., Nawab Muhammad Ali Khan r.a. na Dkt. Khalifa Rashiduddin r.a. pamoja naye. Maongezi yakashika njia ili ile ya jana. Yakazuka pia mabishano kuhusu hitilafu za itikadi baina ya Maulawii Seyyid Muhammad Ahsan r.a. na Maulawii Muhammad Ali, lakini Sahibzada Sahib r.a. akayakomesha, na akamwuliza Maulawii Muhammad Ali itakuwaje ikiwa mwafaka unashindikana baada ya kupita kipindi kirefu asemacho? Kama hapo uamuzi utafanywa na

watu wengi, kwa nini watu wengi hawawezi kuamua sasa?

Huko nyuma watu wakajumuika katika Masjid Nur, nao walikuwa na mahangaiko. Ikaonekana kwamba baada ya Machi 4, Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. alipoandika wasia na akafanya usomwe na Maulawii Muhammad Ali mara tatu, ambamo alikuwa ameandika kwamba *Khalifa* ajaye hana budi kuwa na sifa fulani ndani yake, Maulawii Muhammad Ali akatayarisha kijitabu ambamo haja ya *Khalifa*, inavyofahamika kikawaida, ikapuuziliwa mbali. Kijitabu hicho kilipigwa chapa na nakala zake zikatumwa kwa marafiki zake pamoja na maagizo ya kuzizagaza mara habari ya kifo cha Hadhrat Khalifatul Masihi ikipokelewa. Kila mmoja aliyewasili Qadian baada ya kupata habari yenye kuhuzunisha sana ya kufariki kwa Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. alikuwa amepatiwa nakala yake safarini. Watu wengi sana wakakasirikia propaganda hiyo mbovu na ya ovyo. Na kila mmoja akapenda uchaguzi wa *Khalifa* ufanywe haraka.

Mazungumzo yalikuwa hayasongi mbele, na mlango ukabishwa mfululizo kwamba zengwe limalizwe haraka. Sahibzada Sahib r.a. akapendekeza ya kwamba kwa kuwa hakuna matumaini ya kupatana, hivyo yapaswa wote waondoke waende Masjid Nur na mashauri yafanywe na wale waliokwisha jumuika tayari huko. Hapo Maulawii Muhammad Ali akafoka: "Wasema haya, kwani wajua watamchagua nani."

Sahibzada Sahib r.a.: "Kinyume chake, niko tayari kufanya baiati ya yeyote miongoni mwenu."

Maulawii Muhammad Ali: "Hata hivyo unaelewa wafikirivyo."

Sahibzada Sahib r.a. sasa akawa na yakini kabisa kwamba mwafaka hauwezekani. Basi akasema: "Twaamini kwamba ni wajibu

wa kidini kudumisha *Ukhalifa*, lakini unafikiri *Khalifa* hahitajiki. Hitilafu hii haiwezi kupatanishwa. Uko huru kufanya upendavyo. Sisi tutashauriana na kufanya baiati kwa yule tunayeafikiana juu yake.

Kikao kilimalizika kwa maneno hayo. Sahibzada Sahib na wenzake wakaelekea Masjid Nur ambako mkusanyiko wa watu kati ya elfu moja mia tano na elfu mbili walikuwa wanawasubiri. Sahibzada Sahib akawasalisha sala ya alasiri, kisha Nawab Muhammad Ali Khan r.a. akawasomea wasia wa Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. wa Machi 4, 1914, aliomkabidhi yeye na akaongeza: "Nimekwisha toa amana ya Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. Sasa ni juu yenu kutenda sawa nayo." Tangazo lake likapokelewa kwa kelele za "Hadhrat Mian Sahib, Hadhrat Mian Sahib" kutoka kila upande. Katikati ya kelele hizo akainuka Maulawii Seyyid Ahsan r.a. na akapaza sauti: "Masihi Aliyeahidiwa a.s. alisema kunihusu mimi kwamba mimi ni malaika mmojawapo kati ya malaika wawili waliotajwa katika Hadithi kwamba Masihi atateremka katika zama za mwisho akiegemea juu yao. Mimi nafikiri Sahibzada Bashiruddin Mahmud Ahmad anastahili kabisa kwa kila jiha kuchukua baiati yetu, nami namwomba atupokelee baiati yetu. Hapo Maulawii Muhammad Ali na Seyyid Hamid Shah r.a., wote wawili, wakainuka, ikaonekana wanataka kusema kitu, na wakaanza kuzozana nani aseme kwanza. Waliopo hawakuwa na moyo wa kuwafurahia, na Sheikh Yakub Ali Irfani r.a. akaeleza maono ya watu wote kwa kusema: "Wakati ni wenye thamani sana wala hauwezi kupotezwa kwa mizozo ya aina hii. Mpenzi wetu, tafadhali kubali baiati yetu." Hayo yalipokelewa kwa kelele za *Labeka, Labeka,* na watu wakaanza kusonga mbele upande wa Sahibzada Sahib. Hapo wale wachache wenye shauri jingine wakaondoka. Hakuna aliyewazuia.

Kimya kikaushika mkutano, ingawaje kila mmoja alikuwa na kiherehere cha kumsogelea karibu zaidi Sahibzada Sahib r.a.

Yeye akakaa kimya kana kwamba anashughulikia maombi. Qadhi Amir Husain, Sheikh mheshimiwa, akamwendea akihangaika sana na kamwomba: “Hudhur, tafadhali kubali baiati yangu.” Sahibzada Sahib akaangalia juu, macho yake yakimtafuta mtu fulani. Akamgundua Maulawii Seyyid Muhammad Sarwar Shah r.a. aliyekuwa amebanwa baina ya msongamano wa watu wenye shauku na kumwambia: “Maulawii Sahib, jukumu hili zito nimebebeshwa ghafla isivyotazamiwa. Sikumbuki masharti ya baiati. Tafadhali nieleze hayo.” Basi kuchukua baiati kukaanza. Hadhrat Khalifatul Masihi II akatamka maneno ya baiati kama yalivyonenwa na Maulawii Seyyid Mohammad Sarwar Shah r.a., na kila mmoja akarudia hayo kufanya baiati. Maneno ya baiati ndiyo haya:

> “Nashuhudia kwamba hamna mwabudiwa isipokuwa Mungu, na ninashuhudia kwamba Muhammad ni Mtumishi Wake na Mjumbe Wake, (mara mbili).
>
> “Leo, katika Jumiya Ahmadiyya, natubu kwa dhambi zote juu ya mkono wa Mahmud, na kwa kujaaliwa na Mungu nitajibidiisha kuepukana na dhambi zote katika siku zijazo; sitamshirikisha Mungu na chochote, nitatanguliza dini juu ya mambo ya kidunia, nitajaribu kutekeleza maamrisho yote ya Islam, na nitakutii katika mema yote utakayoniamuru.
>
> Nitamwamini Mtume Mtukufu kuwa *Khatamun Nabiyyin;* nitaamini madai yote ya Masihi Aliyeahidiwa a.s.; na nitatia bidii kuzagaza Islam.
>
> “Namwomba Mungu, Mola wangu, msamaha kwa dhambi zote na ninatubu kwake (mara tatu).
>
> Mola wangu, nimejidhulumu nafsi yangu. Nakiri dhambi zangu, na ninakuomba Unisamehe dhambi zangu, kwani

hakuna awezaye kusamehe dhambi isipokuwa Wewe."

Alipokwisha kuchukua baiati, Hadhrat Khalifatul Masihi r.a. akafanya dua ndefu ya kimya, na kila mmoja akaungana naye, na akamalizia kwa hotuba fupi.

Hivyo wanajumuiya waliokuwa wanahangaika na kuachwa katika ukiwa wakaunganika mara nyingine katika udugu wa kiroho. Nyoyo zote zikatulia, na roho zote zikapata raha. Kila mmoja akapata msukumo mwema wa ndani kabisa. Ukunjufu na utulivu ukaenea.

Hadhrat Khalifatul Masihi II r.a. akasalisha sala ya jeneza ya Hadhrat Khalifatul Masihi I r.a. Halaiki ya watu, Waahmadiya, wasiokuwa Waahmadiyya, Mabaniani, Masingasinga, Wakristo, wanaume kwa wanawake na watoto, wakajumuika wote kumsifu yule ambaye ukarimu wake ulikuwa kwa wote bila ubaguzi, ambaye moyo wake ukafurika mapenzi na huruma kwa wote. Kabla halijachwa jua mwili wake ukazikwa upande wa magharibi wa rafiki yake mpendwa, Masihi Aliyeahidiwa a.s., ambaye kwa ajili yake aliwaacha wote.

Mola, uifanye mvua ya rehema Yako inyeshee kaburini pake;

Umwingize peponi kwa rehema Yako.

Magazeti ya sehemu zote za nchi yakataja sifa bora za mkarimu huyu wa ubinadamu. Hapa twaweza kueleza moja au mawili tu.

*Zamindar* likaandika:

> "Miongoni mwa habari zilizopokelewa kwa simu ya maandishi leo, kuna habari itakayowahuzunisha Waislamu, hususan Waahamadiyya, ya kifo kilichotokea Machi 13, baada ya maradhi yaliyoendelea kwa wiki kadha, cha Maulawii Hakim Nuruddin Sahib, aliyekuwa Sheikh mtaalamu na mwanachuoni aliyeelimika. Sisi ni wa Mungu na Kwake tutarejea.

Maulawii Hakim Nuruddin alijulikana baina ya wafuasi wake kama Khalifatul Masihi na alikuwa mwenye kushika uongozi baada ya Mirza Ghulam Ahmad. Kifo chake ni msiba mkubwa kwa Waahmadiyya watakaouhisi kwa muda mrefu. Mbali na hitilafu za kiitikadi, dhati na vipawa vya Maulana Hakim Nuruddin vilikuwa vya hali ya juu sana hata kwamba Waislamu wote watahuzunika kwa kufariki kwake. Yasemekana kwamba inahitajika karne nzima kudhihirika mtu mwenye akili halisi ya kuvuta macho. Leo tunaomboleza kifo cha mtaalamu mashuhuri wa dini. Tunawapa pole marafiki zetu Waahmadiyya ambao wamepata uchungu wa msiba huu mkubwa. Twaomba Mungu, Mwingi wa ukarimu Amwingize Maulawii Hakim Nuruddin katika rehema Yake na kuwajaalia wafuasi wake na watu wa familia yake subira."

Mhariri wa *Curzon Gazette* akaandika:

"Si tu kwamba tulimjua marehemu Maulawii Hakim Nuruddin, tulijuana sana kikamilifu tulipokuwa huko Jammu kwa miaka mingi. Tukaonana kila jioni. Alikuwa na moyo mwema na mkarimu. Alikuwa mcheshi, mchangamfu. Alikuwa tambo la mtu, mzuri wa sura, mwenye rangi nzuri na ndevu nyingi. Alisimamia shule za serikali na hospitali kwa bidii na uaminifu. Alipata mshahara mkubwa ambao sehemu yake kubwa aliitoa kwa ukarimu wake kwa posho na matumizi ya wanafunzi waliohitaji msaada. Katika maisha yake yote aliwaruzuku mamia ya wanafunzi wenye hali ndogo. Sheikh Abdullah, kijana wa Kikashmiri aliyekuwa Brahmin (Baniani) akasilimu kwa mafunzo yake. Akamsaidia na akamtolea gharama yote ya masomo ya shule na ya elimu ya juu mpaka akawa wakili (mwanasheria) na akaimarisha kazi yake ya uwakili katika

Ali Garh. Sheikh Abdullah alipenda sana kuwaelimisha wanawake na akaanza kutoa jarida *Khatun* (Mwanamke) kutoka Ali Garh.

Basi, Hakim Nuruddin alikuwa mfano hai wa ukarimu wa kweli. Alikuwa na jazba mbili, kufanyiza ustawi wa wanafunzi wenye hali ndogo na kukusanya vitabu vinavyopatikana kwa nadra. Mapato yake makubwa yalikuwa yote kwa miradi hii miwili. Alikuwa mnyenyekevu sana na mwenye staha. Alitimiza wajibu wake wote kwa unyofu. Waliofanya kazi chini yake walipendezwa naye, hawakuwa na manung'uniko. Alikuwa Sheikh mtaalamu na mwanachoni mkubwa; alikuwa bingwa wa Kiarabu. Katika saa zake za faragha alitoa darasa la *Bukhari* na *Muslim*. Alikuwa na utambuzi mwingi wa dini."

Maulana Abul Kalam Azad, aliyekuwa mwenyewe mwanachuoni mashuhuri na mwanasiasa, halafu akawa Mwenyekiti wa All-India Congress, na waziri wa Elimu katika Serikali ya India, akaandika katika *Al-Balagh,* chini ya maelezo mafupi ya habari:

"Buriani, Nuruddin – Nasikitika kwamba mimi ni wa mwisho kutoa rambirambi juu ya Imam wa Jumuiya Ahmadiyya kutuacha mkono, aliyekuwa mchunguzi hodari wa kweli za daima, Hakim Maulawii Nuruddin. Mtu aliyejikusanyia ujuzi mpana sana pamoja na hazina ya mifano ya kiamali ya utakaso na wema wa kweli hayuko tena baina yetu. Utaalamu katika yote yale yaliyoihusu dini na ujuzi mkubwa wa kweli zote, ukichanganywa na elimu pana iliyoenea kila aina ya vitabu kuanzia maandiko ya dini hadi hadihti bora za kubuniwa, vikanyanyua dhamira ya Nuruddin hadi pale ambapo ikaweza kufikiria na kupenya katika siri ya maono ya binadamu. Ndiyo sababu mshtuo hafifu wa maneno yake machache lakini yenye

maana sana ukafumba midomo ya wapinzani wake wenye ufasaha wa kuvutia. Dhati yake nzima ilikuwa mchanganyiko wa utawala wa maono ya kidini na ujuzi. Busara yake iliyoenea ulimwengu mzima ilikuwa wavu wa kisumaku wa hekima. Uchunguzi wake wa kifilosofia ukichanganyika na unyofu kamili ukamtobolea siri za mbinguni. Imani yake timilifu katika hekima ya Mungu ikamtilia moyoni mwake fikara zake zote.

"Sehemu ya mwisho ya maisha yake ilitolewa wakfu kwa Jumuiya Ahmadiyya; siku zake, mchana na usiku, zilitumika katika bidii za kuchosha kwa kupata miradi ya kiroho ya Jumuiya yake. Kujitolea kwake kwa uaminifu na utii halisi alioonyesha kwa mfunzi wake wa kiroho bila shaka yoyote hakuna kifani chake isipokuwa baina ya Waislamu wa zamani. Kusema nabii Isa a.s. alikufa kifo cha ajali, aliyefikiriwa na watu wote kwamba anaishi mbinguni na kiwiliwili chake, na kuchukua Mahdi na Masihi kuwa mtu mmoja tu, ilikuwa ni ujumbe mchungu kwa Masheikh wa Kiislamu wa Bara Hindi, na gharika ya upinzani ambao itikadi hiyo mpya ilisababisha ulikuwa kama radi ya kuteketeza; lakini ukali wa dhoruba hii haukuuathiri uimara wa imani ya Nuruddin. Akasimama imara kama mlima mzito usiotikisika ukiyakabili mawingu yapitayo kasi sana na ngurumo ya mshindo. Uthabiti wake halisi haukuvumilia kwamba aachilie mbali mto wa mawe ambao juu yake roho yake iliyosumbuka na iliyokwenda safari ya kuvumbua habari ikapata raha mustarehe mpaka pumzi yake ya mwisho. Ingawaje siafikiani na baadhi ya itikadi za Jumuiya Ahmadiyya, hata hivyo naangalia sana kwa kushangaa mng'ao wa kiroho ambao mwako wake umeyeyusha maono yangu yaliyogandamana yakawa machozi yatiririkayo ya mapenzi.

> Mheshimiwa Nuruddin sasa amefichikana kwa macho yetu, lakini nyayo zake zinadumu kutambulikana waziwazi juu ya uso wa ulimwengu na zasaidia kutuongoza kwenye jumba la uthabiti. Rehema na huruma ya Mungu imwage marashi ya ambari juu ya vumbi lake."

Hilo ni kumbukumbu fupi la kazi nyingi sana bora za aina mbalimbali ambazo mtu mashuhuri Hafidh Alhaji Hakim Maulawii Nuruddin, Khalifatul Masihi I r.a. alitenda. Uchache wa nafasi umekuwa kizingiti nisiweze kutoa maelezo marefu. Lakini jiha moja ya huduma yake kubwa ya Uahmadiyya, Uislamu na ubinadamu yahitaji kutiliwa mkazo. Kurani Tukufu ilitangaza ya kwamba katika zama za mwisho watu wa Kitabu watashirikiana pamoja dhidi ya Islam na kutafuta njia ya kuiangamiza, lakini Mungu Atavunjilia mbali njama zao na Ataishindisha Islam juu ya dini zote (9:30-33). Ushindi huu ulitakiwa kupatikana kwa njia ya Masihi Aliyeahidiwa, si kwa upanga bali kwa kutumia silaha za kiroho. Masihi Aliyeahidiwa akadhihiri, na chini ya maagizo ya Mungu akakusanya ghala ya silaha zile, na kuonyesha namna zitakavyotumika kuzishinda nyoyo za binadamu kwa huduma ya Islam. Akaeleza kwamba ametumwa kwa kuongoza kazi ya kuishindisha Islam na kutoa silaha ambazo kwa kuzitumia hizo Islam itahuika kwa njia ya Jumuiya iliyoanzishwa naye, chini ya uongozi wa *Makhalifa* zake wa kiroho. Akasema, amekwisha panda mbegu itakayochipua ikawa mti wenye matawi yatakayoenea, na kwamba yeyote hataweza kuzuia ukuaji wake. Baada ya kutimiza kazi yake aliyoagizwa na Mungu kutekeleza akaaga mnamo 26 Mei 1908. Msiba huu ulikuwa pigo kubwa mno kwa wanajumuiya ambao walishikwa na butwaa wasielewe wapi kwa kuelekea. Mungu Akawaimarisha na kwa huruma na rehema Yake Akawaunganisha pamoja chini ya uongozi wa Hadhrat Maulawii Nuruddin r.a. akiwa Khalifatul Masihi. Kulikuwa hamna hata sauti moja isiyokubali. Lakini ole, muda si

muda, haraka zaidi mno, minong'ono, si ya kukaidi kwa wazi, bali manung'uniko wa ndani yakaanza kuibuka na kusikika. Baadhi ya wanajumuiya maarufu wakaanza kufikiria demokrasia, Katiba na Mabunge. Walakini, ni ajabu kabisa kwamba wakaipendelea *Sadr Anjuman Ahmadiyya,* ambamo walijikuta kuwa wengi, kama uwanja wao wa kukusanyika, wakisahau, au pengine kwa sababu, hiyo ni chama kinachojifanyiza upya, hakikufanyiwa uchaguzi wala siyo cha kidemokrasia, ilhali *Khalifa* alikuwa wa hao wenyewe, na pia alikubaliwa na wanajumuiya wote. Lakini jiha hii ilikuwa ya kijuujuu tu. Walichopuuzilia mbali kabisa ni kwamba *Ukhalifa* ni daraja la kiroho lililoahidiwa msaada wa Mungu waziwazi kwa kukazania (24:56). Ushindi wa Islam ulikuwa upatikane kwa njia za kiroho chini ya maagizo ya *Makhalifa* walioongozwa na Mungu. Hivyo, ubishi ukazuka. Je, Jumuiya ilikuwa iongozwe na kuelekezwa na kiongozi wa kiroho mwenye madaraka ya mwisho aliyewekwa na kuongozwa na Mungu, ama isimamiwe na kutawaliwa na Chama kilichosajiliwa kinachojifanyiza upya? Kama Jumuiya iwe ilivyotajwa nyuma, hapo hiyo haitakuwa Jumuiya ya kiroho na itapotewa na ahadi za Mungu na Dhamana Zake zilizotolewa katika sura 24:56. Swala hilo lililowekwa mbele ya yule shujaa aliyeutetea *Ukhalifa*, Hadhrat Maulawii Nuruddin, Khalifatul Masihi I r.a. Hakuliepa wala hakulipiga chenga, wala hakuacha hata inchi moja ya ardhi mbele ya tambio na vitisho vya dhahiri na vya siri. Akasimama imara kama mwamba na mawimbi ya manug'uniko na ukaidi yakampigapiga vikali na yakarudi nyuma yakiwa hoi katika bumbuazi kama povu la mshindo mkubwa. Alimtegemea Mungu kikamilifu; akajua kwamba msimamo wake ulikuwa wa haki machoni mwa Mungu. Theluthi mbili za karne zilizopita tangu atuache mkono zimethibitisha ukweli wake machoni mwa binadamu pia.

Kama juu ya swala la daraja na madaraka ya *Khalifa*, Hadhrat Maulawii

Nuruddin, Khalifatul Masihi I r.a., angelilegea hata kama kidogo mno kwa kushurutishwa mfululizo na wale waliojidhania kushika uongozi katika Jumuiya, mti uliopandwa na Masihi Aliyeahidiwa ungelipata kunyauka haraka haraka, kama kwa hakika inavyoshuhudika katika maanguko ya kusikitisha ya kundi la wenye kukaidi na chama chao. Ahadi ya Mungu kuhusu ushindi wa Islam katika zama za mwisho ingelibaki bila kutimia, na jambo hilo lingetilia shaka ukweli wenyewe wa Islam. Hadhrat Maulawii Nuruddin r.a. alikuwa chombo cha Mungu kwa kudumisha na kuimarisha desturi ya *Ukhalifa* ambao kwa njia ya huo ushindi wa Islam ulitakiwa kutangazwa na kuletwa. Namna chombo hicho kilivyofanya kazi vizuri na barabara yaweza kufahamika kutoka katika kurasa za kitabu hiki, na natija za jinsi ya kufanya kazi yake yaweza kushuhudiwa kutokana na ustawi ulioupata mti wa Uahmadiyya. Mzizi wake upo imara na matawi yake yamefikia mbinguni. Huleta matunda yake mapya mapya nyakati zote kwa amri ya Mola (14:25-26). Kinyume chake mti wa wakaidi umeng'olewa ardhini wala hauna uimara (14:27). Ulezi wa Hadhrat Maulawii Nuruddin r.a. ukahakikisha kwamba mbegu iliyopandwa na Masihi Aliyeahidiwa a.s. haina budi kumea na kuimarika, kisha kunenepa na kusimama imara juu ya shina lake na kuwafurahisha wapandaji; ili makafiri wapate kukasirikia hiyo (48:30).

Hiyo ilikuwa kazi ambayo hekima ya Mungu ilimkabidhi Nuruddin r.a.; akaitekeleza kazi hiyo kikamilifu kabisa.

Mungu na Amjalie, kwa rehema Yake na huruma Yake, daraja la juu kabisa katika Pepo za radhi Yake kuwa makazi Yake. Amin.